PROTECTION international

# Mwongozo Mpya Wa Ulinzi kwa Watetezi Wa Haki Za Binadamu

Umetafitiwa na kuandikwa na Enrique Eguren na Marie Caraj

# Mwongozo Mpya Wa Ulinzi

kwa

# Watetezi Wa Haki Za Binadamu

Umetafitiwa na kuandikwa na Enrique Eguren
na Marie Caraj, Protection International (PI)

Umechapishwa na Protection International

Kimechapishwa na Protection International 2012
Rue de la Linière, 11
B-1060 Brussels, Belgium.

Aliyetafsiri: Kimani Njogu

**Toleo la Tatu**

Haki ya kunakili © 2008 ni ya Protection International. Mwongozo huu umetolewa kwa manufaa ya wateteaji wa haki za binadamu na unaweza kunukuliwa kwa matumizi yasiyokuwa ya kibiashara mradi tu shukurani zitolewe kwa chanzo na waandishi. Tafadhali omba ruhusa ili kuingiza mwongozo huu kwenye machapisho mengine au kwa matumizi mengine.

**Nakala za Mwongozo Mpya kutoka kwa:**
Protection International
Rue de la Linière, 11.
B-1060 Brussels, Belgium
Simu: +32(0)2 609 44 05 / +32(0)2 609 44 07
Faksi: +32(0)2 609 44 07
Barua pepe: pi@protectioninternational.org

Nakala hii inaweza kupakuliwa bila malipo kutoka www.protectionline.org

Nakala hii mpya inapatikana kwa Kiingereza, Kifaransa, Kihispania na Kiswahili (pia inatafsiriwa kwa lugha nyingine na Protection International)

ISBN: 978-2-930539-25-6

# Utangulizi kwa toleo la kwanza na Hina Jilani

*Katika kazi yangu kama Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu nimegundua kwa masikitiko makubwa ongezeko la idadi ya ripoti zinazohusu dhuluma za haki za binadamu dhidi ya watetezi na namna wanavyolengwa kuanzia hali ya chini kama vile kudhalilishwa na kunyanyaswa hadi ukiukaji mkubwa kama vile kushambuliwa na kutishiwa haki zao za kuishi na wengine. Katika mwaka wa 2004, tulishughulikia ripoti za angalau watetezi 47 waliokuwa wameuawa kutokana na kazi yao.*

*Ni dhahiri kwamba wajibu wa kimsingi wa kuwalinda watetezi wa haki za binadamu ni wa serikali, kama inavyodhihirishwa katika Azimio La Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za Binadamu*[1]*. Ni lazima tuendelee kuhakikisha kwamba serikali zote zinachukulia uzito majukumu yake kuhusu suala hili na kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha kwamba watetezi wa haki za binadamu wanalindwa.*

*Hata hivyo, kiwango cha hatari wanazokabiliana nazo watetezi hawa kila siku ni cha juu hivi kwamba ni muhimu pia kutafuta mbinu nyinginezo za kuimarisha ulinzi wao. Kwa hali hii,ninatumai kwamba Mwongozo huu wa Ulinzi utawapa watetezi wa haki za binadamu usaidizi wa kuendeleza mipango yao ya usalama na mikakati ya kujilinda. Watetezi wengi wa haki za binadamu wanajihusisha sana na kazi yao ya kuwalinda wengine kiasi kwamba hawaupi uzito ufaao usalama wao. Ni muhimu kwamba sote tushughulike na haki za binadamu ili tuwe makini kwa usalama wetu na ule wa watu tunaofanya nao au kuwafanyia kazi.*

Hina Jilani
Mwakilishi maalum wa zamani wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za Binadamu

1 Azimio la Haki na Jukumu la Watu, Makundi, na Mashirika ya Kijamii ili Kudumisha na Kuheshimu Haki za Binadamu na Uhuru wa Msingi Kama Ilivyotambuliwa Kimatifa.

# Protection International -PI-

Wanachama wa PI wana uzoefu wa zaidi ya miaka 25 katika kuwalinda watetezi wa haki za binadamu na makundi mengineyo dhaifu[1].

PI inalenga kuchangia katika kuyatimiza majukumu ya kitaifa na kimataifa ya kuwalinda watetezi hao. Tayari mashirika mengi yasiyo ya kiserikali pamoja na taasisi mbalimbali zinayashughulikia masuala ya haki za binadamu pamoja na watetezi wazo.

Mikakati ya kilimwengu ya PI ya kuwalinda watetezi ni kama vile:

## Kujenga uwezo na mafunzo ili kuimarisha ulinzi na usalama

- Tathmini ya Hatari, hifadhi ya ulinzi/ usalama.
- Uhamisho wa maarifa na vifaa.
- Uchapishaji wa miongozo, miongoni mwayo ni huu mpya (pamoja na toleo lake la hapo awali[2]).
- Mafunzo: kati ya 2004 – 2008, zaidi ya watetezi 1700 wameshiriki katika ujenzi wa uwezo na warsha za usalama huku wakiimarisha uwezo wa kuulinda usalama wao binafsi na ule wa watu wengine.

## Utafiti wa ulinzi

- Mafunzo na uwekaji wazi wa zana tendaji za ulinzi/usalama
- Uchapishaji wa habari kutokana na yale waliojifunza pamoja na matendo bora.

## Utetezi wa ulinzi

- Usambazaji wa habari kuhusu ulinzi miongoni mwa taasisi za HRD, IDP, EU na wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya kwa njia za mapendekezo, ripoti na taarifa kwa waandishi wa habari na pia habari halisi za matukio au watu fulani.
- Kuzikumbusha mamlaka za kitaifa na kimataifa kuhusu wajibu wao wa kimataifa wa kulinda watetezi wa haki za binadamu, wakimbizi wa ndani kwa ndani, wakimbizi kutoka nje na wahudumu wengine wa jamii.
- Kuendeleza mijadala na hatua za kulinda watetezi hao, uhusishaji wa bunge, vyama vya wafanyikazi na vyombo vya habari.
- Juhudi za kupinga uhuru wa kutumia mamlaka vibaya dhidi ya watetezi kupitia ushahidi wa kimahakama na rufaa dhidi yake.

---

1 Kufikia tarehe 25 Oktoba 2007, kupitia kwa agizo la kifalme la Federal Public Justice Service, shirika la European Bureau of peace Brigades International, kupitia kwa marekebisho ya makala yake yaliyochapishwa katika Jarida rasmi la Ubelgiji, lilikuwa "Protection International" muungano wa kimataifa usio wa kutengeneza faida.

2 Lilichapishwa mwaka 2005 kwa usaidizi wa kifedha wa Front Line na Development Co-operation of Ireland.

### Ulinzi kwa video (Utetezi wa video)

- Picha za watetezi wa haki za binadamu.

### Dawati la Ulinzi

- Kwa ushirikiano na miungano iliyopo ya watetezi wa haki za binadamu, dawati za ulinzi huwekwa katika sehemu za kitaifa na kimaeneo kwa ajili ya ulinzi na usalama.
- Ukabidhi endelevu wa mchakato mzima wa usalama/ulinzi kwa PD (umilikaji ni sehemu ya mchakato).

### Ulinzi kwa tovuti

- www.protectionline.org ni tovuti tosha inayoweza kutumiwa na au kwa ajili ya Watetezi wa Haki za binadamu na wale wanaotaka kuchangia kwa ulinzi wa watetezi hao.
- Kujenga upya habari,nyaraka,machapisho,ushuhuda, hatua za dharura na zana za kuendeleza ulinzi wa watetezi.

### Mfumo sanifu

PI inafuata kanuni zote za kimataifa katika sheria ya kimataifa kuhusu haki za binadamu. PI itatumia hususan miongozo iliyotolewa na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi haki za binadamu (1998), miongozo ya Umoja wa Nchi za Ulaya ya HRD (2004), na pia maazimio kuhusu watetezi waliopandishwa cheo na PI na kuidhinishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya kule Uhispania, Ubelgiji na Ujerumani.

## Warsha Za Protection International (PI) Za Kujenga Uwezo Na Usalama

Kuanzia mwaka 2004 hadi 2007, jumla ya watetezi 1747 wa haki za binadamu wameshiriki katika warsha za PI za kujenga uwezo na usalama.

- Katika Amerika ya Kati na Kusini: watetezi 558
  (Bolivia, Brazil, Colombia, Guatemala, Honduras, México, Peru)
- Katika Asia: watetezi 650
  (Burma, Indonesia, Nepal, Thailand)
- Katika Afrika: watetezi 441
  (Kenya, Uganda, Democratic Republic of Congo)
- Katika Ulaya: watetezi 98
  (Germany, Belgium, Ireland, Serbia, Republic of Ingushetia)

Watetezi wa haki za binadamu aghalabu huwatetea watu wengine huku wakipuuza usalama wao kutokana na sababu kadhaa. Mafunzo ya PI ya usalama na ulinzi huzishughulikia sababu hizi na kisha hutenga muda wa kutafakari juu ya hatari na vitisho ambavyo walengwa wakuu huwa ni watetezi hawa. Mafunzo ya PI hupelekea kuwepo kwa mchanganuo wa kina wa matishio na pia ufahamu na mantiki inayohitajika kuhusisha usalama katika ratiba za kazi za watetezi wa haki za binadamu. Katika mafunzo haya, mada ya usalama huainishwa katika vipengele mbalimbali ili kuweza kuvichambua, kutafakari juu ya uwezekano wa kuwepo nadharia fulani, hali na matokeo ya machaguo maalum yanayoweza kupatikana na kisha kuchukua chaguo ambalo watetezi hao wanaamini kwamba wanaweza kumudu matokeo yake, wakifahamu fika kwamba hawawezi kuwa na uhakika wa matokeo maalum.

Katika hali yoyote ile hakuna jawabu la kimiujiza linaloweza kufaa kila wakati; mafunzo haya yanakusudiwa kuhakikisha kwamba watetezi wanapata maarifa yanayohitajika kwa ajili ya usalama wao: uchanganuzi, matokeo, usimamizi na ujengaji upya wa mchakato huo mzima. Wanapaswa kufanya hivi kwa kiwango cha mtu binafsi, cha shirika au baina ya mashirika kukitiliwa maanani kwamba wanafaa kuwa na ufahamu wa kiasi wa masuala ya kisiasa, jamii-nafsia na ufahamu wa nje.

# Dibaji

Baada ya zaidi ya mwongo mmoja wa mafunzo, utafiti na mikutano na watetezi wa haki za binadamu na washikadau wengineo wanaohusika na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu, sisi katika **Protection Internationa**l tumeamua kuwashukuru upya watetezi na tena kuihusisha michango yao katika mwongozo huu mpya wa ulinzi ulioandikwa pamoja na, kutoka kwa, na kwa ajili ya watetezi wote wa haki za binadamu.

Kwa miaka mitatu ya nyuma iliyopita, **Protection International** imepiga hatua zaidi katika mafunzo na utafiti wake, huku ikipata uzoefu wa nyanjani na maoni rejea kutoka kwa watetezi wa haki za binadamu.

Katika mwongozo huu mpya, **PI** inapendekeza mantiki ya usimamizi inayoweza kuhusishwa katika miundo na mazingira ya kiuendeshaji huku ikifikia matokeo yaliyo sawa: kuhusisha mpango wa usalama katika utaratibu wa kazi. Hakuna jibu la kimiujiza, bali ni hali ya kumudu machaguo na matokeo tu. Haya yanaweza kufanikishwa kupitia uchangizi wa pamoja wa mawazo, kuuliza maswali halisi, kufanya tathmini ya usalama wa kiuendeshaji pamoja na hatari, kuandika mipango na michakato jumuishi….

Hivyo basi, mwongozo huu mpya unalenga kuwafanya watetezi wa haki za binadamu waimiliki harakati nzima ya usalama na ulinzi.

Umilikaji ni kipengele cha usalama wenyewe. Mwongozo huu mpya unachangia katika kujenga uhuru na uendelezaji wa usalama na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu.

Ijapokuwa hakuna mpango wa usalama wa kijumla,mwongozo huu unavuka mipaka ya tofauti za kitamaduni,kijamii,kidini,mazingira na miundo ya kishirika. Mwongozo huu waweza kutumika na watetezi wa haki za binadamu kuuimarisha usalama na ulinzi wao kama tunavyojua kwamba wanazo mbinu zifaazo za kufanya hivyo:maarifa na uzoefu wa hali zao binafsi.

**Protection Internationa**l hutofautisha baina ya usalama wa watetezi wa haki za binadamu- wa kwake (mtetezi) binafsi- na ule unaotoka kwa washikadau wengineo hadi kwa mtetezi.


## Shukrani

Toleo jipya la mwongozo lilioendelezwa na kuandaliwa kisasa ni matokeo ya mchango wa:

- Watetezi wote wa haki za binadamu ambao wamehudhuria mafunzo ya Protection International kuhusu hifadhi ya usalama na ulinzi. Haiwezekani kuwaorodhesha wote hapa. Wanapatikana Bolivia, Brazil, Burma, Colombia, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Guatemala, Honduras, Indonesia, Ingushetia, Kenya, Mexico, Nepal, Peru, Serbia, Sri Lanka, Thailand, Uganda.
- Wanachama wa PI wa sasa na wa awali: Pascal Boosten, Soledad Briones, Shaun Kirven, Christor Klotz, Rainer Mueller, Michael Schools.
- Washiriki wa PI ni Ana Cornida, Eric Juzen, Maria Martin, Thomas Noirfalisse, Sheila Pais, Flora Petrucci, Sophie Roudil, Catherine Wielant, Jabier Zabala.

- Carmen Díez and Montserrat Muñoz ambao wote walishughulika pakubwa katika kusuka na kuandaa matoleo ya awali na ya sasa ya miongozo. Thomas Noirfalisse alichangia kwa usanifu wake wa nembo ya PI na mawazo ya jinsi ya kulisanifu jalada. Wazo kunjufu kwa Brigitte Scherer.

Tunatoa shukrani kwa usaidizi wa *Bundeministerion fur wirtshchaftliche Zusammenarbeit und Entwicklung* (Wizara ya Ujerumani ya maendeleo na Ushirikiano, na Service public federal Affaires Etrangeres Belgique (Huduma ya Umma na Mambo ya Nchi za kigeni ya Ubelgiji).

Mwongozo Mpya wa Ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu unatia usasa na kuuendeleza mwongozo wa kwanza wa ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu (Mwandishi: Luis Enrique Eguren © 2005 PI) ambao ulichapishwa kwa msaada wa kifedha wa Front Line na wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Ireland.

Muswada wa mwongozo cha kwanza ulitolewa maoni na Arnold Tsunga (Zimbabwe, Lawyers for Human Rights), Sihem Bensedrine (Tunis, Conseil National pour les libertes en Tunisie), Father Bendan Forde (Colombia, Itinerant Franciscans), Indai Sajor (Philippines, Mkurugenzi wa zamani wa Asia centre for human rights), James Cavallaro (Brazil, mshiriki wa haki za binadamu-Chuo cha Sheria cha Havard), Nadejda Marques (Brazil, mshauri na mtafiti-Global Justice) na Marie Caraj (PI former PBIBEO).

Washiriki wengine wamechangia kwa kazi zao binafsi: Jose Cruz na Iduvina kutoka SEDEM (Guatemala), Jaime Prieto (Colombia), Emma Eastwood (Uingereza) na Cintia Lavandera akiwa Human Rights Defenders Program from Amnesty International kule London.

Mpango wa Utetezi wa Haki za Binadamu kutoka shirika la kimataifa la Amnesty International kule London (The Human Rights Defenders Program from Amnesty International in London) pamoja na mradi wa Indonesia wa PBI (the Indonesia Project of PBI) ilitoa pesa za kugharamia tafsiri za toleo la kwanza la Mwongozo hadi katika lugha ya Kireno na Kiindonesia mtawalio. Tume ya Kimataifa ya Wanasheria (The International Commission of Jurists) ilitafsiri toleo hilo hadi katika lugha ya Kithai, na PBI hadi katika lugha ya Kinepali.

Sura ya 2.11 inatokana na kazi ya Robert Guerra, Katitza Rodriguez na Caryn Madden kutoka Privaterra (Canada).

## Shukrani kutoka kwa mwandishi: Luis Enrique Eguren

Pia watu wengi wengineo wamechangia katika ukusanyaji wa maelezo ya asilia yaliyohitajika kuuandika Mwongozo huu,hivi kwamba ni vigumu kuwaorodhesha hapa wote. Ningependa kutaja majina ya wachache wao:

To Kwa watu wote wa PBI na hasa kwa washiriki wenzangu wa karibu wa hapo awali kwenye mradi wa Colombia ambao walikuwa Marga, Elena, Francesc, Emma, Tomas, Juan, Mikel, Solveig, Mirjam, Jacob na wengi wengineo.

Kwa Danilo, Clemencia na abilio na washiriki wenzao kutoka *Comision Interedesial de Justicia Paz* kule Colombia. Walinifunza jinsi ya kuishi na kupendwa na watu.

Kwa watu wa Santa Marta, kule El Salvador, na wale wa Cacarica, Jiguamiando na San Jose de Apartado kule Colombia. Wao miongoni mwa wengine walinifunza jinsi watu wa mashambani wanaishi kwa heshima.

Kwa Irma Ortiz, mkufunzi-mwenza katika warsha nyingi na washiriki wenzangu wengine katika Pensamiento *Accion Social (PAS)* kule Colombia.

Kwa ushauri na maarifa ya awali yaliyotolewa na REDR (London) na Koenraad Van Brabant (Ubelgiji).

Na kwa watetezi wengi waliokutana El Salvador, Guatemala, Colombia, Mexico, Peru, Bolivia, Burma, Sri Lanka, Croatia, Serbia, Kosovo, Rwanda, Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, Ingushetia na kadhalika. Mazungumzo mengi,vilio, tabasamu, kujifunza na hata kujitolea….

Mwisho, hakuna ambacho kingewezekana bila ya mapenzi na kujitolea na usaidizi wa Grisela na Iker na wazazi wangu. Pendo langu lote liwaendee.

**Shukrani kutoka kwa mwandishi-mwenza: Marie Caraj**

Ninahisi upendo, heshima, mshikamano, huruma na shukrani kwa mtetezi yeyote wa haki za binadamu niliyekutana naye. Wameyabadilisha maisha yangu. Siku tulizokuwa nao pamoja zimepelekea kuwepo kwa mshikamano thabiti baina yetu.

Nina ghadhabu kubwa kwa wakiukaji wa haki za kibinadamu na ninatarajia kuwa siku moja wakiukaji hao watakuja kutambua kuwa katu hawabaguliwi na watetezi wa haki za kibinadamu na hivyo watajiunga na vuguvugu hilo wakati ambapo haki zote za kibinadamu zitaheshimiwa na watetezi wazo kufurahia maisha ya kawaida.

Kwa Leze Gegaj, mamangu,ambaye ndiye mtetezi wa haki za kibinadamu wa kwanza mwanamke niliyekutana naye.

Kwa rafiki na washiriki wenzangu wote kwa msaada wao usiosemeka. Wengi wao wamewasimulia wenzao yale yote niliyorejea nayo na wamenisaidia kuzichochea hamasa zangu.

Tunawashukuru wote tuliowataja hapa na watetezi wengi wa haki za binadamu ambao tumefanya nao kazi na tuliosoma kutoka kwao kwa msaada wao. Makosa yoyote yaliyosalia katika Mwongozo huu mpya (ingawa tumejitahidi kuyaondoa yote) yanatokana kikamilifu na sisi katika uhariri wa nakala ya muswada. Tunatarajia kwamba mwongozo huu mpya utakuwa kifaa muhimu katika uimarishaji wa ulinzi na usalama wa watetezi wa haki za kibinadamu, ingawa tunagundua kwamba hakitoi dhamana yoyote na kwa vyovyote vile kila mmoja anapaswa kujiwajibikia kuhusu masuala haya. Tunayatarajia maoni yako.

Protection International
April 2009

## Hati ya kukana

Yale yote yanayopatikana katika mwongozo huu hayawakilishi kwa vyovyote vile msimamo wa Protection International.

Waandishi na wachapishaji hawawezi kuhalalisha kwamba habari inayopatikana katika chapisho hili ni kamilifu na sahihi na hawatawajibikia kasoro zozote zitakazopatikana katika harakati ya kulitumia. Sehemu yoyote ya mwongozo huu haiwezi kutumika kama kanuni au dhamana au kutumika kwa njia isiyofaa kutathmini hatari na matatizo ya usalama anayoweza kukabiliana nayo mtetezi.

# Mwongozo Mpya wa Usalama na Ulinzi kwa Watetezi wa Haki za Binadamu

## Haki za watetezi wa haki za binadamu ziko hatarani

Haki za binadamu zinapewa dhamana chini ya sheria ya kimataifa lakini kufanya juhudi ya kuhakikisha kwamba zinafanikishwa na kuziwasilisha kesi za wale ambao haki zao zimekiukwa,linaweza kuwa jambo hatari katika nchi zote za ulimwengu. Watetezi wa haki za binadamu aghalabu huwa nguzo ya pekee baina ya watu wa kawaida na mamlaka yasiyozuilika ya nchi. Wao ni muhimu kwa maendeleo ya harakati za kidemokrasia na taasisi, na hujitahidi kukomesha utekelezaji wa maovu bila kuadhibiwa pamoja na kuendeleza na kuzilinda haki za binadamu.

Watetezi wa haki za Binadamu aghalabu hukumbana na unyanyasaji, kuzuiliwa, mateso, kuharibiwa sifa, kusimamishwa kazi kwa muda, kunyimwa uhuru wa kutembea na hata miungano yao kupata ugumu wa kutambulika kisheria. Katika nchi nyinginezo, wao huuawa, wakatekwa nyara au "wakapotea".

Kwa miaka michache iliyopita, ufahamu wa kijumla umeongezea hatari kubwa wanayokumbana nayo watetezi wa haki za binadamu wakiwa kazini. Hatari hiyo inaweza kutambulika kwa haraka watetezi hao wanapofanya kazi katika mazingira ya uhasama, kwa mfano, ikiwa sheria za nchi zinaadhibu watu wanaoshughulikia haki fulani za binadamu. Watetezi pia wanakabiliwa na hatari ikiwa sheria kwa upande mmoja, itaiwekea vikwazo kazi ya utetezi wa haki za binadamu, na kwa upande mwingine ipuuze kuwaadhibu wale wanaowatishia au wanaowashambulia watetezi hao.Katika hali za mapigano ya kijeshi, hatari hizo huwa katika upeo wa juu.

Isipokuwa kwa hali chache za machafuko ambapo maisha ya mtetezi wa haki za binadamu yanaweza kuwa mikononi mwa wanajeshi kwenye kituo cha ukaguzi, uhasama wanaotendewa watetezi hauwezi kutambulika kama usio wa mpango. Katika hali nyingi, mashambulizi ya kihasama huwa mwitiko wa kimakusudi na vilevile uliopangwa vizuri dhidi ya kazi ya watetezi, na aghalabu huwa yanahusishwa (mashambulizi hayo) na ajenda wazi ya kisiasa au kijeshi.

Changamoto hizi zinawahitaji watetezi wa haki za binadamu kuitekeleza mikakati ya usalama iliyo thabiti na yenye nguvu katika kazi zao za kila siku. Kuwapa watetezi hawa nasaha nzuri au kuwashauri 'wawe waangalifu' hakutoshi. Ulinzi bora wa usalama ni muhimu. Mwongozo huu hautoi suluhisho zifaazo zinazoweza kutumiwa katika mazingira ya aina yoyote. Hata hivyo, unajaribu kutoa mikakati kadhaa inayodhamiriwa kuimarisha hali ya usalama ya watetezi wa haki za binadamu.

Mafunzo bora zaidi ya usalama hutokana na watetezi wenyewe – kutokana na harakati zao za kila siku na mbinu na mikakati wanayobuni baada ya kipindi cha muda ili kuwalinda wengine pamoja na mazingira yao binafsi ya kazi. Hivyo basi, mwongozo huu unapaswa kueleweka kwamba ni kazi inayoendelea na ambayo itahitaji kuongezewa mambo mengi ili ilingane na hali ya sasa, na upate kutumika huku tukiendelea kukusanya habari mbalimbali kutoka kwa watetezi wa haki za binadamu.

Pia kuna mafunzo ya kupata kutoka kwa mashirika ya kibinadamu na ya kimataifa yasiyo ya kiserikali ambayo hivi majuzi yameanza kubuni kanuni na taratibu zao binafsi ili kuuhifadhi usalama wa wafanyikazi wao.

Ni muhimu kuwa na ufahamu kwamba hatari kuu inayowakabili watetezi wa haki za binadamu ni kuwa matishio dhidi yao hugeuka baadaye kuwa mashambulizi ya kihakika. Washambulizi wanayo nia, mikakati na uwezo wa kutekeleza matishio pasina kuadhibiwa.Kwa hivyo njia bora ya kuwalinda watetezi hao ni hatua ya kisiasa ya kulishughulikia suala moja kubwa lililosalia:haja ya serikali na mashirika ya kiraia kushinikiza na kuchukua hatua dhidi ya wale ambao kila siku wanawatishia na kuwanyanyasa na hatimaye kuwaua watetezi wa haki za binadamu. Ushauri unaotolewa katika mwongozo huu haukusudii kwa vyovyote vile kuchukua nafasi ya wajibu halali wa serikali zote wa kuwapa ulinzi watetezi wa haki za binadamu.

Hayo yakishasemwa, watetezi wanaweza kwa njia wazi, kuimarisha usalama wao kwa kuzifuata kanuni na taratibu chache zilizojaribiwa na kuthibitishwa.

Mwongozo huu ni mchango mchache kwa lengo la kijumla la mashirika mengi tofauti:kulinda kazi ya thamani kubwa inayofanywa na watetezi wa haki za binadamu. Wao ndio washika dau wa kwanza na pia wahusika wakuu katika mwongozo huu.

## Mwongozo

Makusudio ya mwongozo huu ni kuwapa watetezi wa haki za binadamu nyongeza ya maarifa na zana ambazo zaweza kuwa muhimu katika kuimarisha ufahamu wao kuhusu usalama na ulinzi. Inatarajiwa kwamba mwongozo huu utachangia katika mafunzo ya usalama na ulinzi na utawasaidia watetezi kufanya makadirio ya hatari zao wenyewe na vilevile kuzibainisha kanuni na taratibu za usalama zinazoambatana na hali zao mahsusi.

Mwongozo huu ni tokeo la tajiriba sawia ya zaidi ya miaka 25 ya wanachama wa **Protection International (PI)** ya kushughulikia haki za binadamu na sheria ya kibinadamu na vilevile katika kuwalinda watetezi wa haki za binadamu (HRD) na makundi mengineyo dhaifu. Tajiriba ya wanachama wa PI inatokana na kujihusisha na kushiriki kwao hapo awali katika **Peace Brigades International (PBI)** ziara za nyanjani na miundo.

Tumepata kuwa na fursa ya kujifunza na kubadilishana tajiriba na maarifa kutoka kwa mamia ya watetezi wa haki za binadamu kule nyanjani,na hata katika warsha mbalimbali, mikutano na mijadala kuhusu usalama. Mambo mengi katika mwongozo huu yameshatekelezwa,ama katika kazi ya ulinzi au kutoa mafunzo

kwenye warsha na watetezi hawa. Mwongozo huu ni zao la mabadilishano yote haya na tunawapa watetezi shukrani kubwa kwa mchango wao.

Usalama na ulinzi ni masuala tata. Yana msingi katika maarifa ya kimuundo, lakini pia yanaathiriwa na mielekeo ya mtu binafsi na mienendo ya kiuendeshaji. Moja katika jumbe muhimu kwenye mwongozo huu ni kulipa suala la usalama muda,nafasi na nguvu inayohitajika, licha ya ajenda nyingi za kazi na msongo mzito wa akili na pia hofu walio nayo watetezi na mashirika yao. Hii ina maana ya kwenda zaidi ya ufahamu wa kibinafsi wa watu kuhusu usalama hadi kwenye mpangilio wa kitamaduni ambao suala la usalama ni la msingi.

Kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu hali ya mgogoro na kufahamu mantiki iliyopo ya kisiasa ni muhimu pia kwa kuudhibiti ipasavyo usalama wa mtetezi. Mwongozo huu umesheheni mbinu ya kijumla na pia utaratibu wa hatua kwa hatua wa kuandaa mpango (zao) wa usalama na kuudhibiti usalama wenyewe (mchakato). Unajumuisha mawazo fulani kuhusu dhana za kimsingi kama vile hatari, udhaifu na tishio, na mapendekezo machache ya namna ya kuimarisha na kujenga usalama wa watetezi katika harakati zao za kila siku. Tunatarajia kwamba mada zilizoshughulikiwa humu zitaruhusu mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na watetezi wa haki za binadamu kulipangia na hata kulimudu ongezeko la changamoto za usalama katika kazi ya haki za binadamu.

Haya yote yakishasemwa, jambo la kwanza tunalopenda lizingatiwe ni kwamba watetezi wanahatarisha maendeleo yao na hata maisha yao, na hili ni jambo lisilo la utani. Wakati mwingine, njia ya pekee ya kuokoa maisha ni kuingia mafichoni na kisha baadaye kutoroka. Tunataka kuweka wazi kwamba mikakati na mapendekezo yote katika mwongozo huu kwa vyovyote vile, siyo njia ya pekee ya kuwazia kuhusu masuala ya usalama kwa watetezi wa haki za binadamu. Mwongozo huu umeandikwa kwa nia nzuri japo kwa masikitiko makubwa hautoi hakikisho la mafanikio.

## Tuuimarishe mwongozo huu....

Hatari hubadilika. Mwongozo huu ni kazi inayoendelea na utahitaji kuendelezwa, kuimarishwa na kuboreshwa kadiri muda unavyoendelea. Maoni yako kama mtetezi kuhusu kipengele chochote cha mwongozo huu yatakuwa muhimu zaidi.

Tafadhali tuma maoni na mawazo yoyote hasa kwa kurejelea uzoefu wako wa kutumia mwongozo huu kazini pako. Kwa msaada wenu, tunaweza kuufanya mwongozo huu kuendelea kuwa chombo cha manufaa kwa watetezi wa haki za binadamu kote ulimwenguni.

**Tuandikie barua pepe:**

**pi@protectioninternational.org**

**Au tuma barua ya posta kwa PI:**

Protection International. Rue de la Linière, 11, 1060 Bruxelles (Belgium)

**Simu:** +32 (0)2 609 44 05, +32 (0)2 609 44 07

**Faksi:** +32 (0)2 609 44 06

**www.protectioninternational.org, www.protectionline.org**

## Utangulizi Mfupi Kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu

“Mtetezi wa haki za binadamu” ni neno linalotumiwa kufafanua watu ambao, akiwa yeye binafsi au pamoja na wengine, huchukua hatua ya kustawisha au kuzilinda haki za binadamu. Watetezi wa haki za binadamu wanatambuliwa pakubwa zaidi kutokana na yale wafanyayo, na hivyo basi neno hili (mtetezi wa haki za binadamu) linaweza kufafanuliwa vizuri zaidi kwa kuyabainisha matendo yao na baadhi ya maeneo wanayofanyia kazi.

Kazi ya watetezi wa haki za binadamu ni halali na imehalalishwa na mashirika ya kiraia ambayo watetezi hao wanayawakilisha.

Mamia ya watetezi wa haki za binadamu hukumbana na machafuko ya kisiasa kila siku ulimwenguni, kwa sababu ya kutetea haki za watu wengine. Hujitahidi kukomesha hali ya kutekeleza maovu bila kuadhibiwa na pia kuendeleleza haki na amani katika jamii,na katika harakati hiyo huhatarisha uzima wao wa kimwili na kiakili.

Katika mwaka wa 1988, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa liliidhinisha “Azimio la Haki na Uwajibikaji wa Watu binafsi, makundi na Mashirika ya Kiraia" katika kustawisha na kulinda haki za binadamu zinazotambuliwa ulimwenguni kote na pia Uhuru wa kimsingi. (Baadaye likaitwa “Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu’) hii ina maana kwamba, miaka hamsini baada ya Azimio la Kilimwengu la haki za binadamu, na baada ya miaka ishirini ya majadiliano kuhusu maamuzi ya muswada wa watetezi wa haki za binadamu, hatimaye Umoja wa mataifa ulitambua uhakika wa mambo kwamba maelfu ya watu walikuwa wanastawisha na kuchangia katika kuzilinda haki za binadamu katika ulimwengu mzima. Hili ni Azimio jumuishi linaloheshimu idadi na wingi wa watu wanaojihusisha katika uendelezaji na ulinzi wa haki za binadamu.

Kiasili, nafasi ya Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu ilibuniwa “kutafuta, kupokea, kutathmini na kutoa majibu kwa habari kuhusu hali na haki za mtu yeyote, akiwa pekee yake au miongoni mwa watu wengine, kustawisha na kuzilinda haki za binadamu na uhuru wa kimsingi”. Katika mwaka wa 2008 nafasi hiyo ilichukuliwa na ile ya Msemaji Maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu.

Miongozo ya Umoja wa Nchi za Ulaya – **EU** – kuhusu watetezi wa Haki za Binadamu haijafungamanisha tu Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu, bali pia imetoa mapendekezo mahsusi kwa Nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya – MS –

Watetezi wa Haki za Binadamu ni halali na wameidhinishwa na jumuiya za kitaifa na kimataifa. **PI** inakubaliana na ufafanuzi wa maana ya mtetezi wa haki za binadamu ambayo ilitolewa na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu na iliyotiliwa mkazo na Miongozo ya Umoja wa Nchi za Ulaya kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu:

> “**Mtetezi wa haki za binadamu**” *ni kauli inayotumika kueleza mtu ambaye, yeye binafsi au pamoja na wengine, anajitahidi kuendeleza na kuzilinda haki za binadamu. Watetezi wa Haki za*

*Binadamu wanatambulika pakubwa zaidi kwa yale wanayoyafanya na ni kupitia kwa kuyafafanua matendo yao na katika baadhi ya maeneo wafanyayo kazi,ndiposa kauli hii yaweza kupewa ufafanuzi bora zaidi."*[1]

(Tazama kwenye kiambatisho mwishoni mwa mwongozo huu kwa maelezo zaidi kuhusu Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu na kwa Miongozo ya Umoja wa Nchi za Ulaya kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu).

## Ni nani anayewajibika kuwalinda watetezi wa Haki za Binadamu?

Azimio la Watetezi wa Haki za Binadamu linasisitiza kwamba nchi ndiyo ya kwanza katika kuwalinda watetezi wa Haki za Binadamu. Linatambua pia "*kazi muhimu ya watu binafsi, makundi na miungano inayochangia katika kukomesha ukiukaji wa haki za binadamu na uhuru wa kimsingi*."

Lakini kulingana na Hina Jilani[2], Mwakilishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu, "ukiukaji wa haki za binadamu wa wazi na utafutaji wa suluhu yazo unategemea zaidi kiwango cha usalama walio nao watetezi wa haki za binadamu.[3]" Kutazama ripoti yoyote inayohusu watetezi wa haki za binadamu katika ulimwengu mzima kunaonyesha visa vingi vya mateso, utorokaji, mauaji, vitisho, unyang'anyi, uvamizi afisini, unyanyasaji, kuzuiwa kusiko kwa haki, kufanyiwa upelelezi na ujasusi na kadhalika. Kwa bahati mbaya, hii ndiyo sheria wala si kitu kinachoweza kuepukwa na watetezi.

## Usomaji wa ziada uliopendekezwa

### Kuyapata mengi kuhusu watetezi wa haki za binadamu, zuru:

- www.unhchr.ch/defender/about1.htm (The UN High Commissioner on Human Rights)
- www.protectionline.org (Protection International).
- The observatory of the Protection of Human Rights Defenders, ulioundwa na International Federation on Human Rights (FIDH; www.fidh.org) na World Organization Against Torture (OMC T; www.omct.org).
- Amnesty International: www.amnesty.org na http://web.amnesty.org/pages/hrd-index-eng
- www.ishr.ch, tazama chini "HRDO" (The HRD Office of the International Service for Human Rights in Geneva).
- www.frontlinedefenders.org (Front Line, The International Foundation for Human Rights Defenders).

1 Watetezi wa Haki za Binadamu: Kuhifadhi Haki ya Kuzitetea Haki za Binadamu. Fact Sheet No. 29 www.unhchr.ch

2 Margaret Sekaggya (Uganda) alichukua nafasi ya Hina Jilani, mwaka wa 2008, kama Ripota maalum kuhusu hali za watetezi wa haki za binadamu ambaye aliteuliwa na Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu.

3 Ripoti kuhusu watetezi wa Haki za Binadamu, 10 Septemba 2001 (A/56/341).

**Ili kujifunza mengi kuhusu hati rasmi za kisheria za kimataifa na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu, tembelea:**

- www.unhchr.ch: Hii ni wavuti ya Balozi Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu.
- www.protectionline.org (Protection International).
- www.ishr.ch/index.htm (International Service for Human Rights, Geneva), kwa mkusanyiko wa hati rasmi za kimataifa na kikanda za kuwalinda watetezi wa haki za binadamu.

# SEHEMU YA KWANZA

# MAKADIRIO YA HATARI, VITISHO NA ZANA NYINGINEZO

Katika sehemu ya kwanza ya Mwongozo huu, tunashughulikia dhana za kimsingi za usalama, baadhi ya zana halisi na mikabala ya usalama kwa hali mahsusi.

Yote hayo yatajumuishwa katika mpango wa usalama na katika kitabu cha mwongozo wa usalama cha shirika.

## YALIYOMO KATIKA SEHEMU YA KWANZA:


**1.1** Kufanya uamuzi bora kutokana na ufahamu wako wa usalama na ulinzi

**1.2** Kukadiria hatari

**1.3** Kuelewa na kutathmini vitisho

**1.4** Matukio ya usalama

**1.5** Kuzuia na kukabiliana na hatari

**1.6** Kuunda mkakati wa usalama wa kiulimwengu

**1.7** Kuandaa mpango wa usalama

**1.8** Kuimarisha usalama kazini na nyumbani

**1.9** Usalama katika maeneo ya vita vya kijeshi

**1.10** Usalama katika maeneo ya mapigano ya kijeshi

**1.11** Usalama katika teknolojia ya habari na mawasiliano

# Kufanya uamuzi bora kutokana na ufahamu wako wa usalama na ulinzi

**Lengo:**

Kutambua umuhimu wa kuyachunguza mazingira yako ya kazi kwa sababu za kiusalama.

Kujifunza mbinu mbalimbali za kuchunguza mazingira ya kazi na washika dau.

## Mazingira ya kazi ya Watetezi wa Haki za Binadamu

Watetezi wa haki za binadamu hufanya kazi katika mazingira tata, yaliyo na wahusika wengi tofauti na ambayo yanaathiriwa na ushawishi mkubwa wa kisiasa katika harakati za kufanya maamuzi. Matukio mengi aghalabu hutendeka wakati mmoja, huku kila tukio likiathiri jingine. Uwezo wa kila mhusika au mshikadau katika hali hii huwa na nafasi muhimu katika mahusiano yake na watu wengine. Kwa hivyo watetezi wa haki za binadamu wanahitaji habari si tu inayohusiana moja kwa moja na kazi yao, bali pia kuhusu nafasi za wahusika wakuu na washika dau.

Zoezi la kwanza sahili litakuwa kuandaa kundi litakalochangia mawazo ya kujaribu kutambua na kuorodhesha washika dau wote wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ambao wanaweza kuwa na ushawishi kuhusu hali yako ya sasa ya usalama.

## Kuyachunguza mazingira yako ya kazi

Ni muhimu sana kujua na kufahamu vyema iwezekanavyo kuhusu mazingira unamofanyia kazi. Uchunguzi mzuri wa mazingira hayo unamfanya mtu atoe uamuzi bora ambao utapelekea kutumika kwa kanuni na taratibu za usalama. Ni muhimu pia kuwazia kuhusu matukio yanayoweza kutokea baadaye, ili, panapowezekana, hatua ya kuyazuia ichukuliwe.

Hata hivyo, kuyachunguza tu mazingira yako ya kazi hakutoshi. Unapaswa pia kuchunguza namna hatua zote za kulinda usalama zilizochukuliwa zinaweza kuathiri hali hiyo na pia jinsi kila mshika dau anaweza kuhisi. Ni bora pia kuzingatia kuongeza nafasi ya kufanyia kazi. Unaweza kufanya uchunguzi katika kiwango kikubwa kwa kuitafiti nchi au eneo, lakini pia unapaswa kujua jinsi mbinu hizo za utafiti mpana hufanya kazi katika **eneo maalum** unamofanyia

kazi, yaani utafiti mdogo. Kwa mfano, matukio ya kijeshi yanaweza kutendeka katika sehemu fulani kwa njia tofauti kinyume na jinsi ulivyotarajia, kutokana na uchunguzi wa kieneo au kitaifa. Unafaa kuwa na ufahamu wa sifa kama hizo za kikanda. Ni muhimu pia kuepuka kuwa na mtazamo finyu kuhusu hali fulani ya kazi, kwa sababu mambo hukua na kubadilika. Kwa hivyo yanapaswa kurejelewa kila wakati.

**Kuuliza Maswali**, **Uchunguzi wa harakati za nyanjani**, na **Uchunguzi wa Mshikadau** ni mbinu tatu muhimu za kufanya uchunguzi wa maeneo yako ya kazi.

## Kuuliza Maswali

Unaweza kuyaelewa vizuri maeneo yako ya kazi kwa kuuliza maswali yanayofaa kuyahusu. Hii ni njia bora ya kuibua mijadala kwenye kikundi kidogo, lakini hili linawezekana tu iwapo maswali yametungwa kwa njia ambayo itapelekea kupatikana haraka kwa suluhu.

Tuchukue mfano, unyanyasaji unaotekelezwa na utawala wa halmashauri umekuwa tatizo. Ikiwa mtatunga swali kwa mfano: "Ni kitu gani kifanywe ili kupunguza unyanyasaji?" mtajipata wenyewe mkitafuta suluhisho ya dalili, yaani dalili ya unyanyasaji.

Lakini ukilitunga swali litakalochochea kupatikana kwa suluhisho, basi utakuwa unaelekea pafaapo katika kupata suluhu yenyewe. Mathalani, ukiuliza, "Je, hali yetu ya kisiasa na kijamii ni salama kikamilifu katika kufanya kazi kwetu?" hapa majibu ni mawili tu ama ndiyo au la.

Ikiwa jibu ni ndiyo, basi utapaswa kutunga swali jingine litakalokusudia kutambua na kuelewa vizuri zaidi masuala muhimu ya kidharura ili kuulinda usalama wako. Iwapo, baada ya kuzingatia shughuli zote zilizopo, mipango, rasilimali, na pia utungaji sheria, majadiliano ya miafaka, ulinganishi na watetezi wengine waliopo, n.k., jibu linapaswa kuwa 'La' na katika hali kama hii, suluhu ya tatizo lako la usalama itakuwa imepatikana.

### Kutumia mbinu ya kuuliza maswali:

- Yatafute maswali yatakayokusaidia kuyaibua na kuyafahamu vyema masuala muhimu ya kidharura ya kuulinda usalama wako;
- Yatunge maswali yenye jinsi ya kuleta suluhu;
- Urudie mchakato huu mara nyingi iwezekanavyo (kama mjadala).

### Baadhi ya Maswali muhimu ya kuuliza:

- Ni masuala yepi nyeti yaliyo ya dharura katika mahusiko ya kisiasa na kijamii?
- Ni washika dau wepi wakuu kuhusiana na masuala haya muhimu?
- Kazi yetu inaweza vipi kuathiri haja za washika dau hawa wakuu kwa njia chanya au hasi?


- Tunaweza kudhihirisha hisia zetu vipi iwapo tutalengwa na yeyote katika washika dau hawa kutokana na kazi yetu?
- Je, mazingira yetu ya kisiasa na kijamii ni salama kikamilifu katika kufanya kazi kwetu?
- Je, utawala wa halmashauri/wa kitaifa umetoa hisia gani kutokana na kazi ya hapo awali au sawa na hiyo ya watetezi wa haki inayohusiana na masuala haya?
- Je, washika dau muhimu wametoa hisia gani kutokana na kazi ya hapo awali au sawa na hiyo ya watetezi wa haki za binadamu?
- Na kadhalika.

## Uchunguzi wa Harakati za Nyanjani

Uchunguzi wa harakati za nyanjani ni mbinu inayoweza kusaidia kutambua jinsi harakati mbalimbali zinavyochangia au zinavyozuia kuyatimiza malengo yako. Uchunguzi huo hudhihirisha harakati za kukusaidia na kulemaza, na hujikita katika chukulizi kwamba matatizo ya usalama yanaweza kuibuka kutokana na harakati za kuzuia, na kwamba unaweza kuzipatiliza juhudi za kusaidia. Mbinu hii inaweza kukamilishwa na mtu mmoja tu, lakini ina natija kubwa iwapo itatumika kwa kundi pana la watu walio na malengo pevu ya kazi na njia ya kuyatekeleza.

Anza kwa kuchora mshale wa mlalo unaoashiria kwenye kisanduku (unataka kutimiza lengo lako). Andika muhtasari mfupi wa lengo lako la kazi. Hii itakupa mwelekeo wa kutambua harakati zinazochangia na zile zinazozuia. Chora kisanduku kingine juu ya mshale ulio katikati. Ziorodheshe juhudi zote iwekanavyo kwamba huenda ndizo zinazokuzuia kulitimiza lengo lako hapa. Chora kisanduku kama hicho, kilichosheheni harakati zote zinazoweza kuchangia kutimiza lengo chini ya mshale. Chora kisanduku cha mwisho cha harakati ambacho kiashirio chake hakijulikani au hakuna uhakika wacho.


**Chati 1**: Uchunguzi wa juhudi za nyanjani wa kutathmini mazingira ya kazi




Baada ya kukamilisha chati yako, ni wakati sasa wa kutathmini matokeo. Uchunguzi wa harakati za nyanjani unakusaidia katika kuwazia kuhusu harakati unazokabiliana nazo.Lengo ni kutafuta mbinu za kupunguza au kuondoa hatari inayotokana na harakati za kuzuia, kwa hali fulani kupitia kwa usaidizi wa harakati changizi. Ama kuhusu harakati zisizo na mwelekeo maalum, utahitaji kuamua ikiwa utazichukulia kama zinazochangia au utaendelea kuzifuatilia ili hatimaye uweze kutambua dalili yazo kama ni za kuzuia au kuchangia.

**Kwa mfano:**

*Jichukulie kwamba unafanya kazi na shirika linalozishughulikia haki za kutumia rasilimali za asili za wenyeji fulani kwenye ardhi yao wenyewe. Ipo migogoro inayoendelea kati ya washika dau kadhaa kuhusu utumiaji wa mali asili hizo.Sasa ungependa kuitekeleza kazi yako katika eneo jirani lililo na matatizo kama haya.*




## Uchunguzi wa Wahusika (au washika dau)

Uchunguzi wa wahusika (au washikadau) ni njia muhimu ya kuongeza ufahamu ulio nao katika kufanya uamuzi kuhusu ulinzi. Unahusu kuwatambua na kuwafafanua washikadau mbalimbali wanaohusika, pamoja na uhusiano wao, kwa misingi ya sifa na haja zao – yote hayo, ni kuhusu suala la kupewa ulinzi

**Mshika dau katika ulinzi ni mtu yeyote,**
**kundi au taasisi iliyo na haja na,**
**au inayojihusisha katika sera ya**
**matokeo kwenye maeneo ya ulinzi.**[1].

Washika dau katika ulinzi wanaweza wakawekwa katika jinsi zifuatazo**:**

**Washika dau wa kimsingi**. **Katika muktadha wa ulinzi, hawa ndio watetezi wenyewe, na wale wanaofanya kazi nao au wanaowafanyia kazi**, kwa sababu wote wana nafasi ya kimsingi katika ulinzi wao.

1 Imetolewa kutoka Sustainable Livelihoods Guidance Sheets No. 514 (2000).

**Washika dau wenye majukumu, ambao wanawajibika katika kuwalinda watetezi yaani**:

- Taasisi za kiserikali na nchi (ikiwemo vikosi vya usalama, majaji, watungaji sheria n.k.)
- Mashirika ya kimataifa yaliyo ya mamlaka kama vile vya ulinzi, mashirika kama hayo ni Umoja wa Mataifa, vikosi vya kulinda usalama n.k.
- Katika hali ya washika dau pinzani waliojihami, wanaweza wakawajibika kwa kutowahujumu watetezi (kwa vile wao ni raia), hususan washika dau hawa wanapoyadhibiti maeneo.

**Washika dau wakuu, walio na uwezo na ushawishi mkubwa wa kuwalinda watetezi**:

Wanaweza wakawa na nguvu ya kisiasa au uwezo wa kuwashinikiza washika dau walio na majukumu na wasiyoyatimiza (kama serikali nyinginezo, mashirika ya Umoja wa Mataifa), na katika hali hiyo hiyo, aghalabu baadhi yao wanaweza kuhusika kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja katika kuwahujumu na kuwashinikiza watetezi (kama mashirika ya kibinafsi, vyombo vya habari au serikali nyinginezo). Inategemea ni katika muktadha upi, haja na mikakati ya kila mojawapo ya washika dau hawa. Orodha isiyokamilika yao ni kama vile:

- Mashirika ya Umoja wa Mataifa (isipokuwa yale yaliyokabidhiwa mamlaka);
- Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (ICRC);
- Serikali nyingine na taasisi za nchi mbalimbali (kama wafadhili na pia kama waundaji sera);
- Washika dau wengineo waliojihami;
- Mashirika yasiyo ya serikali (ama ya kitaifa au kimataifa);
- Makanisa na taasisi nyingine za kidini;
- Mashirika ya kibinafsi; na
- Vyombo vya habari.

Ugumu mkuu katika uundaji wa mikakati na hatua zipi zinazotekelezwa na washika dau ni kwamba mahusiano baina yao si ya wazi, au hata yanaweza kutokuwepo kabisa. Washika dau wengi walio na wajibu, hasa serikali, vikosi vya usalama na vikosi pinzani vilivyojihami, husababisha au huchangia ukiukaji wa haki za binadamu na pia kutojali kuwalinda watetezi. Baadhi ya washika dau ambao wangekuwa na ari sawa ya kuwalinda watetezi hawa, wanaweza wakawa na maslahi yao shindani. Nao ni kama vile serikali nyinginezo, mashirika ya Umoja wa Mataifa na mashirika yasiyo ya kiserikali. Masuala haya, pamoja na yale ya kiasili katika hali za kimgogoro, yanadhihirisha hali tata katika mazingira ya kazini kwa ujumla.

## UCHUNGUZI WA WASHIKADAU, MIUNDO NA MICHAKATO INAYOBADILIKA

**Washika dau** sio wahusika **wasiobadilika.** Wanahusiana wao kwa wao katika nyanja mbalimbali na katika hali hiyo hujenga mtandao mpana wa mahusiano. Ni muhimu kuwa makini katika mahusiano yanayoelekeza na kubadilisha mahitaji ya usalama wa watu.

**Miundo** ni sehemu zinazohusiana katika sekta ya umma, asasi za kiraia au mashirika ya kibinafsi. Tutaichunguza kwa mtazamo wa kiulinzi. Katika sekta ya umma, twaweza kuiangalia serikali kama ama mkusanyiko wa washika dau walio na mshikamano mmoja wa kikazi, au wale wenye mikakati ya makabiliano ya ndani kwa ndani. Kwa mfano, tunazipata tofauti kubwa baina ya Wizara ya Ulinzi na Wizara ya Mambo ya Nchi za Kigeni tunapozijadili sera zinazohusiana na watetezi wa haki za binadamu, au baina ya afisi ya Mchunguzi Maalum wa Malalamishi ya wananchi na jeshi. Miundo inaweza kuwa na visehemu vilivyochanganyika kama vile,tume ya sekta mbalimbali (wanachama kutoka serikalini, makundi ya kidiplomasia) inaweza kuundwa ili kufuatilia hali ya ulinzi ya shirika fulani la watetezi wa haki za binadamu.

**Michakato:** Ni mkondo wa maamuzi na hatua zinazochukuliwa na moja au zaidi ya mashirika mbalimbali kwa lengo la kuimarisha hali ya usalama ya kundi fulani. Inaweza kuwa michakato ya utungaji sheria, michakato ya kitamaduni na pia michakato ya uundaji sera. Siyo michakato yote hufanikiwa katika kutimiza malengo ya kuimarisha ulinzi. Kati hali nyingi, michakato ya ulinzi hupingana au hujijengea udhaifu fulani baina yayo. Kwa mfano, watu wanaokisiwa kwamba wanapewa ulinzi hawawezi kukubali mchakato wa sera ya ulinzi unaopigiwa debe na serikali, kwa sababu wanauona kama ulio na lengo dhahiri la kuwahamisha watu kutoka eneo fulani.Umoja wa Mataifa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanaweza kutoa usaidizi kwa watu katika hali kama hii.

Ni muhimu kwa mchunguzi wa washika dau kuelewa:

- Mshika dau ni nani? Na ni katika hali gani ambayo "udau" wao unafaa;
- Mahusiano baina ya washika dau katika ulinzi, sifa na haja zao;
- Jinsi haya yote yatakavyoathiriwa na harakati za ulinzi;
- Kupendelea kwa kila mshika dau kushiriki katika harakati hizo za ulinzi.

Kuna njia kadhaa za kufanya uchambuzi wa washika dau. Ifuatayo hutumia mbinu ya moja kwa moja, ambayo ni muhimu katika kuleta matokeo mazuri. Katika kutathmini hali za usalama, ni muhimu kuzitazama kwa muda wa kutosha na daima kuzingatia maslahi na malengo ya washika dau wote wanaoshiriki.

**Uchunguzi wa ushika dau katika hatua nne:**

1. Tambua suala pana la usalama (yaani, hali ya usalama ya watetezi wa haki za binadamu katika eneo fulani nchini).
2. Je, washikadau ni akina nani? (kwa kuorodhesha,ni taasisi,makundi na watu binafsi wepi walio na jukumu au haja ya kutoa ulinzi?) Tambua na uorodheshe washikadau wote wanaofaa kwa hilo suala la ulinzi, kupitia kwa mijadala na kuchangizana mawazo
3. Chunguza mienendo na sifa mahsusi za washikadau, kama vile majukumu katika ulinzi, uwezo wa kushawishi hali ya ulinzi, malengo, mikakati, uhalali na maslahi (ikiwemo nia ya kuchangia katika ulinzi).
4. Kuchunguza na kuyachambua mahusiano baina ya washika dau.

Baada ya kufanya uchunguzi huu, labda utapenda kutumia matriki kama ifuatayo:

Andaa orodha ya washika dau wote wafaao kwa suala zima la ulinzi katika kalibu (tazama chati 1.2): Rudia orodha hiyo ya washika dau katika safu ya kwanza kwenye mstari wa kwanza. Kisha:

- Zichambue sifa za kila mshika dau (malengo na maslahi, mikakati, uhalali na mamlaka), jaza visanduku katika mstari mshazari mahali ambapo kila mshika dau anajigawa nao (mstari):

**Kwa mfano:**

*Yaweke malengo, maslahi na mikakati ya makundi pinzani yaliyojihami kwenye kisanduku "A".*

- Yachambue mahusiano baina ya washika dau, vijaze visanduku vinavyoyaelezea mahusiano muhimu kulihusu suala la usalama. Kwa mfano, kile kisanduku kinachojigawa baina ya jeshi na Balozi Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa Wakimbizi, katika kisanduku "B" na kadhalika.

Baada ya kujaza vile visanduku vifaavyo, utakuwa na wazo la malengo, mikakati na mwingiliano miongoni mwa washika dau wakuu kuhusiana na suala fulani la usalama.

## **Chati ya 2**: Mfumo wa kimatriki kwa uchambuzi wa ushika dau

| | Serikali | Jeshi | Polisi | Kundi pinzani lililoji-hami | Mashirika yasiyo ya kiserikali ya haki za kitaifa za binadamu | Makanisa | Serikali nying-inezo | Maajenti wa Umoja wa Mataifa | Shirika la kimataifa lisilo la kiserikali |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Serikali | Mshika dau | | | | | | | | |
| Jeshi | | Mshika dau | | | | | | B | |
| Polisi | | | Mshika dau | | | | | | |
| Makundi pinzani yaliyojihami | | | | A | | | | | |
| Mashirika yasiyo ya kiserikali ya haki za kitaifa za binadamu | | | | | Mshika dau | | | | |
| Makanisa | | | | | | Mshika dau | | | |
| Serikali nyinginezo | | | | | | | Mshika dau | | |
| Maajenti wa Umoja wa Mataifa | | | | | | | | Mshika dau | |
| Shirika la kimataifa lisilo la kiserikali | | | | | | | | | Mshika dau |

Kisanduku "**A**":

**Kwa kila mshika dau:**

- Malengo na maslahi
- Mikakati
- Uhalali
- Mamlaka

Kisanduku "**B**":

**Uhusiano baina ya washika dau:**

Uhusiano baina yao kulihusu suala la usalama na kuhusu mikakati ya washika dau wote

## Muhtasari

- Watetezi wote wa haki za binadamu wanakabiliwa na hatari.
- Siyo watetezi wote wa haki za binadamu wanalingana katika kukabiliana na hatari zao.
- Hatari zinategemea hali ya kisiasa.
- Hali ya kisiasa hubadilika, haisalii hivyo daima.
- Hivyo basi, hatari nayo hubadilika.

Hii ni nadharia tunayoijengea umuhimu wa kutafuta habari kuu kwa mbinu ya kuuliza maswali mwafaka.

Kisha, wapange na uwachambue washika dau pamoja na wasaidizi wao katika vitabaka vyao vingi.

Fanya uchunguzi wa jinsi wanavyotagusana kuhusu masuala ya usalama na namna masuala hayo yanavyohusisha masuala ya mikakati yao.

Yatafute mapendeleo yao yanayofanana na yasiyofanana, miungano, mbinu a kiutendaji n.k.

Ichunguze misingi ya miundo na michakato.

Utaweza kutambua harakati mbalimbali (za kupinga, zinazoafiki na zile zisizo na mwelekeo maalum).

Inaweza kuwa vigumu kuzipitia hatua hizi kwa mara ya kwanza. Japo itakuwa sahali sana iwapo unaongeza mambo mapya katika uchunguzi wako.

Hii itakusaidia kufanya uamuzi mwafaka kuhusu usalama na ulinzi.

# Kutathmini hatari: vitisho, udhaifu na uwezo

**Lengo:**

Kuzielewa dhana za vitisho, udhaifu na uwezo katika usalama.

Kujifunza jinsi ya kutathmini hatari.

## Uchambuzi wa Hatari na Mahitaji ya Ulinzi

Kazi ya watetezi wa haki za binadamu inaweza kuwa na athari hasi kwa maslahi ya wahusika mahsusi, na hii inaweza kuwahatarisha watetezi baadaye. Kwa hivyo ni muhimu kusisitiza kwamba kukabiliwa na **hatari ni sehemu ya msingi ya maisha ya watetezi katika nchi fulani.**

Suala la kukabiliwa na hatari linaweza kuainishwa zaidi katika njia ifuatayo:

> Yachambue maslahi na mikakati mikuu ya mshika dau ⇨ tathmini athari ya kazi ya watetezi kuhusu maslahi na mikakati hiyo ⇨ tathmini vitisho dhidi ya watetezi ⇨ tathmini udhaifu na uwezo wa watetezi ⇨ tambua hatari.

Yaani, kazi unayofanya kama mtetezi inaweza kuzidisha hatari unayokabiliana nayo.

- **Yale** uyafanyayo yanaweza kuchangia kwa vitisho
- **Vipi**, **wapi** na **lini** unafanya kazi huibua mambo mengi kuhusu udhaifu na uwezo wako.

Hakuna ufafanuzi maalum wa hatari, lakini twaweza kusema kwamba hatari ni matukio yanayoweza kutokea, japo haijulikani lini yatatokea, na ambayo huleta madhara.

Katika hali yoyote ile, yeyote anayeshughulikia haki za binadamu anaweza kukumbana na kiwango cha kawaida cha hatari, lakini si kila mmoja anaweza kudhuriwa na hali hiyo kutokana na kuwa mahali pamoja tu. Uwezekano wa mtetezi au kundi la watetezi kudhuriwa au kuhujumiwa kunatofautiana kutokana na masiala kadhaa, kama tutakavyoona.

**Mfano**:

> *Panaweza kuwepo na nchi ambayo serikali inatoa tishio la kijumla dhidi ya kazi zote zinazohusiana na utetezi wa haki za binadamu. Hii ina maana kwamba watetezi wote wanaweza kukabiliwa na hatari. Lakini tunajua pia kwamba watetezi wengine wanakabiliwa zaidi na hatari kuliko wengine. Kwa mfano shirika kubwa lisilo la kiserikali lenye msingi mzuri na lililo na makao yake jijini halitakuwa na uwezekano mkubwa wa kudhuriwa kama vile shirika jingine lisilo la kiserikali ambalo ni dogo. Tunaweza kukadiria kwamba hili ni jambo la kawaida, lakini pia inaweza kushangaza tunapofanya uchunguzi wa sababu zinazopelekea kuwepo kwa hali kama hii, ili tuwe na ufahamu bora na hata kuyashughulikia matatizo yanayowakabili watetezi.*

Kiwango cha hatari kinacholikabili kundi la watetezi huongezeka kulingana na vitisho wanavyovipokea, uwezekano wao wa kudhuriwa na uwezo wao wa kukabiliana na vitisho hivyo, kama inavyoonyeshwa kwenye mchoro huu[1]:

$$\textbf{HATARI} = \frac{\textbf{VITISHO} \times \textbf{UWEZEKANO WA KUDHURIWA}}{\textbf{UWEZO}}$$

**Vitisho**: Ni uwezekano kwamba mtu atamdhuru mtu mwingine kimwili, au kimaadili ama kimali kupitia kwa fujo za kimakusudi, na za kila mara[2]. Tathmini ya hatari huchunguza uwezekano wa kutendeka kwa matishio.

Watetezi wanaweza kukumbana na matishio mbalimbali katika hali ya mgogoro, ikiwemo kuwalenga wao binafsi, uhalifu wa kawaida dhidi yao na matishio yasiyo ya moja kwa moja.

Aina ya tishio la kawaida – kuwalenga – linakusudia kuizuia au kuibadilisha kazi ya kundi, au kuuathiri mwenendo wa watu wanaohusika. Mbinu ya kuwalenga aghalabu huwa na uhusiano wa karibu na kazi inayofanywa na watetezi husika, na pia maslahi na mahitaji ya watu wanaoipinga kazi ya watetezi.

Kwa uchache, **vitisho vya kimatukio** hutokana na:

- Kuwa katika **maeneo ya vita kwenye mapigano ya kijeshi** ('kuwa mahala pasipofaa, wakati usiofaa').
- **Mashambulizi ya kawaida ya uhalifu**, hasa ikiwa kazi ya watetezi itawapeleka katika maeneo ya hatari. Hali nyingi za ulengaji zinatekelezwa 'kwa kisababu' kwamba ni matendo ya kawaida ya uhalifu.

Ulengaji (vitisho vilivyolengwa) pia unaweza kutazamwa kwa njiaya kujalizana. Watetezi wa Haki za Binadamu wanaweza kukumbana na vitisho vya moja kwa moja (vilivyoko

### Muhtasari wa aina za vitisho

- Ulengwaji (vitisho vya wazi/vilivyobainishwa), vitisho visivyo vya wazi: yale yanayotokana na kazi yako.
- Matishio ya hujuma za kawaida za uhalifu.
- Vitisho vya kimatukio: yale yanayotokana na mapigano ya kijeshi.

1 Imetolewa kutoka kwa Van Brant(2000) na REDR.
2 Dworken (1999).

wazi), kwa mfano kupata tishio la mauaji (tazama sura ya 1.3, kwa namna ya kutathmini vitisho vilivyotangazwa). Pia kuna hali za vitisho visivyo vya moja kwa moja, pale mtetezi aliye karibu nawe kikazi anapotishiwa kisha pasiwe na sababu za kuamini kwamba ni wewe unayefuatia katika kukumbana na vitisho hivyo.

## Udhaifu

Hali hii hurejelea kiwango ambacho watu wanaweza kupata hasara, madhara, mateso na kifo, pale shambulizi linapotokea. Hali hii hutofautiana kutoka mtetezi au kundi moja hadi jingine, na hubadilika kadiri muda unavyoenda. Udhaifu daima haujikiti katika hali mahsusi kwa kuwa watu wote na hata makundi wanaweza kwa kiwango fulani kupata madhara. Hata hivyo, kila mmoja ana kiwango na aina yake ya kuweza kudhuriwa, kulingana na hali zao. Hebu tutazame baadhi ya mifano:

- Udhaifu unaweza kuhusu mahali:aghalabu mtetezi anaweza kudhuriwa zaidi iwapo yuko nyanjani kuliko jinsi atakavyokuwa katika afisi iliyo mahali pa wazi ambapo shambulizi lolote likitokea linaweza kushuhudiwa.
- Udhaifu unaweza kutokana na ukosefu wa simu katika harakati ya usafirishaji ulio salama au kufanya vifuli vya mlango wa nyumba viwe thabiti. Lakini udhaifu huo unahusiana pia na ukosefu wa miungano ya watetezi na miitikio ya pamoja miongoni mwao.
- Udhaifu unaweza pia kutokana na kazi za makikundi na pia kuwa na hofu: mtetezi anayepokea vitisho anaweza kuwa na hofu, na hapo kazi yake itaathirika bila shaka. Iwapo hana mbinu mwafaka ya kukabiliana na hofu (mtu wa kuzungumza naye, au kundi zuri la wafanyikazi wenza, nk) kuna uwezekano kwamba atajipata katika makosa au afanye uamuzi usio mwafaka utakaompelekea kuwa na matatizo mengi ya usalama.

(Ipo orodha sawia udhaifu pamoja na uwezo mwishoni mwa sura hii).

## Uwezo

Hii ni nguvu na rasilimali ambazo mtetezi au kundi la watetezi linaweza kuwa nazo ili kufikia kiwango fulani cha usalama. Mifano ya uwezo inaweza kuwa mafunzo katika masuala ya usalama au sheria, watu wanaofanya kazi pamoja katika kundi, kuweza kumiliki simu na usafirishaji ulio wa salama, kuwa na miungano mizuri ya watetezi, kuwa na mikakati bora ya kukabiliana na hofu na kadhalika.

**Aghalabu, hali za udhaifu na uwezo hufanana.**

**Kwa mfano:**

*Kutojua vya kutosha kuhusu mazingira yako ya kazi ni hali ya uwezekano wa kupata madhara, ilhali kuwa na ufahamu juu ya mazingira hayo ni uwezo. Ni sawa tu na kuwa au kutokuwa na uwezo wa kupata usafirishaji ulio wa salama au kuwa na miungano ya watetezi iliyo mizuri.*

**Hata hivyo, aghalabu hali hii hutegemea mienendo ya watetezi**

**Kwa mfano:**


*Kuwa na simu kunaweza kuwa kwa madhara au uwezo,kutegemea na namna itakavyotumika. Ikiwa ujumbe wa siri utapokezwa kwa sauti ya juu, basi hayo ni madhara. Ikiwa utapokezwa kwa uaminifu na habari ya siri kufichwa basi huo ni uwezo.*

(Kuna orodha sawia ya udhaifu na uwezo mwishoni mwa sura hii).

## Kwa muhtasari

Ili kupunguza hatari hadi viwango vinavyokubalika;kama vile ulinzi- ni lazima:

- Upunguze vitisho
- Uyapunguze masiala ya madhara
- Uongeze uwezo wa ulinzi.




**Hatari** ni dhana inayobadilika na wakati pamoja na mabadiliko ya aina za vitisho, udhaifu na uwezo. Hii ina maana kwamba hatari hizi zinafaa kufanyiwa tathmini kila baada ya kipindi fulani, hasa iwapo mazingira yako ya kazi, matishio au udhaifu hubadilika. Kwa mfano, udhaifu unaweza kuongezeka ikiwa badiliko la uongozi litaacha kundi la watetezi katika hali dhaifu kuliko hapo mwanzo. Hatari huongezeka mno kutokana na tishio liliopo na lililo la wazi. Katika hali

hiyo, si salama kujaribu kupunguza hatari kwa kuzidisha uwezo kwa kuwa hilo huchukua muda.

Hatua za kuleta usalama, kama vile mafunzo ya kisheria au vizuizi vya ulinzi huweza kupunguza hatari kwa kuyapunguza masiala yanayohusu uwezekano wa kupata madhara. Hata hivyo, hatua kama hizo hazikubaliani na chanzo kikuu cha hatari, yaani vitisho au nia ya kuvitekeleza, hususan katika hali ambazo wahalifu wanajua kwamba hawataadhibiwa kamwe. Hivyo basi, hatua zote kuu za ulinzi zinapaswa kupunguza vitisho, juu ya kupunguza hali za udhaifu na pia kuimarisha uwezo.

**Mfano:**

*Kundi dogo la watetezi linayashughulikia masuala ya ardhi katika mji fulani. Watakapoanza kuyaingilia maslahi ya wamiliki wa ardhi wa sehemu hiyo, basi watapata tishio la moja kwa moja la mauaji. Ukilihusisha jedwali la kukabiliwa na hatari katika utendaji wa hali yao ya usalama, utapata kwamba hatari wanayokabiliwa nayo hawa watetezi ni ya kiwango cha juu, zaidi ya yote ni kutokana na vitisho vya mauaji. Iwapo ungependa kupunguza hatari hiyo, basi huu sio wakati mwafaka wa kuanza kubadilisha vifuli vya mlango wa afisi yao (kwa kuwa hatari hiyo haihusisiani na uhalifu katika afisi), au pia si wakati wa kumnunulia kila mtetezi simu ya mkononi, (hata kama mawasiliano yanaweza kuwa muhimu kwa usalama, haitafaa chochote wakati unaandamwa na mtu ili akuue). Katika hali kama hii, mkakati ufaao utakuwa wa kuunda miungano na kujenga hisia za kisiasa zitakazotumiwa kukabiliana moja kwa moja na tishio hilo (na kama njia hii haitafanya kazi barabara kwa haraka, njia ya pekee iliyo bora ya kupunguza hatari yaweza kuwaweka watetezi katika hali isiyo dhahiri, labda kwa kuwapeleka mbali kidogo kwa muda.Ile hali ya kuhamia katika eneo jingine la usalama pia ni uwezo). Kuunda na kutekeleza jukumu kama hilo pia kunahusisha uwezo wa kijamii nafsia kwa mtetezi ili kuona kwamba hali ya kujitenga kwake haifanani na woga au kushindwa…. Hali ya kujitenga kunaweza kumfanya mtu aweze kujitathmini na kurejelea upya kazi yake baada ya kujiandaa.*

Udhaifu pamoja na uwezo,na baadhi ya matishio, vinaweza kutofautiana kulingana na umri na jinsia. Unapaswa hivyo basi kuyaainisha matokeo yako ipasavyo.

## Kutathmini Udhaifu pamoja na Uwezo

Kuandaa tathmini ya uwezekano wa kudhuriwa pamoja na uwezo kwa kundi fulani (au mtu) kunahusu kwanza, utolewe ufafanuzi wa kundi lenyewe, (laweza kuwa jumuiya, mkusanyiko, shirika lisilo la kiserikali, watu binafsi) kisha mahali palipo kundi hilo na kipimo cha wakati (sifa zinazohusu uwezekano wako wa kudhuriwa zitabadilika kadiri muda unavyosonga). Kisha unaweza kuendelea na utathmini wa uwezekano huo wa kudhuriwa pamoja na uwezo, ukitumia **chati 1.3** mwishoni mwa sura hii kama mwongozo.

**Tanbihi:** Utathmini wa udhaifu na uwezo lazima uonekane kama shughuli isiyo na kikomo inayolenga kuendeleza habari juu ya ile iliyopo ili kudumisha taswira ya hali inayobadilika kila wakati. Katika utathmini huo, ni muhimu kwanza kuandaa orodha ya sasa,na ni baada tu ya hapo, ambapo utaorodhesha udhaifu na uwezo unaopendelewa. Baadaye, utapaswa kuanza shughuli ya kuutimiza.

## Chati ya 3: Habari inayohitajika katika kutathmini pamoja na uwezo.

"Kumbusho: Kwa jumla, habari iliyoko katika safu ya kulia inaonyesha uwezekano wa kudhuriwa au uwezo wa kila kijenzi"

| Udhaifu na uwezo | Habari inayohitajika kutathmini udhaifu na uwezo wa watetezi kuhusiana na vijenzi hivyo |
|---|---|
| **Vijenzi vinavyohusiana na sifa za kijiografia, za kimaumbile na za kiufundi** | |
| Uwekaji wazi | Haja ya kuwa katika, au kupitia sehemu za hatari katika kutekeleza shughuli za kila siku au za wakati fulani washika dau wenye vitisho wakiwa katika sehemu hizo. |
| Majengo ya nje | Sifa za maeneo ya makao (afisi, manyumbani, makazi) vifaa vya ujenzi, milango, madirisha, kabati. Vizuizi vya usalama. Taa za usiku. |
| Afisi na maeneo ya umma | Je, afisi zako ziko wazi kwa wageni kutoka nje? Je, kuna maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya watumishi pekee? Je unahitajika kushughulikia watu usiowajua wanaokuja katika makazi yako? |
| Maeneo ya kujificha, njia za kutorokea | Kuna maeneo yoyote ya kujificha? Maeneo hayo yanaweza kufikiwa vipi (umbali wake) na kwa nini (kwa watu binafsi au kundi lote)? Je, unaweza kujitenga na mahali hapo kwa muda ikiwezekana? |
| Kupafikia mahali penyewe | Je, ni ugumu gani uliopo kwa washika dau wa nje (watumishi rasmi wa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, nk) kufikia, kwa mfano, katika maeneo jirani hatari? Kuna ugumu gani kwa wahusika wenye vitisho kupafikia mahali hapo? |
| Usafiri na hifadhi | Je, watetezi wanapata usafiri ulio salama (usafiri wa umma au wa kibinafsi)? Je, aina hizi ya usafiri zina manufaa au madhara mahsusi? Je, watetezi wanapata hifadhi salama wanaposafiri? |
| Mawasiliano | Je, mifumo ya mawasiliano ya simu na redio ipo? Je, watetezi wanaweza kuzipata kwa urahisi? Je,vyombo hivi vinafanya kazi barabara kila wakati? Vinaweza vikasimamishwa na wahusika wanaotoa vitisho kabla ya shambulizi? |
| **Vijenzi vinavyohusiana na pingamizi** | |
| Mahusiano na makundi pingamizi | Je, watetezi wana mahusiano na makundi pingamizi (jamaa, kutoka sehemu moja, maslahi yanayofanana?) ambayo yanaweza kutumika kwa njia isiyo sawa dhidi ya watetezi? |
| Shughuli za watetezi zinazoathiri kundi pingamizi | Je, kazi ya watetezi inayaathiri moja kwa moja maslahi ya washika dau? (kwa mfano, wanapolinda mali asili muhimu, haki ya kuwa na ardhi, au malengo kama hayo kwa washika dau wenye mamlaka) Je, watetezi wanashughulikia suala nyeti kabisa la wahusika walio mamlakani? (kama vile, umiliki wa ardhi) |
| Usafirishaji wa vitu na bidhaa pamoja na habari iliyoandikwa | Je, watetezi wana vitu, bidhaa au habari inayoweza kuwa ya thamani kwa makundi yaliyojihami, na hivyo basi kuzidisha hatari ya kulengwa? (mafuta ya petroli, msaada wa kibinadmu, betri, vitabu vya mwongozo wa afya nk) |

| | |
|---|---|
| Ufahamu kuhusu vita na maeneo ya machimbo | Je, unao ufahamu kuhusu maeneo ya vita yanayoweza kukuhatarisha? Na pia kuhusu maeneo ya usalama yanayoweza kukusaidia katika usalama wako? Je, unazo habari za kuaminika kuhusu maeneo yaliyochimbwa migodi? |
| **Vijenzi vinavyohusiana na mfumo wa kisheria na kisiasa** | |
| Kutaka kupewa haki zako kutoka kwa mamlaka na sheria | Je, watetezi wanaweza kuibua michakato ya kisheria ili kudai haki zao? (kuwa na uwakilishi wa kisheria, uwepo wake kimwili kwenye vipindi vya kesi na mikutano nk) je, watetezi wanaweza kupata usaidizi ufaao kutoka kwa mamlaka zilizopo katika kazi na mahitaji yao ya usalama? |
| Uwezo wa kupata matokeo kutoka kwa mfumo wa kisheria na mamlaka | Je, watetezi wana uwezo wa kisheria wa kudai haki zao? Au wao ni vyombo vinavyotumiwa na sheria zilizopo zenye kulemaza? Wanaweza kushawishi vya kutosha mamlaka ili iweze kuzipa uzito haki zao? |
| Usajili, uwezo na kuweka hesabu na uwiano wa kisheria | Je, watetezi wananyimwa usajili wa kisheria au wanasubirishwa kwa muda mrefu? Je, kuna shirika linaloweza kuweka hesabu ya pesa vizuri na kuwa na uwiano wa kisheria na ule wa kitaifa? Je, unatumia programu za tarakilishi zilizonakiliwa kiharamu? |
| **Vijenzi vinavyohusiana na usimamizi wa habari** | |
| Vyanzo na uhalisi wa habari | Je, watetezi wanalo chimbuko la kutegemewa la habari ili kujengea msingi wa shutuma zao? Je, watetezi wanatangaza habari kwa uhalisi na kwa kutumia mbinu ifaayo? |
| Kuhifadhi, kutuma na kupokea ujumbe | Je, watetezi wanaweza kuhifadhi habari katika sehemu inayoaminiwa? Je, habari hiyo inaweza kuibiwa? Je, inaweza kulindwa dhidi ya virusi na wezi wa mtandaoni? Unaweza kutuma na kupokea habari kwa usalama? Watetezi wanaweza kutofautisha baina ya siri kuu na ujumbe wa kibinafsi? Je, watetezi huhifadhi habari zao katika sehemu hizo hata katika nyakati zisizo za kazi? |
| Kuwa shahidi au kuwa na habari kuu | Je, watetezi ni mashahidi wakuu wanaoweza kuwafikisha wahusika wenye mamlaka kizimbani? Je, watetezi wanayo habari maalum na ya kipekee kuihusu kesi au harakati fulani? |
| Kuwa na ufafanuzi unaoeleweka na kukubalika kuhusu kazi na malengo yako | Je, watetezi wanao ufafanuzi wa wazi, unaohimilika na kueleweka kuihusu kazi na malengo yao? Je, ufafanuzi huu unakubalika, au kwa uchache kustahimilika, na washika dau wote/wengi (hasa waliojihami)? Je, wanachama wote wa kundi wanaweza kutoa ufafanuzi huu watakapoulizwa kwa mfano katika maeneo ya ukaguzi? |
| **Vijenzi vinavyohusiana na sifa za kijamii na kishirika** | |
| Kuwepo kwa muundo wa kundi | Je, kundi limeundwa au kuandaliwa kivyovyote vile? Je, muundo huu unatoa kiwango kinachokubalika cha mshikamano katika kundi? |


| | |
|---|---|
| Uwezo wa kuunda uamuzi wa pamoja | Je, muundo wa kundi unaonyesha maslahi ya watu fulani au unawakilisha kundi lote (ukubwa wa uanachama)? Je, ipo mifumo ya usaidizi wa kutoa uamuzi na kutekelezwa kwa majukumu? Ni kwa kiwango gani shughuli ya utoaji uamuzi inakuwa shirikishi? Je, muundo wa kundi unaruhusu: (a) utoaji na utekelezaji wa maamuzi ya pamoja (b) kuyajadili masuala mbalimbali pamoja (c) mikutano isiyofaa na isiyo na malengo maalum (d) hakuna lolote katika hayo ni jibu. |
| Mipango na taratibu za usalama | Je, kanuni na taratibu za usalama zipo? Je, kuna ufahamu na umiliki mpana wa taratibu za usalama? Je, watu hufuata kanuni za usalama (kwa maelezo zaidi, tafadhali tazama Sura ya 1.8) |
| Ulinzi wa usalama nje ya kazi (familia na wakati wa mapumziko) | Je, watetezi wanatumia vipi wakati wao nje ya kazi (familia na wakati wa mapumziko)? Matumizi ya pombe na mihadarati hupelekea uwezekano wa kupata madhara. Mahusiano pia yanaweza kuleta madhara hayo (na pia kuwa ya faida) je, familia na marafiki wanajihusisha vipi katika shughuli za mtetezi? |
| Masharti ya kufanya kazi | Je, zipo kandarasi mwafaka za kazi kwa kila mmoja? Je, kila mmoja aweza kupata faida ya fedha za kidharura? Bima? |
| Kuajiri watu kazi | Je, mnazo taratibu zifaazo za kuajiri watumishi au washiriki na wanachama? Je, mnao mfumo fulani wa kiusalama kwa ajili ya watu wanaojitolea kwa wakati fulani (kama vile wanafunzi) au wageni katika shirika lenu? |
| Kufanya kazi na watu au na mashirika ya pamoja | Je, kazi yenu inafanyika moja kwa moja na watu? Je,unawafahamu hawa watu vizuri? Na je, unafanya kazi na shirika linalokuunganisha na watu? |
| Kuulinda ushahidi au waathiriwa tunaofanya kazi nao. | Je, sisi hufanya tathmini ya hatari ya waathiriwa,mashahidi na watu wengineo,tunapozishughulikia kesi maalum? Je, tunachukua hatua mahususi za usalama tunapokutana au wanapokuja afisini mwetu, je, wao wanakuwa na hisia gani? |
| Ujirani Na Mazingira Ya Kijamii | Je, watetezi wanatangamana vizuri na jamii katika maeneo wanamoishi? Je, yapo makundi fulani ya kijamii yanayoichukulia kazi ya watetezi kama nzuri au inayodhuru? Je, watetezi wamezingirwa na watu walio na uwezo wa kuwahujumu ( yaani jirani wachochezi, mathalan)? Je, jirani wanaounga mkono watetezi huwasaidia katika kuyabainisha matatizo yao? |
| Uwezo Wa Kuwahamasisha Watu | Je, watetezi wanaweza kuhamasisha watu ili kushiriki katika harakati za kujenga umma? |
| **Vijenzi vinavyohusiana na athari za kisaikolojia ya jamii (makundi/watu binafsi)** | |
| Uwezo wa kudhibiti msongo wa akili na hofu | Je, kuna watu muhimu, au kundi kwa jumla, wanaojiamini kuhusu kazi yao? Je, wanachama wa makundi/jumuiya wanadhihirisha wazi hisia zao za amani na lengo la kufanya kazi pamoja (katika maneno na vitendo)? Je, viwango vya msongo wa akili vinaathiri mawasiliano bora na mahusiano ya watu? Je, watu wanaweza kuupata usaidizi wa nje wa kisaikolojia na/au wameupata ujuzi wa ndani wa masuala ya kisaikolojia ya jamii? |
| Hisia nzito za kuvunjika matumaini au mateso | Je, hisia za kinyong'onyevu na ukosefu wa matumaini zinadhihirishwa wazi (kwa maneno na vitendo)? |

| Vijenzi vinavyohusiana na jamii, utamaduni na dini | |
|---|---|
| Ubaguzi | Je, watetezi wanabaguliwa (nje na ndani ya shirika) kwa misingi ya kijinsia, kikabila, dini au hali tofauti ya kijinsia? Je, kuna suitofahamu yoyote baina ya haki za kibinadamu, kijamii, kiuchumi, kiutambulishi, kitamaduni au kidini? |
| **Vijenzi vinavyohusiana na rasilimali za kazi** | |
| Uwezo wa kuelewa mazingira ya kazi na hatari | Je, watetezi wanayo habari sahihi kuhusu mazingira yao ya kazi, ya washika dau wengineo na maslahi yao? Je, watetezi wanaweza kuitafakari habari hiyo na kuvielewa vitisho, udhaifu na uwezo wao)? |
| Uwezo wa kubainisha mipango ya utendaji | Watetezi wanaweza kubainisha na hasa kuitekeleza, mipango ya utendaji? Je, kuna mifano kama hii ya awali? |
| Uwezo wa kupata ushauri kutoka kwa watoaji habari walio na ufahamu mpana. | Je, kundi laweza kupata ushauri wa kutegemewa kutoka kwa watu waaminifu? Je, kundi linaweza kufanya uamuzi wa kibinafsi kuhusu ni watu gani watakaolipa habari hizo? |
| Watu na kiwango cha kazi | Je, watu au watumishi waliopo wanalingana na kiwango cha kazi kinachohitajika? Je, unaweza kuandaa safari za nyanjani katika makundi (kwa uchache watu wawili)? |
| Rasilimali za kifedha | Je, unazo rasilimali za kifedha za kutosha? Mnaweza kutumia pesa taslimu kwa usalama? |
| Ujuzi kuhusu lugha na maeneo | Je, mnafamu lugha zinazohitajika kufanya kazi katika sehemu hiyo? Mnaijua sehemu hiyo vizuri? (barabara, vijiji, simu za umma, maeneo ya afya na kadhalika) |
| **Vijenzi vinavyohusiana na mawasiliano ya kitaifa na kimataifa na pia vyombo vya habari** | |
| Kuifikia miungano ya kitaifa na kimataifa | Je, watetezi wanao watu wa kuwasiliana nao katika kiwango cha kitaifa na kimataifa? Je,wanaweza kuwa na mawasiliano na ujumbe wa nchi nyinginezo unaozuru nchini, balozi, serikali nyinginezo na kadhalika? Wanaweza kuwasiliana na viongozi wa kijamii, kidini au watu wengine wenye ushawishi fulani? Je, mnaweza kuyafikia mashirika fulani au kuwa na hadhi ya kiuanachama inayoimarisha uwezo wenu wa ulinzi? |
| Kutangamana na vyombo vya habari na uwezo wa kupata matokeo kutoka kwavyo | Je, watetezi wanaweza kushirikiana na vyombo vya habari (vya kitaif na kimataifa)? au vyombo vinginevyo vya habari (vilivyo huru)? Je, watetezi wanafahamu namna ya kuyalinda mahusiano ya vyombo vya habari ipasavyo? |


## Mizani inayoonyesha hatari: Njia mbadala ya kuelewa hatari

Mizani hutoa njia nyingine ya kuelewa dhana hii ya hatari: hiki ni kitu tunachoweza kusema… "mita – ya hatari." Iwapo tutakuwa na visanduku viwili kisha tuweke matishio na udhaifu katika kisahani mojawapo kwenye mizani, na tuweke uwezo katika kisahani kingine, tutaona jinsi hatari huongezeka au hupunguka.

Picha ya 1





Picha ya 2





Jinsi tunavyokuwa na ongezeko la madhara, ndipo hatari nayo inaongezekae.

Picha ya 3




Jinsi tunavyokuwa na uwezo mkubwa, ndivyo hatari inayotukabili hupungua. Na namna hatari inavyopungua, tunaweza kupunguza madhara kisha kuzidisha uwezo.

Picha ya 4




Lakini… tazama kama tungekuwa na vitisho vingi. Usijali kwamba tutakuwa tunajaribu kuongeza uwezo wetu wakati huo. Mizani itaonyesha kiwango kikubwa cha hatari

**Muhtasari**

$$\text{HATARI} = \frac{\text{Vitisho x Udhaifu}}{\text{Uwezo}}$$

Udhaifu na uwezo ni vitu vya ndani vinavyobadilika (watetezi wanaweza kuvishughulikia).

Vitisho ni vitu vya nje vinavyobadilika (vitisho vinaweza kubuniwa hata kama ni vitu visivyowezekana).

1. Kuushughulikia udhaifu na uwezo kutaibua uwezekano mdogo wa vitisho. Tengeneza orodha yako ya sasa ya udhaifu na uwezo. Kuchangizana mawazo kunaweza kufaa.
2. Uutenganishe kwa mujibu wa vijenzi vya kimviringo na tena, kwa mujibu wa vijenzi mahsusi.
3. Tayarisha uwezo unaoupendelea: ushughulikie ipasavyo na zingatia njia zifaazo ili kuutimiza.
4. Aghalabu, hatua zinazofanana na zilizochukuliwa, zinaweza kutatua mambo kadhaa ya kijenzi kimoja.
5. Tokeo la taratibu za hapo juu litakuwa na athari ya uwezekano mdogo wa kuwepo kwa tishio na hivyo basi kupunguka kwa hatari.

Ingawa vijenzi fulani vinaweza kutokana na mazingira, vijenzi vinaweza kufahamika kama ubadilikajibadilikaji wa ndani ambao utamruhusu mtetezi kufanya kazi. Yaani sehemu ya hatari bila shaka ni "nje" ilhali, mtetezi aweza kujenga maarifa ya ("ndani") ili kukabiliana nayo.

Tishio ni badiliko la nje na chochote kinachofanywa,mwenye kutishia anaweza kuendelea kutoa vitisho. Mtetezi aweza "tu" kujitahidi kupunguza uwezekano wa tishio kutekelezwa na sio lazima kwamba aliondoe kabisa, labda kupatikane mabadiliko ya kisiasa.

# Kufahamu na Kutathmini Vitisho

**Lengo:**

Kupata ufahamu wa kina wa vitisho na jinsi ya kukabiliana navyo.

## Utathmini wa Vitisho: Ufahamu wa kina wa Vitisho

Kulemazwa kwa nguvu kwa Watetezi wa haki za binadamu ni kwa kisaikolojia. Vitisho hutumika pakubwa kuwafanya watetezi wahisi unyonge, wasiwasi kuchanganyikiwa na hali ya kutojiweza. Baadaye, kulemazwa huko pia hupelekea kuvunjika kwa vyama na kuwafanya watetezi kukosa imani kwa viongozi na wafanyikazi wenzao. Watetezi wanapaswa kuwa waangalifu kabisa na wafahamu jinsi ya kukabiliana na vitisho na pia wajue kuulinda usalama katika sehemu zao za kazi. Hili pia ndilo lengo kuu katika sura hii.

Katika sura ya 1.2 vitisho vilifafanuliwa kama uwezekano kwamba mtu aweza kumdhuru mwingine kimwili, kimaadili au kwa mali yake, kupitia vitendo vya kimakusudi na ambavyo mara nyingi huwa ni vya machafuko. Tulizungumzia pia vitisho vinavyoweza kutolewa (visivyo vya moja kwa moja (pale mtetezi mwenziyo kazini anapotishiwa na zipo sababu zinazoaminika kwamba wewe utatashiwa baada ya yeye), na **vitisho vilivyotangazwa** (vya moja kwa moja) (kupokea tishio la mauaji, kwa mfano). Tutashughulikia namna ya kukabiliana na **vitisho vilivyotangazwa**.

'**Tishio lililotangazwa**',ni **ile hali ya kutangaza waziwazi au kuionyesha nia ya kudhuru, kuadhibu au kuumiza, ili kwa kawaida kutimiza malengo fulani. Watetezi wa haki za binadamu** hupokea vitisho kutokana na athari ya kazi yao na vitisho vingi huwa na malengo ya wazi, ama kukomesha ayafanyayo mtetezi au kumlazimisha afanye jambo fulani.

Kwa kawaida, tishio lolote lile huwa na **asili** yake, yaani, huwa mtu au kundi lilioathirika kutokana na kazi ya mtetezi kisha baadaye hutoa tishio. Tishio pia lina **lengo** fulani linalotokana na athari ya kazi ya mtetezi, na pia huwa na **jinsi ambazo huwasilishwa**, yaani namna linavyojulikana kwa mtetezi.

Vitisho hukanganya. Twaweza kusema hili kwa kinaya fulani kwamba vitisho ni "mfumo usio wa madhara," kwa kuwa hutumiwa ili kupata matokeo mengi kwa kutumia kiwango kidogo cha nguvu. Mwenye kutoa vitisho huamua kufanya hivyo, badala ya kuchukua hatua – ambayo itahitaji nguvu nyingi. Kwa nini hivi? Kuna sababu kadhaa za hali hii, na ni bora kuzitaja hapa:

- Mwenye kutoa vitisho anao uwezo wa kuchukua hatua lakini kwa kiwango fulani anahofia hasara ya kisiasa itakayotokana na kutekeleza hatua hiyo kwa njia ya wazi dhidi ya mtetezi wa haki za kibinadamu.
- Mwenye kutoa vitisho huwa na uwezo finyu wa kuchukua hatua na hupania kuafiki lengo hilo kwa kuficha hali yake ya ufinyu na uwezo,nyuma ya tishio. Uwezo huu finyu unaweza kuwa wa muda kutokana na vipaumbele vingine, au uwe wa kudumu, japo katika hali zote, baadaye mambo yaweza kubadilika na kupelekea kuchukuliwa hatua ya moja kwa moja dhidi ya mtetezi.

Tishio huwa ni uzoefu wa kibinafsi wa mtu. Vitisho huathiri watu daima kwa njia fulani. Mtetezi mmoja aliwahi kusema: "vitisho hupelekea kuwepo kwa athari fulani, hata kama ni kuzungumza kwetu pekee juu ya vitisho". Kihakika, tishio lolote linaweza kuwa na athari maradufu: kihisia, na katika mahusiko ya usalama. Hapa tutajikita zaidi katika usalama, lakini tusisahau ule upande mwingine wa kihisia wa kila tishio au athari za hisia kuhusu usalama.

Tunajua kwamba kwa kawaida tishio hutokana na athari ya kazi yetu. Kupokea tishio ni kama maonirejea ya namna kazi yako inavyomwathiri mtu mwingine. Ukitumia mtazamo wa aina hii, utapata kwamba tishio ni chimbuko la habari yenye thamani kubwa na hivyo linapaswa kuchanganuliwa kwa uangalifu.

### "Kujenga" dhidi ya "kutoa" tishio

Watu hutoa vitisho dhidi ya watetezi wa haki binadamu kwa sababu mbalimbali, lakini ni wachache tu walio na nia au uwezo wa kutekeleza tendo la fujo au ghasia. Hata hivyo, wafu fulani binafsi wanaweza kuwakilisha tishio baya zaidi bila ya wao wenyewe kulitoa. Tofauti baina ya **kuunda** na **kutoa** ni muhimu:

- Watu wengine wanaojenga vitisho baadaye hutoa tishio.
- Watu wengi wanaojenga vitisho huwa hawatoi tishio.
- Watu wengine wasiojenga vitisho hutoa tishio.

Tishio linaweza kusadikika tu ikiwa mtu anayelitoa ana uwezo wa kuchukua hatua dhidi yako. Linapaswa kudhihirisha matumizi ya nguvu kwa uchache au kuwa na chembechembe fulani za makero yatakayochochea hofu.

Mwenye kutoa tishio anaweza kudhihirisha uwezo wake wa kulitekeleza kwa njia rahisi kabisa, kwa mfano, kuacha tishio la kimaandishi ndani ya gari lililofungwa milango, hata kama umeliegesha kwa dakika chache tu, au kwa kupiga simu baada tu ya wewe kufika nyumbani, kukuarifu kwamba unachunguzwa.

Watu waweza kujaribu kukutia hofu kwa kuweka vitu fulani vya kiishara kwenye vitisho, mfano, kwa kukutumia mwaliko wa matanga yako mwenyewe au kuweka mzoga wa mnyama mlangoni au kitandani pako nyumbani.

Vitisho vingi hudhihirisha sifa sawia zilizozungumziwa hapa. Ni muhimu kuzitofautisha, kwa kuwa baadhi ya watu wanaotoa vitisho hujifanya kwamba wao wana uwezo wa kuvitekeleza (kuviweka katika matendo) vitisho hivyo kwa kutumia mbinu za kiishara na zenye kuogofya.

*Mtu yeyote aweza kujenga tishio, lakini si kila mtu aweza kutoa tishio.*

Hatimaye, unapaswa kuwa na ufahamu wa iwapo tishio linaweza kutekelezwa kivitendo. Ikiwa unao uhakika kwamba huenda halitatekelezeka, basi mkabala wako utakuwa tofauti kuliko jinsi ulivyofikiria kwamba tishio lina msingi fulani katika uhalisia.

Malengo matatu makuu unapovitathmini vitisho ni:

- Kupata habari nyingi iwezekanavyo kuhusu kusudio na asili ya tishio (yote yatafungamanishwa na athari ya kazi yako)
- Kufikia suluhisho lililofikiriwa babara na lenye mantiki kuhusu iwapo tishio litatekelezwa au la
- Kuamua la kufanya.

## Hatua tano za kutathmini tishio

1 • **Tafuta ukweli kuhusu tishio.** Ni muhimu kujua bayana kilichotendeka. Hili laweza kutekelezwa kupitia kwa mahojiano au kuwauliza watu fulani muhimu, na wakati mwingine kutumia ripoti zifaazo.

2 • **Tambua iwapo kuna mkondo fulani wa vitisho katika kipindi cha wakati**. Iwapo vitisho hujengwa kutokana na fujo (kama inavyotendeka kila wakati) ni muhimu kuitafuta mikondo, kama vile, mbinu zilizotumika kutisha, nyakati ambapo vitisho hutokea, viashiria vya vitisho hivyo, habari andishi au ongezi iliyotolewa, n.k. Haiwezekani kila mara kuitambua mikondo hiyo, lakini ni muhimu katika kufanya kadirio bora la matishio.

3 • **Tambua dhamira ya tishio**. Kama kawaida ya kuwa na lengo la wazi linalofungamana na athari ya kazi yako, kufuata mkondo wa athari hiyo kunaweza kukusaidia kutambua lengo ambalo tishio hilo lingependa kutimiza.

4 • **Tambua chanzo cha tishio** (hili laweza kutendeka tu kwa kupitia hatua tatu za kwanza). Jaribu kuwa na uwazi zaidi na pia tofautisha baina ya chanzo kikuu na kile cha kisehemu. Kwa mfano, ungesema kwamba "serikali" inakutishia. Lakini kwa kuwa serikali yoyote ni mhusika tata, ingekuwa bora iwapo ungejibidiisha kutambua ni upande gani wa serikali unaweza kuhusika namatishio haya. Wahusika kama "vikosi vya usalama" na "makundi ya kupigana ya mwituni" ni wahusika tata vilevile: kumbuka pia kwamba tishio lililowekwa sahihi laweza kuwa la uwongo. Hii inaweza kuwa njia ya manufaa kwa yule anayetoa matishio kuepuka hasara za kisiasa na bado akatimiza lengo lake la kuleta hofu kwa mtetezi na pia kumzuia kufanya kazi.

5 • **Andaa suluhisho pevu na lenye mantiki kuhusu iwapo tishio litatekelezwa kwa vitendo au la**. Ghasia haziwezi kuepukika. Huwezi kuwa na uhakika kamili kwamba tishio litatekelezwa au hapana. Kutabiri kuhusu kutokea kwa ghasia kuna maana kwamba, katika hali fulani, kuwepo kwa hatari mahsusi hupelekea mtu au kundi maalum kumvuruga mlenga mahsusi.

Watabiri sio wapiga ramli na hawawezi kujifanya kwamba wanajua litakalotendeka. Hata hivyo unaweza kulifikia suluhisho lenye mantiki kuhusu iwapo tishio fulani linaweza kutekelezwa au la. Unaweza kuwa hujapata habari za kutosha kuhusu tishio katika hatua nne za hapo juu na hivyo basi usiwe hujafikia suluhisho.

Unaweza pia kuwa na maoni tofauti kuhusu ni jinsi gani "tishio" lililotolewa ni la hakika. Kwa vyovyote vile, unafaa kuendelea na harakati hiyo kwa msingi kwamba hali ni mbaya zaidi.

**Kwa mfano:**

> *Vitisho vya mauaji vimetolewa dhidi ya mhudumu wa haki za binadamu. Kundi lake linayachanganua vitisho hivyo kisha linafikia suluhu mbili zinazopingana, zote zikitokana na mantiki nzuri. Wengine husema kwamba tishio hilo ni bandia, huku wengine wakiona ishara zinazoogofya kuhusu uwezekano wa lo kutekelezwa. Mwishoni mwa mkutano, kundi linaamua kuchukua mtazamo wa hali mbaya zaidi, yaani, kwamba tishio linaweza kutekelezwa, na kuwa hatua mbalimbali za usalama zichukuliwe.*

Utathmini huu wa vitisho unapiga hatua kutoka kwa uhakika wa mambo (hatua ya 1) hadi utoaji unaoendelea wa makisio. Hatua ya 2 inahusu ufasiri wa hoja za kweli, na hii inaelekeza kwa hatua ya 3 hadi 5. Kuna sababu nzuri za kufuata utaratibu wa hatua hizo. Kwenda moja kwa moja kwa hatua ya 2 au 4, kwa mfano, kutaifungia nje habari muhimu inayoibuka kutoka kwa hatua za awali.

## Kuiendeleza na kuitamatisha kesi kuhusu vitisho

Tukio la vitisho au usalama linaweza kuhadharisha kundi la watetezi, lakini kwa kawaida huwa vigumu kudumisha ufahamu huu wa hadharisho kadiri tishio linavyoendelea kuwepo. Kutokana na shinikizo la nje na la kila mara kazini, mahadharisho ya mara kwa mara kwa kundi hilo yanaweza yakapelekea kuishiwa kwa hamu na kutofanya kazi barabara.

Kuleta hadharisho katika kundi kunafaa kufanywe tu kutokana na ushahidi wa kutegemewa na pia kulenga tukio maalum linalotarajiwa. Kufanya hivyo pia kunafaa pia kutekelezwe kwa jinsi ya kuwapa motisha wanakundi ili wachukue hatua, na pia kupelekea kuchukuiliwa kwa aina fulani za hatua. Ili kuwa na utendaji mzuri zaidi, hadharisho linapaswa kuchochea kiwango cha wastani cha motisha: kiwango cha chini zaidi hakiwachochei watu kutenda jambo lakini kile cha juu zaidi kinasababisha kuelemewa na hisia. Iwapo tishio linaonekana kwamba litadumu kwa muda, ni vyema kuwahoji watu na kufanya ufuatilizi baada ya hadharisho la awali kutolewa ili kuondoa suitafahamu, kubadilisha mapendekezo yasiyo ya natija, na kutilia mkazo uaminifu wa kundi katika juhudi zao za pamoja.

Hatimaye, iwapo tishio halitatokea, ni lazima sababu fulani zitolewe, na kundi litafaa kujulishwa kuwa ama ni tishio dogo au limeshatokomea.

Unaweza kuitamatisha kesi ya vitisho iwapo mshambulizi amekoma kabisa kutoa tishio. Katika hali hiyo, kuwa na uhakika kwamba unafanya vizuri katika kuitamatisha kesi, unafaa kwanza kuweza kusema ni kwa nini unafanya hivyo. Pia, maswali yanafaa kuulizwa kuhusu hali zilizobadilika zinazoweza kumchochea mtoaji wa matishio kutekeleza fujo.

## Kukabiliana na vitisho katika hali za usalama

- Tishio linaweza kuchukuliwa kama tukio la usalama. Ili kupata mengi kuhusu jinsi ya kukabiliana na matukio ya usalama, rejelea sura ya 1.4
- Tathmini ya vitisho vilivyotangazwa inaweza kukupelekea kufikiri kwamba unaweza kushambuliwa. Tafadhali tazama sura ya 1.5 kuhusu namna ya kuyazuia mashambulizi.

### Muhtasari

Vitisho vinaweza kuwa vya kimatukio, vya wazi (moja kwa moja) au visivyo vya moja kwa moja (visivyotangazwa)

Tishio lililotangazwa huwa ni tamko au hali ya kuonyesha nia ya kuweza kutimiza jambo fulani dhidi ya mtu.

Hatua 5 zitatambulisha uwezekano wa tishio ili kuchukua hatua ya ni nini cha kufanya:

1. Tambulisha ukweli
2. Tambulisha mkondo wa vitisho katika kipindi fulani cha muda
3. Tambulisha lengo
4. Tambulisha chanzo
5. Andaa suluhisho mwafaka na lenye mantiki kuhusu uwezekano wa tishio kutekelezwa.

Epuka masuluhisho ya "papo hapo" na jaribu kuwa na uwazi kadiri ya uwezo wako kwa kudhihirisha hali za ukweli na mikondo na pia kwa kuziendeleza kwa umbali unaoweza kujenga uthibitisho.

# Matukio ya Usalama: Ufafanuzi na Uchanganuzi

**Lengo:**

Kujifunza jinsi ya kutambua na kukabiliana na matukio ya usalama

## Tukio la usalama ni nini?

Kwa urahis, tukio la usalama laweza kuelezwa kama, **jambo lolote la hakika au kadhia unayofikiri inaweza kuathiri usalama wako binafsi au ule wa shirika.**

**Matukio a usalama yanaweza kuwa ya kimatukio au yaliyochochewa au bila ya kukusudia.**

Mifano ya matukio ya usalama yaweza kuhusisha mifano kama vile kulitazama gari fulani, unalolishuku na ambalo limeegeshwa nje ya afisi yako au nyumbani kwa siku kadhaa au simu inayolia usiku bila kujibiwa au mtu kukuulizia katika mji au kijiji jirani, wizi katika nyumba yako, na kadhalika.

Hata hivyo si kila kitu unachokigundua kinahusu tukio la usalama. Hivyo basi, unafaa **kulisajili** tukio kwa kuliandika chini, kisha **ulichanganue**, ni vizuri ufanye hivyo na wahudumu wenziyo, ili kutambulisha iwapo kweli litaweza kuathiri usalama wako. Kwa kiwango hiki unaweza **kukabiliana** nalo. Utaratibu wake ni kama ufuatao:

> Unagundua kitu Fulani ⇨ unafahamu kwamba kinaweza kuwa tukio la usalama ⇨ unalisajili/unawaambia wenzio ⇨ unalichanganua ⇨ unatambua kwamba kweli ni tukio la usalama ⇨ unakabiliana nalo ipasavyo.

Iwapo jambo hilo ni la kidharura, basi utaratibu huu utaendelea kutumika, ili kufanya hivyo kwa haraka kuliko kawaida. (tazama hapa chini).

### Jinsi ya kutofautisha kati ya matukio ya usalama na matishio:

Ikiwa unasubiri kuabiri basi na mtu aliyesimama kando yako anakutishia kwa sababu ya kazi yako, hii licha ya kuwa ni tishio – ni tukio la usalama. Lakini ukigundua kwamba afisi yako inamulikwa na gari la polisi kutoka upande mwingine wa barabara, au simu yako ya mkononi imeibiwa, hayo ndiyo matukio ya usalama na siyo lazima yawe matishio. Hata hivyo, matukio ya usalama yasiyo ya makusudio na/au ya kimatukio (yaani kuwa katika umati na/au kupoteza funguo) yanaweza

kutofautishwa bayana kutokana na matishio, kumbuka, matukio yaliyochochewa kimakusudi huwa na lengo fulani na siyo lazima yawe kama matishio (tazama sura ya 1). Lengo la chini zaidi la tukio lilichochewa kimakusudi ni kukusanya habari kuhusu watetezi iwapo habari hiyo itatumika dhidi yao.

Kutambulisha tofauti ya wazi ni muhimu angalau kwa ajili ya utulivu wa kimawazo wa watetezi.

**Vitisho vyote ni matukio ya usalama, lakini siyo matukio yote ya usalama huwa vitisho.**

## Kwa nini matukio ya usalama ni muhimu zaidi?

Matukio ya usalama ni mambo ya dharura katika kuushughulikia usalama wako kwa sababu **hutoa habari muhimu kuhusu athari ya kazi yako, na pia kuhusu hatua zinazoweza kuchukuliwa au kupangwa dhidi yako**. Hivyo hivyo, matukio kama hayo yanakuruhusu kubadili tabia au harakati zako na pia kukuepusha na maeneo hatari zaidi kuliko kawaida. Hivyo basi matukio ya usalama yanaweza kuchukuliwa kama viashiria vya hali iliyoko ya usalama. Kama hukuweza kugundua mabadiliko ya aina hizo, itakuwa vigumu kuchukua hatua zifaazo na za wakati mwafaka wa kubaki katika hali ya usalama.

Kwa mfano, unaweza kugundua kwamba unafanyiwa upelelezi baada ya kushuhudia matukio kadhaa ya usalama: sasa waweza kuchukua hatua kuhusu upelelezi.

**Matukio ya usalama huwakilisha"kiwango cha chini zaidi" cha kipimo cha usalama na huashiria upinzani/shinikizo kwa kazi yako. Usiyawache yakapotea bila kuyatambua.**

## Ni lini na vipi utayagundua matukio ya usalama?

Hii hulingana na kwa jinsi gani tukio hilo ni la wazi. Iwapo litaweza kupotea pasina kujulikana, uwezo wako wa kulitambua utategemea mafunzo yako kuhusu usalama, tajiriba yako na pia kiwango chako cha ufahamu kuhusu tukio kama hilo.

**Kadiri ufahamu na mafunzo yako yalivyo mapana, ndivyo utakavyoweza kukosa kutambua matukio machache.**

Wakati mwingine, matukio ya usalama hupuuzwa au huonekana kwa uchache kisha hutupwa upande mwingine, au wakati mwingine watu huyapokea kwa mihemko mikubwa kupita kiasi kwa yale wanayohisi kwamba ndiyo matukio ya usalama.

### Kwa nini tukio la usalama linaweza kupotea bila kugunduliwa?

**Mfano**:

*Mtetezi anakumbana na tukio la usalama, lakini shirika anamofanya kazi halitoi hisia zozote kuhusu tukio hilo. Hii inaweza kutokana na…*

- Mtetezi hajui kwamba kulitokea tukio la usalama
- Mtetezi anafahamu kuwa lilitokea lakini analipuuza kama lisilo muhimu

- Mtetezi hajajulisha shirika (alisahau, haoni kama ni muhimu, au ameamua kulinyamazia kwa sababu lilitokea kutokana na makosa yao)
- Baada ya kufanya tathmini ya kikundi, pale mtetezi aliposajili katika kitabu cha matukio, shirika anamofaya kazi linakataa kuliona tukio hilo kama ni muhimu

**Kwa nini wakati mwingine watu huyapokea matukio ya usalama kwa mihemko mikubwa?**

**Kwa mfano:**

*Mfanyikazi mwenziyo anaweza kuwa anahadithia kuhusu tukio fulani la usalama au linginelo, lakini baada ya kutathmini zaidi, inatambulika kwamba matukio hayo hayana msingi wowote. Hali halisi ya tukio la usalama katika muktadha huu ni ukweli kwamba mfanyikazi mwenziyo analo tatizo linalomfanya ayaone matukio ya usalama yasiyokuwepo. Anaweza kuwa labda anayo hofu, au anakabiliana na msongo wa akili, na anapaswa kupewa usaidizi ili kulitatua tatizo hilo.*

**Usisahau kuwa matukio ya usalama hupuuzwa au kutojaliwa mara kwa mara:kuwa mwangalifu kwa hili.**

## Kukabiliana na Matukio ya Usalama

Kuna njia nyingi za kukabiliana haraka na tukio la usalama. Hatua zifuatazo zinazingatia wakati na aina ya mkabiliano kutoka wakati tukio la usalama limeripotiwa, linapoendelea kutendeka na baada ya kutendeka.

Hatua 3 za kimsingi za kukabiliana na matukio ya usalama:

1 • **Yasajili**. Matukio ya usalama yaliyoshuhudiwa na mtetezi yanapaswa kusajiliwa, ama katika kitabu kidogo chake binafsi au kile kinachoweza kulifikia kundi zima.

2 • **Yachanganue**. Matukio yote ya usalama yaliyosajiliwa yanafaa kuchanganuliwa vizuri pindi tu yanapotokea au kila wakati. Ni aula kuyachanganua kwa kikundi badala ya mtu binafsi kwa kuwa kufanya hivyo hupunguza hatari ya kuacha nje kipengele chochote. Anapaswa kuwepo mtu wa kuhakikisha kwamba haya yanatendeka. Maamuzi pia yanapaswa kufanywa kuhusu iwapo usiri wa matukio maalum utahifadhiwa au la (matukio kama vile matishio). Je, ni uadilifu na haki kulificha tishio ili lisijulikane na wafanyikazi wenza pamoja na watu wengine unaofanya nao kazi? Siyo kila sheria hutumika katika hali zote lakini mara nyingi ni bora zaidi kuwa wazi iwezekanavyo katika hali ya kubadilishana habari na kushughulikia mipango ya haja na pia hofu.

3 • **Kabiliana nayo**. Kwa vile matukio ya usalama huwa na maonirejea kutokana na athari ya kazi yako, matukio hayo yanaweza kupelekea kwa haya:

- Kutoa hisia kutokana na tukio lenyewe
- **Maonirejea**, katika muktadha wa usalama, kuhusu jinsi unavyofanya kazi, **mipango** au **mikakati** yako ya kufanya kazi

### Mifano

Mfano wa tukio linalotoa **maonirejea** ya kufanya kazi kwa usalama zaidi:

*Kwa mara ya tatu,mwenziyo katika shirika unalofanyia kazi amekuwa na matatizo ya kupita kwenye sehemu ya ukaguzi wa polisi kwa sababu kila mara amekuwa akisahau kubeba stakabadhi zake zifaazo. Kwa hivyo, unaamua kutayarisha orodha ya kukaguliwa ambayo kila mfanyikazi atapaswa kupata maelekezo kabla ya kutoka jijini. Unaweza pia kubadilisha barabara zitakazotumika kwa safari kama hizi.*

### Mifano

Mfano wa tukio ambalo linatoa maonirejea ya namna ya kuandaa **mpango** wa usalama:

*Katika sehemu ile ile ya ukaguzi wa polisi, unazuiliwa kwa muda wa nusu saa kisha unaambiwa kwamba kazi yako haijathaminiwa sana. Matishio yasiyo dhahiri zaidi yanatolewa. Unapotaka kupewa maelezo zaidi katika makao makuu ya polisi, unazuiliwa tena. Unaandaa mkutano wa kundi ili kuipitia tena mipango ya kazi yako, kwa sababu inaonekana dhahiri kwamba lazima mabadiliko yafanywe ili kuendelea na kazi. Kisha unapanga msururu wa mikutano na watumishi wa serikali katika Wizara ya Ndani ili polisi aliye katika maeneo ya ukaguzi aagizwe kwamba aepuke kukunyanyasa, badilisha baadhi ya vipengele vya mipango yako na kisha tayarisha mikutano ya kila wiki ya kufuatilia kadhia hiyo.*

### Mifano

Mfano wa tukio linalotoa maonirejea ya **mkakati** wako wa usalama:

*Mnapoanza kufanya kazi kama watetezi katika eneo jipya, mnapata vitisho vya mauaji kisha mmoja wenu anashambuliwa. Hamkutarajia upinzani kama huo mnapokuwa kazini, au hamkuupangia kama sehemu yenu ya kuunda mikakati. Hivyo basi, mtabadilisha mikakati yenu kisha myazuie matishio na mashambulizi mengine ya ziada. Ili kutekeleza haya ipasavyo mtaweza kuiacha kazi yenu kwa muda mchache, mtoke eneo hilo kisha muuzingatie upya mradi wote.*

## Kukabiliana *kidharura* na tukio la usalama

Kuna njia nyingi za kukabiliana haraka na tukio la usalama. Hatua zifuatazo zimeandaliwa kwa jinsi kwamba zinaonyesha ni lini na vipi ya kukabiliana na tukio tangu kuripotiwa kwalo , linapoendelea kutendeka na baada ya kutendeke.

### Hatua ya 1: Kuripoti Tukio

- Ni nini kinatendeka/kimetendeka (jaribu kulenga mambo ya halisi)
- Tukio lilitendeka lini na wapi?
- Nani amehusika kwenye tukio hilo (iwapo anaweza kujulikana)
- Je, kuna yeyote aliyeumia au chochote kilichoharibika au mali?

**Hatua ya 2: Amua ni lini utakabiliana nalo. Kuna uwezekano wa aina tatu:**

- Kabiliano la **papo hapo** linanitajika ili kuwashughulikia watu walioumia au kukomesha / kuzuia shambulizi

- Kabiliano la **haraka** (kwa saa au hata siku chache zijazo) linafaa ili kuzuia uwezekano mpya wa matukio ya usalama kuibuka tena. (tukio limeshatendeka)

- Kabiliano la **kufuatilia** (katika siku chache, wiki au hata miezi). Iwapo hali imetulia, kabiliano la haraka au la papo hapo halitafaa labda. Hata hivyo, ni sharti tukio lolote la usalama linalohitaji kabiliano la haraka au papo hapo lifuatiliwe na hatua fuatilizi ili kuyarejesha mazingira yako ya kazi katika hali ya kawaida.

**Hatua ya 3: Amua ni vipi utakabiliana na tukio la usalama na pia ubainishe malengo yako:**

- Iwapo pana ulazima kwamba kabiliano lako liwe la papo hapo, malengo tayari yako wazi: washughulikie walioumia na/au zuia shambulizi jingine kutokea.

- Iwapo kabiliano ni la haraka, malengo yatabainishwa na msimamizi au kundi linaloshughulikia hatari hiyo (au yeyote mwingine wa mfano huo) kisha **lenga kurejesha usalama kwa wale walioathiriwa na tukio hilo**.

Makabiliano/Hatua za baadaye zitachukuliwa kupitia kwa njia za kawaida za shirika za kufanya uamuzi, kwa lengo la kurejesha mazingira bora ya nje ya kufanya kazi, kuziweka upya taratibu za ndani za kiuendeshaji na pia kuimarisha makabiliano ya baadaye ya matukio ya usalama.


Ni sharti kabiliano lolote lizingatie usalama na ulinzi wa watu wengineo, mashirika au taasisi nyinginezo ambazo kwamba mna uhusiano wa kufanya kazi nazo.

**Tambulisha malengo yenu kabla ya kuchukua hatua. Hatua ya kidharura ni muhimu lakini ufahamu wa kwa nini mnachukua hatua ni muhimu zaidi. Kwanza, kwa kutambulisha mnalotaka kuafiki (malengo) mnaweza kuamua ni kwa namna gani mtalitimiza (njia za kulitekeleza).**

**Kwa mfano:**

*Ikiwa kundi la watetezi litapokea habari kuwa mmoja wao hajawasili kule mjini ambako alidhamiria kwenda, wanaweza kuanza kujenga kabiliano kwa kuwasiliana na hospitali, au wale wanaofahamiana nao katika mashirika mengine yasiyo ya serikali na pia Afisi jirani ya Umoja wa Mataifa au hata polisi. Lakini kabla ya kuanza kuwasiliana nao, ni bora zaidi kutambulisha mnalotaka kutimiza na lile mnaloenda kusema. La si hivyo mtaibua kamsa isiyofaa (chukulia kwamba mtetezi amechelewa tu kwa sababu alikosa gari kwa wakati na kisha akasahau kupiga simu afisini) au mtajenga kabiliano lililo kinyume na lile lililopaniwa.*

Kuweka rekodi ya matukio ya usalama (na matishio) husaidia katika kuyachanganua kwa mtazamo wa kuyatarajia wakati maalum. Kwa mfano, iwapo rekodi itadhihirisha matukio ya usalama katika vipindi vya kabla ya uchaguzi, inawezekana kwamba yatatokea tena katika kipindi cha kabla ya uchaguzi. Rekodi pia yaweza kusaidia katika kutathmini mfanano wa hatua zilizochukuliwa na mtu fulani mwenye nia mbaya dhidi ya watetezi wa haki za binadamu au, katika hali ya matukio ya usalama kutokana na kutokuwa makini kwa watetezi wa haki za binadamu, utachangia katika kutathmini jinsi usalama unavyohifadhiwa na watetezi wenyewe.




**C:** uwezekano wa hatua kali zaidi kuchukuliwa na watu wanaoweza kuwa waovu dhidi ya watetezi wa haki za binadamu.

**C1:** CHINI KABISA (A1: upelelezi wa afisi kwa kutumia gari linaloonekana + B1: wakati uo huo na saa ile ile kila siku).

**C2:** CHINI: (A2: uvamizi katika afisi ya sheria: habari ya umma pekee imeibiwa + B2: mara mbili mwaka huu kwa wakati usio maalum).

**C3:** JUU: (A3: Afisi ya umma kuvamiwa: siri kuu kuibiwa (majina ya mashahidi wa siri kuu kuchukuliwa) + B3: mara tu kabla ya ushuhuda wa umma.

**C4:** Juu zaidi: (A4: kombora kurushwa afisini + B4: baada tu ya uvamizi afisini C3)

(...)

## Muhtasari

Tukio la usalama ni jambo au tendo lolote halisi unalofikiria linaweza kuathiri usalama wako binafsi au ule wa shirika.

Matukio ya usalama yanaweza kuwa ya kimatukio au yaliyochochewa kimakusudi au bila kujua.

Matukio ya usalama hupima usalama na athari ya kazi ya mtetezi kwa maslahi ya watu wengine.

Watetezi wote wanayo matukio ya usalama. Kinyume chake itaashiria kwamba:

- Athari ya kazi ya watetezi haionekani, ama kwa kuwa kazi haifanyiki vizuri na/au kwa sababu hakuna maslahi ya mtu yeyote yanayoathiriwa: hakuna yeyote aliye na haja nao.
- Anayeweza kutekeleza maovu dhidi yao tayari ameshapokea habari yote inayowahusu watetezi na hahitaji kujali sana: watetezi hawakuweza kuyatambua matukio ya usalama yaliyochochewa wakati huo (upelelezi, ukusanyaji wa habari…).

Tukio la usalama sio tishio, hata hivyo linahitaji kupewa makini fulani. Hatua tatu za kukabiliana na matukio ya usalama ni:

1 • Kuyasajili

2 • Kuyachanganua

3 • Kukabiliana nayo

# Kuzuia na kukabiliana na Hujuma

**Lengo:**

Kutathmini uwezekano wa kutekelezwa kwa aina mbalimbali ya hujuma

Kuzuia hujuma zinazoweza kutekelezwa dhidi ya watetezi

Kukabiliana na ujasusi

## Hujuma dhidi ya watetezi wa haki za binadamu

Ghasia ni harakati, na pia kitendo. Hujuma zenye ghasia dhidi ya mtetezi hazitendeki tu katika ombwe tupu. Uchunguzi wa makini aghalabu huonyesha kwamba hujuma huwa ni hali ya kufikia kileleni kwa migogoro, ubishi, matishio, matukio ya usalama na makosa ambayo yanaweza kubainishwa chanzo chake kadiri muda unavyosonga.

Hujuma dhidi ya watetezi ni zao la angalau masiala matatu yanayohusiana:

1 • **Kundi linalotekeleza hujuma zenye ghasia na mbinu zake** Hujuma dhidi ya watetezi aghalabu huwa zao la michakato ya kififikra na tabia tunazoweza kuelewa na kujifunza kutoka kwazo hata kama ni haramu. Kundi hilo litahitaji kujihami na mbinu ambazo angalau litatumia kukusanyia habari (ya matukio ya usalama) kuhusu watetezi wa haki za binadamu.

2 • **Hali ya nyuma pamoja na vichochezi vinavyompelekea mshambulizi aamue kutumia fujo kama hiari.** Watu wengi wanaohujumu watetezi huona mashambulizi kama njia 'muhimu' ya kuafiki lengo lao au "kutatua shida yao". Uhuru wa kufanya mambo bila kuadhibiwa na/au kuwa na nia ya kulipa gharama ya kisiasa huwa kama jambo "linalofaa" hali hiyo.

3 • **Hali inayorahisisha** kuwepo kwa ghasia, kwa maana kwamba huifanya ghasia kutekelezwa au haipelekei katika kukomesha ghasia hiyo, dhidi ya watetezi wa haki za binadamu.

## Ni nani basi aliye hatari kwa hawa watetezi?

Kwa jumla, yeyote anayefikiri kwamba kumhujumu mtetezi ni njia inayowezekana, inayopendelewa inayokubalika au inayoweza kuwa bora katika kutimiza lengo lake, anaweza kuchukuliwa kama mhujumu. Tishio huongezeka iwapo pia yeye anao, au anaweza kuwa na uwezo wa kumhujumu mtetezi.

**Tishio la kuhujumu laweza kupungua kutokana na mabadiliko ya uwezo wa mhujumu wa kutekeleza hujuma, mwelekeo wake wa namna gani hujuma hiyo inakubalika, au inawezekana vipi kwake kukamatwa na kuadhibiwa**

Hujuma nyingine hutangulizwa kwa kutolewa matishio. Nyingine haziwi hivyo. Hata hivyo, mwenendo wa watu binafsi wanaopanga kutekeleza hujuma yenye ghasia dhidi ya mtu au kundi fulani, mara nyingi hudhihirisha werevu fulani, kwa kuwa wanapaswa kukusanya habari kuhusu wakati mwafaka wa kutekeleza hujuma, kupanga jinsi ya kuwafikia walengwa wao, na jinsi ya kutoweka.

Hivyo basi, ni muhimu kupeleleza na kuchunguza ishara za uwezekano wa kutekelezwa hujuma. Hii inaweza kuhusisha yafuatayo:

- Kuchunguza uwezekano wa tishio linalopaniwa kutekelezwa
- Kutambua na kuchanganua matukio ya usalama.

Matukio ya usalama yanayojumuisha upelelezi wa watetezi au maeneo yao ya kazi yanalengwa katika kadhia nzima ya ukusanyaji wa habari. Habari hii huwa haikusudiwi kutumiwa katika ushambulizi, lakini ni muhimu kujaribu kutambulisha iwapo ni hiyo au la. (tazama sura ya 1.4). upelelezi waweza kutumika kwa malengo kadhaa:

- Kutambulisha harakati zinazoendelezwa,zinafanywa lini na/pamoja na nani.
- Kutumia habari hii baadaye ili kuwahujumu watu binafsi au mashirika.
- Kukusanya habari ifaayo katika kutekeleza hujuma.
- Kukusanya habari ili kuchukua hatua za kisheria au kunyanyasa kwa njia nyinginezo (bila ya ghasia za moja kwa moja)
- Kukuogofya wewe, waungaji mkono wako au watu wengine unaofanya nao kazi.

Ni muhimu kuelewa kuwa kwa kawaida, upelelezi unafaa ili kutekeleza hujuma, lakini upelelezi wenyewe hauwezi kuwa hujuma. Pia, si upelelezi wote hufuatwa na hujuma. Ghasia zilizopangwa hutokea wakati mwingine katika hali ambazo,kwa ghafla, mhujumu anapata fursa ya kuhujumu, japo hata kwa wakati huo, kiwango fulani cha maandalizi huwa tayari yamefanywa mwanzoni.

Kuna habari finyu inayoweza kukusaidia kutambua hujuma inayopangwa. Ukosefu wa masomo kuhusu kadhia hii ni kinaya kikubwa kutokana na ukweli kwamba hujuma dhidi ya watetezi zimekuwa nyingi. Hata hivyo, masomo yaliyopo kuhusu jambo hili hutoa ufahamu ufuatao.[1]

1 Claudia Samayoa na Jose Cruz (Guatemala) na Jaime Prieto (Colombia) wametoa masomo yanavutia kuhusu mashambulizi dhidi ya watetezi wa haki za binadamu. Mahony na Eguren (1997) pia walifanya uchanganuzi wa mashambulizi kama hayo

- **Kumhujumu mtetezi siyo jambo rahisi na linahitaji rasilimali**. Upelelezi unahitajika kutambulisha harakati za mtu binafsi na sehemu bora zaidi ya kutekeleza hujuma. Kumfikia mlengwa na kisha kutoweka kwa haraka ni muhimu. (Hata hivyo, iwapo mazingira yatamfaa mhujumu, basi atayatekeleza mashambulizi kwa urahisi mno).

- **Watu wanaowahujumu watetezi kwa kawaida huonyesha kiwango fulani cha kuendelea kufanya hivyo**. Nyingi ya hujuma huwalenga watetezi ambao wanajihusisha kwa kiwango kikubwa katika masuala yanayowaathiri wenye kuhujumu. Yaani, hujuma huwa zina mpangilio fulani maalum na huafiki haja za washambulizi.

- **Masiala ya kijiografia huwa na nafasi**. Kwa mfano, hali ya kuwahujumu watetezi katika maeneo ya mashambani inaweza kukosa umaarufu na hivyo basi kuchochea hisia chache katika kiwango cha utekelezaji wa sheria na kile cha kisiasa, kuliko hujuma dhidi ya watetezi zinazotekelezwa katika maeneo ya mijini. Mashambulizi dhidi ya makao makuu ya shirika lisilo la kiserikali au mashirika yanayosifika katika sehemu za mijini, huibua makabiliano makubwa zaidi.

- **Machaguo na uamuzi hufanywa kabla ya hujuma**. Watu wanaopania kutoa shambulizi dhidi ya shirika la watetezi wanafaa kuamua iwapo wanawahujumu viongozi au wanachama wa mashinani na kisha wachague baina ya shambulizi moja (dhidi ya mtu aliye muhimu na mwenye cheo na katika hali hiyo kuzidisha gharama ya kisiasa kwa mshambulizi) au msururu wa mashambulizi (yanayoathiri uanachama wa shirika). Utafiti mdogo kuhusu mashambulizi uliofanywa dhidi ya watetezi unaonyesha kwamba kwa kawaida mbinu zote mbili hutumika.

## Kutambulisha uwezekano wa shambulizi kutokea

Ili kutaka kujua iwapo hujuma inaweza kutekelezwa,unapaswa kuchanganua masiala yanayohusishwa nazo. Kutambulisha kwamba masiala hayo ni yepi, ni vizuri utofautishe aina mbalimbali za hujuma yaani, uhalifu, hujuma za kimatukio (kuwa katika sehemu isiyofaa wakati usiofaa) na mashambulio ya moja kwa moja (kulenga), kwa kutumia majedwali matatu kama ifuatavyo.[2]

2 Upambanuzi huu wa hujuma unajumuisha makundi sawa na yale ya matishio: Tafadhali angalia kwenye sura inayohusu matishio kwa maelezo zaidi.

**Jedwali 1:** Kutambulisha uwezekano wa hujuma za moja kwa moja (ulengaji)

(**WK** inasimamia watu wanaoweza kuhujumu)

| Uwezekano wa kuhujumu wa moja kwa moja (ulengaji) | | | |
|---|---|---|---|
| Masiala | Uwezekano mdogo | Uwezekano wa wastani | Uwezekano mkubwa |
| Uwezo wa kuhujumu | **WK** wana uwezo finyu wa kutekeleza hujuma katika sehemu yenu ya kazi | **WK** wana uwezo wa kiuendeshaji karibu na maeneo yenu ya kazi | Maeneo yenu ya kazi yanadhibitiwa kikamilifu na **WK** |
| Sababu ya kifedha | **WK** hawahitaji vifaa au pesa zenu kwa ajili ya shughuli zao | **WK** wana haja ya vifaa, pesa au aina yoyote ya shughuli za kuwaletea pesa (yaani kuteka nyara) | **WK** wana haja isiyofichika ya pesa na vifaa |
| Nia ya kisiasa na kijeshi | Kazi yenu haihusu chochote katika malengo yao | Haja ya kiasi – kazi yenu inalemaza malengo yao ya kisiasa na kijeshi | Kazi yenu inazuia kabisa malengo yao, inawafaidisha wapinzani wao, nk. |
| Rekodi ya hujuma za awali | Haipo au inapatikana kwa nadra | Matukio yasiyo ya kila mara | Matukio mengi ya hapo nyuma |
| Mielekeo au dhamira | Mwelekeo wa huruma au ule wa kutojali | Hali ya kutojali matishio yasiyo ya mara kwa mara. Maonyo ya kila wakati | Ushambulizi na matishio ya wazi na yale yaliyopo |
| Uwezo wa vikosi vya usalama wa kuzuia mashambulizi | Upo | Uko chini | Haupo, au vikosi vya usalama vinashirikiana na (au vinageuka kuwa) **WK** |
| Kiwango chako cha ushawishi wa kisiasa dhidi ya **WK** | Ni mzuri | Wa kadiri au chini | Ni finyu (kutegemea hali) au haupo |

## Mfano

wa uwezekano wa mashambulizi ya moja kwa moja (ulengaji):

*WK wanadhibiti maeneo unamofanyia kazi lakini hawana sababu yoyote ya kifedha ya kukuhujumu. Kwa kiasi fulani, kazi yako ndiyo inayolemaza malengo yao ya kisiasa na kijeshi, na hakuna vitangulizi vya mashambulizi kama hayo katika mji. Mwelekeo wao ni ule wa kutojali, na kwa wazi kabisa hawana haja ya kuvuta makini ya kitaifa au kimataifa au shinikizo linalotokana na kukuhujumu.*

**Uwezekano wa mashambulizi ya moja kwa moja katika hali hii unachukuliwa kama ule wa chini au wastani**

**Jedwali la 2:** Kutambulisha uwezekano wa hujuma za kihalifu kutokea

(**WU** inasimamia **Watekelezaji wa Uhalifu**)

| Uwezekano wa hujuma za uhalifu kutokea | | | |
|---|---|---|---|
| Masiala | Uwezekano mdogo | Uwezekano wa wastani | Uwezekano mkubwa |
| Makao na uwezo wa **WU** kusonga | WU kwa kawaida huishi katika maeneo yao binafsi yaliyo mbali na yenu | Kwa jumla, **WU** huingia katika maeneo mengine usiku (au huendeleza harakati zao karibu na maeneo yenu ya kazi) | **WU** hujishughulisha mahali popote, mchana au usiku |
| Ukakamavu wa **WU** | **WU** huepuka makabiliano (kwa hali nyingi hutekeleza uhalifu katika maeneo msiyoishi | **WU** hutekeleza uhalifu barabarani (lakini sio katika afisi za wafanyikazi) | **WU** hutekeleza uporaji wa wazi katika barabara za mijini na huingia katika majengo ili kutekeleza uhalifu |
| Kumiliki/kutumia silaha | Hawana silaha au wanatumia zile zisizodhuru | Silaha ghafi ikiwemo mundu | Silaha za bunduki, wakati mwingine huwa ni zile za hali ya juu |
| Ukubwa na maandalizi ya **WU** | Hutekeleza yeye binafsi au kundi la watu wawili | Watu 2-4 hutekeleza kwa pamoja | Hutekeleza kwa makundi |
| Makabiliano ya polisi na uzuiaji | Makabiliano ya haraka yanayoweza kuzuia ushambulizi | Makabiliano ya polepole, mafanikio machache ya kuwakamata wahalifu wakiwa wanatekeleza uhalifu | Polisi hawajitokezi kukabiliana kwa uthabiti hali hiyo |
| Mafunzo na utaalamu wa vikosi vya usalama | Wamepata mafunzo vizuri na ni wataalamu (labda tu wakose rasilimali) | Mafunzo ya kila mara, malipo duni, rasilimali chache | Polisi ama hawapo au ni wafisadi (wanashirikiana na wahalifu) |
| Hali ya kijumla ya usalama | Hakuna uzingatiaji wa sheria japo kuna hali ya usalama | Ukosefu wa usalama | Haki hazitekelezwi, watu wanafanya uhalifu bila kukabiliwa kisheria |

## Mfano

wa tathmini ya uwezekano wa shambulizi la uhalifu kutokea:

*Katika jiji hili, wahalifu hutekeleza vitendo vyao wakiwa wawili wawili au kwa makundi madogo, na wakati mwingine mchana. Aghalabu wao hubeba bunduki na hufanya hima ya kushambulia. Polisi hukabiliana nao ndio, lakini kwa njia ya polepole na bila umakini, na vikosi vya usalama havina utaalamu na rasilimali za kutosha. Hata hivyo kuna nidhamu katika uongozi wa polisi. Kuna ukosefu wa wazi wa usalama, na ni dhahiri pia kwamba, uwezekano wa uhalifu kutekelezwa kwenye maeneo jirani yaliyotengwa ni wa hali ya juu zaidi mradi tu viashirio* ***vyote*** *viwe ni vya kiwango cha juu.*

**Uwezekano wa hujuma za kihalifu kutekelezwa katikati mwa jiji kama hili unatoka katika kiwango cha juu hadi wastani**

**Jedwali la 3:** Kutambulisha uwezekano wa hujuma za kimatukio kutokea

(**WH** husimamia **watu wanaoweza kuhujumu**)

| Uwezekano wa hujuma za kimatukio | | | |
|---|---|---|---|
| Masiala | Uwezekano mdogo | Uwezekano wa wastani | Uwezekano mkubwa |
| Ufahamu wako wa maeneo yaliyo na migogoro | Ni mzuri | Ni wastani | Unafahamu kwa uchache kuhusu maeneo ya mapambano |
| Umbali wako kutoka maeneo ya migogoro | Kazi yako inafanywa mbali mno na maeneo haya | Unafanya kazi karibu na maeneo haya na wakati mwingine wewe huyaingia | Kazi yako iko hasa ndani ya maeneo haya |
| Kusonga kwa maeneo ya migogoro | Maeneo ya migogoro hayasongi, au yanabadilika polepole na yanathibitika | Hubadilika kwa kiasi cha mara kwa mara | Hubadilika kila wakati, hili huleta ugumu wa kutabiri maeneo ya mashambulizi |
| Ufahamu wako wa maeneo yaliyo na mabomu ya ardhini | Unao ufahamu mzuri au hakuna maeneo kama hayo | Unao ufahamu wa wastani | Huna ufahamu wowote |
| Umbali kati ya mahali pako pa kazi na maeneo yenye mabomu ya ardhi | Mahali pako pa kazi ni mbali zaidi kutoka maeneo hayo, au hayapo | Unafanya kazi karibu na maeneo hayo | Kazi yako imo hasa katika maeneo yenye mabomu ya ardhi |
| Mbinu za mapigano na silaha | Mbinu baguzi | Za kubagua, pamoja na matumizi ya wakati mwingine ya mizinga mikubwa, uvamizi na washambulizi wa kisiri | Zisizo za kubagua: mashambulizi ya mabomu, mizinga mikubwa, mashambulizi ya ugaidi au ya mabomu |

## Mfano

wa tathmini ya uwezekano wa kutekelezwa hujuma za kimatukio kutokea:

*Katika sehemu hii, unayafahamu vizuri maeneo ya mapigano, yanayobadilika polepole na kihakika. Mahala pako pa kazi ni karibu na maeneo ya mapigano na wewe huyatembelea maeneo hayo wakati mwingine. Hauko karibu na maeneo yaliyotegwa mabomu ya ardhini. Mbinu za mapigano ni za kuchagua na hivyo basi mara nyingi haziathiri raia.*

**Mtu hukabiliwa na kiwango cha chini cha hatari ya kitukio anapofanya kazi katika eneo hili.**

**Kuzuia hujuma za moja kwa moja/zisizo za moja kwa moja zinazoweza kutokea**

Ingawa mtetezi ndiye anayelengwa katika hali zote mbili, hebu tutofautishe baina ya:

- Hujuma ya moja kwa moja dhidi ya mtetezi
- Hujuma isiyo ya moja kwa moja dhidi ya mtetezi anapohusishwa mtu mwingine aliye wa karibu kwa mtetezi.

Katika hali zote mbili uzuiaji utahitaji mantiki ya kimsingi inayolingana kwa wote.

Unafahamu sasa kwamba tishio linaweza kupungua kutokana na mabadiliko ya:uwezo wa wale wanaoweza kushambulia, mielekeo/mitazamo yao kuhusu jinsi gani hujuma inaweza kukubalika, au kuna uwezekano wa yeye kukamatwa na kuadhibiwa.

**Ili kuzuia shambulio ni muhimu basi:**

- Kumsihi mtu anayeweza kuhujumu au anayetoa matishio kwa kumweleza kwamba shambulizi hilo litakuwa na hasara na madhara mengi.
- Kulifanya shambulizi liwe na uwezekano mdogo wa kutokea.

Aina hii ya uzuiaji wa shambulizi unalingana na uchanganuzi uliofanywa katika sura ya 1.2, unaosema kwamba hatari inayomkabili mtu hutegemea udhaifu pamoja na uwezo wa watetezi. Ili kujilinda na kupunguza hatari kama hii, unapaswa kuchukua hatua dhidi ya tishio, punguza udhaifu wako na uimarishe uwezo wako.

Tishio linapotolewa na unataka kuipunguza hatari inayohusiana nalo, ni muhimu kuchukua hatua – sio tu dhidi ya tishio lenyewe, bali pia kwa **udhaifu** na **uwezo** unaonasibiana nalo kwa karibu sana. Wakati wa shinikizo kubwa, unapotaka kukabiliana nalo haraka iwezekanavyo, mara nyingi utazingatia udhaifu ambao ndio mwepesi zaidi wa kushughulikia au ulio karibu zaidi nawe kuliko huo unaofaa zaidi kwa tishio.

**Kuwa mwangalifu**: Iwapo hatari ya kushambuliwa ni ya hali ya juu (yaani, ikiwa tishio ni la nguvu na la hakika, na kuna udhaifu mwingi na uwezo mdogo), kuushughulikia udhaifu au uwezo ili kupunguza hatari hakujengi mantiki kubwa kwa kuwa huhitaji muda ili kubadili uwezo au udhaifu na kuufanya kuwa tendi. Iwapo hatari ni ya hali ya juu zaidi (shambulio kali na la moja kwa moja linakaribia kutekelezwa) unaweza kufanya mambo matatu ili kuizuia:

**a** • Likabili tishio moja kwa moja na kwa makini, ukijua kwamba unaweza ukapata jibu la haraka na la moja kwa moja ambalo litazuia shambulizi. (Kwa kawaida ni vigumu zaidi kuwa na uhakika kwamba kutakuwa na jibu la haraka na la moja kwa moja, kwa sababu makabiliano huchukua wakati na wakati ni muhimu sana katika hali hii).

**b** • Punguza zaidi udhihirikaji wako, kwa kujificha au kutoweka mahala hapo.[3]

3 Hata hivyo, kutakuwa na nyakati ambapo kujaribu kusafiri kutamweka mtu katika hali ya hatari kubwa.

**c** • Tafuta ulinzi mzuri! Tazama mifano miwili ya ni nini kinachoweza kuwa ulinzi bora (kulingana na hali).

- Ulinzi wa kijamii: Utakapojificha katika jumuiya ya watu huenda jicho la umma na mashahidi wakamtatiza mwenye kuhujumu.

- Ulinzi wa kujihami: Unaweza kuwa muhimu katika hali fulani, lakini chukulia kwamba ni wa papo hapo, hivyo utamtatiza mwenye kuhujumu na hautamweka mtetezi katika hali ya hatari zaidi kwa muda wa wastani au mrefu. Kihakika, masharti kama hayo ya ulinzi wa kujihami ni magumu zaidi kuyatimiza! Serikali nyingine huwapa watetezi, walinzi waliojihami wa kuwasindikiza baada ya shinikizo la kitaifa na kimataifa kutolewa; katika hali kama hizi, kukataa au kukubali kusindikizwa na walinzi hao kunaweza kuwa kama kuifanya nchi iwajibikie usalama wa watetezi lakini serikali haiwezi kudai kwamba imeshamaliza majukumu yake iwapo mtetezi hatakubali kupewa ulinzi wa kujihami. Kampuni za kibinafsi za kulinda usalama zinaweza kupelekea kuwepo kwa hatari zaidi ikiwa zitakuwa na uhusiano wa karibu na wahujumu.[4] Na kwa watetezi, kubeba silaha hakutoshi katika kukabiliana na mashambulio yaliyopangwa, na kunaweza pia kuwafanya watetezi waweze kudhuriwa kwa urahisi ikiwa serikali itatumia hii kama sababu ya kuwashambulia kwa misingi ya kupambana na ugaidi au uanamgambo. Fauka ya hayo, hali ya kubeba silaha inaweza kubadilishwa na kuwa dhidi ya mtetezi kama vile kuenda kinyume cha Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa Haki za Binadamu.

Hali za kutishia zinazoweza kupelekea kuwepo kwa shambulio zinaweza kudhibitika kwa urahisi ikiwa wahusika au washika dau wengineo wanajumuishwa na kufanya kazi pamoja. Mifano ni kama vile mfumo tendi wa kimahakama, makundi yanayotoa misaada (ya kitaifa na kimataifa) yanayoweza kuleta shinikizo la kisiasa kwa washika dau wenye kubeba majukumu, makundi ya kijamii (ndani au miongoni mwa mashirika), makundi ya kibinafsi au ya kifamilia, wadumisha amani wa Umoja wa Mataifa/wale wa kimataifa, na kadhalika.

## Upelelezi na ukomeshaji wa upelelezi

Kuukomesha upelelezi kunaweza kukusaidia kutambua iwapo unachunguzwa. Ni vigumu kujua iwapo mawasiliano yako yanaingiliwa kati, na kwa sababu hii daima unafaa kuchukulia kwamba ni kweli yanaingiliwa kati[5]. Hata hivyo, inawezekana kukisia ikiwa harakati na afisi zenu zinapelelezwa.

### Ni nani anaweza kuwa anawapeleleza?

Watu ambao kila mara huwa katika maeneo yenu kama vile mabawabu wa milangoni wachuuzi walio karibu na lango la jengo lenu, watu walio karibu na magari katika maeneo yenu, wageni nk, wanaweza kuwa wanazichunguza harakati

4 Kwa maelezo zaidi tafadhali tazama katika Mwongozo huu sura ya "Kuimarisha usalama kazini na nyumbani."

5 Kwa maelezo zaidi tazama katika Mwongozo huu sura inayohusu kujifadhi mawasiliano.

zenu. Watu hufanya upelelezi ili: kupata pesa, kwa sababu wanashinikizwa kufanya hivyo, kwa sababu ya huruma wao au kwa kujumuisha masiala haya yote. Wale wanaofanya upelelezi wanaweza pia kuweka washirika wa chama au muungano wao katika maeneo yenu. Watu wanaweza pia kuwachunguza kwa umbali. Katika hali hii wao aghalabu huwa ni wanachama wa shirika fulani na wanaweza kutumia mbinu za kuchunguza kwa kujificha. Hii ina maana ya kufanya upelelezi kwa:kujiweka katika umbali fulani, watu kadhaa kuchunguza kwa kubadilishana nafasi, na kuchunguza wakiwa katika sehemu tofautitofauti, wakitumia magari tofautitofauti n.k.

## Jinsi ya kutambua iwapo unachunguzwa

Unaweza kutambua ikiwa unachunguzwa kwa kuwatazama wale wanaokupeleleza na kwa kutumia mbinu zifuatazo (bila ya kujishuku):

- Iwapo una sababu ya kufikiri kwamba mtu aweza kukuchunguza, ni lazima uwe mwangalifu kuhusu matembezi ya watu katika sehemu yako na mabadiliko ya mielekeo yao, kwa mfano, wakianza kuulizia kuhusu shughuli yako. Kumbuka kwamba kama wanavyoweza kufanya upelelezi wanaume na wanawake,nao wazee na watoto wanaweza kufanya hivyo pia.

- Ukishuku kwamba unafuatwa, unaweza kuchukua hatua ya kukomesha hali hiyo kwa kuhusisha mtu mwingine unayemwamini, na asiyejulikana kwa wale wapelelezi wanaokuchunguza. Akiwa hapo mapema na awe kwa umbali mzuri, huyu mtu anaweza kuchunguza harakati zinazoendelea pindi unapowasili, unapoondoka au unapoenda popote. Anayechunguza ataweza kufanya hivyo katika mahali ambapo utaonekana wakati wote, pakiwepo kwako nyumbani, afisini na katika sehemu nyinginezo unakofanyia kazi.

**Mfano**

*Kabla ya kufika nyumbani, unaweza kumwomba mmoja katika watu wa familia yako au jirani unayemwamini akufanyie jambo fulani (kwa mfano, kubadilisha gurudumu la gari) ili nawe utazame iwapo kuna mtu anayesubiri kuwasili kwako. Jambo kama hili laweza kufanywa pale unapotoka afisini pako ukitembea kwa miguu. Iwapo unatumia gari la kibinafsi, itakuwa bora kwa gari jingine liondoke baada ya lako ili umpe mtazamaji wakati mwafaka wa kuanza kusogea mahala ulipo.*

Faida ya kuukomesha upelelezi ni kwamba, angalau pale mwanzoni, mtu anayekutazama hawezi kugundua kwamba unafahamu kuwa yeye yupo hapo. Inapaswa hivyo basi kuwekwa wazi kwa yeyote anayeukomesha upelezi ya kwamba huenda si jambo la busara la kukabiliana ana kwa ana na mtu anayekutazama. Baadaye watagundua (wanaokutazama) kwamba unafahamu harakati zao, na hili pia linaweza kuchochea hisia za kighasia. Ni muhimu kuwa mwangalifu zaidi na kujiweka mbali iwapo unafahamu kwamba kuna mtu anayekupeleleza. Mara tu upelelezi utakapogundulika, unaweza kuchukua hatua inayopendekezwa katika mwongozo huu.[6]

6 Tazama sura inayohusu "kuimarisha usalama kazini na nyumbani."

Mengi ya mashauri haya ya kuukomesha upelelezi hutumika mno katika maeneo ya mijini. Hali ni tofauti kabisa katika sehemu za mashambani, japo watetezi na jamii zinazoishi katika maeneo kama hayo zimezoea kuwa na uangalifu kuhusu wapita-njia wa karibu. Hivyo basi, ni vigumu kwa yeyote anayetaka kukuchunguza, kupenya hadi kwa wakaazi wa mashambani – labda tu wakaazi hao wawe wanataka kuihujumu zaidi kazi yako.

**Tanbihi**: Kujenga uhusiano na vikosi vya usalama vinavyokufuatilia kunaweza kuwa kwa faida katika hali nyinginezo. Wakati mwingine upelelezi hautakuwa jambo la siri kwa kuwa mojawapo wa malengo yake ni kuufanya uweze kuwa wa wazi/wenye kudhalilisha. Katika hali nyinginezo watetezi hujenga urafiki na watu kutoka katika vikosi vya usalama ambao wanaweza wakati mwingine kuwadokezea iwapo upelelezi au hatua zinapangwa kuchukuliwa dhidi yao.

### Wakati wa kubainisha iwapo unachunguzwa

Ni jambo la kimantiki na lenye busara kubaini iwapo unafanyiwa upelelezi ikiwa unayo sababu ya kuamini hivyo – kwa mfano, kwa sababu ya matukio ya usalama yanayoweza kuhusiana na shughuli ya upelelezi. Iwapo kazi yako ya kutetea haki za binadamu inakabiliwa na hatari fulani, litakuwa wazo zuri kutafuta jinsi ya kuuzuia upelelezi kila mara, ikiwa hali kama hiyo itatokea.

Unafaa pia kufikiri kuhusu hatari unayowaletea watu wengine iwapo unapelelezwa – hatari yaweza kuwa mbaya zaidi kwa shahidi au mmoja wa wanafamilia wa mwathiriwa unayekutana naye,kuliko itakavyokuwa kwako. Jaribu kutafuta mahali palilo salama kwao ili wakutane hapo. Unaweza kuwaonya kwa kuwaeleza kwamba harakati zako zinaweza kuwa zinapelelezwa.

## Kukabiliana na hujuma

Hakuna sheria yoyote inayoweza kutumiwa kwa hujuma zote dhidi ya watetezi. Dhuluma pia ni matukio ya usalama, na unaweza kupata njia za kukuongoza za jinsi ya kukabiliana na matukio ya usalama katika sura 1.4.

**Katika hali yoyote ya kudhulumiwa kuna mambo mawili ya kimsingi ya kukumbuka:**

- Daima uufikirie usalama! Nyakati zote kutendeka kwa hujuma na baada yake (iwapo unadhulumiwa na huna budi kuchagua baina ya mambo mawili, chagua lile la usalama kwako)

- Ni jambo linalofaa kupata nafuu ya kimwili na ya kisaikolojia baada ya kuhujumiwa na ni bora pia uchukue hatua ya kutatua hali hiyo, na kisha udumishe tena mazingira bora ya kazi, kwako na shirika lako. Ni muhimu kuhifadhi habari za kina iwezekanavyo kuhusu hujuma: ni nini kilitendeka, nani/ni watu wangapi walihusika, nambari za usajili za magari, maelezo kuhusu magari hayo, nk. Maelezo haya yanaweza kuwa muhimu ili kuiandikisha kesi na yanafaa yakusanywe haraka iwezekanavyo. Hifadhi nakala za stakabadhi zozote zilizowasilishwa kortini ili kuiandikisha kesi.

### Muhtasari

Hujuma ni kilele cha harakati ambayo bila shaka, kwa kuhusisha matukio ya usalama,yanaweza kuwa matishio.

Hivyo basi hujuma sio tukio "lisilotarajiwa".

Hujuma inaweza kutokea bila kutarajiwa au ikapangwa tu.

Si rahisi kuwahujumu watetezi wa haki za binadamu kwa kuwa ni watu maarufu kwa umma na wanapata usaidizi wa aina fulani.

Hujuma ni zao la masiala matatu yanayohusiana:

- Mtu anayechukua hatua na mikakati ya kighasia.
- Vichocheo na matukio ya nyuma yanayomfanya mwenye kuhujumu kuchukulia matendo ya ghasia kama chaguo lake.
- Mazingira yanayofaa.

Hujuma huhitaji rasilimali na uwezo wa kutosha, kumfikia mtu binafsi, kutoroka kwa haraka, kuhujumu kwa kiwango fulani pasina kuadhibiwa au uamuzi wa mwenye kuhujumu kwamba hujuma hiyo inaafiki gharama ya kisiasa.

Hivyo basi, kuzuia hujuma kunahitaji hatua za kudumisha hasara za kisiasa iwezekanavyo (kupunguza ule uhuru wa kutoadhibiwa) na kujaribu iwezekanavyo kumzuia mtu asikabiliwe na hatari.

# Kuunda mkakati wa kilimwengu wa Usalama

**Lengo:**

Kutambua mikakati na mbinu zilizopo tayari

Kuichanganua mikakati na mbinu zilizopo tayari

Kutoa ufafanuzi wa mkakati wa kilimwengu wa kuchukua nafasi ya kazi

## Mkakati wa uzuiaji maalum na mbinu yake

Watetezi na makundi yanayotishiwa hutumia mikakati ya aina mbalimbai ya uzuiaji wa kusudi fulani ili kukabiliana na matishio. Mikakati hii hutofautiana sana kulingana na:mazingira inamotumika (mijini au mashambani) aina ya tishio, rasilimali zilizopo za kijamii, za kifedha na kisheria n.k.

Mikakati mingi ya malengo fulani inaweza ikatumilizwa papo hapo na kwa hali hiyo kushughulikia maazimio ya kipindi cha muda mfupi. Hivyo basi, mikakati ya aina hiyo hufanya kazi zaidi kama mbinu kuliko mikakati mingine ya kilimwengu. Mikakati mingi vilevile hurejelea chukulizi za mtu binafsi kuhusu hatari, na wakati mwingine huweza kusababisha kiwango fulani cha madhara hususan iwapo mikakati iliyotumika haiwezi ikarejeshwa nyuma.

Mikakati hiyo maalum ina uhusiano wa karibu na aina na uzito wa tishio na pia uwezo na udhaifu wa kundi.

**Unapokuwa unafikiria kuhusu usalama na ulinzi, ni lazima uzingatie mikakati maalum yako binafsi pamoja na ile ya wenzako. Sisitiza mikakati iliyo thabiti, jaribu kupunguza ile ya madhara na pia jaribu kuheshimu ile iliyosalia (hasa mikakati maalum inayohusiana na imani za kitamaduni au kidini)**

## Mikakati kadhaa maalum inayitumiwa na watetezi wa haki za binadamu:

- Kutilia mkazo vizuizi vya ulinzi, kuficha vitu vyenye thamani.
- Kuepuka tabia inayoweza kumtatiza mhusika mwingine, hasa iwapo udhibiti wa kimaeneo unamofanya kazi una mzozano wa kijeshi.

- Kuenda kujificha wakati wa hatari kuu, yakiwemo maeneo ambayo si rahisi kuyafikia, kama vile milimani na porini, kubadilisha nyumba n.k. Wakati mwingine familia zote huenda kujificha na wakati mwingine ni watetezi tu wanaojificha. Kitendo cha kujificha kinaweza kutendeka usiku au kikaendelea kwa majuma kadhaa na huenda mtu mwingine wa nje asihusike katika shughuli hiyo.
- Kufatuta ulinzi wa silaha au ulinzi wa kisiasa kutoka kwa mmoja wa wahusika waliojihami.
- Kujitenga kwa muda na shughuli,kufunga afisi, kuhama, kuhamishwa kwa lazima (ukimbizi wa ndani) ama kuenda uhamishoni.
- Kutegemea "bahati nzuri" au kufanya uamuzi wa kutegemea imani za kidini au "kimiujiza".
- Kuwa msiri zaidi, hata kwa wafanyikazi wenza: kukataa ukweli wa mambo yalivyo kwa kuepuka mijadala inayohusu matishio; ulevi uliozidi kiasi, kazi nyingi, tabia za kichakaramu.

Watetezi pia wanaweza kuifikia mikakati ya kutolewa hisia. Hii inaweza kuwa kutoa ripoti zinazonuiwa kutangaza suala fulani, kujenga tuhuma, kutekeleza maandamano nk. Katika hali nyingi mikakati hii haijumlishi mkakati wa kipindi kirefu cha wakati, lakini hujibu matendo ya muda mfupi. Wakati mwingine mikakati ya majibu inaweza hata kuleta matatizo zaidi ya kiusalama kuliko yale waliyopania kuyashughulikia.

## Kuchanganua mkakati wa kuzuia

Zingatia yafuatayo iwapo ni mkakati wa kiulimwengu au ulio maalum:

- **Uwezo wa kukidhi mahitaji**: Je, mikakati yenu inaweza ikakidhi mahitaji ya hasara ya mtu binafsi au usalama wa kundi?
- **Uwezo wa kutumika**: mikakati yenu inaweza kutumika kwa haraka katika mazingira mapya, ambapo hatari ya kushambuliwa itakuwa imekamilika? Mtetezi aweza kuwa na hiari kadhaa, kwa mfano, ama kujificha au kukaa nyumbani kwa watu wengine kwa muda. Mikakati kama hii inaweza kuonekana kana kwamba ni dhaifu au hailingani, lakini mara nyingi huhitaji uvumilivu mkubwa.
- **Uwezo wa kudumu**: Je, mikakati yenu inaweza kudumu kwa muda, licha ya kuwepo vitisho au mashambulizi yasiyo ya madhara makubwa?
- **Utendakazi bora**: Je, mikakati yenu inaweza kuwalinda watu au makundi yaliyopo ipasavyo?
- **Uwezo wa kurejeshwa nyuma**: Iwapo mikakati yenu haitafanya kazi ilivyotarajiwa au hali ibadilike, je, mikakati hiyo inaweza kurejeshwa nyuma/au kubadilishwa?

## Kukabiliana na hatari baada ya kuifanyia tathmini

Baada ya kukamilisha kuitathmini hatari,unafaa kuyatazama matokeo. Kama ilivyo vigumu kukadiria "kiwango" cha hatari unayokabiliana nayo, unafaa kutambulisha ufahamu wa 'kiwango' cha hatari ilivyo.

Watetezi na mashirika tofauti yanaweza wakatambua viwango tofauti vya hatari. Kisichokubalika kwa watetezi wengine kinaweza kukubalika kwa wengine,hata ikiwa ni ndani ya shirika moja. Badala ya kujadili ni nini "kisicho na budi" kutendeka ama iwapo umejiandaa kuendelea mbele nacho, viwango vya juu mbalimbali vya hatari za watu vina ulazima wa kushughulikiwa: unapaswa kujenga kiwango cha kawaida na kinachokubalika kwa wanachama wote wa kundi.

Hayo yakishanenwa, kuna njia tofauti za kukabiliana na hatari:

- Unaweza **kukubali** hatari jinsi ilivyo, kwa sababu unahisi kwamba waweza kukaa nayo.
- Unaweza **kupunguza** hatari, kwa kushughulikia matishio, udhaifu na uwezo.
- Unaweza **kubadilisha** hatari, kwa kuchukua hatua za pamoja na watetezi wengineo ili mtoe matishio kwa mtetezi au shirika lisilokuwa na natija nzuri.
- Unaweza kuwa na hiari ya **kuahirisha** hatari, kwa kubadilisha harakati zako au mbinu utakayotumia ili kupunguza hatari.
- Unaweza **kuepuka** hatari kwa kupunguza au kukatiza shughuli zako (katika hali nyinginezo, inaweza kuwa maana ya kwenda uhamishoni)
- Unaweza **kupuuza** hatari, kwa kujifanya huioni. Hakuna haja ya kusema kuwa hii si njia bora.

Kumbuka kwamba kiwango cha hatari kwa kawaida huwa tofauti kwa kila shirika na watu binafsi wanaohusika katika utetezi wa haki za binadamu, na kuwa washambulizi hupenda kulenga maeneo dhaifu zaidi.

**Kwa mfano:**

*Hebu tuangalie mfano wa mkulima mdogo aliyeuawa na jeshi la kibinafsi la mwenye ardhi. Labda mashirika kadhaa na watu binafsi wameshughulikia kesi hiyo; kama vile, kundi la mawakili kutoka katika jiji lililo karibu, chama cha wakulima wadogo na mashahidi watatu (wakulima wadogo wanaoishi katika kijiji jirani). Ni muhimu kukadiria viwango mbalimbali vya hatari ya kila mshika dau ili kuupunguza vizuri usalama wa kila mmoja.*

### Muhtasari

Kuhusu suala la usalama, watetezi hawaanzi bila chochote. Wote wamebuni mikakati na mbinu za kukabiliana na hatari pamoja na matishio. Kinyume chake kinaweza kuashiria kuwa hawapo tena na/au wameiacha kazi yao. Angalau watetezi wamebuni mikakati na mbinu maalum kwa shughuli ya uzuiaji. Wengine wanaweza pia kuwa wamebuni mkakati wa kilimwengu wa uzuiaji.

Pasina kujali ni mikakati ya aina gani, wanapaswa kujibu kwa kutumia angalau mbinu hizi.toaji majibu, uwezo wa kutumika, uwezo wa kudumu, uwezo wa kutenda kazi na kuleta natija nzuri, na uwezo wa kurejeshwa nyuma. Ni lazima kadirio la hatari litekelezwe ili kutambulisha iwapo "linakubalika". La si hivyo, mtetezi atapunguza, atabadilishana, atatofautiana, au atakimbia hatari.

## Watetezi wa haki za binadamu hufanya kazi katika mazingira ya uadui

Mara nyingi, watetezi hufanya kazi katika mazingira ya uhasama. Kuna sababu nyingi za hali kama hii.Mno ni ukweli kwamba kazi yao inaweza kuwapelekea kukabiliana na wahusika maarufu wanaozikiuka sheria za kimataifa za haki za binadamu. Zaweza kuwa serikali au tawala za nchi, vikosi vya usalama, makundi pinzani yaliyojihami kwa silaha au magenge ya kibinafsi yaliyojihami pia. Wahusika hawa maarufu waweza kujibu kwa kujaribu kuwasimamisha watetezi kufanya kazi yao kupitia kwa chochote yaani kuanzia kwa kuwanyamazisha katika uhuru wao wa kujieleza hadi kuwatishia na kuwahujumu kwa nji ya wazi. Kiwango cha uvumilivu cha wahusika kitategemea kazi ya watetezi –shughuli nyingine zaweza kuchukuliwa kama zilizokubaliwa, na nyingine zisichukuliwe hivyo. Mara nyingi ukosefu huu wa uhakika huwa wa makusudi.

Mazingatio mawili muhimu yafanywe hapa. Katika hali nyingi, ni watu fulani pekee **miongoni** mwa wahusika tata (kama wote waliotajwa hapo juu) ambao ni maadui wa watetezi. Kwa mfano, watu fulani katika serikali wanaweza kuwa na ari ya kuwalinda watetezi, huku wengine wakidhamiria kuwashambulia. Watetezi pia wanaweza kupata uhasama mwingi wakati wa machafuko ya kisiasa kama vile wakati wa uchaguzi, au wakati wa matukio mengine ya kisiasa.

## Nafasi ya kazi ya kijamii na kisiasa ya watetezi

Mwongozo huu unalenga ulinzi na usalama wa ufanyaji kazi wa watetezi wa haki za binadamu katika mazingira ya uhasama. Bila shaka hatua yaweza kuchukuliwa katika kiwango cha kijamii na kisiasa: kufanya kampeini na kuendeleza harakati za watetezi wa haki za binadamu aghalabu kunanuiwa kujenga ukubalifu mpana wa haki za binadamu katika jamii au hatua madhubuti zaidi kuchukuliwa na wahusika wa kisiasa. Kwa kawaida, huwa hatufikirii kuhusu harakati za aina hiyo kama zenye kuhusu usalama lakini zinapofanikiwa, zinaweza kujenga athari chanya katika kuihifadhi nafasi ya kijamii na kisiasa ya watetezi wa haki za binadamu.

Nafasi ya kijamii na kisiasa inaweza kufafanuliwa kama **hatua mbalimbali ambazo mtetezi aweza kuchukua wakati anapokabiliwa na hatari yoyote**. Yaani, mtetezi anatambua "hatua mbalimbali za kisiasa zinazoweza kuchukuliwa na hatimaye kuihusisha kila hatua na gharama fulani au matokeo kadhaa. Mtetezi anatambua baadhi ya matokeo haya kama "yanayokubalika na mengine yasiyokubalika, hivyo basi kuweka bayana mipaka ya nafasi tofauti ya kisiasa."[1]

**Kwa mfano:**

> *Kundi la watetezi wa haki huweza kufuatilia kesi ya haki za binadamu hadi mmoja wao apate tishio la kifo. Wakitambua kwamba wana nafasi tosha ya kijamii na kisiasa, wanaweza kuamua kutangaza wazi kwamba wamepokea matishio na hatimaye kuendelea na kesi hiyo. Lakini wakitambua kwamba nafasi yao ya kisiasa ni finyu, wanaweza kuamua kwamba kukataa tishio hadharani kutakuwa na hasara kubwa. Wanaweza hata kuamua kuiacha hiyo kesi kwa muda kisha waimarishe uwezo wao wa usalama kwa wakati huo.*

1 Ufafanuzi huu na sehemu nyinginezo muhimu za dhana nii zimetolewa kutoka Mohony na Eguren (1997), uk. 93. Wameunda pia mtindo wa nafasi ya kisiasa unaojumuisha nafasi ya kazi ya watetezi wa haki za binadamu pamoja na kisaidizi cha ulinzi wao.

Dhana ya hatari "inayokubalika" inaweza kubadilika kwa wakati na kutofautiana sana kutoka kwa mtu binafsi hadi mwingine au vivyo hivyo kwa mashirika. Kwa wengine, mateso au kifo cha mmoja wa wanafamilia inaweza kuwa hatari isiyokadirika. Watetezi wengine huamini kwamba kufungwa jela ni jambo linalofaa mradi tu linawasaidia kuafiki malengo yao. Kwa wengine, wanaweza kufikia kileleni kwa tishio la kwanza.

Licha ya kuwekewa mipaka na wale wanaoitumia,nafasi hii ya shughuli ya kisiasa ina uwezekano mkubwa wa kubadilika katika mazingira yanayoizunguka ya kisiasa ya taifa. Unapaswa, hivyo basi, kuipa mtazamo wa nafasi yenye kubadilika.

## Nafasi ya kazi ya watetezi na usalama wao


Mikakati yote ya usalama inaweza kupewa muhtasari wa maneno haya: unataka kuipanua nafasi yako ya kazi na kuidumisha kwa njia hiyo. Kwa kujikita kabisa katika suala la usalama, nafasi ya kazi ya watetezi inahitaji angalau kiwango cha chini sana cha ridhaa kwa wahusika wakuu katika eneo hilo – hasa viongozi wa kisiasa na kijeshi na hata makundi yaliyojihami wanaoweza kuathirika na kazi ya watetezi na kuamua kuchukua hatua dhidi yao.

Ridhaa hii inaweza kuwa ya **wazi**, kama vile kibali rasmi kutoka kwa mamlaka, au **iliyo dhahiri bila kutangazwa**, kwa mfano, katika hali ya makundi ya kujihami. Ridhaa itakuwa thabiti zaidi iwapo mhusika atashuhudia faida kadhaa kutoka kwa kazi ya watetezi. Vivyo hivyo, ridhaa itapunguza iwapo mhusika atatambua hasara zinazotokana na ridhaa hiyo. Katika hali hii, kiwango chao cha ridhaa kitategemea hasara ya kisiasa inayotokana na shambulizi dhidi ya watetezi. Masuala haya yanafaa hasa katika makundi pinzani yaliyojihami hasa pale watetezi wanakabiliana na zaidi ya mhusika mmoja aliyejihami. Mhusika mmoja aliyejihami aweza kuichukulia kazi ya watetezi kama yenye manufaa kwa mpinzani wao. Hivyo hasi, kwa mhusika mwingine kuikubali wazi kazi ya watetezi kunaweza kuchangia uhasama kutoka kwa mpinzani wao.

Nafasi ya kazi ya watetezi inaweza kuwakilishwa kwa vipengo viwili:

- Kimoja kikiwakilisha kiwango ambacho mhusika atavumilia au atakubali kazi yako kutokana na kiasi ambacho kazi yenyewe inaathiri malengo yake au mikakati ya maslahi yake (yaani uvumilivu-ukubalifu wa kuendelea).

- Kingine kikiwakilisha kiwango ambacho utaweza kuzuia mashambulizi, kwa sababu ya gharama nyingi za kisiasa, hadi wakati ambapo utaweza kushawishi serikali kuhusu utekelezaji wa haki au hata kuitia tamaa ya kupata faida za kisiasa kwa kuepuka mashambulio au ukiukaji wa haki za binadamu (uzuiaji-ushawishi wa kuendelea).



Upanuzi wa nafasi yako ya kazi unaweza kutimia kadiri muda unavyosonga. Kutimiza ukubalifu wa kazi ya watetezi kupitia kwa mbinu ya ubembelezaji kunafaa kuzingatia mahitaji ya watu, sifa yako, taratibu, ujumuishaji nk, kama inavyowakilishwa katika nafasi "b". Lakini katika maeneo yaliyo na migogoro ya watu waliojihami, kwa kawaida, nafasi huwa finyu tu kwa lile linalotokana na ridhaa ya wahusika waliojihami, lililoibushwa kwa sehemu fulani kutokana na hasara ya kuwashambulia watetezi (uzuiaji), kisha kuipunguza nafasi hadi "a".

Kwa jumla, "b" inaweza kukaliwa na watetezi wasiyoleta utata kuliko kukaliwa na wale wanaokana dhuluma kwa wazi. Labda tu anayeweza kutekeleza dhuluma awe na maadili na pia avutiwe na uzuri wa kazi ya watetezi kwa kiwango cha kuikubali.

### Mkakati wa usalama wa kiulimwengu

- Kuipanua nafasi ya kazi yako kwa kuzidisha uvumilivu na ukubalifu.
- Kuipanua nafasi ya kazi yako: kuzidisha uzuiaji na ubembelezaji.

Kuubainisha na kuufanyia kazi mkakati wa usalama wa kiulimwengu utachangia kuleta hatua zinazochukuliwa za kisiasa dhidi ya watetezi kwa kupunguza kiwango cha uhuru wa kutoadhibiwa wa wale wanaoweza kudhulumu na kuipanua nafasi ya kazi ya watetezi.

Hivyo basi, mkakati wa usalama wa kiulimwengu unategemea sana utetezi.

### Kuipanua nafasi yako ya kazi kwa kuzidisha uvumilivu na ukubalifu

Kazi yako inaweza kuathiri malengo au maslahi ya mtu mwingine asiyejali zaidi kuhusu haki za binadamu, kupelekea kuwepo kwa mazingira hasama ya kufanya kazi kwa watetezi. Ili kupata ukubalifu, au angalau ridhaa, ni muhimu kupunguza makabiliano hadi kiwango cha chini. Baadhi ya mapendekezo ya jinsi ya kufanya hili ni:

- **Toa habari na mafunzo kuhusu hali na uhalali wa kazi ya watetezi.** Watumishi rasmi wa serikali na washikadau wengineo wanaweza kupenda kushirikiana na mtetezi iwapo wanajua na kuelewa kazi yake na sababu za kuifanya. Haitoshi tu kwa Watumishi wakuu wa serikali kuwa na ufahamu wa yale uyafanyayo kwa sababu kazi ya kila siku ya watetezi huhusisha viwango kadhaa vya watumishi rasmi katika serikali tofauti. Unafaa kufanya juhudi ya kila wakati ya kuwapa habari na mafunzo watumishi hao katika viwango vyote.

- **Bainisha malengo ya kazi ya watetezi.** Katika migogoro yote, ni muhimu kubainisha na kuwekea mipaka nafasi na malengo ya kazi yako. Hii itapunguza suitafahamu au makabiliano yasiyofaa yanayoweza kukwamiza juhudi za watetezi wa kuafiki malengo yao.

- **Wekea mipaka malengo yako ya kazi ili yaafikiane na nafasi ya kijamii na kisiasa ya kazi yako.** Kazi ya watetezi itakapoathiri mikakati maalum ya maslahi ya mhusika aliyejihami, mhusika huyo atajibu kwa fujo, bila kutilia maanani sana sifa yake. Baadhi ya kazi nyinginezo huwafanya watetezi waweze kudhuriwa zaidi kuliko wengineo, hivyo basi, hakikisha kwamba malengo yako yanaafikiana na hatari unayoweza kukabiliana nayo pamoja na uwezo wako wa kujilinda kadiri iwezekanavyo.

- **Kuwa na nafasi ya "kuhifadhi cheo chako"katika mikakati yako.** Iwapo hutakuwa na budi ya kuwakabili washikadau kuhusu dhuluma za haki za kibinadamu, basi tafuta mbinu ya kuwaacha wakiwa wanatambua juhudi zako za kuchukua hatua ya kukabiliana na dhuluma kama hizo.

- **Unda miungano mipana na sekta nyingi** za kijamii kadiri iwezekanavyo.

- **Tafuta usawa baina ya uwazi katika kazi yako**, kuonyesha kwamba watetezi halali wa haki za binadamu hawana chochote cha kuficha, na haja ya kuepuka kutoa habari inayoweza kuhatarisha kazi au usalama wako.

- **Mwishowe, kumbuka kwamba uhalali na ubora wa kazi yako** ni kuwepo kwa masharti yafaayo katika kuidumisha nafasi ya kazi yako, japo hilo huenda lisitoshe. Unaweza pia kuwazuia watu wanaoweza kudhulumu (tazama hapa chini).

## Kupanua kazi yako: kuzidisha uzuiaji na ubembelezaji

Watetezi wa haki za binadamu wanaofanya kazi katika mazingira ya uhasama wanafaa kubainisha gharama za kutosha za kisiasa ambazo zitamhofisha mwenye kudhulumu ili asitekeleze uovu dhidi yao. Huu ndio **uzuiaji.**

Ni muhimu kutofautisha baina ya uzuiaji wa "kijumla" na ule wa "papo hapo".

"**Uzuiaji wa kijumla**" unajumuisha athari sawia za juhudi zote za kitaifa na kimataifa za kuwalinda watetezi, yaani chochote kinachosababisha uelewa wa kijumla kwamba hujuma dhidi ya watetezi una matokeo hasi. Hili linaweza kutekelezwa kupitia kampeini za uhamasishaji au mafunzo na habari kuhusu kuwalinda watetezi. Kwa upande mwingine, "**uzuiaji wa papo hapo**" hutoa ujumbe maalum kwa mtekelezaji maalum wa dhuluma kutomhujumu mlengwa mahususi. Uzuiaji wa papo hapo unafaa wakati uzuiaji wa kijumla unaposhindwa au unapoonekana kana kwamba hautatosha, na pale juhudi za kulinda zinapolenga hali maalum.

**Ubembelezaji** ni dhana jumuishi zaidi. Inaweza kufafanuliwa kama matokeo ya matendo ambayo yanamshawishi mpinzani asichukue hatua ya uhasama anayofikiria. Majadiliano ya kirazini, mvuto wa kimaadili, ushirikiano mwingi, ufahamu bora kuhusu ubinadamu,uchachawizwaji,kuidhinisha sera zisizo za uhasama, na uzuiaji, yote haya yaweza kutumika ili kutimiza ubembelezaji. Kila mojawapo wa mbinu hizi hutumiwa na watetezi kwenye viwango vya kitaifa na kimataifa katika nyakati tofauti. Bila shaka, watetezi hawawezi kutumia "matishio" ya moja kwa moja mara nyingi: mkakati huo unahusu zaidi kuwakumbusha wengine kuwa, kutegemea uamuzi wao, matokeo kadhaa **yanaweza** kutokea.

## Kutekeleza uzuiaji

Ili kupima iwapo umekuwa ukitekeleza uzuiaji kwa njia bora zaidi, masharti kadhaa yanapaswa kutimizwa:

1 ♦ **Ni lazima watetezi wambainishe na wawasiliane na mwenye kudhulumu kuhusu aina za hatua zisizokubalika**. Uzuiaji hautatekelezeka iwapo mdhulumu hajui ni matendo gani yatakayochochea kupatikana jibu.

2 ♦ **Shirika la watetezi linapaswa kudhihirisha kujitolea kwake katika kuzuia hujuma kwa njia ambayo itamfanya mdhulumu aifahamu**. Ni sharti pia kwa shirika kuwa na mkakati wa uzuiaji.

3 ♦ **Shirika la watetezi linapaswa kuwa na uwezo wa kutekeleza uzuiaji, na kumfanya mhujumu kufahamu hili**. Ikiwa tishio la kuchochea makabiliano ya kitatifa na kimataifa halitathaminiwa, hakuna sababu ya kutarajia ya kwamba litaleta ulinzi wowote.

4 ♦ **Watetezi wanapaswa kumtambua mwenye kuhujumu.** Mara nyingi, kikosi cha usalama hufanya shughuli zao usiku wa manane na ni nadra sana kwao kudai kwamba wametekeleza jambo fulani. Hilo, basi, hurejelewa kwa kutaka kujua ni nani anayeweza kupata faida ya hujuma. Ili kuimarisha makabiliano ya kitaifa na kimataifa, chukulizi ya "wajibu wa kiserikali", ingawa ni sawa, inahitaji habari zaidi mahsusi kuhusu ni makundi yepi katika serikali yanayoaminika kutekeleza hujuma hiyo.

5 ♦ **Mhujumu anafaa kuwa amepania sana kuhujumu kisha akaamua kutotekeleza hujuma hiyo** kwa sababu hasara zinazotokana na kujitolea kwa watetezi zitakuwa nyingi kuliko faida.

Ni vigumu kwa watetezi kumshawishi mhujumu ambaye atabaki bila kuathiriwa kutokana na uamuzi wa kuzuia: hili hutendeka zerikali zinapokuwa zinaweza kuadhibiwa na jumuiya ya kimafaita, japo jumuiya hiyo haiwezo kuwadhibu wakiukaji hasa wa haki za binadamu. Kwa mfano, majeshi ya kibinafsi yanaweza kuwa hayafikiwi na harakati za serikali au hayana shughuli nayo tu. Katika hali kama hiyo, mhujumu anaweza hata kufaidika kutokana na kuwahujumu watetezi wa haki za binadamu, kwa kuwa hujuma hizo zitaiweka serikali katika hali ngumu na vilevile kuiharibia sifa.

Watetezi hawatawahi kujua mapema iwapo "kujitolea kuzuia" kwao kuna nguvu ya kutosha kuweza kuzuia hujuma inayotaka kutendeka. Mwenye kuhujumu anaweza kutarajia faida ambazo watetezi hawazijui. Kutathmini hali kwa makini iwezekanavyo ni changamoto ya milele na huenda labda isiwezekane kutokana na ukosefu wa habari muhimu. Hivyo basi, mashirika ya watetezi hayana budi kuunda mipango thabiti ya kinyume na inayoweza kubadilishwa na vilevile uwezo wa kukabiliana kwa haraka na matukio yasiyotarajika.

**Jedwali**: kuzuia hujuma ya moja kwa moja - matokeo tofauti ya ulinzi

| Kuzuia hujuma ya moja kwa moja: matokeo tofauti ya ulinzi | |
|---|---|
| 1 ♦ **Mabadiliko katika mwenendo wa mwenye kufanya uovu:** kuwazuia wahujumu kwa kuongeza hasara zinazoweza kuwepo za kuhujumu. → <br><br> 2 ♦ **Mabadiliko katika utii wa washika dau wenye-majukumu na Maazimio ya Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa Haki za Binadamu**:[2] Kuwashawishi wahujumu kwa kuimarisha uwezekano wa utawala kuchukua hatua ya kuwalinda watetezi au kuwaadhibu watekelezaji wa hujuma. → | **Kukabiliana** na kupunguza **matishio** (kwa kukabiliana moja kwa moja na chanzo, au dhidi ya hatua iliyochukuliwa na chanzo). |
| 3 ♦ **Kupunguza uwezekano wa shambulizi.** Kupunguza udhihirikaji nje wa watetezi, kuimarisha mazingira yako ya kazi, kudhibiti vizuri hofu na msongo wa akili, kukuza mipango ya usalama nk. → | Kupunguza **udhaifu**, wa kuweza kudhuriwa, kuimarisha **uwezo.** |

2 Tazama sura 1. Kwa mfano, baada ya mtetezi kukana matishio hadharani, ama mwendesha mashtaka au polisi au shirika jinginelo kufanya uchunguzi wa lile lililotendeka kisha uchunguzi huu ukapelekea kuchukuliwa hatua dhidi ya wale wanaomtishia mtetezi. Angalau hili linaweza kuwa lengo la makabiliano ili kuzuia hujuma.

# Kuandaa Mpango wa Usalama

**Lengo:**

Kujifunza jinsi ya kutengeneza mpango wa usalama

## Kuutengeneza mpango wa usalama

Sasa kwa vile umeshawabainisha washikadau katika ulinzi, umeshachagua vikosi vya kwenda nyanjani, umeshatathmini hatari inayokukabili, umetambua mikakati yako uliyo nayo, na pia kutambulisha mkakati wako wa kilimwengu, isiwe vigumu kutengeneza mpango wa usalama.

Suala la usalama ni changamoto na linajumuisha masiala kadhaa. Ni sharti masiala mengine yawepo. Mengine yaweza kuongezwa baadaye. Kwa pamoja yanaunda mpango wa usalama.

Masiala haya yanapaswa kufanyiwa kazi katika kiwango cha mtu binafsi, shirika au kati ya mashirika.

**Vipi utaendelea? Hapa kuna hatua chache za mchakato huo:**

1 ♦ **Vijenzi vya mpango.** Mpango wa usalama unalenga kupunguza hatari. Hivyo basi, utakuwa na angalau malengo matatu, kutokana na utathmini wako wa hatari:

- Kupunguza kiwango cha hatari inayokukatiza
- Kupunguza udhaifu wako
- Kuimarisha uwezo wako.

Mpango wa usalama unafaa kuhusisha sera za kila siku, hatua za kuchukuliwa na itifaki ili kudhibiti baadhi ya hali fulani.

Sera ya kila siku na hatua za kazi ya kawaida:

- Utetezi wa kudumu, kuunda miungano, taratibu za kimaadili, utamaduni wa usalama, ulinzi wa usalama nk.
- Hatua za kudumu, ili kuhakikisha kwamba kazi ya kila siku inafanywa kulingana na kanuni za usalama.

Itifaki ya hali mahsusi:

- Itifaki za uzuiaji: kwa mfano kwa jinsi ya kuandaa kongamano la vyombo vya habari au ziara ya eneo la mbali.
- Itifaki za kidharura za kukabiliana na matatizo maalum, kama vile kuzuiliwa korokoroni au kutoroka.

Kadiri sera na hatua za kila siku zinavyoendelea kutekelezwa, ndivyo itifaki za hali mahsusi zitakavyozidi kufanya kazi.

**Baadhi ya mifano:**

■ Ikiwa mkusanyiko wa sera na hatua za kudumu kuhusu ulinzi wa habari utatekelezwa, uvamizi wa afisi (wa kidharura) utakuwa na athari ndogo kuliko pale ambapo sera na hatua hazipo.

■ Iwapo mkusanyiko wa sera na hatua za kudumu kuhusu mahusiano ya kijamii utatekelezwa, onyo la mapema lililochochewa na shambulizi dhidi ya mtetezi wa haki za binadamu litaweza kuibua hisia kali kutoka kwa washika dau muhimu, na katika hali hiyo lengo la mtetezi litakuwa likitimia wakati wa shambulizi kutokea. Ili kutimiza malengo ya mtetezi, mpango wa usalama utajumuisha utetezi wa kudumu ulio na washika dau na wenyemajukumu. Mpango huo, utahitaaji sera ya kimaadili ya kudumu inayotekelezwa katika Nyanja zote za kazi ya shirika, na pia katika kiwango cha mtu binafsi/shirika/kati ya mashirika.

■ Iwapo hali ya kuzuiliwa itatokea, kisha mpango wa kudumu uliojumuisha sera ya kimaadili ya watu binafsi uwepo, basi ukiukaji wa sheria ya kawaida wa mtu binafsi hautachukuliwa kama sababu, kisha itifaki ya dharura itaweza kutekelezwa. Bila shaka, uvunjaji wa sheria ya kawaida unaweza kuwa kisingizio, hata hivyo wakili au mwanasheria wa shirika atajua la kufanya. Fauka ya hayo, mtetezi aliyezuiliwa atafahamu kuwa hatua zinachukuliwa na anaweza kujikariria hatua hizi kwa karibu na makataa ya muda uliowekwa kisha"atulie" (athari ya kisaikilojia), akijua kwamba mapambano yameanza. Hakuna haja ya kubishana na wenye mamlaka na kujiweka katika hatari zaidi kuliko ile aliyo nayo (ya kuzuiliwa).

■ Katika hali ya kufanya kazi nyanjani kwenye maeneo hatari, washikadau muhimu na wanaofaa watakuwa wameshapashwa habari awali na watakuwa macho hadi kundi lirejee salama.

2 ♦ **Majukumu na rasilimali za kutekeleza mpango.** Ili kuhakikisha kwamba mpango unatekelezwa harakati za kidesturi za usalama zinafaa kujumuishwa katika shughuli za kila siku za kazi:

- Ongeza tathmini ya mazingira na masiala ya usalama kila siku katika ratiba yako.
- Yasajili na uyachanganue matukio ya usalama.
- Gawa majukumu.
- Gawa rasilimali, yaani wakati na pesa, kwa ajili ya usalama.

3 ♦ **Kuandaa mpango – jinsi ya kuanza.** iwapo ushamaliza kutathmini hatari inayomkabili mtetezi au shirika, unaweza kuwa na orodha ndefu ya udhaifu, aina mbalimbali za matishio na uwezo kadhaa. Kihalisi, huwezi kumaliza kila kitu kwa wakati mmoja. Kwa hivyo utaanzia wapi? Ni rahisi sana:

- **Teua matishio machache**. yape kipaumbele matishio uliyoyaorodhesha, yawe ya hakika au yanayoweza kutokea, na kwa kutumia **mojawapo** wa mbinu hii: **tishio baya zaidi** – matishio ya wazi ya mauaji, kwa mfano: **AU** tishio baya zaidi na linaloweza kutokea – iwapo mashirika yaliyo kama hilo lenu yameshambuliwa, hilo ni tishio la wazi linaloweza kutekelezwa dhidi yako; **AU** tishio linalolingana zaidi na udhaifu wako – kwa sababu umekabiliwa zaidi na hatari kutokana na tishio hilo mahsusi.
- **Orodhesha udhaifu wako ulio nao:** udhaifu huu unafaa kushughulikiwa mwanzo, lakini kumbuka kwamba siyo udhaifu wote unalingana na matishio yote (tazama mfano huu).
- **Uorodheshe uwezo wako ulio nao.**

**Mfano**

wa harakati ya uteuzi itakayopelekea kuundwa kwa mpango wa usalama:

*Kiongozi wa shirika la watetezi wa haki za binadamu (liwe la mjini au mashambani) amepokea matishio mabaya zaidi ya mauaji. Shirika linafanya tathmini ya tishio hilo na kisha kuorodhesha udhaifu na uwezo walo.*

Kwa kuhitimisha, shirika linaamua kutekeleza hatua zifuatazo za usalama: kuziweka kabati zote katika hali ya usalama, kuyafanya madirisha ya afisini yawe thabiti kwa kuyawekea vyuma, kuwanunulia simu mpya za mkononi wanashirika walio katika hatari zaidi na kutangaza hadharani matishio hayo ya mauaji.

**Kwa jumla, hoja hapa ni kuuliza na kudhihirisha wazi namna kila hatua itachangia katika kupunguza hatari mahsusi. (yaani ni kwa namna gani hatua hiyo itapelekeakuongezeka kwa usalama unaohusiana na hatari mahsusi?)**

Kwa hivyo, ni kwa vipi hatua hizi zitapunguza tishio fulani la mauaji dhidi ya kiongozi? (Bila shaka, wanaweza kuhusisha usalama wa kiulimwengu lakini huu si wakati mwafaka kwa hilo).

Jiulize: Kuna uwezekano upi wa tishio la mauaji kutekelezwa afisini ukijua kwamba kuna watu hapo? Je, kiongozi anafaa kuuawa akiwa afisini? Kiongozi huyo aliyetishiwa hatakuwa daima afisini. Kwa hivyo kuna uwezekano mwingineo wa kudhuriwa kama vile unapotoka afisini peke yako usiku sana, au kelekea katika maeneo yasiyo na watu, kupuuza hatua za usalama uwapo nyumbani…

Ingawa kuziweka kabati katika hali ya salama ni muhimu, hakutapunguza tishio na uwezekano wa kudhuriwa kwa kiongozi. Vivyo hivyo hata kwa vyuma vilivyowekwa kwenye madirisha. Wangefanya nini kwa mshambulizi wa siri au kombora?

Ni kwa namna gani simu ya mkononi itapunguza hatari hiyo? (Ni nini hasa kinaweza kufanywa na simu ya mkononi katika kuzuia kumwua kiongozi?)

Lingekuwa ni jambo la manufaa zaidi kupunguza udhihirikaji nje wa kiongozi anaposafiri kutoka nyumbani hadi afisini aukwenye wikendi. Huu ni udhaifu unaoweza kuleta madhara na ambao unapaswa kushughulikiwa mwanzo kwa kuwa unahusiana zaidi na tishio la aina hiyo.

**Ikiwa mchakato wa uteuzi u sawa na wewe unaweza kukabiliana barabara na matishio, udhaifu na uwezo uliobainishwa katika mpango wako wa usalama, kimantiki, unaweza kuwa na hakika kwamba utaweza kupunguza hatari yako mara moja.**

Kumbuka kwamba hii ni mbinu ya malengo maalum ya kuandaa mpango wa usalama. Zipo mbinu "rasmi" nyingi za kufanya hivyo, lakini hii ni ya moja kwa moja na hukufanya wewe kuchukua tahadhari ya haraka kuhusu masuala ya usalama – mradi tu tathmini yako ya hatari ni sawa – na hatimaye utaishia kuwa na mpango "hai" na wa "kihakika": hiyo ndiyo sehemu muhimu ya usalama. (*Tafadhali tazama mwishoni mwa sura hii orodha ya kina ya mfano wa vijenzi vya mpango wa usalama unavyoweza pia kutumia katika utathmini wa hatari zako*).

## Vipengele vinavyoweza kuwekwa katika mpango wa usalama

"Menu" hii inatoa mapendekezo ya kina kwa masiala yatakayojumuishwa katika mpango wa usalama. Baada kukadiria hatari, unaweza kuchagua na kuchanganya fikra hizi ili ukamilishe mpango wako wa usalama.

Mpango wa usalama huhusisha vipengele ambavyo huwa taratibu za kisiasa (kama kukutana na wenye mamlaka na mashirika ya kimataifa ili kudai haki ya ulinzi kutoka kwa serikali) na taratibu za kiutendaji (kama maandalizi ya kila siku ya kazi za nyanjani).

### Vipengele vya sera za kudumu pamoja na hatua kwa kazi ya kawaida:

- Mamlaka ya shirika, makusudio na malengo ya kijumla (kuwajua na kuwaheshimu).
- Kauli ya shirika kuhusu sera ya usalama.
- Usalama unapaswa kufumbatwa katika harakati zote za kila siku za kazi: tathmini ya mazingira, tathmini ya hatari na uchanganuzi wa tukio, na pia tathmini ya usalama.
- Namna ya kuhakikisha kwamba wanashirika wote wamepata mafunzo bora katika usalama kwenye kiwango kifaacho na kwamba majukumu ya watu ya usalama yanapokezwa kwa watu wengine wanapomaliza kazi.
- Kugawa majukumu: Nani anatarajiwa kufanya nini katika hali gani?
- Jinsi ya kushughulikia hatari ya usalama; Kuunda kamati ya kidharura au kundi la kuishughulikia, lipe kundi jukumu la kushughulikia vyombo vya habari, mawasiliano na jamaa nk.
- Majukumu ya usalama ya shirika: kupanga, kufuatilia, kuweka bima, jukumu la kiraia, nk.
- Majukumu ya mtu binafsi ya usalama: kuendelea kupunguza hatari, jinsi ya kutumia vizuri muda wake usio wa shughuli, kuripoti na kusajili

matukio ya usalama, kuwekea vikwazo (baadhi ya hoja hizi zinaweza kujumuishwa katika kandarasi za kazi, inapofaa).

- Sera za shirika kuhusu:
  - Mapumziko, wakati usio na shughuli, na kudhibiti msongo wa akili
  - Usalama wa waathiriwa na mashahidi.
  - Afya na uzuiaji wa ajali.
  - Muunganisho wa mamlaka, vikosi vya usalama na makundi yaliyojihami.
  - Kudhibiti habari na uhifadhi wake, kulinda stakabadhi za na habari za siri.
  - Sifa yako mwenyewe mbele ya amali za kidini, kijamii na kitamaduni.
  - Ulinzi wa usalama katika maofisi, na majumbani (yakiwemo ya wageni).
  - Kulinda pesa taslimu na vitu vinginevyo vya thamani.
  - Mbinu za mawasiliano na itifaki.
  - Kutunza gari.
  - Usalama wa watetezi wa kike.
  - Usalama wa wateezi wa LGBTI.

## Vipengelele vya hatua mahsusi za kazi na hali isiyo ya kawaida

- Itifaki za uzuiaji na utoaji hisia:
  - Kuandaa safari za nyanjani
  - Mabomu ya ardhini
  - Kupunguza hatari ya kujihusisha katika uhalifu wa kawaida, matukio ya kujihami au unajisi.
  - Kupunguza hatari ya kupata ajali unaposafiri au unapokuwa katika maeneo hatari
  - Itifaki za kukabiliana na: dharura za kiafya na kisaikolojia (hata katika nyanja).
  - Kujeruhiwa kwa kibinafsi, mashambulizi, ukiwemo unajisi.
  - Ujambazi
  - Mtu anapokosa kwenda mahali wakati anahitajika.
  - Kukamatwa au uzuiwaji.
  - Utekaji nyara, utorokaji.
  - Moto na ajali nyinginezo.
  - Uhamishwaji.
  - Majanga ya asili
  - Upekuzi wa halali na usio wa halali au uvamizi katika afisi au majumbani.
  - Iwapo mtu atafyatuliwa risasi.
  - Iwapo mtu ameuliwa
  - Katika hali ya mapinduzi ya serikali.

## Kutekeleza mpango wa usalama

Mipango ya usalama ni muhimu, lakini si rahisi kuitekeleza. Utekelezaji ni zaidi ya mchakato wa kiufundi – ni mchakato wa kiuendeshaji. Hii ina maana ya kutafuta mbinu za kutekeleza,fursa zilizopo, pamoja na vizuizi na matatizo.

**Mpango wa usalama unapaswa kutekelezwa katika angalau viwango vitatu:**

1 ♦ Kiwango cha **mtu binafsi**. Kila mtu anapaswa kuufuata mpango ili utekelezeke.

2 ♦ Kiwango cha **shirika**. Shirika kwa jumla linafaa kufuata mpango huo.

3 ♦ Kiwango cha **baina ya mashirika.** Hali fulani ya kushirikiana katika ya mashirika huhusishwa ili kulinda usalama.

### Mifano

ya mbinu na fursa unapoutekeleza mpango wa usalama:

- Matukio kadhaa madogo ya usalama yametendeka katika shirika lenu au jingine na baadhi ya wafanyikazi wameyaogopea.
- Haja ya kijumla ya kutaka kuwepo usalama nchini kutokana na hali iliyopo nchini.
- Mfanyikazi mpya anawasili na anaweza kupewa mafunzo ili awe na matendo ya usalama kwa urahisi.
- Shirika jingine linaamua kuwapa mafunzo ya usalama.

### Mifano

ya matatizo na vizuizi katika utekelezaji wa mpango wa usalama:

- Watu wengine wanafikiri kwamba hatua zaidi za usalama zitapelekea kuwepo kwa kiwango kikubwa cha kazi.
- Wengine hufikiri kwamba tayari shirika lina usalama mzuri na wa kutosha.
- “Hatuna wakati wa jambo hili.”
- “Sawa, basi tutenge muda zaidi wa kujadili suala la usalama siku ya Jumamosi asubuhi, lakini ni hivyo!”
- “Tunapawa kuwalinda vizuri watu tunaopania kuwasaidia, sio sisi wenyewe.”

## Njia za kuimarisha utekelezaji wa mpango wa usalama

- Zipatilize fursa na kukabiliana na matatizo na kuepuka vizuizi.

- Kuendelea hatua kwa hatua. Hakuna haja ya kuchukulia kwamba kila kitu kitafanywa wakati mmoja.

- Sisitiza umuhimu wa usalama kwenye kazi kuu kwa niaba ya waathiriwa. Sisitiza kwamba usalama wa mashahidi na wanafamilia ni muhimu kwa uthabiti wa kazi yenyewe na kwamba hili laweza kusimamiwa vizuri kwa kuhusisha matendo mema ya usalama katika maeneo yote ya kazi. Tumia mifano katika mafunzo/mijadala inayoonyesha athari hasi zinazoweza kutokea za uzembe katika usalama wa mashahidi na waathiriwa.

- Mpango ulioandaliwa na "waatalamu" wawili na kuwasilishwa kwa shirika zima unaweza kuporomoka. Ni **muhimu Kushiriki** katika usalama.

- Mpango unafaa uwe wa kihalisia na unaoweza kutekelezwa. Orodha ndefu ya mambo unayopaswa kufanya kabla ya safari si muhimu. Yafanyie kazi yale machache yanayostahiki ili kuhakikisha kwamba usalama upo. Hii ni sababu nyingine ya kuhusisha wale hasa wanaofanya kazi – kwa mfano, wale waendao katika safari za nyanjani.

- Mpango wa usalama siyo stakabadhi ya kuundwa mara moja tu – ni sharti upitiwe na kuongezewa mambo mapya.

- Mpango huo usionwe kama ni "kazi nyingi", lakini kama "njia bora ya kufanya kazi". Watu wanafaa kuona faida yake, kwa mfano, kujiepusha na kutoa taarifa mara mbili. Kuhakikisha kwamba ripoti za nyanjani zina kipimo fulani cha usalama, yajumuishe masuala ya usalama katika ajenda za mikutano ya kundi, pia yahusishe vipengele vya usalama katika mafunzo mengineyo, nk.

- Sisitiza kwamba suala la usalama siyo hiari ya kibinafsi. Uamuzi wa mtu binafsi, mielekeo na mienendo yake inayoathiri usalama inaweza ikawa na matokeo fulani kwa usalama wa mashahidi, wanafamilia wa waathiriwa na wafanyikazi wenza. Kuna haja za kujitolea kwa pamoja katika kutekeleza matendo mema ya usalama.

- Ni lazima muda na rasilimali zitengwe katika utekelezaji wa mpango huo kwa kuwa usalama hauwezi kuimarishwa kwa kutumia wakati usio wa shughuli wa watu. Ili kuonekana kama jambo "muhimu" shughuli za usalama zafaa zifanywe kwa pamoja na shughuli nyinginezo "muhimu".

- Ni sharti kwa kila mmoja aonekane kwamba anaufuata mpango wa usalama, hasa wasimamizi na wale wanaowajibikia kazi ya watu wengine. Ni lazima yawe matokeo kwa watu binafsi ambao hukataa sana kuuzingatia mpango.

## Muhtasari

Mpango wa usalama unafaa kupunguza uwezekano wa kudhuriwa (udhaifu) na kuzidisha uwezo ili matishio yapungue au yasiweze kutokea na hivyo basi hatari kupunguka.

Mpango wa usalama unafaa kuenda sambamba na mahitaji yako halisi na pia nafasi yako ya kazi.

Hoja siyo kukamilisha nafasi pana ya kijamii –kisiasa, bali ni kufanya kazi katika nafasi inayofaa na kutumia iwezekanavyo kiwango kikubwa cha mazingira ya kazi kupitia uundaji wa miungano kwa kushirikiana na mashirika mengineyo. Tambulisha taratibu za usalama zinazovuka mipaka ya tofauti za kisiasa.

Usalama ni maslahi ya kila mmoja na ni suala la kibinafsi, kishirika na baina ya mashirika.

Usalama ni suala tata na ni zao la masiala kadhaa. Masiala mengine hayana budi kuwepo. Mengine yataongezwa kwa nyakati maalum. Pamoja yanaunda mpango wa usalama.

Mpango wako wa usalama unafaa kujumuisha sera za kila siku, hatua na itifaki ya hali mahsusi.

Yote hujumuisha taratibu za kisiasa na zile za kiutendaji.

# Kuimarisha Usalama Kazini na Nyumbani

**Lengo:**

Kutathmini usalama kazini au nyumbani.

Kupanga, kuimarisha na kukagua usalama katika afisi na nyumbani.

## Usalama kazini na nyumbani

Usalama katika makao makuu ya shirika au afisini na hata nyumbani kwa wafanyikazi ni muhimu zaidi kwa kazi ya watetezi wa haki za binadamu. Kwa hivyo, tutachunguza kwa kina fulani namna usalama wa afisini au nyumbani unaweza kuchanganuliwa na kuimarishwa. (kwa ajili ya wepesi, tutarejelea *"afisi" tu kuanzia hapa, ingawa maelezo ya hapa chini yaweza kutumiwa katika usalama wa nyumbani*).

## Vipengele vya kijumla vya usalama wa afisini

Lengo letu katika kuimarisha usalama linaweza kufupishwa kwa maneno haya machache: **kuzuia uingiaji** uliokatazwa. Huu ni ukweli hata kama afisi yenu iko mashambani au mjini. Katika hali nadra sana, itaweza pia kuwa muhimu kulinda afisi dhidi ya shambulizi linaloweza kutokea (ulipuaji kwa mfano). Hili linatupelekea katika uzingatio wetu wa kwanza na wa kijumla – udhaifu wa afisini. Udhaifu huu unaongeza hatari, kutegemea tishio linalokukabili. Kwa mfano, iwapo unakabiliwa na hatari ya mtu kuiba vyombo au hata habari fulani, ni lazima uondee udhaifu wako ipasavyo. King'ora cha usiku (cha umeme, iwapo umeme unapatikana, au mlinzi wa usiku au hata mbwa) ni cha manufaa machache iwapo hakuna yeyote atakayekuja kukagua ikiwa kumetokea jambo. Katika hali nyingineyo, ikiwa kulikuwa na uvamizi wa fujo wakati wa mchana, nguzo za izio zilizoundwa madhubuti au king'ora havitasaidia sana. Kwa ufupi, chukua hatua kulingana namatishio yanayokukabili na pia mazingira unamofanyia kazi.

**Udhaifu wa afisi unafaa kutathminiwa kulingana na matishio yanayokukabili.**

Hata hivyo, ni muhimu kusawazisha kati ya kuchukua hatua zifaazo za usalama na kujenga dhana kwa watu walio nje kwamba kuna kitu “kinichofichwa” au “kinacholindwa”, kwa sababu hili pekee linaweza kukuweka katika hatari. Kuhusu usalama wa afisini, unafaa kuchagua baina ya kukaa pembeni/kunyamaza au kuchukua hatua za kawaida inapohitajika. Kwa upande mwingine, mwenye kuweza kuhujumu atajua kwamba afisi yenu ina vitu vya thamani au habari tata na kwamba “mnahitaji” kuilinda.

**Usalama wa ndani ya afisi si muhimu kuliko kiingilio chake.**

Iwapo watu wanataka kuingia ndani bila ya wewe kujua, hawatachagua mahali pagumu pa kuingilia. Kumbuka kwamba,wakati mwingine,njia rahisi zaidi ya kuingia afisini na kuchunguza kinachoendelea ndani ni kama tu kugonga mlango na kuingia.

## Mahali palipo na afisi

Iwe mashambani au mjini, mambo ya kuzingatia unapotaka kujenga afisi ni: ujirani; iwapo jengo hilo la afisi lina uhusiano wowote wa kizamani na watu fulani au harakati mahsusi; kuweza kufikiwa na vyombo vya usafiri wa umma au vya kibinafsi; hatari za ajali; ni vipi jengo linafaa katika uchukuaji wa hatua za usalama nk (pia tazama hapa chini kwa hatari ya tathmini ya mahali)

Ni muhimu kuchunguza kwamba ni hatua gani za usalama zinachukuliwa na watu wengine katika maeneo jirani. Ikiwa zipo nyingi, basi hii ni dalili kwamba mahali hapo si salama, kwa mfano, katika hali ya uhalifu wa kawaida. Ni muhimu pia kuzungumza na watu wa eneo hilo kuhusu hali iliyopo ya usalama. Katika hali yoyote ile hakikisha kwamba hatua za usalama zinaweza kuchukuliwa bila kuvutia makini isiyofaa ya watu. Ni aula pia kuwafahamu wenyeji wa maeneo hayo kwa kuwa wanaweza kudokeza habari muhimu kuhusu chochote kinachotendeka kwenye maeneo jirani.

Ni vizuri pia kuwajua wamiliki wa sehemu ya kujenga afisi. Wana hadhi gani? Je, wanaweza kupata shinikizo kutoka kwa uongozi? Je, wataridhika iwapo utaweka mikakati ya usalama mahali hapo?

Ni uamuzi wa afisi kuchagua ni nani anafaa kuingia afisini. Afisi ambayo waathiriwa wanakuja kupata ushauri wa kisheria itakuwa na masharti tofauti kuliko afisi ya kawaida ya wafanyikazi kuingia. Ni muhimu pia kuzingatia wepesi ambao utakuwa nao wa kufika afisini kwa kutumia usafiri wa umma. Je, kutatokea hali zisizo za usalama kati ya hapo na mahali wanakoishi wafanyikazi/maeneo ambayo kuna harakati nyingi nk. Maeneo jirani yanafaa kufanyiwa tathmini, hasa ili kuepuka kusafiri katika maeneo yasiyo salama.

Katika hali nyinginezo, afisi inaweza kuwa makao ya mtetezi (tazama maeneo ya mashambani hapa chini). Mazingatio yaliyotajwa hapo juu yafaa kupewa uzito.

Mahali pa kujenga patakapoteuliwa, ni muhimu kufanya tathmini ya baada ya kipindi fulani ya vipengele vilivyotumiwa kuteua eneo hilo na ambavyo pia vinaweza kutofautiana, kwa mfano, iwapo “chochote kisichohitajika” kitaingia katika eneo jirani

| Orodha ya kuchagua mahali pa kujenga afisi bora katika maeneo yaliyohifadhiwa | |
|---|---|
| Ujirani | Takwimu za uhalifu; ukaribu na walengwa wa mashambulizi ya watu waliojihami kama vile vituo vya kijeshi au kiserikali; maeneo salama ya kujificha; mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa mlio na uhusiano nayo. |
| Mahusiano | Aina ya watu katika maeneo jirani; mmiliki, wapangaji wa awali; matumizi ya awali ya jengo hili. |
| Kufikiwa | Njia moja au kadhaa nzuri za kupafikia afisini (ni bora zikiwa nyingi. Lakini kumbuka kwamba yule asiyefaa kuingia katika maeneo hayo atakuwa na hiari nyingi), kupafikia hapo kwa usafiri wa umma na ule wa kibinafsi. |
| Huduma za kimsingi | Maji na umeme, simu. |
| Taa za barabarani | Katika maeneo jirani. |
| Uwezekano wa kupata ajali au hatari za kiasili | Moto, mafuriko mengi, mporomoko wa ardhi, kutupa vitu vyenye hatari kubwa, viwanda vinavyotoa sumu nk. |
| Muundo wa nje | Ubora wa vitumizi vya ujenzi, chombo cha kuwekea vifaa vya usalama, milango na madirisha, uzingo na vizuizi vya usalama, maeneo ya kuingilia nk. |
| Kwa magari | Gereji au angalau sehemu fiche, iliyo na kizuizi cha kuegesha magari. |

Iwapo afisi imewekwa mahali palipojitenga, mbali au palipo na hatari fulani, tokeo la orodha linaweza kuonyesha kwamba vipengele vingi havipo katika sehemu hiyo. Uwezo utafaa kutayarishwa ili kufidia udhaifu fulani. Kwa mfano, iwapo hakuna mashirika mengine yoyote hapo, unaweza kuamua kutaka msaada wa wenyeji wa hapo. Au, iwapo hakuna maji yanayotiririka au kuzima moto; hakikisha una hifadhi kubwa iliyojaa maji kila mara.

## Kuingia afisini kwa mtu mwingine: vizuizi vya nje na taratibu za kupokea wageni

Sasa unajua kwamba lengo la kimsingi la usalama wa afisi ni kuwazuia watu wasioruhusiwa kuingia. Mtu au watu kadhaa waweza kuingia kwa nia ya kuiba, kupata habari fulani, kuwacha kitu kinachoweza kutumiwa dhidi yenu baadaye, kama vile mihadarati au silaha, kukutishia nk. Hali zote hutofautiana, lakini lengo linasalia kuwa sawa: Epukana na hali hii.

Kuingia katika jengo kunazuiwa na vizuizi vya nje (ua, milango, malango), kupitia kwa hatua za kiufundi (kama vile ving'ora vinavyomweka) na taratibu za kumpokea mgeni. Kila kizuizi na utaratibu ni kichungi ambacho yeyote anayetaka kuingia afisini hana budi kupitia. Kikamilifu, vichungi hivi vinafaa kuwekwa pamoja ili kuunda safu kadhaa za ulinzi, zinazoweza kuzuia watu wengi wasioruhusiwa kuingia.

## Vizuizi vya nje

Vizuizi hutumiwa kuzuia yeyote au chochote kilicho nje na ambacho hakiruhusiwi kuingia. Umuhimu wa vizuizi hivi hutegemea **uthabiti** na uwezo wavyo wa kujaza **mapengo yote ya udhaifu** kwenye ukuta.

Afisi yenu yaweza kuwa na vizuizi vya nje kwa maeneo matatu:

1 ♦ Mzingo wa **nje**: Ua, kuta au kama hizo, mbali na bustani au uga. Iwapo mzingo wa nje haupo, unaweza ukajenga mipaka unapuzi wa mzingo wa nje ambao utaweza kuudhibiti.

2 ♦ Mzingo wa **jengo au majumba**.

3 ♦ Mzingo wa **ndani**: vizuizi vinavyoweza kuundwa katika afisi ili kulinda chumba au vyumba kadhaa.Huu ni muhimu hasa katika afisi zinazopitiwa na wageni wengi, kwa kuwa unatenganisha sehemu ya makutano ya watu wa nje na yale ya kibinafsi na ambayo inaweza kulindwa kwa vizuizi vinginevyo.

### Mzingo wa nje

Afisi inafaa kuzingirwa na mzingo wa nje ulio wazi, ikiwezekana uwe na ua wa juu au chini, na bora zaidi uwe thabiti na ulio mrefu ili pawe na ugumu zaidi kwa yeyote kuingia. Nguzo za uzio wa waya wa wavu utafanya kazi ya shirika ionekane wazi zaidi, na hivyo basi ni bora kujengea matofali au chochote kama hicho.

Iwapo mzingo wa ua wa nje ulio wazi utakosekana, unaweza kuamua kiwango cha upanuzi wa nje unaoweza kuudhibiti kwa kuangalia ili kitu/mtu yeyote asiyeruhusiwa kuingia asikaribie afisi yenu. Waweza kuamua kutumia vioo vinavyobinukia nje.

### Mzingo wa jengo au majumba

Hii itahusisha kuta, milango, madirisha na dari au paa. Ikiwa kuta ni thabiti, milango yote na hata paa itakuwa thabiti. Milango na madirisha vyapaswa kuwa na makufuli ya kutosha na pia yafanywe madhubuti kwa kutumia vyuma, hasa kwa mitaimbo ya mlalo wa wima iliyotiwa vizuri ukutani. Paa linafaa kuwa na ulinzi mzuri – sio tu bati jepesi au safu ya magae. Iwapo paa haliwezi kufanywa madhubuti, jaribu kuzuia uwezekano wowote wa kulifikia kutokea chini au kupitia kwa majengo jirani.

Iwapo dirisha la afisi yenu linakaa mkabala na barabara au eneo la wazi, liweke dawati lako kwa namna kwamba unaweza kuona nje lakini huwezi kuonwa ukiwa ndani. Ikiwa litakaa mkabala na kichaka, hakikisha kwamba hakuna yeyote anayeweza kujificha nyuma bila kuonwa.

Baadhi ya afisi zaweza kuwa na milango mingi na hivyo basi mlango mmoja unaweza kutumika kama "mlango wa kutoka kwa dharura". Kumbuka mlango wa kutoka kwa dharura unaweza kutumiwa kama sehemu ya kuingilia kwa watu wasioruhusiwa.

Katika mahali palipo na hatari ya kuvamiwa kivita,ni muhimu kutambulisha maeneo yaliyo salama ndani ya afisi (tazama katika mwongozo huu, sura inayoeleza kuhusu usalama katika maeneo ya kivita).

## Mzingo wa ndani

Hali kama ile ya mzingo wa jengo na majumba inatumiwa pia hapa. Ni muhimu zaidi kuwa na sehemu iliyo na usalama wa ziada ndani ya afisi, na hili ni rahisi sana kuandaa. Hata kisanduku cha usalama kinaweza kuchukuliwa kama mzingo wa ndani wa usalama.

Afisi yenu inaweza kuwa ya chumba kimoja pekee na katika hali hiyo, unaweza kutumia vioo vya kusongasonga/vigawanyiko ili kulinda usiri wa ndani dhidi ya mgeni anayeweza kutazama.

## Mambo muhimu kuhusu funguo

- Funguo zozote zisionekane au zisipatikane kwa wageni. Zihifadhi kabatini au kwenye droo iliyo na kufuli ambalo ni watu wachache katika kundi ndio wanaofahamu nambari za siri… hakikisha kwamba nambari za siri zinabadilishwa wakati mwingi kwa ajili ya kuimarisha usalama.
- Iwapo ufunguo binafsi umewekwa alama yake, basi usiweke alama kama hizo kwenye mlango,kabati au droo,kwa kuwa hili litarahisisha kutokea kwa uvamizi. Tumia nambari, herufi au rangi ya siri badala yake.

## Hatua za kiufundi: Taa na ving'ora

(Iwapo afisi yenu ina huduma ya umeme au imewekewa mtambo wa jenerata).

Hatua za kiufundi huimarisha vizuizi vya nje au taratibu za kumpokea mgeni (kama mashimo ya kuchungulia, mawasiliano ya ndani na kamera za video. Tazama hapa chini). Hii ni kwa sababu **hatua za kiufundi ni muhimu tu zinapochochewa ili kuwazuia wadukizi**. Ili ufanye kazi, hatua ya kiufundi inafaa kuchochea hisia fulani, kwa mfano, kuvuta makini ya majirani, polisi au kampuni ya kibinafsi ya usalama. Ikiwa hili halitatendeka, na mdukizi anajua kwamba halitatendeka basi hatua kama hizo zitakuwa na manufaa machache na zitatumiwa tu kuzuia wizi mdogo au kutumiwa kuwahesabu watu wanaoingia.

- **Taa** ni muhimu kwenye maeneo yanayolizingira jengo (ugani, bustanini au njiani) na maeneo ya utuaji.
- **Ving'ora** vina majukumu kadhaa, kama vile kuwapeleleza wadukizi na pia kuwazuia wanaoweza kuingia au wanaoendelea kujaribu kuingia.

King'ora kinaweza kuamsha sauti ya kuonya ndani ya afisi; taa ya usalama; sauti ya juu, kengele au kelele; au kutoa sauti ya kuashiria hali ya hatari kule nje. King'ora cha kusikika ni muhimu kwa kuvuta makini lakini pia kinaweza kuwa na matokeo hasi katika hali ya migogoro au iwapo hutarajii kwamba wenyeji au watu wengine watakuwa na hisia fulani dhidi yacho. Uchaguzi bora unapaswa kufanywa baina ya king'ora cha sauti na kile cha taa (taa yenye mwangaza mzuri, na taa ya rangi nyekundu inayomweka). Taa kama hii inaweza kutosheleza kumzuia mdukizi, kwa kuwa inaleta dhana kwamba kuna jambo lingine litakalotendeka kutokana na upelelezi wa mwanzo.

Ving'ora vinapaswa kuwekwa kwenye maeneo kama vile viwanjani/ugani, milangoni na madirishani. Ving'ora vile vya moja kwa moja aghalabu huwa ni vya kugundua **mwendo wowote**, na ambavyo huchochea kuwaka kwa taa, kutoa kelele au huchochea kuwaka kwa kamera pindi tu kunapokuwa na usogevu fulani.

- Vong'ora vinapaswa:
  - Viwe na betri, ili vifanye kazi kunapokosekana umeme.
  - Viweze kutaahiri kidogo kabla ya kuchochewa vifanye kazi ili pia viweze kuzimwa bila ya kujua na mfanyikazi yeyote.
  - Vijumuishe chaguo la kuashwa kwa kutumia nguvu iwapo mfanyikazi yeyote ataamua kufanya hivyo.
  - Viweze kuwekwa na kudumishwa kwa urahisi.
  - Viweze kutofautishwa kwa urahisi.

### Kamera za video

Hizi zaweza kuchangia katika uimarishaji wa taratibu za kuingia (tazama chini) au kuandikisha watu wanaoingia afisini. Hata hivyo uandikishaji unapaswa kufanywa mahali ambapo mdukizi hawezi kupafikia, la si hivyo anaweza kuivunja na kuifungua kamera na kuharibu ukanda.

Unapaswa vilevile kuzingatia iwapo kamera zitawaogofya watu unaotaka waje wakutembelee, kama vile waathiriwa au mashahidi, au iwapo watachukuliwa kama kitu cha thamani kitakachowavutia wezi. Ni vizuri kuweka ilani ya onyo unapotumia kamera (haki ya kuhifadhi siri pia ni haki ya binadamu).

### Uashaji taa na ving'ora iwapo afisi yenu haina huduma ya umeme au haijawekewa mtambo wa jenereta.

- Epuka kukaa afisini mwako kunapokuwa na giza.
- Badala ya king'ora cha umeme, mfumo mwingineo wa utoaji kamsa unaweza kutumiwa: mlinzi wa usiku, majirani, mbwa; jaribu kuwatumia na utaona natija yao.

### Kampuni za kibinafsi za usalama

Kitengo hiki kinahitaji uangalifu mkubwa. Katika nchi nyingi, kampuni zinazotoa huduma ya usalama huajiri vikosi vya walinda usalama waliostaafu. Kuna ushahidi wa kimaandishi wa watu kama hao wanaojihusisha na upelelezi na hata kuwashambulia watetezi wa haki za binadamu. Hivyo basi ni jambo la kimantiki kutoziamini kampuni zinazotoa huduma ya usalama iwapo una sababu ya kuhofia upelelezi au mashambulizi kutoka kwa vikosi vya usalama. Iwapo kampuni inayotoa huduma ya usalama inaweza kufikia afisi zenu, basi vikosi hivyo vinaweza kuweka vipaaza sauti hapo au kuruhusu watu wengine kuingia.

Unapohisi kwamba unahitaji kupata huduma ya kampuni ya usalama, hakikisha kwamba umetayarisha mkataba wa wazi kabisa, kuhusu ni nini vikosi vyake

vinaruhusiwa kufanya, ni yepi hawaruhusiwi kufanya kwa niaba yako, na ni maeneo yepi ya afisi wanaweza kuyafikia. Bila shaka, nawe pia unafaa kuweza kuthibitisha kwamba makubaliano haya yanatimizwa.

**Mfano:**

> *Iwapo umechukua huduma ya usalama ambapo mlinzi ataweza kutumwa iwapo king'ora kitalia, huyu mlinzi anaweza kwenda katika maeneo muhimu ya afisi yenu na anaweza kuchomeka vifaa fulani vya kusikilia katika jumba la mikutano.*

Ni vizuri mkikubaliana (na ikiwezekana mkague) mfanyikazi/mhudumu wa usalama atakayewatumikia japo hili hutokea kwa nadra.

Iwapo walinzi wa usalama hubeba silaha ni muhimu kwa shirika la kutetea haki za binadamu kuwa na ufahamu wa wazi kuhusu kanuni zao za kutumia silaha. Lakini ni muhimu zaidi kukadiria faida zinazoweza kupatikana kwa kutumia silaha dhidi yao. Bunduki za mkononi haziwezi kutumiwa kukabiliana na washambulizi walio na zana za hali ya juu za vita (kama ilivyo kawaida), lakini iwapo washambulizi watagundua kwamba kuna watu walio na silaha ndogo katika afisi zenu, wanaweza kuamua kuzivamia kwa nguvu huku wakitumia silaha zao kujilinda. Yaani, uwezo fulani wa kujihami (silaha ndogo) utaweza kuwachochea washambulizi kutumia silaha zao madhubuti. Kufikia hapa unafaa kujiuliza ikiwa unahitaji walinzi walio na bastola za rashasha, je una nafasi gani ya chini ya kijamii na kisiasa ya kufanya shughuli zako?.

## Vichujio vya taratibu za kuidhinisha kuingia

Vizuizi vya nje vinafaa viwe na **utaratibu wa kuidhinisha kuingia** "vichujio". Taratibu kama hizo huamua ni lini, vipi na nani anayeingia katika sehemu yoyote ya afisi. Kuyafikia maeneo yaliyosheheni vitu muhimu kama vile funguo, habari na pesa, kunafaa kuwekwa vizuizi.

Njia rahisi ya kuingia ambamo watetezi wa haki za binadamu wanafanyia kazi ni kubisha mlango kisha ukaingia ndani. Watu wengi hufanya hivi kila siku. Ili kuoanisha utaratibu kama huu wa afisi ya watetezi na haja ya kuwachuja watu wanaoitembelea afisi na kwa lengo gani, unapaswa kuunda taratibu na mikakati ifaayo ya kuwaruhusu ndani.

Kwa jumla, watu wana sababu maalum ya kutaka kubisha mlango wenu. Aghalabu hutaka kuuliza swali au kuacha mzigo fulani, bila ya haja ya kuomba ruhusa kwanza. Hebu tuangalie hali kama hii:

## Mtu anapiga simu na kuomba ruhusa ya kuingia kwa lengo fulani.

Unapaswa kufuata hatua tatu rahisi:

1 ♦ **Mwambie ajitambulishe na atoe sababu ya kuja/ziara yake.** Iwapo angependa kumwona mtu afisini, shauriana naye (aliyekuja kuonwa). Ikiwa hayupo, mwambie mgeni arejee wakati mwingine au asubiri mahali popote nje ya afisi. Ni muhimu kuangalia kwa nje kwa kutumia matundu ya ukutani,

kamera au simu zinazokuwa langoni kuepuka kufungua au kuusogelea mlango, hasa unapotaka kumkanya mtu kuingia au ikiwa kuna mtu/watu wanaotaka kuingia kwa lazima. Ni vizuri hivyo basi kuwa na eneo la kusubiria ambalo liko mbali kidogo na lango la kuingia ndani ya afisi. Iwapo ni muhimu kuwa na eneo ambalo watu wanaweza kulifikia kwa urahisi, basi hakikisha kwamba kuna vizuizi vya wazi vinavyozuia watu kuingia katika maeneo ya afisi yaliyokatazwa. Mtu aweza kuomba ruhusa ya kuingia ili kukagua au kurekebisha ugavi wa maji au umeme au kufanya kazi nyinginezo za ukarabati. Anaweza pia kudai kwamba yeye ni mwanahabari au mhudumu wa serikali, nk. Daima hakikisha kwamba wamejitambulisha na kampuni au shirika wanalodai kuliwakilisha kabla ya kuwaruhusu kuingia. Kumbuka kwamba sare ya kazi na kitambulisho haviwezi kutumiwa kama vigezo bora vya kujitambulisha, hasa katika hali ya wastani au ya juu ya hatari.

2 ♦ **Amua iwapo utawaruhusu au hutawaruhusu kuingia.** Baada ya utambulisho na sababu ya wageni wako kukutembelea kubainishwa, utafaa kuamua iwapo utawaruhusu kuingia ndani au la. Kwa sababu tu kwamba mtu ametoa sababu yoyote ya kutaka kuingia haitoshi kumruhusu ndani. Iwapo huna uhakika wa lengo lao, usiwaruhusu kuingia.

3 ♦ **Wasimamie wageni hadi watakapoondoka.** Mgeni anapoingia afisini, hakikisha kwamba kuna mtu anayemsimamia wakati wote hadi atakapoondoka. Ni vizuri kutenga sehemu ya kukutana na wageni, mbali na maeneo yaliyokatazwa kuingiwa. Ni sharti pawe na rekodi ya kila mgeni anayeingia, yaani jina lake, shirika analofanyia kazi, lengo la ziara, watu aliokutana nao, wakati alipowasili na alipoondoka. Hili ni linaweza kuwa na manufaa hasa unaporejelea kutaka kujua kilichotokea baada ya tukio lililotokea.

### Mtu anawasili au anapiga simu akiuliza maswali.

Bila kujali anachoweza kusema mgeni au mpiga simu, hufai kabisa kumwambia anakokaa mfanyikazi mwenza au watu wengine waliokaribu, na pia hufai kumpa maelezo yoyote ya kibinafsi ya mtu. Iwapo mgeni/mpiga simu anasisitiza, basi mwambie aache ujumbe, apige simu au aje baadaye au aandae miadi na yule anayetaka kumwona.

Watu wanaweza kujipata mahali wakiwa wanauliza ikiwa mtu fulani anaishi pale au kitu chochote kinauzwa hapo, nk pasina kuwa na ufahamu wa hali hiyo. Kuna wengine pia wanaotaka kuuza vitu au pia waombaji wanaokuja kutaka usaidizi. Ukiwakataza watu kama hawa kuingia au kuwapa habari fulani basi utakuwa umekwepa hatari yoyote dhidi ya usalama.

### Kuna mtu anayetaka kuwasilisha kitu au kifurushi.

Hatari unayokabiliwa nayo hapa ni kwamba vilivyomo ndani ya kifurushi vinaweza kukuletea janga au kukudhuru, hasa iwapo kifurushi hicho ni cha barua yenye bomu. Haijalishi kwamba kifurushi hicho kinaweza kuwa hakina madhara,bali usikiguse hadi uchukue hatua tatu sahili:

1 ♦ **Bainisha iwapo mpokezi wa kifurushi hicho anakitarajia.** Haitshi tu kwamba mpokezi anamfahamu mwenye kutuma mzigo kwa sababu utambulisho wa mtumaji unaweza kuwa ghushi. Ikiwa mpokeaji

mtarajiwa hatarajii kifurushi chochote, basi hana budi kuhakikisha kwamba aliyemtumia kifurushi hicho alifanya hivyo kikahika. Ikiwa mzigo huo umelengewa afisi yenu, basi bainisheni aliyetuma. Ngojeni na mjadilianeni kuhusu suala hilo kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho.

2 ♦ **Amua iwapo utakubuali kuchukua kifurushi au la.** Iwapo huwezi kubainisha aliyetuma kifurushi, au ikiwa kadhia hii itachukua muda, chaguo bora ni kuacha kuchukua kifurushi hicho, hasa katika mazingira ya hatari wastani au ya juu. Unaweza kutaka kiwasilishwe baadaye au ukakichukua katika kituo cha kutuma barua.

3 ♦ **Tambua mahali kilipowekwa/kinapopelekwa kifurushi hicho.** Hakikisha kila wakati kwamba unajua mahali kilipowekwa kifurushi hicho, hadi mpokezi atakapokubali kukichukua.

Katika nchi nyingine, kifurushi hutangazwa kwa simu na ni mtetezi anayepaswa kukichukua. Inaweza kuwa hila ya kumvutia mtetezi na hatimaye kumhujumu. Kwa sababu simu inaweza kuwa haijasajiliwa, ni vigumu zaidi kumtia nguvuni mpigaji. Mtetezi atakapomaliza kupeleleza kulikotoka kifurushi, anaweza kuchunguza maelezo yake pamoja na mtumaji na kumuuliza kuhusu njia iliyotumiwa kutuma kifurushi hicho. Mpigaji simu aweza pia kuitwa afisini na kisha taratibu za hapo juu zikafuatwa kwa ajili yake. Inawezekana kwamba ikiwa ilikuwa hila, mpigaji simu hatakifa katika afisi.

## Wakati wa shughuli au sherehe.

Katika hali hizi, sheria ni rahisi. Usimruhusu yeyote usiyemjua kuingia. Watu wanaojulikana tu kwa wafanyikazi wenza waaminifu wanaweza kuingia, na iwapo tu mfanyikazi mwenza huyo yupo na anaweza kumtambua mgeni wake. Ikiwa mtu atajitokeza kwa madai kwamba anamfahamu mtu fulani afisini, basi ikague habari kamili ya mtu huyo anayezungumziwa na iwapo hayupo, usimruhusu mgeni kuingia.

Watetezi wanaweza kutaahiri na kuona ugumu wa kumchunguza mgeni na pia kumfukuza. Hata hivyo, hawahitaji kufanya hilo wao binafsi. Wanaweza tu kusema kwamba hawaruhusiwi kumruhusu mgeni ndani.

Pia, kwa taratibu zote za kumruhusu mgeni ndani, kumbuka kwamba iwapo mgeni ana sababu inayokubalika kuingia, basi atafurahia hatua zote za usalama zinazochukuliwa na shirika hilo na iwapo si mgeni halali, atafahamu kwamba watetezi nao pia wanatekeleza taratibu za usalama. Kwa hivyo, katika hali yoyote, watetezi wanaweza kujipa mamlaka ya kuwakataza wageni wasiotambulika kuingia. Kama itasaidia, wanaweza kutumia kauli ya "hapana na … siruhusiwi kuwaruhusu wageni wasiotambulika kuingia, hata hivyo, ikiwa utapendelea kuwacha kadi yako ya ziara, nitafurahi kukutaarifu kuhusu hafla za baadaye tunazoweza kuandaa".

## Kuhifadhi orodha ya wageni na simu zilizopigwa.

Inaweza pia kuwa muhimu kuhifadhi rekodi ya simu zilizopigwa, nambari za simu na wageni waliokuja (katika mashirika mengine, wageni wapya huombwa kuonyesha stakabadhi za kujitambulisha na kisha shirika kusajili nambari ya stakabadhi hiyo).

## Kufanya kazi afisini kwa masaa ya ziada.

Kunapaswa kuwepo taratibu za wafanyikazi kufanya kazi kwa masaa ya ziada. Wanachama wa shirika fulani wanaotaka kufanya kazi kwa masaa ya ziada, yaani masaa ya kuchelewa ya usiku wanahitaji kuwasili kazini katika saa fulani pamoja na mwanachama mwingine aliyeteuliwa na pia wachukue tahadhari maalum wanapotoka kazini.

| ORODHA YA KUKAGULIWA: KUTAMBULISHA MAENEO DHAIFU KATIKA TARATIBU ZA KURUHUSU WAGENI KUINGIA |
|---|
| ♦ **Nani** huenda maeneo **yepi** kila wakati na **kwa nini**? Zuia watu kuenda katika maeneo hayo ila iwapo kuna dharura zaidi. |
| ♦ Tofautisha baina ya **aina** tofauti za wageni (tarishi, wafanyikazi wa kukarabati, wataalamu wa kompyuta, wanachama wa mashirika yasiyo ya serikali waliokuja kwa ajili ya mikutano, wageni muhimu zaidi, wageni wa kawaida na hafla, nk) **kisha andaa taratibu za kila mmoja za kuwaruhusu kuingia ndani**. Wafanyikazi wote wanafaa kuwa na ufahamu wa taratibu zote za kufuatwa kwa aina zote za wageni, na kisha wachukue jukumu la kuzitekeleza. |
| ♦ Mgeni anapoingia afisini, je, anaweza kuyafikia maeneo dhaifu? Una mikakati ya kuzuia hili. |
| **ORODHA YA KUKAGULIA: KUZIFIKIA FUNGUO** |
| ♦ Ni **nani** anayeweza kuzifikia funguo **gani** na **lini**? . |
| ♦ Ni wapi na vipi **funguo** hizo na nakala yazo **zinawekwa**? |
| ♦ Je, kuna rekodi ya nakala za funguo zinazosambazwa? |
| ♦ Je, kuna hatari kwamba mtu aweza kutengeneza **nakala ya ufunguo kiharamu?** |
| ♦ Ni nini hutokea **mtu anapopoteza ufunguo**? Kufuli la ufunguo huo lafaa kubadilishwa, ila labda uwe na uhakika tosha kwamba ufunguo umepotea kiajali na kwamba hakuna yeyote anayeweza kutambua mwenyewe au anwani yako. Kumbuka kwamba ufunguo unaweza kuibiwa kwa mfano, katika hali ya ujambazi uliopangwa ili mtu aweze kuingia afisini. |

Wafanyikazi wana jukumu la kuchukua hatua dhidi ya mtu yeyote asiyezingati taratibu za kuruhusu ndani wageni. Wanapaswa pia kunakili mizunguko ya watu au magari wanayoshuku katika kitabu cha matukio. Vivyo hivyo kwa kitu chochote kilichowekwa nje ya jengo la afisi, ili kuondoa shaka ya hatari yoyote ya bomu linaloweza kutokea. Ukishuku kwamba ni bomu, usilipuuze, **usiliguse**, bali wasiliana na polisi kwanza. Mnapohamia kwingine, au iwapo funguo zimeibiwa au zimepotea, ni muhimu angaa kubadilisha makufuli yote ya eneo la kuingilia.

## Orodha ya kukagua taratibu za kijumla za usalama wa afisi

- Andaa vizima moto na taa za mmuliko (zinazoweza kubadilishwa betri). Hakikisha kwamba wafanyikazi wote wana ujuzi wa kuzitumia.
- Hakikisha kuwa jenereta ya umeme ipo hasa kama una hakika kwamba umeme utakatwa. Ukosefu wa umeme unaweza kuhatarisha usalama (taa, ving’ora, simu nk) hasa katika maeneo ya mashambani.

- Weka orodha ya nambari za dharura za polisi za maeneo hayo, wazima moto, gari la wagonjwa, hospitali jirani kwa ajili ya dharura yoyote nk.
- Iwapo kuna hatari ya kutokea mgogoro hapo karibu, weka hifadhi ya chakula na maji.
- Tambua maeneo yaliyo ya usalama nje ya afisi kwa ajili ya dharura yoyote (kwa mfano, afisi za mashirika mengineyo).
- Kusiwe na yeyote kutoka nje ya shirika atakayeachwa **pekee yake** katika eneo hafifu na uwezo wa kuzifikia funguo, habari yoyote au vitu vya thamani.
- **Funguo**: usiwahi kuacha funguo mahali ambapo wageni wanaweza kuzifikia. Usiwahi "kuzificha" nje ya sehemu ya kuingilia afisini – hili litazifanya zionwe, wala si kwamba zimefichwa.
- **Taratibu za kuruhusu kuingia**: vizuizi vya usalama havitoi ulinzi wowote iwapo mhalifu ataruhusiwa kuingia afisini. Mambo muhimu ya kuzingatia ni:
    - Wanachama wote wa kundi wana wajibu sawa wa kudhibiti uingiaji na kuruhusiwa kuingia kwa wageni.
    - Wageni wote wanafaa kusindikizwa wakati wote wanapokuwa afisini.
- Ikiwa mgeni asiyeruhusiwa kuingia atapatikana afisini:
    - Usiwahi kumkabili yeyote anayeonekana kujiandaa kuzua fujo ili apate atakalo (kwa mfano, iwapo amejihami). Katika hali hiyo, watahadharishe wenzako, tafuta mahala popote salama ujifiche na jaribu kupata usaidizi wa polisi.
    - Mkaribie huyo mgeni kwa uangalifu au taka usaidizi afisini au kutoka kwa polisi.
- Katika hali za hatari kubwa, jitahidi kuzuia vitu vinavyoweza kuleta madhara, kama vile habari iliyohifadhiwa kwenye diski ngumu ili visiweze kufikiwa, au unaweza kuviondoa katika hali ya uhamishwaji wa dharura.
- Kumbuka kwamba katika hali ya makabiliano na yeyote mwenye nia ya uhalifu, watu wanaofanya kazi afisini ndio walio katika mstari wa mbele. Hakikisha kwamba wanapata mafunzo yafaayo na usaidizi wanaohitaji kila mara wanapokabiliana na hali yoyote na bila ya kuyahatarisha maisha yao.

## Ukaguzi wa kila mara wa usalama wa afisi

Ukaguzi wa kila mara wa usalama wa afisini ni muhimu kwa sababu hali na taratibu za usalama zinatofautiana baada ya kipindi cha wakati, kwa mfano, kwa sababu vifaa huharibika au iwapo kuna hali kubwa ya wafanyikazi kuacha kazi. Ni muhimu pia kuhakikisha kwamba wafanyikazi wanazielewa kanuni za usalama wa afisini.

Mtu anayesimamia usalama anapaswa kuurejelea tena usalama wa afisini: **kila baada ya miezi sita**. Kwa msaada wa orodha ya hapa chini, jambo hili laweza kuchukua muda wa chini kama vile saa moja au masaa mawili. Mtu anayeusimamia usalama anafaa kuhakikisha kwamba maonirejea ya wafanyikazi yanatolewa kabla ya ripoti ya mwisho kuandikwa, kisha aiwasilishe ripoti ya usalama kwa shirika ili uamuzi mwafake ufanywe na hatua zichukuliwe. Ripoti kuhusu usalama inafaa ihifadhiwe kwenye faili hadi itakaporejelewa tena baadaye.

## Orodha ya kukagulia uchunguzi mpya wa usalama wa afisi

**Uchunguzi mpya wa:**
**Uliofanywa na:**
**Tarehe:**

### 1 ♦ Mawasiliano ya dharura

- Je, kuna orodha yoyote ya nambari za simu na anwani za mashirika yasiyo ya kitaifa yaliyo nchini, hospitali za matibabu ya kidharura, polisi, wazima moto, magari ya kubeba wagonjwa, mashirika ya kimataifa na afisi za ubalozi?

### 2 ♦ Vizuizi vya kiufundi na vile vilivyo dhahiri (vya nje, vya ndani na ndani kabisa)

- Kagua hali na utendakazi wa malango/ua wa nje, milango ya jengo, madirisha, kuta na paa.
- Kagua hali na utendakazi wa taa za nje, ving'ora, kamera au simu za video.
- Zichunguze taratibu za kutumia funguo, kwamba zinahifadhiwa sehemu salama na kuwa zimewekwa kitambulishi cha siri, utoaji wa majukumu ya kulinda funguo na nakala za funguo hizo, na kwamba funguo na nakala zake zinafanya kazi vizuri. Hakikisha kwamba makufuli yanabadilishwa mara tu funguo zayo zinapopotea au kuibiwa na kwamba matukio kama hayo hubatilishwa.

### 3 ♦ Taratibu na "vichujio" vya kumruhusu mgeni kuingia

- Je, taratibu za kuingia zinafanya kazi kwa aina zote za wageni? Je, wanachama wote wa kundi na pia wafanyikazi wanazifahamu na kuzitekeleza?
- Yapitie tena matukio yote ya usalama yaliyorekodiwa na ambayo yanahusiana na taratibu na "vichujio" vya kuingia ndani.
- Waulize hao wafanyikazi wanaotekeleza taratibu za kuruhusu kuingia ikiwa taratibu hizo zinafanya kazi vizuri, na kwamba zinahitaji uimarisho upi?

### 4 ♦ Usalama katika hali ya ajali

- Kagua hali ya vizima moto, vali/boma za gesi na mifereji ya maji, kizibo cha umeme na nyaya zake, jenereta za umeme (zinapoweza kutumiwa).

### 5 ♦ Wajibu pamoja na mafunzo

- Je, wajibu wa usalama wa afisi umetolewa? Unafanya kazi?
- Je, kuna mpango wowote wa mafunzo ya usalama wa afisini? je, mpango huo unashughulikia sehemu zote zilizojumuishwa katika upitiaji huu? Je, wafanyikazi wapya wamepewa mafunzo? Mafunzo hayo ni ya natija?

## Katika maeneo ya mashambani:

Watetezi pia hufanya kazi katika sehemu za mashambani, kijijini au kwenye eneo la mbali na lililotengwa. Hawawezi kuwa na hiari kubwa ya mahali patakapokuwa afisi yao ilhali wanahitajika kulinda nafasi yao kutokana na vitu au wageni wasiohitajika.

Kijiji: iwapo kinaweza kulinganishwa na eneo dogo zaidi la mjini, mazingatio mengi ya hapo nyuma yanaweza kuchukuliwa na kujalizwa na yale yanayoyafuata.

**Mahali palipotengwa na palipo mbali**: hakikisha kwamba wakaazi walio jirani, familia na rafiki zako wanaweza kuchangia katika utoaji kamsa. Jaribu kuwahusisha katika afisi yako (kama ndiko nyumbani kwako). Unaweza kuamua kufuga mbwa anayeweza kupewa mafunzo ya kuwabwekea wageni. Hakikisha kwamba hawashambulii watu na kwamba hawezi kusogolewa au kupewa sumu kwa urahisi. Pafike mahali hapo kwa usalama na epuka kuwa nje wakati wa giza.

Unaweza kuamua kuunda mawasiliano ya kupokezana na watu waaminifu watakaoweza kukupa usaidizi haraka iwezekanavyo iwapo utauhitaji.



### Muhtasari

Lengo la hatua za usalama wa nyumbani/afisini ni kupunguza hatari ya kuyafikia maeneo yasiyoruhisiwa.

Usalama wa afisi si mkubwa kuliko sehemu hafifu yake.

Bila kujali ikiwa afisi yenu iko maeneo ya mjini au mashambani mnaweza kutumia mbinu ya hapo juu ili kupunguza hatari ya hali ya kuingia kusikoruhusiwa.

Matishio yanaweza kubadilishwa yakawa matokeo ya hatari.

Orodhesha matishio/matokeo yako yote ya hatari ya kuingia kusikoruhusiwa. Kisha, kwa kila tishio/tokeo, orodhesha udhaifu na uwezo wa kila mojawapo, kisha uushughulikie.

# Usalama wa Watetezi Wanawake wa haki za binadamu

**Lengo**

Kuchunguza usalama katika mtazamo wa watetezi wanawake wa haki za binadamu.

Kuwapa watetezi wa kiume na wa kike wa haki za binadamu maarifa na zana zaidi za usalama/ulinzi.

## Utangulizi

Ingawa usalama wa watetezi wa kike wa haki za binadamu unalingana na usalama wa watetezi wote wa haki za binadamu, tumeamua kuandaa sura maalum ya kuangazia usalama wa watetezi wanawake wa haki za binadamu kwa sababu uzoefu wa nyanjani unaonyesha kwamba usalama wao haujapewa uzito ufaao. Kuna sababu nyingi za jambo hili na hususan zinazotokana na mazingira ya kijamii, kitamaduni na kidini.[1] Hii ndiyo sababu tumeamua kutoa utangulizi wa mada hii kwa mkusanyiko mfupi wa maoni yaliyokusanywa moja kwa moja kutoka kwa uzoefu wa nyanjani unaoangazia maslahi ya pamoja na ushirikiano ufaao baina ya watetezi wanawake na wanaume wa haki za binadamu.

## Watetezi wanawake wa Haki za Binadamu

Siku zote wanawake wamekuwa washikadau muhimu katika uendelezaji na ulinzi wa haki za binadamu. Hata hivyo, kazi yao hiyo aghalabu huwa haitambuliki. Wanawake hushughulika pekee yao au pamoja na wanaume katika harakati zao za utetezi wa haki za binadamu. Kwa bahati mbaya, mara nyingi:

- Hukabiliwa na si tu dhuluma za kijinsia nje ya mashirika yao bali pia mapendeleo ya kijinsia na hata ubaguzi ndani mwa mashirika yenyewe ya kutetea haki za binadamu.

1 Maadili ya Hadhari: Katika kitabu chake In a *different voice (1982), Carol Gilligan* (mwanasaikolojia wa Havard) anathibitisha kuwa hamasa ya kiume ina msingi katika uadilifu na haki, hamasa ya kike inatokana na tahadhari inayotambua umuhimu wa mahusiano ya kibinadamu na makini inayosawiriwa kwenye haja za wengine. Hivyo basi, ni halali kuamini kwamba iwapo wanaume watafuata maadili ya hadhari, fujo itakuwepo kwa uchache.

- Mara nyingi hutokea kisingizio cha "kuahirisha" kipengele kinachohusu haki za wanawake kwenye ajenda au kukifanya kuwa "kisicho cha kawaida", kana kwamba kulikuwa na utaratibu fulani wa kukipa kipaumbele badala ya kutegemeana kwenye mahusiko ya haki za binadamu. Hili hutendeka katika mashirika yaliyochanganyika ya watetezi wa haki za binadamu.

- Watetezi wa kike wa haki za binadamu bado wanachukuliwa kama wasaidizi tu na wenzi wa kiume.Hao wenzi wao kiume aghalabu hukataa kutekeleza kazi wanazoziona kama zisizo muhimu, ni kana kwamba zinategemea udume wao.

Upendeleo wa kijinsia, utabaka, ukabila, "nafasi katika jamii", chuki dhidi ya wageni, kuwaogopa watu wengine, yote haya au machache yake ni vipengele hafifu vya mantiki moja ambayo ni msingi wa ukiukaji wa haki za binadamu dhidi ya wanaume, wanawake, watu wa jinsia tofauti, watoto, wazee, makundi ya kikabila, watu masikini... wote wana athari fulani juu ya usalama. Kwa mfano, katika sehemu nyinginezo watu waliotengwa na jamii hawapewi mazingatio yoyote katika mpango wa usalama: siyo kwa namna chanya (yaani kama wachongezi dhidi ya watetezi).

Mara nyingi dhana ya ghasia hubadilishwa:

- Kupambana na"dhuluma dhidi ya wanawake" badala ya kupambana na dhuluma ya wanaume.

- "dhuluma za nyumbani" kama tasfida kwa dhuluma ya wanaume.

Ili kukomesha dhuluma za wanaume,kauli ya dhuluma za kinyumbani inapaswa kutotumiwa. Mara nyingi, wanawake wangali wanachukuliwa kama viumbe ambavyo si kamilifu, ingawa sayansi ya sasa imeonyesha kuwa tofauti za kijinsia hazimaanishi taratibu za kiuwezo. Inaonekana kama kawaida lakini uzoefu wa warsha za nyanjani za watetezi umedhihirisha kwamba wazo hili si lazima lijumuishwe. Hali hii inafafanua msisitizo wetu.

Hii ni kwa kuwa wanawake wameenda shuleni na elimu walio nayo inathibitisha kwamba ni werevu kama walivyo wanaume (kwa kutaja tu jinsi werevu ulivyo shuleni). Aghalabu hutokea suitafahamu baina ya werevu na uwezo wa kuifikia habari. Vivyo hivyo inaweza kurejelewa kwa makabila madogo madogo na kundi jinginelo lililobaguliwa. Sio suala la kianthropolojia, bali la kijamii. Mtu/kundi lililosoma linaweza kujihusisha katika mazungumzo ya kihirimu na yaliyothibitishwa kisha likapinga kubuniwa kwake. Hii inaweza kueleza kwa nini wasichana na wanawake wengi wangali hawaruhusiwi kwenda shuleni kusoma.

Wanawake hutambua upinzani uliopo baina ya kuzitetea haki za binadamu kwa upande mmoja na ubaguzi dhidi ya wanawake kwa upande mwingine. Ni lazima wakati mwingine wanawake kupenda kuwaambia wenzi wao wa kiume wajitathmini kisha wajitokeze baada ya kuzitambua na kuwa tayari kuzirekebisha tabia zao. Hata hivyo, wanawake huendelea kufanya kazi pamoja na wenzi wao wa kiume: wanawake wengi hushiriki katika matendo yanayohusu haki za binadamu ambayo yameandaliwa na wanawake.

Kunapotekelezwa dhuluma dhidi ya wanawake, hata awe mmoja (au kundi lingine lolote au hata mtu binafsi), hili si suala la kitamaduni wala dini, bali ni suala la kimamlaka.

Katika mfano wa Nelson Mandela na Desmond Tutu, ubaguzi wa rangi haukuisha kwa sababu ya hadhi ya watu weusi ilitambulika papo hapo, lakini kwa sababu baadhi ya watu weupe walitambua kuwa walikuwa wamepoteza hadhi yao. Hali hii inaweza kutumiwa kuonyesha mfano wa ubaguzi wa kijinsia au mwingineo.

Maadamu watetezi wa kiume wa haki za binadamu wanashindwa kutambua kwamba ubaguzi wa kijinsia unachipuka kutoka kwa mantiki ile ile kaidi inayohalalisha aina nyingine zote za ubaguzi, basi vuguvugu la watetezi wa haki za binadamu litakuwa kama nusu ya nguvu inayoweza kuwa yalo. Pia litaendelea kutekeleza malengo ya wakiukaji wa haki za binadamu: kugawanya na kutawala.

**Haki za wanawake sio tu haki za wanawake**

Sura hii haikusudii kubadili ufahamu na amali, bali kuangazia namna ubaguzi wa kijinsia na aina nyingine zote za ubaguzi zinavyoathiri sio tu usalama na ulinzi wa wanawake, bali pia watetezi wanaume wa haki za binadamu. Kwa namna hii, wakati ambapo mabadiliko ya ufahamu wa mwanzo unaweza kutokana na kuwa na tamaa ya kuafiki lengo fulani, sivyo hivyo kwa uzuiaji, na hili linahitaji mabadiliko katika tabia. Katika hali hii, umoja wa wanaume kuhusu masuala ya usalama wa wanawake unachangia kwa usalama wa watetezi wote wa haki za binadamu.

Zana nyinginezo zimetolewa katika muktadha wa Mashauriano ya Kimataifa kuhusu watetezi wa Haki za Binadamu – Colombo – Sri Lanka, 2005.[2]
http://defendingwomen-defendingrights.org/pdf/WHRD-Proceedings.pdf

## Mashambulizi dhidi ya watetezi wa kike wa Haki za Binadamu

Katika ripoti yake ya **2002 ya kila mwaka ikielekezwa kwa Tume ya Haki za Binadamu**, Hina Jilani ambaye alikuwa Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa alinena:

> *Watetezi wanawake wa haki za binadamu wako sawa na wenzi wao wa kiume kwenye mstari wa mbele katika kustawisha na kuzilinda haki za binadamu. Kwa kufanya hivi, hata hivyo, kama wanawake, wao hukabiliana na hatari ambazo ni mahususi kwa jinsia yao na pia zile za ziada zinazowakabili wanaume.*
>
> *Katika mfano wa kwanza, kama wanawake,* **wao huwa dhahiri zaidi***. Hivyo ni kwamba, watetezi wanawake wanaweza kuibua uhasama kuliko wenzi wao wa kiume kwa sababu kama watetezi wanawake wanaweza kukaidi kaida za kitamaduni, kidini na kijamii kuhusu uke na nafasi ya wanawake katika nchi*

2 Mwongozo muhimu kwa wanawake wa haki za binadamu UNHCR, tovuti ikiwa **http://www. unhcr. Ch/defenders/tiwomen.htm**. Pia tazama Ripoti: Mashauriano kuhusu wanawake watetezi wa Haki za Binadamu pamoja na Mwakilishi Maalum wa Katibu mkuu wa umoja wa mataifa kuhusu watetezi wa Haki za Binadamu, Aprili 4-6 2003, iliyochapishwa na Asia Pacific Forum on women, Law and Development na Essential Actors of our time: Human Rights Defenders in the Americas, na Amnesty International.

*au jamii fulani. Katika muktadha huu, hawatakumbana tu na ukiukaji wa haki za binadamu katika kazi yao kwa sababu ya jinsia yao na ukweli kwamba* **kazi yao inaweza kwenda kinyume na ufahamu hasi wa kijamii** *kuhusu hali ya kimaumbile ya unyenyekevu wa wanawake, au kuzipa changamoto dhana za kijamii kuhusu hadhi ya wanawake.*

*Pili, haitawezekana kwamba uhasama,unyanyasaji na unyamazishwaji unaowakabili watetezi wanawake utachukua mwelekeo mahususi wa kijinsia,mathalan kuanzia kwa, matusi ya moja kwa moja yanayowalenga wanawake kutokana na udhaifu wa jinsia yao wa kunyanyaswa kimapenzi na unajisi.*

*Kwa kuongezea, u***taalamu halisi na nafasi ya wanawake katika jamii inaweza kutishiwa na hata kushushwa hadhi** *kwa njia zilizo mahususi kwao kama vile kufanyiwa uchunguzi usio wa msingi–kwa mfano – wanawake wanapodai haki yao ya afya ya kijinsia na uzazi, au ya usawa na wanaume, ikiwemo maisha huru yasiyo na ubaguzi wala dhuluma. Katika mkabala huu, kwa mfano, wanawake watetezi wa haki za binadamu wamefikishwa mahakamani kwa kutumia sheria zinazohalifu hali ya kufurahia na kutekeleza haki zinazolindwa chini ya sheria ya kimataifa kuhusu mashtaka ghushi yaliyoletwa dhidi yao kwa sababu tu ya maoni waliotoa na utetezi wa kazi yao katika kutetea haki za wanawake.*

*Tatu, dhuluma za haki za binadamu dhidi ya watetezi wanawake wa haki za binadamu zinaweza kuwa na matokeo ya baadaye, ambayo yana umahususi fulani wa kijinsia. Kwa mfano,* **dhuluma za kimapenzi na unajisi wa mtetezi mwanamke wa haki za binadamu aliyefungwa zinaweza kumpelekea kushika mimba na pia kupata magonjwa ya zinaa, ukiwemo UKIMWI.**

*Haki fulani zilizo mahususi kwa wanawake zinakaribia kabisa kupewa kipaumbele au kulindwa na wanawake watetezi wa haki za binadamu. Kustawisha na kuzilinda haki za wanawake kunaweza kuwa jambo la hatari zaidi, kwa kuwa hakikisho la haki nyingine kama hizo huonekana kama tishio kwa* **ubabedume na kukatika kwa desturi za kitamaduni, kidini na kijamii.** *Kutetea haki ya wanawake ya kuishi na kuwa huru katika nchi nyinginezo kumepelekea kuwepo kwa ukiukaji wa haki hizo za watetezi wanawake wenyewe. Katika hali kama hiyo, kuyapinga matendo ya ubaguzi kumechangia kushtakiwa kwa watetezi wanawake maarufu wa haki za wanawake kwa makosa ya uasi.*

Masiala kama vile umri, ukabila, masomo, hali ya kijinsia na hali ya ndoa ni sharti yazingatiwe, kwa kuwa makundi tofauti tofauti ya wanawake hukabiliana na changamoto mbalimbali na hivyo basi wanapaswa kupewa mahitaji tofauti ya ulinzi na usalama.

**Tathmini ya mahitaji ya ulinzi wa watetezi wanawake yatasaidia kubainisha udhaifu wao mahsusi na ambao mara nyingi huwa tofauti, mikakati ya kukabiliana na udhaifu huo pia itabainishwa. Hivyo basi watapaswa kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu matukio ya kila sikuna yale ya dharura**

**AZIMIO LA KUONDOA DHULUMA DHIDI YA WANAWAKE (1993) LINAFAFANUA DHULUMA DHIDI YA WANAWAKE KAMA:**

Tendo lolote la dhuluma ya kijinsia linalosababisha au linaloweza kusababisha, dhara la kimwili, kimapenzi au kisaikolojia au mateso dhidi ya mwanamke, yakiwemo matishio ya matendo kama hayo, unyimaji wa lazima na wa kiholela wa uhuru, iwapo linatendeka katika maisha ya kibinafsi au ya wazi (kifungu cha 1).

Dhuluma dhidi ya wanawake itaeleweka iwapo itajumuisha mambo yafuatayo:

a) ♦ Dhuluma za kimwili, kijinsia na kisaikolojia katika familia, yakiwemo mapigo, dhuluma za kimapenzi za watoto wa kike wa nyumbani, dhuluma zinazohusiana na mahari, unajisi wa kindoa, ukeketaji wa wasichana na matendo menginenyo ya kitamaduni yenye madhara kwa wanawake, dhuluma zisizo za kindoa na dhuluma zinazohusiana na unyonyaji.

b) ♦ Dhuluma za kimwili, kimapenzi na kisaikolojia zinazotendeka katika mazingira ya kijumla ya jamii ukiwemo unajisi, dhuluma za kijinsia, unyanyaaji wa kimapenzi, na kutishwa kazini, katika taasisi za elimu na mahali kwingineko, wanawake kufanyiwa biashara na ukahaba wa kulazimishwa.

c) ♦ Dhuluma za kimwili, kimapenzi na kisaikolojia zinazotekelezwa au zinazokubaliwa na nchi, poppte zinazotekelezwa (kifungu cha 2).

## Usalama wa watetezi wanawake wa haki za binadamu

Wanawake watetezi wa haki binadamu hupata matatizo makubwa kutokana na kazi yao ya kulinda na kuendeleza haki za watu wengine. Ni lazima watetezi wanawake wakabiliane na hatari za kijinsia, na hivyo basi usalama wao unahitaji mbinu maalum ya kuupata.

Yale yanayosababisha hatari hizi yanafaa kuzingatiwa katika sera na itifaki za usalama wa shirika. Hapa kuna orodha ya sababu ambazo si zote zilizotajwa katika ripoti ya 2002 ya Hina Jilani ya hapo juu:

- Wanawake wanaweza kuvuta makini isiyofaa
- Watetezi wanawake wanaweza kulazimika kukiuka sheria za kibabedume na miiko ya kijamii.
- Kuna aina mahsusi za dhuluma dhidi ya watetezi wa kike.

- Wanawake watetezi wanaweza kuwa na shinikizo la "kuthibitisha" uaminifu wao.
- Wafanyikazi wenza wa kiume wanaweza kukosa kuelewa, au wanaweza pia kuikataa kazi ya watetezi wa kike.
- Wanawake watetezi wanaweza kukumbana na dhuluma za nyumbani.
- Wanawake watetezi mara nyingi huwa na majukumu ya ziada ya kifamilia.
- Mashinikizo haya yote yanaleta mzigo mwingineo wa kazi na msongo wa akili kwa watetezi wanawake.

## Kuhusu upatikanaji wa usalama na ulinzi bora kwa watetezi wanawake wa haki za binadamu

Hatua na sera za usalama wa kudumu wa kiulimwengu

### Kuhusisha zaidi ushiriki wa wanawake

Kwa ufupi, hii ni kuhakikisha kwamba wanawake wanashiriki pakubwa pamoja na wanaume katika harakati za ufanyaji uamuzi kuyapa masuala ya usalama wa wanawake mazingatio na kuwaweka wanawake katika kiwango sawa na wanaume katika harakati ya kuchukua tahadhari za usalama. Ni aula kuuhusisha uzoefu au tajiriba na utambuzi wa wanawake na pia kuhakikisha kwamba wanawake wanabainisha sheria za usalama na taratibu zake, licha ya kuzisimamia na kuzitathmini.

### Kuhakikisha kwamba mahitaji na usalama wa jinsia fulani unashughulikiwa

Kuhusu mahitaji mengineyo ya usalama, kugawa majukumu ya kushughulikia dhuluma za kijinsia na hatari za usalama wanazokabiliana nazo wanawake ni muhimu katika shirika au kundi lolote la utetezi wa haki. Watu binafsi walio na wajibu wa kushughulikia usalama watakuwa na uelewa mzuri wa mahitaji mahususi ya wanawake watetezi. Wakati mwingine, inaweza kuwa inafaa kumtambua mtu mwingine anayeweza kuleta maarifa na uelewa fulani wa suala hilo. Kwa mfano, mtu mmoja anaweza kusimamia usalama, lakini baadaye shirika linaamua kumteua mtu mwingine aliye na mafunzo na maarifa zaidi yafaayo awe kama mwenye kushauriwa kuhusu dhuluma za kijinsia. Katika hali kama hizo, wote wawili wanafaa kufanya kazi pamoja ili kuhakikisha kwamba taratibu zote za usalama zinaendelea bila tatizo na pia kuwakidhia watu mahitaji yao tofauti.

### Utoaji mafunzo

Mafunzo kwa wale wote wanaofanya kazi katika mashirika ya kutetea haki za binadamu ni muhimu katika kuimarisha usalama na ulinzi na yanafaa kuhusisha ufahamu unaoendelea kuhusu mahitaji mahususi ya wanawake watetezi.

#### Kujenga ufahamu

- Kuhusu suitafahamu baina ya amali za kijamii, kitamaduni, kidini na haki za wanawake, haki za binadamu.

- Kuhusu dhuluma zinazotendeka nyumbani dhidi ya wanawake na ambazo zinajumuisha madhara ya kimwili, kimapenzi, na kisaikolojia katika familia kama vile kupigwa, unajisi wa kindoa, ukeketaji wa wanawake na aina nyinginezo za matendo ya kitamaduni yaliyo na madhara na yanayohatarisha maisha ya wanawake.
- Miongoni mwa familia za watetezi wanawake wa haki za binadamu, na haja ya kuchukua mkondo ule ule wa hatua kama wafanyavyo dhidi ya dhuluma kama hizo zisizo za nyumbani. Mashirika yanafaa kutilia maanani uwezekano wowote wa kutokea kwa upinzani baina ya malengo yao na wanachama wa shirika wanaokubaliana na dhuluma za kinyumbani. Kutokana na mtazamo wa kiusalama, inaashiria uwezekano wa kuleta fedheha kwa shirika zima na pia uwezekano wa tokeo la kupungua kwa usaidizi wa washika dau muhimu.
- Kuhusu ukweli kwamba kutokana na usalama, wanawake wengi watafahamu kwamba wao watalazimika kuwalinda watoto pamoja na jamaa zao wengineo, licha ya kufanya kazi yao. Kuhusu namna wanaume wangeimarisha hali ya kugawana majukumu ya nyumbani bila kuharibu udume wao.
- Kuhusu ukweli kwamba watetezi wanaume na wanawake hukashifiwa mara nyingi kutokana na kujitolea kwao kwa ajili ya watu wengine badala ya aila zao zenyewe.

**Kwa muhtasari**

Tofauti katika mahitaji ya usalama ya wanawake hufungamana na majukumu yao tofauti, matishio yao tofauti na kwa tofauti baina ya hali zao mahsusi (kama vile kuzuiliwa, kazi ya nyanjani nk). Lengo ni kubuni maitikio ya masuala nyeti ya kijinsia yanayohusiana na dhuluma dhidi ya wanawake na watetezi wengineo.

## Maoni ya kuongezea

Dhuluma za kijinsia **hazijaripotiwa vya kutosha**. Utambuzi wa kijumla kuhusu dhuluma za kijinsia katika shirika au kindini unaweza kuwasilishia watu kuzungumzia kuhusu matukio na vitisho vinavyolenga jinsia maalum. Wafanyikazi walio na haja wanaweza pia kuhudumu kama "vielelezo" vya watetezi wa kike na kiume wanaotafuta suluhu za vitisho vya kijinsia au dhuluma dhidi yao au wengine katika shirika au jamii

## Dhuluma za kimapenzi na usalama wa kibinafsi

Takwimu zinaonyesha kwamba wanawake wanaathirika na unajisi zaidi kuliko wanaume. Wanaume kadhaa wanaotetea haki za binadamu na ambao wameathirika na tatizo hilo wanalitaja kama mateso ya kimapenzi na wanafahamu kwamba hili ndilo wanalopitia wanawake. Unajisi ni mateso kivyake kwa kuwa unajaribu kuhasiri mwili na wa saikolojia ya mtu.

Kama vile mara nyingi sheria za kawaida za uhalifu zinavyokuwa kisingizio dhidi ya watetezi wa haki za binadamu kwa ajili ya uwiano, unajisi unaweza kuchukuliwa

kama uhalifu wa kihakika wa kawaida na wa kisheria nayo mateso [3] ya kimapenzi yanapaswa kuchukuliwa kama uhalifu wa kisiasa (kuizima kazi ya watetezi ambapo waathiriwa wanaweza ama kupewa uteuzi wa kabla au walengwe kwa ajili ya kupata faida fulani).

Ni uhalifu wa kimamlaka na kidhuluma. Mateso ya kimapenzi ni njia mbadala ya dhalimu ya kudhihirisha mamlaka yake juu ya mwathiriwa. Mateso ya kimapenzi ni moja katika matokeo ya dhuluma za kimwili. Kwa hivyo, uzuiaji unafaa kuanza kwa kutekeleza hatua zote za usalama zilizofafanuliwa hapo nyuma ili kupunguza hatari ya dhuluma hizo. Hii ndiyo maana, uzuiaji wa dhuluma za kimapenzi unaweza kufanana na ule wa dhuluma nyinginezo. Kumbuka kwamba katika hali nyingi, wanawake waliowekwa katika maeneo tofauti yaliyo na mtu anayeweza kuhujumu mara nyingi wao hunajisiwa (na kupigwa au hata kuuawa). Kwa hiyo daima wanawake wanapaswa kufanya uamuzi wa kihakika wa kutomfuata mhujumu huyo (labda iwapo kukaidi huko kuyahatarishe zaidi maisha yake au ya wengine).

Wanawake wote walio watetezi wa haki za binadamu hukabiliwa na hatari ya kuteswa kimapenzi japo si wanawake wote watetezi wa haki wanaoweza kukumbana na hatari hiyo. Hutegemea mazingira ya kisiasa, kijamii, kitamaduni, na hata kidini. Wanawake wengine hulazimika kushughulika na afya ya kimwili huku wengine wakiyashughulikia matokeo ya kisaikolojia pamoja na afya ya kimwili, kisaikolojia, kijamii na matokeo ya kitamaduni, masaibu wanayoyapitia wanapoyashtaki na kuulizwa maswali kuhusiana nayo katika kipindi chote cha kutekeleza hatua ya kisheria.

Dhuluma za kimapenzi zinapaswa kushughulikiwa kwa mitazamo na matokeo yote, ukiwemo mtazamo wa kijamii nafsia. Kama ilivyo kwa mateso yote, mtu aliyepata mateso ya kimapenzi aweza kuwa na hisia kwamba kafanya hatia, "hadhi iliyopotea", kutoaminiwa na katika hali ya unajisi, aweza kuhisi kuwa yeye ni mchafu… Mashirika yanaweza kuzingatia uwezekano wa kuchanganua dhana ya hadhi: hadhi ni nini? Ni nani huamua kuhusu hadhi ya mtu mwingine? Ni akina nani hasa ambao wamepoteza hadhi yao: Yule ambaye anatesa au anayeteswa?

### Sera ya kudumu ya kiuendeshaji inapaswa kuhusisha:

- Kuyapa mazingatio makubwa mahitaji mahsusi ya wanawake wanaotetea haki za binadamu.
- Kushughulikia ubaguzi wa kijinsia wa shirika.
- Kuzingatia athari ya kitamaduni kwa waathiriwa wa dhuluma za kimapenzi na mateso.

### Itifaki mahsusi:

- Wanawake walio watetezi wa haki wakiwa kwenye kazi maalum ya nyanjani.
- Mahusiano ya jamii na washika dau katika ulinzi.
- Kushughulikia matokeo ya dhuluma za kimapenzi na mateso kama vile mimba zisizohitajika na ugonjwa wa UKIMWI.

3 Azimio la Umoja wa Mataifa dhidi ya mateso " (…) mateso yana maana ya tendo lolote ambalo linasababisha maumivu makali au ya kuumwa, liwe la kimwili au kiakili na ambalo limetekelezwa kwa makusudi kutokana na kwa uchochezi wa mtumishi wa umma dhidi ya mtu fulani kwa malengo ya kupata kutoka kwake au kutoka kwa mtu mwingine habari au ushuhuda, kumwadhibu kwa tendo alilolitekeleza au analotuhumiwa kwamba kalifanya, au hata kumwogofya yeye ama watu wengineo (…)"

Unapozifafanua itifaki hizi, usisahau kwamba:

- Wanawake wengine wanaotetea haki za binadamu hawawezi kuthubutu kusema kwamba wamekumbana na dhuluma za kimapenzi na mateso kutoka kwa wenzi wao wa kiume kwa vile wanaogopa unyanyapaa dhidi yao au kudharauliwa (tukumbuke kwamba waathiriwa huwa wana hisia za kuwa wamefanya hatia japo hawana sababu ya kuhisi hivyo).
- Katika nchi nyinginezo, mashirika yaliyochanganyika huwa hayazungumzii suala hilo ila kwa nadra sana.
- Wanaume wengine walio watetezi wa haki za binadamu wana maoni makubwa kuhusu uavyaji mimba. Kwa upande mwingine, hawako tayari kumlea mtoto huyo asiyehitajika. Katika nchi nyingi, kwa vile uavyaji mimba hauruhusiwi kisheria, kitamaduni au kidini, uuaji wa watoto wachanga pamoja na kuwatelekeza ndilo chaguo halisi la watu. Utelekezaji umechangia kuwepo kwa dhana ya uchawi wa kutumia watoto na pia ongezeko la wanajeshi watoto,yakiwemo matatizo mengine mengi ya kijamii. Pia, wanawake wangeamua kumeza vidonge vya kila siku (vidonge vitakavyochochea damu ya hedhi bila kujali iwapo alikuwa na mimba au la).
- Hakuna chaguo lililo la sawa au la makosa, kuna matokeo yanayofaa kutathminiwa kwenye shirika.
- **Ni muhimu kutumia zana za kutathmini hatari.**

**Mfano:**

**Hatari:** *wanawake waweza kuvuta makini isiyofaa.*

Orodhesha matishio /matokeo yote yanayoweza kutokea kuhusiana na hatari iliyopo hapo juu. Kisha, kwa kila tishio/tokeo, orodhesha udhaifu na uwezo wa sasa wa kila mojawapo. Kisha chagua uwezo ufaao kutumiwa ili kupunguza udhaifu halafu sasa uushughulikie. Yaani, hatari inafaa kudhihirishwa zaidi iwezekanavyo, kama vile unavyolitoa ganda la kitunguu tabaka baada ya tabaka. Kwa kila tabaka(tishio/tokeo) chagua udhaifu na uwezo unaohusiana na kila mojawapo.

**a)** Kunyanyaswa katika sehemu ya ukaguzi
**a)** Haki halali kubadilishwa na kuwa fadhila "iliyotolewa" ili kila mmoja akumbushwe eneo lake.

**a)** Usalama wa watetezi wanawake wa haki za binadamu haujapewa uzito katika mpango wa usalama. Wanawake hao wanaenda nyanjani peke yao.
**b)** Ukosefu wa mafunzo kuhusu mahusiano ya kijamii. Mwanamke yu pekee au yu na mwanaume asiyemjua ambaye ni mfanyikazi mwenziye. Huyu mwenziye wa kiume hampi nafasi.

$$\textbf{HATARI} = \frac{\textbf{Matishio/matokeo} \times \textbf{udhaifu}}{\textbf{uwezo}}$$

*Wanawake waweza kuvuta makini isiyofaa*

- Mashirika yaliyo na uwazi wa kupokea maoni
- Ufahamu hasi kuhusu watetezi wa kike wa haki za binadamu ni sehemu ya utendakazi na pia unafaa kujenga ufahamu kuhusu hali ya kuwa na mwelekeo wa kitaalamu
- Huduma kwa wafanyikazi ipo.

(Onyesho, miongoni mwa orodha ya uwezo wa kijumla wa hapo juu, ni upi una uhusiano mahususi na udhaifu "a" na "b". Kisha, chagua ni upi utahitaji kuendeleza).

## Kukabiliana na dhuluma ya kimapenzi[4]

Chaguzi na majibu kutokana na dhuluma za kimapenzi ni finyu tu kama zilivyo kwa kila dhuluma nyinginezo za kimwili na hili huwa juu ya mwathiriwa kulishughulikia. Hakuna njia ya sawa au isiyo ya sawa ya kukabiliana nazo. Kuhusu chaguzi nyingine zote, zinaashiria matokeo. Katika hali zote, lengo la kimsingi ni kuendelea kuishi. Chaguzi zilizopo kwa mwathiriwa za dhuluma za kimapenzi zinaweza kuwa:

1 ♦ **Kujisalimisha:** iwapo mwathiriwa ataogopa maisha yake, ataamua kukubali atendewe unyama huo

2 ♦ **Upinzani wa kimyakimya:** fanya au sema chochote kinachobugudhi au kinachokera ili kuiharibu tamaa ya kufanya mapenzi. Sema kwamba una UKIMWI (ingawa jibu la mwenye kutekeleza hilo laweza kuwa: kwa hivyo? Nami pia ninao, au anaweza kuwa na fujo zaidi).

3 ♦ **Upinzani wa nguvu:** jaribu aina yoyote ya kukabiliana kwa nguvu dhidi ya ovu hilo. Inaweza kuwa, kugonga, kupiga teke, kukwaruza, kupiga kamsa na kukimbia.

**Katika hali zote:**

- Ikiwezekana, jaribu kutaja kuhusu mipira ya kondomu. Katika tamaduni na dini nyinginezo huchukuliwa kiuongo kama"kukubali" lakini baadaye huwa juu ya waathiriwa. Wewe unaweza kuwa na tatizo kubwa zaidi kwa kuwa unaweza kulazimika kukaa na mimba, au pawe na matokeo ya kiafya na, miongoni mwa fikra nyinginezo zinazoweza kujirudia, bila kusahau, dhana ya "nini kinaweza kutokea iwapo..." Ina maana ya kuzungumzia jambo hilo katika mashirika na pia kulijumuisha kwenye bajeti. Vivyo hivyo kwa vidonge vya kumezwa kila siku na tiba nyinginezo za hospitalini.

- Ikiwezekana jaribu kukusanya maelezo mengi iwezekanavyo kuhusu (m)(wa)tekelezaji wa dhuluma hiyo. Hali hii inaweza kukufaa papo hapo kisha unaweza kujimakinisha kwa kitu fulani na bila shaka itasaidia katika kuandikisha kesi mahakamani,na hivyo kupunguza uwezekano wa kutenda uhalifu bila kuchukuliwa hatua.

- Ikiwezekana jitahidi kuutenganisha mwili kutoka kwa fikra au mawazo.

Katika hali zote, fanya chochote uwezacho ili uokoke na hali hiyo. Endelea na yale unayohisi kwamba yanakufaa. Hakuna yeyote ajuaye watatekeleza nini katika hali kama hizo (au namna nyingineyo ya mateso) na namna utakavyokabiliana na hali hiyo itakuwa sawa kwako na pia kwa hali yenyewe.

Katika maeneo mengi, mateso ya kimapenzi hutendeka kwa viwango vya juu sana. Wakati ambapo kungekuwa na fikra ya kimsingi kuhusu kutoenda nyanjani kwa shughuli maalum kabla ya kuandaa mikakati ya kutosha ya kuzuia uhalifu huku hatari ya kudhulumiwa kimapenzi baina ya makundi yanayopigana ikiwa juu, mashirika mengine ya watetezi wa haki za binadamu pamoja na ya watetezi binafsi wanawake wa haki za binadamu huamua kuvuka mipaka katika kufikiria kwao kuhusu usalama wa waathiriwa wengine. Ingawa mpaka baina ya hatari zinazokubalika na zisizokubalika ni wa kibinafsi na kishirika, sisi hatuna budi kusisitiza kuhusu sheria za

4 Mengi ya maelezo haya yametolewa kutoka kwa kitabu cha Van Brabant cha *Operational Security in Violent Environments* na pia *World Council of Churches Security Manuals*.

kimsingi za usalama. Wakati wa mafunzo, kuchangizana mawazo kumefikia umbali wa kuchanganua chaguzi zifuatazo iwapo kutatokea dhuluma ya kimapenzi wakati wa shughuli za nyanjani: mwanamke mtetezi wa haki anaweza kuambukizwa UKIMWI (iwe ni unajisi wa pamoja au la) na kujenga shaka kwamba kwa kuwa hakuna yeyote anayeweza kujua kama ni nani ana UKIMWI, kwamba wanajisi wote wanaweza kuwa nao. Anaweza pia kumwambia mwenye kudhulumu kwamba yuko katika damu yake ya hedhi na hilo lina maana kwamba kama mbinu ya kujizuia, anaweza kuamua kuvaa sodo zilizovurugwa kwa doa jekundu katika harakati yote anapokuwa nyanjani. Anaweza kuvaa nguo nyingi akitarajia kwamba nusura itatokea kwa wakati mwafaka.

Maradhi ya UKIMWI yanaangamiza na hayana mipaka ya kijnsia katika jamii. Katika nchi nyinginezo ambapo mateso ya kimapenzi dhidi ya wanawake yamekuwa silaha ya vita, wanawake wengi wameamua "kuwaeleza" wahujumu namna wanavyoathirika na matendo yao:kuhusu namna matendo yao ya kuwatesa kimapenzi hayapelekei tu katika kuwanyamazisha bali kusababisha vifo vya pamoja: limekuwa suala la kufa na kupona kwa wote, wahujumu wakiwemo. Ni jambo linaloweza kuleta balaa baada ya wakati maalum kwa watu wote, si tu maangamizi ya kitamaduni.

Wanaume wengi wanaotetea haki za binadamu pia hushughulikia dhuluma za kimapenzi dhidi ya wanawake na kukataliwa kwao katika misingi ya kitamaduni. Baadhi yao huthibitisha kwamba watawakataa wake zao iwapo wangefanyiwa mambo kama hayo.

Mwanamume mmoja mtetezi wa haki za binadamu aliwahi kumuuliza mfanyikazi mwenziye wa kiume (anayeshughulikia kuhusu kubadilisha mwelekeo wa kifamilia kuhusiana na wanawake wanaodhulumiwa kimapenzi) ambaye alilichukulia jambo hili kama uzinzi. Alimweleza wazi mwenziye huyo wa kiume: "inategemea mkeo ana thamani gani kwako."

Ndilo swali la kimsingi. Mara nyingi, mwanamke huchukuliwa kama mali/ kifaa cha mapenzi "kinapovunjika" achana nacho, kisha uchukue kingine.

**Aghalabu mwanamke huchukuliwa kama mama, binti, dada au mke wa mume. Ni nadra yeye kuwa na utambulisho wa kibinafsi: kwa bahati nzuri, wanawake wengi wanao wenzi wao wanaume wanaowapa wenzi wao wa kike usaidizi ufaao.**

**Mashirika na makundi yote ya kutetea haki za binadamu yanafaa kuwa na mipango ya kuzuia na kukabiliana na dhuluma za kimapenzi.**

Inapowezekana, kutegemea mazingira yaliyopo na uwezekano wa kuenda katika maabara, ni aula kuwepo haya yafuatayo:

- Ziara /huduma za hospitalini kabla ya kuosha – (sampuli ya kupeleka manii au sampuli nyingineyo ili yafanyiwe uchunguzi wa kubainisha nasaba yake).
- Picha za waathiriwa.
- Msaada wa kisaikolojia.
- Kuwasilisha mashtaka kwa mamlaka iliyo na umilisi tosha na vilevile kusajili kesi hizo.

Katika hali zote, mpango wa kukabiliana na dhuluma unafaa kuhusisha, angalau, **kumpa huduma bora** ya **kimatibabu**, ya kisaikolojia, ikufuatwa na msaada wa kisheria.

Ili kuzuia mimba, mwathiriwa anafaa kupewa vidonge vya kuzuia mimba (katika masaa 24): hii ni huduma ya kidharura ya kuzuia mimba (siyo ya uavyaji mimba).

Ingawa hakutakuwa na uhakikisho wa kuwepo mimba kwa sababu inategemea mabadiliko mengi, "tiba ya kuzuia UKIMWI baada ya kukisiwa kuwa umeupata" inaweza kutolewa. Kisanduku cha huduma ya baada ya kunajisiwa kinapatikana katika hospitali kadhaa, na huwa kinatumiwa kwa matibabu yanayokusudiwa kukomesha maambukizi ya magonjwa mbalimbali ya waathriwa ambao wameweza kuhudumiwa katika muda wa masaa 72 baada ya kunajisiwa. Katika hali yoyote ile, jaribu kuchunguza haraka na kila wakati kuhusu magonjwa ya zinaa.[5]

**Usawazisho wa makini unafaa kuwepo baina ya kuhakikisha kwamba mwathiriwa anapata huduma/usaidizi wa mtaalamu, na kuhakikisha kwamba shirika linakabiliana na jambo hilo kwa njia ifaayo na ile ya kiusaidizi**

Tazama pia *Kuzuia na kukabiliana na dhuluma hizo* katika sura ya 1.5.

### Kwa Muhtasari

**[Wanawake wanakabiliwa na dhuluma za kijinsia, unyanyasaji na mateso yanayotokana na utamaduni wa kibabedume. Mashirika tofauti ya kutetea haki za binadamu nayo pia aghalabu huyaibua tena katika kiwango cha chini zaidi]**. Usalama wa watetezi wanawake wa haki za binadamu ni usalama wa watetezi wote wa haki za binadamu.

Unafaa upewe uzito katika sera na itifaki za usalama wa mashirika. Mengi yanahitajika zaidi ya tathmini halisi ya hatari pekee.

Inahitajika vilevile:

- Kuhoji kuhusu wajibu na mielekeo yao.
- Kushughulikia chukulizi zisizo za ukweli na kubadili mielekeo ya kijinsia.
- Ubaguzi chanya ili kuleta mabadiliko.
- Bajeti ya usalama inapaswa kuhusisha mipira ya kondomu, vidonge vya kidharura vya kuzuia mimba, tiba inayotolewa kwa sehemu tatu….

Pia, hakuna hakikisho la kuwepo matokeo. Dhuluma za kimapenzi huja baada ya mateso ya mwili. Kwa kupunguza mateso ya kimwili, uwezekano wa dhuluma za kimapenzi utapungua pia.

5 Taarifa zaidi: Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu: http://icrc.org/web/eng/siteeng0.nsf/html/congo-kinshasa-feature-201207A

# Usalama Katika Maeneo ya Mapigano ya Kijeshi

**Lengo:**

Kupunguza hatari za kimsingi katika maeneo ya mapigano ya kijeshi

## Hatari katika hali za mapigano

Kufanya kazi katika maeneo ya mapigano kunawaweka watetezi wa haki za binadamu katika hatari mahususi, hususan katika maeneo ya mapigano ya kijeshi. Vifo vingi vya sasa vya raia vinatokana na mauaji ya kiholela,na vingi vinginevyo vinatokana na ukweli kwamba raia wanalengwa kwa njia ya moja kwa moja, na tunapaswa kutambua hili. Hatua za kisiasa zinapaswa kuchukuliwa ili kuliangazia jambo hili na pia kujaribu kulikomesha.

Ingawa huwezi kudhibiti kwa njia yoyote mapigano ya kijeshi yanayoendelea, unaweza kubadili mwenendo wako ili kuzuia kupata athari za mapigano hayo au kukabiliana kwa njia ifaayo na chochote kitakachotokea.

Iwapo umeweka makao katika maeneo ambayo mapigano haya hutokea kila wakati, basi pana uwezekano kwamba tayari utakuwa umeshapata mawasiliano ya watu wafaao watakaokulinda wewe, familia yako na watu ufanyao nao kazi unapoendelea na shughuli zako za kazi.

Hata hivyo, iwapo unafanya kazi katika maeneo yaliyo na mapigano ya kijeshi ambayo siyo maeneo yako halisi, **huna budi kuzingatia mambo haya kuanzia mwanzo:**

**a** ♦ Ni kiwango gani cha hatari ambacho umejiandaa kulikabiliana nacho? Hili pia litazingatiwa na watu binafsi au shirika unalofanyia kazi.

**b** ♦ Je, faida unazopata ukifanya kazi hapo ni nyingi kuliko hatari unazokabiliana nazo? Kazi ya muda mrefu ya haki za binadamu haiwezi kudumishwa ikiwa itawekwa katika hatari ya hali ya juu.

**c** ♦ Kule "kulifahamu eneo hilo" au "kuwa na ufahamu mpana kuhusu silaha" pekee hakutakulinda iwapo utakabiliwa na mapigano ya bunduki au utakaposhambuliwa kwa kombora au mshambulizi wa siri.

## Aina za bunduki

Unaweza kukabiliwa na mashambulizi ya kutumia bunduki kubwa ya mifuo na ile ya rashasha, makombora, roketi, mabomu na makombora ya kurushwa kutoka ardhini, hewani au baharini. Kwa kadiri, silaha za aina hii zinaweza kulengwa, kuanzia kwa mshambulizi ya siri au ndege aina ya helikopta inayoonekana vizuri hadi kwa makombora yaliyolengwa au eneo lililosheheni mizinga mikubwa. Silaha hizo pia zinaweza kuwa za aina nyingi zaidi, ambazo zimekusudiwa "kuponda ponda" eneo lote.

**Kadiri** unapolengwa na silaha zaidi, ndipo hatari inayokukabili itapungua – maadamu tu silaha hizo hazikuelekezwa moja kwa moja kwako, au eneo ambalo unapatikana, au lililo jirani yako. Katika hali kama hizo, hatari huja ikapotea ukiamua kutoka mahali hapo. **Katika hali yoyote, kumbuka kwamba ukikabiliwa na shambulizi la kutumia silaha kama hizo, itakuwa vigumu kujua iwapo unalengwa au la. Kutambulisha hili siyo suala la kupewa upaumbele**, kama tutakavyoona hapa.

## Kuchukua tahadhari: kupunguza uwezekano wako wa kushambuliwa na silaha hizo

1 ♦ **Epuka maeneo ya hatari**: Epuka kabisa kuweka makao yako katika maeneo ya mashambulizi au kunakotokea vitendo vya kigaidi,kuweka afisi au kusalia kwa muda mrefu mahali kunakoweza kutokea shambulizi kwa mfano,eneo kama ngome au palipowekwa mawasiliano ya simu. Vilevile, maeneo maalum kama vile yanayokaribia kuingia au kutoka mjini, viwanja vya ndege sehemu zinazotumiwa kuangalia mandhari, yanafaa kuepukwa.

2 ♦ **Tafuta ulinzi unaotosha wa kujilinda na shambulizi**: Vioo vinavyochopoka kutoka kwa dirisha lililo karibu ndiyo mojawapo wa chanzo kikuu cha majeraha. Kuyafunga hayo madirisha kithabiti kwa mbao au kuyafunika kwa ukanda unaonata kunaweza kupunguza hatari ya kukabiliana na shambulizi la aina hiyo. Iwapo shambulizi litatokea,songa mbali na madirisha kisha jilaze sakafuni, chini ya meza au katika chumba chenye kuta nene kilicho mbali na madirisha, au bora zaidi uteremke chini ya ghorofa.

Mifuko ya mchanga inaweza kutumiwa wakati mwingine, lakini mradi tu vyumba vinginevyo vina hifadhi ya mifuko hiyo – la si hivyo unajenga hatari ya kuvuta makini isiyohitajika. Iwapo hakuna chochote kinginecho, sakafu au shimo lolote ardhini vinaweza kuleta uzuiaji wa kiasi. Ukuta wowote uliojengwa kwa matofali, au mlango wa gari hautakuzuia kupigwa risasi ya bunduki au kukabiliwa na silahaza hali ya juu kama vile bunduki. Makombora na roketi ni zana za vita zinaweza kuua kwa umbali wa hata kilomita kadhaa, kwa hivyo huhitaji kuwa karibu zaidi katika eneo la kushambulia. Bomu au milipuko ya makombora inaweza kuhasiri usikizi wa masikio yako: yafunike kwa mikono na ufungue mdomo wako kiasi tu. Kuyatambua yalipo makao makuu yenu, eneo au hata magari yenu kunaweza kuwa muhimu, lakini tahadhari kwamba **hali hii inawezekana tu iwapo washambulizi huheshimu kazi yenu**. Ikiwa hali siyo hii, basi mtakuwa mnajidhihirisha nje kwa njia isiyofaa. Mkipenda kujitambulisha, fanyeni kwa kutumia bendera au rangi au hata ishara kwenye kuta na paa (iwapo kuna hatari ya shambulizi la hewani).

3 ♦ **Kusafiri katika magari**: Iwapo umeabiri gari linalopigwa risasi kwa njia ya moja kwa moja, unaweza kukadiria hali kama hiyo, lakini kufanya kadirio halisi ni vigumu. Kwa jumla, **ni vizuri kuchukulia kwamba gari linalengwa au litalengwa, na kwamba jambo bora la kufanya, kwa hivyo, ni kutoka nje na kutafuta ulinzi wa haraka**. Gari ni kitu cha wazi kinacholengwa. Linaweza kushambuliwa, na pia linaweza kukuweka katika hatari ya kujeruhiwa kwa vioo vinavyochopoka kutoka kwa dirisha au tangi la mafuta lililolipuka, ikiwemo kuathiriwa na moto wa moja kwa moja. Ikiwa moto haupo karibu sana, jaribu kuendelea kusafiri katika gari hadi utakapofika maeneo yaliyo salama.

## Mabomu yaliyotegwa ardhini na mizinga ambayo haijalipuka[1]

Silaha hizi zinajenga tishio kali kwa raia katika maeneo ya vita. Zinaweza kuchukua maumbo tofauti:

- **Mabomu ya kutega:**
  - ♦ Mabomu ya ardhini ya kukabiliana na vifaru vya vita hutegwa kwenye barabara na njia na huwa yanaharibu vifaru hivyo. Yanaweza pia kuchochewa na gari la kawaida hadi yalipuke.
  - ♦ Mabomu kama hayo japo madogo yanaweza kupatikana mahala popote pa watu kupitia. Mengi yayo hutegwa ardhini. Usisahau kwamba watu wanaoyatega mabomu barabarani wanaweza pia kuchimba migodi katika maeneo yaliyo karibu na barabara hizo, na pia njia ndogo zilizokaribu.
- **Mabomu yanayolipuka:**
  - ♦ Hivi ni vijibomu vidogo ambavyo hufichwa kwenye chombo cha kawaida tu na ambacho huvutia, (kilicho na rangi, mathalan) na ambacho hulipuka pindi tu kinapoguswa. Neno hili pia laweza kutumika kufafanua mabomu yanayofungamanishwa kwa kitu kinachoweza kusogezwa au kuchochewa (chochote kama vile mzoga au gari lililoachwa bure).
- **Mizinga ambayo haijalipuka:**
  - ♦ Hii hurejelea aina yoyote ya zana/baruti ambayo tayari ishatolewa lakini haijalipuka.

Siku hizi kumezuka mkusanyiko mpya wa zana za vita. Zana hizi hutumiwa kwa ukaribu kama yalivyo mabomu ya ardhini ya kukabiliana na watu binafsi, makundi ya zana za vita ni mabaki ya makundi ya mabomu ambayo hayajalipuka.[2] Kila kundi la bomu limeundwa kutokana na mamia ya silaha ndogo zilizotolewa kutoka maeneo yote. Makundi hayo yameundwa kwa namna ya kuweza kulipua eneo kubwa na pia kuweza kulipuka yanapotolewa kwa kuwa uwezekano wa kushindwa kulipuka ni wa juu zaidi.[3] Pia mabomu ya aina hii si imara zaidi ya yale ya ardhini kwa hivyo yanaweza kulipuka wakati wowote. Mengine yana rangi za kuvutia na hivyo yanawavutia watoto.

[1] Maelezo mengi katika sehemu hii yametolewa kutoka kwa mwongozo bora wa *Koenraad van Brabant, Operational Security Management in Conflict Areas*. Tazama marejeleo.

[2] Tazama *Principes de droit des conflits armes, Eric David (ULB, Brylant, 2002)*. Tazama pia kampeni za juzi za Handicap International, Amnesty International nk; www.clustermunition.org, www.controlarms.org.

[3] Makadirio ya kiwango cha kufeli ni baina ya 5-80% kutegemea makundi ya mabomu na ulaini au ughafi wa kudumu wa udongo. Hivyo mabomu hayo yanakuwa hayapingiki.

## Kujilinda dhidi ya mabomu ya ardhini na mizinga ambayo haijalipuka.

Njia ya pekee ya kuepuka maeneo yaliyotegwa mabomu ni kuyajua yalipo. Iwapo hujaweka makao au huishi katika eneo fulani, unaweza tu kutambua sehemu zilizotegwa mabomu kwa kuendelea kuwauliza wenyeji wa sehemu hiyo au wataalamu[4] kuhusu suala hilo, yaani iwapo kumetokea mlipuko au mapigano yoyote katika eneo hilo.

Ni bora kutumia barabara kuu za lami, njia pana zinazopitika na zinazotumika sana, na kufuata alama za magari mengine yaliyopitia barabara hizo. **Usiwache barabara kuu, siyo hata kwenye ukingo wa barabara au maeneo magumu ya barabara ambayo gari linaweza kusimama kwa dharura, ukiwa au usipokuwa na gari**. Mabomu ya ardhini na mengine ambayo hayajalipuka yanaweza kusalia yakiwa yamejificha au yawe na uwezo wa kulipuka kwa miaka mingi.

Mizinga/mabomu ambayo hayajalipuka yanaweza kupatikana katika maeneo yoyote ambayo vita au mapigano ya risasi yametokea, na yanaweza kuonekana. Sheria muhimu ni kuwa: **usiyasogelee, usiyaguse, weka alama mahala hapo iwapo unaweza, na pafanye pajulikane mara moja**.

Kwa kawaida mitego ya mabomu hupatikana maeneo ambayo wapiganaji wameyaondoka. Katika maeneo haya hapana budi kwa yeyote kutogusa au kutosongesha chochote na ni bora kujiweka mbali na majengo yaliyohamwa.

## Iwapo mabomu yaliyotegwa ardhini yatalipuka karibu na gari au mahali alipo mtu.

Kuna kanuni mbili muhimu:

- Kuliko na bomu moja la ardhini, kuna mengine yaliyo hapo
- Usiwe mtu wa papara, hata ingawaje kunaweza kupatikana watu waliojeruhiwa.

Ikiwa huna budi kuepukana na hali hiyo, zifuate nyayo zako iwapo zinaonekana. Iwapo unasafiri kwa gari, na unashuku kwamba kuna mabomu ya kulipua vifaru, ondoka kwenye gari kisha utembee kwa kurejea nyuma ukifuata alama za magurudumu ya gari hilo. Ikiwa unatembea kuelekea aliko mwathiriwa, au unaondoka kutoka maeneo yaliyotegwa mabomu, njia ya pekee ya kufanya hivyo ni kupiga magoti au kulala chini na kuanza kudukua ardhi kwa kuchomeka kudukuzi (kipande cha ubao au chuma kilicho chembamba) kwa makini kwenye ardhi pembe ya nyuzi 30, na kwa utaratibu kujaribu kuhisi iwapo kuna kitu chochote yabisi. Ukikipata kimoja (kitu kigumu), jaribu kuondoa udongo ili mahali hapo pawe wazi na na pepesi pa kubainisha kilichoko. Mabomu ya ardhini yanaweza pia kuchochewa ili yalipuke na nyaya za ardhini. Usikate nyaya zozote ukizipata. Bila shaka haya yote yanaweza kuchukua muda wa kiasi.[5]

4 Mashirika yasiyo ya serikali ama vikosi vya usalama vya Umoja wa Mataifa vyenye utaalamu wa kuondoa mabomu ya ardhini. Pia mashirika mengine ya kimataifa mara nyingi huwa na ramani ya maeneo yaliyo au yasiyo mabomu.

5 Unaweza kupata miongozo na machapisho kuhusu ufahamu wa mabomu ya ardhini na pia masomo ya Kampeini ya Kimataifa ya Kukomesha utegaji wa Mabomu ya Ardhini katika tovuti www.icbl.org.

# Usalama Katika Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

**(kwa ushirikiano wa Privaterra-www.privaterra.org)**

**Lengo:**

Mianya mikubwa katika teknolojia ya habari iliyojengeka katika ulimwengu mzima pia huathiri watetezi wa haki za binadamu. Sura hii inajikita hasa katika teknolojia ya habari – yaani tarakilishi na mtandao.[1] Watetezi wasio na uwezo wa kuzipata tarakilishi au mtandao hawataweza kufaidika kwa sasa na yale yaliyomo. Badala yake, wanahitajika, kwa dharura, kupata mbinu na mafunzo ya kuyawawezesha kutumia teknolojia ya habari katika kuzitetea haki za binadamu.

## Mwongozo kuhusu matatizo ya usalama wa mawasiliano na jinsi ya kuyaepuka

Elimu ni nguvu na kwa kufahamu yalipo matatizo yako ya usalama wa mawasiliano, unaweza kuhisi kuwa u salama zaidi unapofanya kazi yako. Orodha ifuatayo inaonyesha mbinu mbalimbali ambazo habari na mawasiliano yako yanaweza kuingiliwa kwa njia ya haramu au yakabadilishwa, na hatimaye mapendekezo ya njia za kujaribu kuepuka matatizo kama hayo ya usalama yametolewa.

## Kuzungumza

Si lazima habari ipitie mtandaoni ili mtu aweze kuipata kiharamu. Unapoyajadili masuala nyeti, zingatia maswali yafuatayo:

1 ♦ Je, unawaamini watu unaozungumza nao?

1 ♦ Je, wanafaa kufahamu habari unayowapa?

1 ♦ Je, u katika mazingira salama? Vinasa sauti vya siri na vifaa vinginevyo vya kusikiliza mara nyingi hupachikwa katika maeneo ambayo watu huchukulia kwamba ni salama, kama vile afisi za kibinafsi, barabara zenye harakati nyingi, vyumba vya kulala nyumbani na magari.

---

1 Sura hii inatokana na kazi iliyofanywa na Robert Guerra, katika Rodr-guez y Caryn Mladen kutoka Privaterra, shirika lisilo la kiserikali linalotoa mafunzo na huduma za ushauri katika ulimwengu mzima kuhusu usalama na Teknolojia ya Mawasiliano kwa watetezi wa haki za binadamu. (Matini hii imechukuliwa kwa kiasi fulani na Marie Caraj na Enrique Eguren).

Inaweza kuwa vigumu kujua jibu la swali la tatu, kwa kuwa vipaaza sauti au vinasa sauti kwa siri vinaweza kupachikwa katika chumba ili kurekodi au kusambaza kila kitu kinachozungumzwa hapo. Vipaza sauti vya leza vinaweza pia kuelekezwa kwenye madirisha kwa umbali zaidi ili kusikiliza kinachozungumzwa katika jengo hilo.Pazia nzito hujaribu kuzuia vinasa sauti vya siri vya leza, kama yafanyavyo madirisha yaliyosimikwa vioo viwili. Majengo fulani yaliyo salama yana seti mbili za madirisha yaliyosimikwa kwenye afisi ili kuzuia hatari ya vifaa vya leza vya kusikiliza.

## Unaweza kufanya nini?

■ **Daima chukulia kwamba kuna mtu aliye ndani ya afisi na anasikiliza kinachotendeka**. Kutokana na mwelekeo mzuri wa dhana ya akili isiyotibika, kuna uwezekano mkubwa wa wewe kuwa makini zaidi unapoyashughulikia mambo ya kibinafsi.

■ **Vinasa sauti vya siri au vifaa vya kunusa vinaweza kutumiwa kugundua vifaa vya kusikiliza**, japo inaweza kuwa vigumu au ghali kuvipata vifaa hivyo. Pia, wakati mwingine watu waliokodishwa kuondoa vinasa sauti hivyo ndiyo wanaotuhumiwa kuvipachika kwa mara ya kwanza. Wakati wa kuviondoa, wao hupata ama vichache "vilivyotupwa" (vinasa sauti visivyo ghali vilivyoundwa kwa namna ya kugunduliwa rahisi) au kutopata chochote katika hali inayokanganya na kisha kutangaza wazi kuwa afisi ni "safi".

■ **Mfanyikazi yeyote msafishaji anaweza kuwa tishio kali la usalama**. Wao huingia afisini mwenu baada ya muda wa kazi kisha huchukua taka zote kila usiku.Wafanyikazi wote wanafaa kuchunguzwa kwa uangalifu kwa sababu za kiusalama kutokana na harakati inayoendelea, kwa kuwa wafanyikazi wanaweza kuwa hatarini baada ya kujiunga na shirika lenu.

■ **Badilisha vyumba vya mikutano mara kadhaa iwezekanavyo**. Kadiri vyumba au maeneo mnayoyatumia katika kujadiliana na kubadilishana habari yanavyokuwa mengi ndipo pia idadi ya wafanyikazi na vifaa vya kusikilizia itakavyoongezeka.

■ **Tahadhari na zawadi unazopewa wewe ili uzihifadhi**, kama vile kama kalamu ghali, pini inayowekwa kwenye mkunjo wa koti au kibanio, kama vile kigandamizio maridadi cha karatasi au picha kubwa. Vifaa vya aina hii vimetumiwa hapo awali kusikilizia mijadala.

■ **Chukulia kwamba sehemu fulani ya habari yako iko hatarini wakati wowote ule**. Aghalabu unaweza kupenda kubadilisha mipango na kanuni, hivyo ukawapa wasikilizaji wako vipande vipande tu vya habari sahihi. Jaribu kuwapa habari isiyo sahihi ili kubainisha ikiwa kuna yeyote anayeitolea hisia au anayeitumia.

■ Ili kupunguza utendakazi mzuri wa kipaza sauti cha leza, **yajadili mambo yaliyo nyeti katika sehemu ya chini ya jengo au ndani ya chumba kisicho na madirisha**. Vifaa vingine vya leza vya kusikiliza vinaweza kukosa nguvu wakati wa mvua kubwa au kutokana na madadiliko ya hali ya anga.

■ **Weka rekodi ya sauti inayosikika ya wimbo maarufu** kwa umbali au ili kuchachawiza mawimbi ya sauti kwa kuwa vipo vifaa vya nje vya kusikizia vinavyoweza kuyachukua mazungumzo kutoka umbali wa takriban mita 50. Yaani, mahali penu pa mikutano hapalazimiki kupachikwa na vinasa sauti hivyo vya siri. Ni teknolojia ya hali ya juu tu inayoweza kuchuja kelele yenye mkondo wowote ili upate kuyasikiliza mazungumzo.

■ **Maeneo ya wazi sana yanaweza kuwa na manufaa au madhara**. Kukutana katika sehemu iliyojitenga kunarahihisha kutambua iwapo mnafuatwa au mnatazamwa, lakini hali hiyo hufanya kutoroka kuwe kugumu kutokana na kuchanganyika. Mikusanyiko ya watu husababisha wao kuungana, lakini inakuwa rahisi zaidi kuonwa au kusikilizwa.

■ **Iwapo afisi yenu au mahali penu pa mikutano patakuwa pa wazi katika maeneo ya mashambani**, mwombe mwanachama mwenziyo mmoja asalie nje kisha akujulishe iwapo wanaweza kuyasikia mazungumzo yenu na kuwafanya watazame vitu visivyofaa wakati wa mkutano wenu.

## Simu za mkononi

Simu zote zinazopokelewa zinaweza kusikilizwa iwapo msikilizaji ana uwezo wa kutosha wa kiteknolojia. Hakuna simu yoyote inayoweza kuchukuliwa kwamba ni salama. Simu za mkononi za kimfanano si salama zaidi kuliko zile za kitarakimu na zote si salama zaidi kuliko simu za mezani.

Mahali mlipo pamoja na mazungumzo yenu yanaweza kubainishwa kupitia uchunguzi wa simu ya mkononi. Si lazima uwe unazungumza ndiposa mahali ulipo pawe panafuatiliwa – hii inaweza kufanyika wakati wowote ambao simu yako ya mkononi imewashwa.

Usihifadhi habari kama vile majina nyeti na nambari katika kumbukumbu ya simu yako. Iwapo simu yako itaibiwa, habari hii itatumiwa kuwashika na kuwahatarisha watu unaotaka kuwalinda.

Kwa hali za dharura, panapowezekana unaweza kupata nambari mbili za simu zisizojulikana (kadi za simu za kutumia kupigakisha ukazitupa). Kadi hizi zaweza kutumika tu kipiga simu baina yao bila ya kupigia au kupigiwa na nambari nyingineyo "isiyojulikana" (kwa vile nambari inayojulikana itakuwa kwenye orodha ya watu wabaya na hivyo kuisaliti nambari mpya). Usizitumie katika maeneo unayoweza kuyafikia kwa urahisi. Kumbuka kutoziacha kwenye simu yako iwapo huzihitaji kwa kuwa zinaweza kupatikana. Zibadilishe zote kila mara. Kuwa na tahadhari kama vile unapokuwa ukizungumza kupitia kwa simu yako.

## Usalama wa nje wa habari katika afisi

Ifunge afisi yenu kila wakati, ikiwemo milango na madirisha. Tumia funguo zinazoweza kunakilishwa kwa idhini ya maalum ya shirika kisha mpate kuzifuatilia nakala za funguo hizo jinsi zinavyotumika. Msiwape funguo watu wengine, sio hata wafanyikazi wa kukarabati au kunadhifisha afisi, halafu hakikisha kwamba wewe au mwingine unayemwamini upo kila mara afisini kunapokuwa na hao watu wengine. Iwapo haitawezekana, hakikisha kwamba unapata chumba kisichoingiwa na mtu yeyote ambamo faili muhimu zinahifadhiwa. Jitahidi kuifunga milango yote ya afisi kisha unaweza kuwacha taka ambayo haina usiri wowote nje wakati usiku.

Tumia kifaa cha kuharibu chochote chenye usiri fulani. Vifaa vya kubandua na kuharibu kama hivyo mara nyingi huwa si vizuri. Ili kuondoa chochote hasa kilicho cha siri, ni vizuri iwapo utakichoma, upondeponde jivu lake kisha ukitupe chooni.

## Usalama wa kimsingi wa Kompyuta na Faili[2]

Zima kompyuta unapoondoka afisini, ikiwezekana ondoa vioo vya kompyuta kutoka madirishani vilikoelekea.

Tumia vidhibiti vya mawimbi makali katika kulinda nguvu ya umeme (kubadilika kwa nguvu ya umeme kunaweza kuharibu kompyuta).

Hifadhi **habari ya itakayokusaidia baadaye**, zikiwemo faili, katika mahali palipo salama, na palipojitenga. Hakikisha kwamba vyombo hivyo visaidizi vimehifadhiwa kwa njia salama kama vile kuvihifadhi kwenye **diski nguvu ya kompyuta iliyo na mkusanyiko wa habari uliolindwa salama**, au kufuli za nje zilizo za hali ya juu.

Ili kupunguza hatari ya mtu kuifungua kompyuta yako, ilinde kwa kuweka neno au nambari za siri na izime kila mara unapomaliza kuitumia.

Zihifadhi kwa siri zaidi faili zako za kompyuta ikiwa mtu aweza kuifungua kompyuta yako, au anaweza kugundua neno/nambari ya siri.

Iwapo kompyuta yako imeibiwa au imeharibiwa, bado utaweza kuzipata faili zako iwapo ulikuwa umeunda kitengo kisaidizi cha kuhifadhi kila siku. Viweke vitengo hivi vya kuhifadhi faili mbali na afisi yako. Unaweza pia kutumia hifadhi ya mtandao unaotoka nje ili kuihifadhi habari yako kwenye mtandao. Hali hii itakuruhusu kuzipata faili zako zote zilizohifadhiwa kwenye kitengo kisaidizi hata ikiwa kompyuta yako itaharibiwa au kuibiwa.

Faili zilizofutwa haziwezi kutengenezwa upya iwapo umezifuta kwa kutumia chombo maalum cha kufuta kiitwacho PGP au kinginecho.Badala yake zitaenda katika kitengo cha kuweka taka au kwenye jaa linaloweza kutumiwa tena.

Kompyuta yako inaweza kuagizwa kuzituma faili zako la si hivyo hali hii inaweza kukufanya ukose habari yako uliyohifadhi. Ili kuepukana na hili, nunua kompyuta yako mahali inapopaamini, kisha uisawazishe (yaani ichunguze na uitengeze upya **diski draivu**) unapoipata mwanzo, kisha waweza kuweka program uitakayo. Waruhusu wataalamu waaminifu pekee kuifanyia kazi kompyuta yako na pia daima uwe karibu nao wanapofanya hivyo.

Ni aula kuchomoa plagi ya **modemu**/kiunganisho cha simu ya kompyuta yako, au kuharibu muunganisho wa mtandao, unapoiacha kompyuta bila ya kuifanyia kazi. Katika hali kama hii, programu zisizofaa hazitaweza kufanya kazi. Usiiwache komyuta bila kuizima unapomaliza shughuli za siku. Zingatia kuweka programu ambayo itasababisha kompyuta yako isifunguliwe baada ya muda fulani wa kuwa imezima. Hivi, kompyuta yako haitafunguliwa utakapokuwa umeshughulika na mambo mengine.

Kuhusu mapendeleo yako ya kiwavuti, kubalisha mwendeleo wa faili kabla ya kuifungua ili kubainisha ni faili ya aina gani. Hutaki kusababisha kuingia virusi kwenye kompyuta kwa kufungua faili uliyodhani kuwa ni faili ya maandishi tu lakini inayoweza kuwa navyo. Katika *Internet Explorer*, nenda kwa menu ya Zana kisha chagua *Chaguzi za Kasha*. Bonyeza Tazama halafu hakikisha kuwa kisanduku, *Ficha maendelezo ya aina za faili zinazojulikana*, hakijakaguliwa.

2 Ushauri zaidi wa kina kuhusu usalama wa kompyuta unapatikana kutoka 'Front Line' kwa kuwasiliana na barua pepe info@frontlinedefenders.org au kutoka Privaterra kwa info@privaterra.org

## Matatizo ya usalama wa mtandao

Barua pepe yako haitoki moja kwa moja kutoka kwa kompyuta yako hadi kwa mlengwa. Hupitia vitovu mbalimbali na katika hali hiyo, huacha nyuma habari fulani. **Inaweza kusomwa inapoendelea kuenda kwa mlengwa (si tu ndani au nje ya nchi yako)**.

Mtu yeyote anaweza kuwa anakuchunguza unapouandika ujumbe wako. Hili huwa tatizo hasa katika migahawa ya mtandao. Iwapo una muunganisho wa mitandao, barua pepe yako inaweza kusomwa na kila mtu afisini. msimamizi wa mfumo mzima wa kompyuta anaweza kuwa na uwezo wa kimamlaka wa kuzisoma barua zako.

Msambazi wako wa huduma ya mtandao (Internet Service Provider) anao uwezo wa kuzifikia barua pepe zako, na mtu yeyote aliye na ushawishi juu ya usambazi huo anaweza kushinikiza ili nakala za barua pepe zako zote zitumwe kwake au hata kuzisimamisha baadhi ya barua zisikufikie.

Zinapopitia mtandaoni, barua pepe zako hupitia kwenye mamia ya maeneo ya watu wengine yasiyo salama. Wataalamu wa kompyuta wanaweza kuzisoma barua pepe zinapopita. Msambazi wa huduma ya mtandao kwa mpokezi wako mkusudiwa anaweza pia kuwa katika hatari, pamoja na mtandao na afisi yake.

### Usalama wa kimsingi wa mtandao

Virusi pamoja na matatizo mengine, kama vile Trojan Horses au Trojans, yanaweza kutokea popote; hata rafiki wanaweza kusambaza virusi. Tumia programu nzuri ya kukabiliana na virusi na endelea kujipa habari kadiri inavyoingia mtandaoni. Virusi vipya vinaundwa na kugunduliwa kila wakati kwa hivyo fanya utafiti katika *Maktaba ya Maelezo kuhusu virusi* kwenye www.vil.nai.com kwa habari za sasa za kukabiliana na virusi.

Mara nyingi virusi husambazwa kupitia kwa barua pepe, kwa hivyo jitahidi kutuma barua hizo kwa njia salama (tazama hapa chini). Virusi ni programu za pekee zilizoundwa kujirudia tena na zinaweza au zisiweze kudhuru. Trojans ni program zilizoundwa ili zipeanwe kwa watu wengine (au yeyote) wanaoweza kuitumia kompyuta.

*Kizuizi kizuri cha moto* kinaweza kukusaidia usionekane kwa wapenyezi katika kompyuta yako, na kuwaweka mbali wadukizi wanaojaribu kupenya katika tarakilishi yako. Jambo hili huhakikisha kwamba ni harakati zilizoruhusiwa tu ndizo zinazoweza kuunganishwa kwenye mtandao kutoka kwa kompyuta yako na huzuia programu kama vile Trojans kutuma maelezo au kufungua "milango ya nyuma" ya kompyuta yako ambayo wapenyezi hao haramu wanaweza kuitumia kuingia.

Mfumo wa "kibonyezo cha kujisajili" unaweza kufutilia ubonyezo wote unaoufanya. Program hizi husambazwa ama na mtu anayezipachika kwenye kompyuta yako unapokuwa haupo au kupitia kwa virusi au Trojan inayoharibu mkondo wa mtandao wako. Vibonyezo vya kujisajili hufuatilia ubonyezo wako na hutoa ripoti ya matendo yote uliyoyafanya mara nyingi kupitia kwa maneno ya siri, kutuma barua pepe kwa usalama, kutumia programu za kukabiliana na virusi na kutumia programu zinazoongozwa na kipanya ili kupiga taipu maneno ya siri, kunaweza

kuzuia hatari inayotokana na programu za madhara zinazombazwa kwenye kompyuta yako. Vibonyezo vya kujisajili pia vinaweza kumalizwa nguvu kwa kuondoa muunganisho wa mtandao kwenye kompyuta yako – mara nyingi kwa kuchomoa plagi za simu ya kompyuta – unapokuwa huitumii kompyuta hiyo.

Anwani ya barua pepe inaweza "kughushiwa" au kutumiwa na mtu mwingine licha ya kuwa inatumiwa na mwenyewe halisi. Hii inawezekana kwa kutumia kompyuta ya mtu mwingine na kufahamu neno lake la siri, kwa kupenyeza kwa siri katika huduma ya mtandao, au kwa kutumia anwani inayoonekana ni ya mtu fulani mahsusi. Kwa mfano, kwa kubadilisha herufi ndogo "i" kwa nambari "1", unaweza kuunda anwani inayofanana na nyingine na watu wengi hawatatambua tofauti. Ili kuepuka kudanganywa na mwenye kughushi, tumia anwani za maneno yaliyo na maana na baada ya kipindi fulani, uliza maswali ambayo mwenye anwani hiyo halisi ndiye atakayejibu kisahihi. Tambua ombi lolote unalolishuku la kutaka maelezo fulani kwa kulifuatilia kupitia kwa mtindo mwingine au mawasiliano.

Kufanye kuzuru kwako mtandao kuwe kwa siri kwa kutokubali kuki ("cookies") na kwa kufuta hifadhi yako kila mara unapomaliza kuzuru mtandao. Katika *Internet Explorer,* nenda kwa Zana, kisha Chaguzi. Katika *Netscape Navigator,* nenda kwa Edit, kisha *Preferences*. Utakapokuwa kwenye mojawapo wa menu hizi, futa kabisa yale yote uliyotangulia kufanya, "cookies" kuki zozote unazoweza kuwa nazo kisha uiwache hifadhi yako bure bila kitu. Kumbuka pia kufuta yote uliyoyawekea alama ya labda kuyarejelea baadaye. Visakuzi pia huweka hifadhi ya tovuti unayozuru katika faili za hifadhi kwa hivyo chagua faili zinazofaa kufutwa katika kompyuta yako.

Sawazisha visakuzi vyote vya tovuti ili viambatane na mgawo wa 128 wa ufichaji habari. Hili litapelekea katika kulinda habari yoyote unayotaka kuituma kwa njia salama kupitia kwa mtandao, yakiwemo maneno ya siri na habari nyinginezo nyeti zilizowasilishwa kwenye fomu. Weka zana za sasa za usalama kwenye programu zote zinazotumika, hasa kwenye *Microsoft Office*, *Microsoft Internet Explorer*, na *Netscape*.

Kuzuru mtandao kusikokwa lazima hakufai kufanywa kwenye kompyuta iliyo na habari muhimu.

## Utumiaji wa kimsingi wa barua pepe ulio salama

Kuna njia au namna ya kutuma barua pepe zilizo salama ambazo wewe, rafiki zako na washirika wengine wako wanafaa kufuata. Waache wajue kwamba hutafungua barua pepe zao mpaka watumie njia za salama katika utumiaji wa barua hizo.

1 ♦ Usiwahi kufungua barua pepe kutoka kwa mtu usiyemjua.

2 ♦ Usiwahi kumtumia mwingine barua pepe kutoka kwa mtu usiyemjua, au asili yake huijui. Barua pepe hizo zote za "mawazo ya furaha" ambazo watu huwatumia wengine zinaweza kuwa na virusi. Kwa kuwatumia rafikizo na washirika wako unaweza kuwa unaambukiza kompyuta zao. Ukiwa unazipenda hisia zao vya kutosha,andika upya ujumbe huo na uutume wewe binafsi. Iwapo huna muda wa kuandika upya, basi huenda si ujumbe muhimu.

3 ♦ Usiwahi kuhamisha au kukifungua kiambatisho ila uwe unajua kimebeba nini na kwamba hakina madhara. Zima chaguzi za moja kwa moja za uhamasishaji katika programu yako ya barua pepe. Virusi vingi pamoja na Trojans hujisambaza kama "minyoo" na minyoo ya sasa mara nyingi huonekana ni kana kwamba imetumwa na mtu unayemjua. Minyoo mierevu huchunguza kitabu chako cha anwani, hasa ukiwa unatumia Microsoft *Outlook* au *Outlook Express*, kisha hukitoa upya kwa kujifanya kuwa viambatisho halisi kutoka watu halisi waliotuma. Kusajilisha barua pepe zinazotumwa bila viambatisho kunaweza kupunguza zaidi utata kuhusu viambatisho visivyo na virusi unavyowatumia wenzi wako (PGP ni programu inayotumiwa kuficha maelezo, tazama hapa chini kuhusu "usimbaji fiche").

4 ♦ Usitumie HTML, MIME au matini nyingi katika barua pepe – tumia tu matini ya kawaida. Barua pepe zilizowekewa madoido zinaweza kusheheni programu zilizotiwa ambazo zinaweza kuruhusu kuzifikia faili au kuziharibu.

5 ♦ Iwapo unatumia Outlook ama Outlook Express, ondoa sehemu ya kioo cha kompyuta ya majaribio.

6 ♦ Jaribu kuficha barua pepe zako kadiri ya uwezo wako. Barua pepe iliyofichwa ni kama postikadi ya picha inayoweza kusomwa na yeyote anayeitazama au anayeweza kuifikia. Barua pepe iliyofichwa ni kama barua kwenye bahasha ndani ya kasha.

7 ♦ Tumia anwani za maneno zilizo muhimu ili msomaji ajue kwamba ulikusudia kutuma ujumbe. Waambie rafiki zako wote pamoja na wafanyikazi wenziyo kwamba anwani ili ibainike wazi kuwa ni wao kikahika waliotuma ujumbe. La si hivyo kuna mtu anayeweza kuwa anawafanyia mzaha, au Trojan inaweza kuwa imetuma programu iliyoambukizwa kwenye orodha yao nzima ya watu wanaotumiwa, wewe ukiwemo. Hata hivyo, usitumie anwani za maneno yanayotoa habari iliyo salama kwenye barua pepe zilizohifadhiwa. Kumbuka kwamba anwani za maneno hazijafichwa na zinaweza kupoteza uasili wa ujumbe uliofichwa, hivyo kuchochea hujuma. Programu nyingi za kupenya kwenye kompyuta kiharamu sasa zinaweza zenyewe kuchunguza na kunakilisha jumbe za barua pepe zilizo na mada "zinazovutia" kama vile "za ripoti", " za siri", "za kibinafsi" na viashiria vingine kwamba ujumbe huo ni mzuri.

8 ♦ Usiwahi kutuma barua pepe kwa kundi kubwa lililoorodheshwa kwenye mistari ya "kwa(To)" au "kwa(cc)". Badala yake jitumie barua pepe hiyo na lijumuishe jina la kila mmoja katika mistari ya "bcc". Hii ni adabu ya kawaida na pia tendo zuri la kibinafsi. La si hivyo, unaweza kuwa unatuma anwani ya barua pepe ya MY kwa watu usiowajua na hilo ni tendo lisilo bora, lenye kuchukiza na linaloweza kuvunja tamaa na vilevile linaweza kuwa hatari.

9 ♦ Usiwahi kujibu ujumbe uliotumwa kupitia kwa barua taka(spam), hata jaribu kuomba uondolewe kwenye orodha kama hiyo. Watumaji wa barua taka hutuma barua pepe kwa anwani nyingi na hua hawajui ni zipi "zinafanya kazi" – kumaanisha kwamba kuna mtu anayeitumia anwani ya barua pepe hiyo yako. Kwa kujibu barua kama hizo, huduma ya mtandao inakutambua kwamba akaunti yako ni "hai" na kuna uwezekano kwamba utapokea barua taka nyinginezo.

10 ♦ Ikiwezenana, kuna na kompyuta nyingine kando, isiyounganishwa kwa nyingine, inayoweza kutumiwa kupokea barua pepe na isiwe na faili zozote za data.

11 ♦ Unaweza pia kutumia ama anwani mbili za barua pepe kuwasiliana nao (kama ule mfano wa nambari mbili za dharura za simu na sheria zile zile kutumika) au, anwani moja pekee ambayo kisanduku cha barua chake kinaweza kutumiwa na watu waaminifu wa shirika lenu: barua pepe hizo hazitahitaji kutumwa zaidi ya mara moja na zinaweza kushauriwa na wengi. Kumbuka kwamba kadiri watu wengi wanavyoijua, ndivyo usalama wake unapopungua. Badilisha anwani yako kila wakati.

## Ufichaji data: Maswali na Majibu

Ifuatayo ni orodha ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara pamoja na majibu yake. Kuwa huru kutuuliza chochote ambacho ungependa kujua kwa kuwasiliana na Shirika lisilo la Kitaifa la Privaterra kupitia kwa www.privaterra.org.

### S: Ni nini maana ya ufichaji wa data?

**J:** Hii ina maana ya uvurugaji data na kuiweka katika msimbo wa siri ambao hauwezi kufumbuliwa ila na watu waliokusudiwa. Kwa kuwa na muda wa kutosha na uwezo mkubwa wa kutumia kompyuta ujumbe uliofichwa unaweza kusomwa, lakini hali hii inaweza kuchukua muda mrefu na rasilimali nyingi. Hivi ni kusema, ufichaji wa data ni njia ya kuhifadhi faili zako na barua ili zisisomwe na watu wapekuzi. Faili zako huhawilishwa hadi katika msimbo – mkusanyiko usio maalum wa nambari na barua – ambao haujengi mantiki kwa mtu yeyote anayeutazama... Kuficha faili, "unaifunga" kwa ufunguo, unaowakilishwa na kauli ya siri. Inaweza tu kufunguliwa na mpokezi mkusudiwa, akitumia kauli yake binafsi ya siri.

### S: Kwa nini makundi ya watetezi wa haki za binadamu watumie mbinu iliyo ya ufichaji data?

**J:** Kila mtu afaa kutumia mbinu hii, kwa kuwa kimsingi, mawasiliano ya kitarakimu si salama. Hata hivyo, wafanyikazi wa kutetea haki za binadamu wanakabiliwa na hatari zaidi kuliko watu wengine wengi, kisha faili na mawasiliano yao ni nyeti zaidi. Ni muhimu zaidi kwa watetezi wa haki za binadamu kutumia mbinu hii ya ufichaji wa data ili wajilinde na pia kuwalinda watu wanaowasaidia.

Teknolojia ya kitarakimu ni faida kwa makundi ya kutetea haki za binadamu, kwani hawaruhusu kuwasiliana kwa wepesi, huwa na utendakazi thabiti na fursa nyinginezo hupatikana. Hata hivyo, palipo na faida bila shaka hatari hutokea. Kwa sababu tu kwamba umejifunga mkanda wa usalama haina maana kwamba utapata ajali wakati wowote utakaoendesha gari. Kuendesha gari katika hali hatari zaidi, kama vile katika mashindano, hukupelekea zaidi kutumia mkanda wa usalama, ili tu uwe salama.

Wafanyikazi wa kutetea haki za binadamu ni walengwa wa ujasusi wanaojulikana. Kwa vile barua pepe zilizofichwa zinaweza kusomwa na yeyote, kuna uwezekano wa mkubwa kwamba barua pepe zako ambazo hazijafichwa zitasomwa. Jumbe

zako zinaweza kuwa tayari zinachunguzwa na wapinzani wako na huwezi kujua hilo. Wapinzani wa watu unaofanya kazi ili kuwasaida wanaweza pia kuwa wapinzani wako.

**S: Je, ni haramu kutumia njia hii ya ufichaji data?**

**J:** Wakati mwingine. Ni halali bila shaka kutumia mbinu ya ufichaji data katika nchi nyingi za ulimwenguni. Hata hivyo kuna vighairi. Katika nchi ya Uchina, kwa mfano, mashirika hayana budi kupata kibali ili kutumia mbinu hii, na teknolojia yoyote ya aina hii kwenye kompyuta yako ndogo inayoweza kuwekwa mapajani ni lazima ijulikane unaoingia nchini. Nchi za Singapore na Malysia zina sheria zinazomhitaji yeyote anayependa kutumia teknolojia hii aweze kujulisha funguo za binafsi. Sheria kama hizo hazijaanza kutumiwa nchini India. Vighairi vingine vingalipo pia.

Makazi ya habari za kibinafsi za kielektroniki(Electronic Privacy Information Centre (EPIC)) hutoa sera ya ufichaji data ya uchunguzi wa kimataifa inayojadili sheria katika nchi kadhaa kwenye http://www.zepic.org/reports/crypto 2000/. Orodha hii ilisawazishwa mwaka 2000. Iwapo una haja basi waweza kuangalia kwenye Privaterra kabla ya kutumia mbinu hii ya ufichaji data katika nchi mahsusi.

**S: Tunapaswa kufanya nini ili kulinda usalama wa mifumo ya kutumia kompyuta?**

**J:** Inategemea mfumo wako wa kompyuta na shughuli zako, lakini kwa jumla, kila mmoja anapaswa kuwa na:

- Kizuizi cha umeme
- Diski ya kuficha data
- Barua pepe iliyofichwa ambayo pia yaweza kutia sahihi kitarakimu kama vile PGP
- Programu za kugundua virusi
- Kisaidizi cha kuhifadhi kilicho salama: tuma barua pepe ya kila kitu kwa tovuti iliyo salama na fanya hifadhi ya kila siku kwenye santuri ya CD-RW. Kisha uihifadhi mahali palipojitenga na penye salama
- Kauli za siri zinazoweza kukumbukwa lakini sio za kukisia
- Utaratibu wa kuzifikia faili – kila mmoja katika shirika hafai kuweza kuzifikia faili
- Matumizi ya kila mara – hakuna zana zozote zinazoweza kufanya kazi usipozitumia kila mara!

Lakini kuwa na programu ifaayo siyo suluhisho la kila kitu. **Watu binafsi mara nyingi ndiyo huwa kiunganisho kilicho dhaifu zaidi, siyo teknolojia**. Ufichaji data wa siri hauwezi kufanya kazi iwapo watu binafsi hawafanyi hivyo kila mara, iwapo wanabadilishana kauli siri zao bila kuwatambua wale wanaowapa au wanapozidhihirisha wazi zikaonekane, kwa mfano, kwenye muonekano uliogandishwa kwenye kiwambo chao cha kompyuta. Programu za kusaidia kuhifadhi data kutokana na dharura inayoweza kutokea hazitakusaidia wakati wa janga kama

moto au uvamizi iwapo hutaweka hifadhi ya nakala ya programu hiyo katika eneo jingine salama. Habari nyeti inafaa kuchukuliwa kwa msingi wa kutaka kkufahamu badala ya kubadilishana na kila mmoja kwenye shirika, kwa hivyo unafaa kujenga daraja na itifaki. Kwa jumla, ni muhimu kutahadhari kuhusu usiri na usalama katika shughuli zako za kila siku. Hii inafahamika kama "wazimu unaofaa".

**S: Nitachagua vipi programu ya ufichaji data inayofaa?**

**J:** Unaweza kuwauliza rafikizo – kisha uthibitishe na sisi. Unafaa kuwasiliana na watu na makundi fulani, kwa hivyo iwapo wanatumia mfumo wa ufichaji data ulio mahsusi, uitumie nawe pia ili kurahisisha mawasiliano. Hata hivyo, pata kujua kutoka kwetu kwanza. Programu nyingine huwa si nzuri tu, nyinginezo huwa ni nzuri zaidi. Hizo zinazofanya kazi vizuri zaidi hukuvutia katika kutumia programu huru na zilizo bora zaidi zinazotolewa na watu wenyewe wanaotaka kukufanyia ujasusi. Ni uzuri ulioje kutambua udhaifu wako katika mawasiliano kuliko kuwa msimamizi wa programu yako ya ufichaji data? Katika hali hiyo, zipo brandi nyingi za programu za kibiashara na zile zilizo huru – kumbuka kuzifanyia uchunguzi tu kabla ya kuzitumia.[3]

**S: Je, kutotumia ufichaji wa data kutaniweka katika hatari zaidi ya kukamatwa?**

**J:** Hakuna yeyote atakayejua kwamba unatumia mbinu kama hiyo ila tu labda barua yako pepe iwe inachunguzwa. Kama ni hivyo, habari yako ya kibinafsi basi itakuwa inasomwa. Hivyo basi ina maana kuwa wewe u katika harakati ya kusakwa na wale wanaokupeleleza. Kuna haja kwamba wanaokupeleleza wanaweza kutumia mbinu nyinginezo iwapo hawataweza tena kusoma barua pepe zako, kwa hivyo ni muhimu kujua wafanyikazi wenzi wako kisha utekeleze sera salama za kusaidia baadaye na usimamizi mzuri wa kila mara wa afisi, wakati huo huo ukianza kutumia mbinu ya kuficha data.

(Tanbihi: Hatuna habari yoyote kwamba ufichaji data umesababisha matatizo kwa watetezi wa haki. Hata hivyo, zingatia uwezekano huu kwa makini kabla ya kuanza kuficha data, hasa utakapokuwa katika nchi iliyo na mapigano makali ya kijeshi – upelelezi wa kijeshi unaweza kuwa na tuhuma kwamba unaweza kusambaza habari inayofaa kutokana na mtazamo wa kijeshi – au iwapo watetezi wachache watatumia mbinu ya ufichaji data – basi hali hii itafanya watu wawe na shaka nawe.

**S: Pana haja gani ya sisi kuficha barua pepe na stakabadhi nyingine kila wakati?**

**J:** Utakapotumia mbinu hii kwa masuala fulani nyeti, wale wanaokuchunguza wewe au wateja wako wanaweza kukisia ni lini shughuli muhimu inatendeka, hivyo wanaweza kuanza kuwasaka nyakati hizo. Kwa kuwa hawataweza kusoma ujumbe wako uliofichwa, wanaweza kutambua iwapo umefichwa au la. Kuongezeka kwa ghafla kwa ujumbe uliofichwa kunaweza kuchochea uvamizi, kwa hivyo ni wazo zuri kuanza kutumia mbinu hiyo kabla ya miradi maalum kuanza. Kihakika, ni bora

3 Kwa mfano, PGP- "*Pretty Good Privacy*" –ni brandi iliyo maarufu na salama. Unaweza kuipata kutoka kwa www.pgpi.org

kuhakikisha kwamba mikondo yote ya mawasiliano inatiririka vizuri. Tuma barua pepe zilizofichwa baada ya kipindi fulani cha wakati, hata iwapo hakuna chocote kipya cha kuripoti. Hivi, utakapopaia kutuma ujumbe nyeti, hautatambulika kwa haraka.

**S: Iwapo nina kizuizi cha umeme, kwa nini ninahitaji kuficha barua pepe yangu?**

**J:** Vizuizi vya umeme huzuia wapenyezi haramu kutoifikia draivu ngumu na hata mtandao japo, pindi utakapotuma barua pepe kwenye mtandao, itakuwa wazi kusomwa na kila mtu. Unapaswa kuilinda kabla ya kuituma.

**S: Hakuna yeyote anayeivamia afisi yangu kwa hivyo, kwa nini nitumie programu ya siri?**

**J:** Hujui iwapo kuna mtu anayepenya katika mfumo wa kompyuta yako, au anayefichua habari. Bila ya mawasiliano yaliyofichwa, usalama wa nje ya itifaki za kisiri, mtu yeyote aweza kuwa anazichokora faili zako, akisoma barua pepe zako na akibadilisha apendavyo stakabadhi zako bila ya wewe kujua. Mawasiliano yako ya wazi yanaweza pia kuwahatarisha watu wengine hasa katika maeneo ambayo uvamizi uliochochewa kisiasa unaweza kutokea. Ukifunga milango yako, unapaswa kuwa umeficha faili zako. Ni hivyo tu rahisi.

**S: Hatuna huduma ya mtandao na lazima tutumie mgahawa wa mtandao. Tutaweza vipi kuuhifadhi ujumbe uliotumwa kutoka kwa kompyuta ya nje?**

**J:** Ungali unaweza kuficha barua pepe na faili zako. Kabla ya kwenda kwa mgahawa wa mtandao, zifiche faili zozote unazokusudia kutuma na zinakilishe katika mtindo fiche kwenye mgahawa wa mtandao, jisajili kwa huduma ya ufichaji data kama vile kwenye www.husmail.com au huduma isiyojulikana jina, kama vile www.anonymizer.com kisha uzitumie tovuti hizi unapotuma barua pepe zako. Hakikisha kwamba wapokezi wa barua pepe zako wamejisajili kwa huduma hizi pia.

**S: Ikiwa ni muhimu kuziweka salama faili na mawasiliano yetu, kwa nini kila mtu hafanyi hivyo?**

**J:** Teknolojia ni mpya kiasi, lakini matumizi yake yanaongezeka sana.Benki, mashirika ya kimataifa, mashirika ya habari na serikali nyingi hutumia mbinu hii ya kuficha data, wakiichukulia kama uwekezaji bora na njia mwafaka ya kufanya biashara. Mashirika yasiyo ya kiserikali yanakabiliwa na hatari zaidi kuliko kampuni, ambazo hukubaliwa na serikali nyingi. Mashirika haya yanaweza kulengwa zaidi na wapelelezi na hivyo basi yanapaswa kufanya juhudi kubwa ya kuishirikisha teknolojia hiyo. Wafanyikazi wa haki za binadamu wana haja ya kuwatetea watu binafsi walioteswa na pia makundi ya aina hiyo. Ili kufanya hivyo, wao huhifadhi faili wanazoweza kutumia kutambua na kujua mahali waliko watu. Faili hizi zikipatikana, watu hawa binafsi wanaweza kuuawa, kuteswa, kutekwa nyara au "kubembelezwa" ili wasilipe shirika lisilo la kiserikali tena msaada. Habari kutoka kwa faili yaweza pia kutumiwa kama ushahidi dhidi ya shirika hilo la serikali na wateja walo katika mashtaka ya kisiasa.

**S: Moja katika kanuni zetu ni wazi. Tunaishawishi serikali kadri iwezekanavyo ifanye mambo kwa uwazi. Itakuwaje tutumie teknolojia ya usiri?**

**J:** Usiri huenda sambamba na uwazi. Iwapo serikali ingependa kuziona faili zenu, inaweza kufanya hivyo kwa kutumia taratibu zifaazo na zinazotambulika. Teknolojia ya usiri huwakomesha watu kuchokora habari yako kwa njia ya siri.

**S: Tunazifuata itifaki zote za usiri na usalama kisha habari yetu ingali inafichuka-ni kitu gani kinaendelea?**

**J:** Mnaweza kuwa na mpelelezi katika shirika lenu au mtu asiyeweza tu kuhifadhi usiri wa habari. Zingatieni upya utaratibu mnaotumia katika utoaji wa habari ili kuhakikisha kwamba ni watu wachache tu wanaoweza kuifikia habari nyeti – kisha jaribu kuwachunguza kwa karibu watu hao. Kila mara mashirika makubwa hutoa vipande vya habari isiyo ya kweli kwa watu mahsusi. Ikiwa habari hii ya uwongo itafichuka, ufichuo huo unaweza kufuatiliwa nyuma hadi kwa mwajiriwa aliyepewa habari ya asili hiyo ya uwongo.

## Yanayofaa na yasiyofaa katika utumiaji wa mbinu ya ufichaji:

- Tumia mbinu hii ya ufichaji data kila mara. Ukiificha habari nyeti pekee, yeyote anayechunguza mkondo wa barua pepe zako atajua ni lini jambo la muhimu linakaribia kutendeka. Kuongezeka kwa ghafla kwa matumizi ya ufichaji data kunaweza kusababisha uvamizi.

- Usiweke habari nyeti kwenye kichwa cha ujumbe. Mara nyingi habari hiyo huwa haikufichwa, hata kama ujumbe umefichwa.

- Tumia kauli pekee ya siri yenye herufi, nambari, nafasi baina ya maneno na uakifishaji unayoweza kukumbuka. Mbinu nyingine za kuunda kauli ya siri iliyo salama ni kwa kutumia maumbo kwenye ubao wa kubonyeza kwa kompyuta au maneno yasiyo na mpangilio maalum yaliyotungwa pamoja na alama fulani kuwekwa baina yao. Kwa jumla, kadiri ilivyo ndefu kauli ya siri ndiyo itakavyokuwa bora zaidi.

- Usitumie neno moja pekee, jina, kauli maarufu au anwani katika kitabu chako cha anwaniili kuunda kauli yako ya siri. Kauli hiyo yaweza kugunduliwa kwa haraka.

- Hifadhi kando ufunguo wa kisiri (faili iliyosheheni ufunguo wako wa siri kwa ajili ya programu ya ufichaji data), mahali palipo salama, kama vile kufichwa kwenye diski tepetevu au kwenye "mtungo wa ufunguo" ulio mdogo sana na unaoweza kutolewa, kifaa cha kuhifadhi cha USB.

- Usimtumie mtu ujumbe ulio nyeti kwa sababu tu kwamba amekutumia barua pepe iliyofichwa kwa kutumia jina unalolitambua. Mtu yeyote anaweza kughushi jina kwa kutumia anwani yake ya barua pepe ikakuonekania kama

mtu unayemjua. Daima jitahidi kuthibitisha utambulisho wa mtu yeyote kabla ya kuamini chanzo cha barua kama hiyo – wasiliana naye binafsi, chunguza kwa kutumia simu au tuma barua nyingineyo pepe ili kukagua mara dufu.

- Wafundishe wengine kutumia mbinu ya ufichaji data. Kadiri watu wanavyotumia zaidi ndipo tutakapokuwa sote salama zaidi.

- Usisahau kuweka sahihi yako kwenye ujumbe wako licha ya kuuficha. Ungependa mpokeaji wa ujumbe wako ajue iwapo habari unayotuma imebadilishwa wakati wa kutumwa.

- Zihifadhi faili zilizotumwa kama viambatanisho vya kando kwa jumla faili hizi huwa hazijafichika zenyewe unapokuwa unatuma barua pepe iliyofichika.

## Mwongozo wa usimamizi salama wa afisi na habari

### Usimamizi ulio wa salama wa afisi

Usimamizi wa aina hii unahusu kuwa na mazoea. Mazoea ya usimamizi wa afisi yanaweza kuwa na manufaa au madhara. Ili kukuza mazoea kama haya inapelekea kufahamu mantiki yake. Tumaeikusanya orodha za mazoea yanayoweza kukusaidia kusimamia kazi yako kwa njia salama zaidi – lakini tu iwapo utayakuza mazoea haya kisha uwazie umuhimu wake.

Ni nini kilicho muhimu kwa usiri na usalama katika usimamizi wa afisi?

- Kuwa na utambuzi wa habari unayomiliki na kufahamu ni nani anayeweza kuifikia
- Kukuza mazoea yaliyo ya salama na kuyatumia kila mara
- Kutumia zana ipasavyo.

### Usimamizi

Mashirika mengi yana msimamizi anayeshughulika na mfumo mzima wa mawasiliano ya kompyuta au mtu aliye na istihaki ya kiutawala ya kuzisoma barua pepe, kuunda mtandao wa kompyuta na kusimamia uwekaji wa programu mpya. Iwapo kuna mtu angewacha kazi au hayupo tu, msimamizi huyo anaweza kupekua habari ya kibinafsi ya mtu huyo na hiyo basi shughuli kuendelea kama kawaida. Pia, hii ina maana kwamba kuna mtu anayepaswa kuhakikisha kwamba programu za kompyuta ni safi na kwamba asili yake ni inabainika kama iliyo bora. Shida ni kwamba baadhi ya mashirika huchukulia kwamba kazi hii ni usaidizi wa kiufundi kisha huruhusu mtu mwingine kuchukua majukumu hayo ya kiusimamizi. Msimamizi huyu ana udhibiti mzuri wa habari yote katika shirika, na hivyo ni lazima awe mwaminifu zaidi. Mashirika mengine hugawana majukumu ya kiusimamizi baina ya Mkuu wa Shirika na mtu mwingine binafsi anayeaminika.

Mashirika mengine huchagua kukusanya funguo za kibinafsi za PGP pamoja na maneno ya siri, kisha huyaficha halafu baadaye huyaweka kwenye shirika jingine la mbali lililo salama. Hali hii huzuia matatizo iwapo watu binafsi watasahau maneno yao ya siri au wanapopoteza ufunguo wao wa kibinafsi. Hata hivyo, mahali panapohifadhiwa faili panafaa pawe salama zaidi na penye kuaminiwa, na itifaki nyingi mahsusi zinazohusiana na jinsi ya kuzifikia faili zinafaa kubuniwa.

**Kanuni:**

1 ♦ Usiwahi kutoa haki za kiusimamizi kwa mwanakandarasi mwingine. Si tu kwamba wanakandarasi hao hawaaminiwi zaidi kuliko wafanyikazi wa shirika, bali mtu mwingine aliye nje ya afisi aweza pia kupata ugumu wa kufika hapo katika hali za kidharura.

2 ♦ Watu binafsi pekee wanaoaminiwa ndio wanaopaswa kupewa haki za kiusimamizi.

3 ♦ Kadiria kiwango cha habari inayofaa kumfikia msimamizi: kompyuta zote, kauli za siri za kompyuta, kauli za siri za kujisajili kwenye kompyuta, funguo za PGP na kauli za siri nk.

4 ♦ Ukiamua kuhifadhi nakala za kauli za siri na funguo za kibinafsi za PGP kwa shirika jinginelo, huna budi kujenga itifaki za kuzifikia nakala na funguo hizo.

5 ♦ Iwapo mtu binafsi ataacha kazi, kauli zake za siri na misimbo ya kutumia kwenye kompyuta inafaa kubadilishwa mara moja.

6 ♦ Iwapo mtu aliye na haki za kiusimamizi ataacha kazi, kauli zote za siri na misimbo ya kutumia kwenye kompyuta inafaa kubadilishwa mara moja.

## Usimamizi wa programu

Kutumia programu zilizonakiliwa kiharamu kunaweza kulitumbukiza shirika kwenye hatari kwa sababu ya kutumia programu haramu, kulipa faini kubwa na hatimaye kulifunga kabisa hilo shirika. Shirika hilo huhurumiwa au hupata msaada wa wachache kutoka kwa vyombo vya habari vya mataifa ya Magharibi kwa kuwa haitaonekana kwamba huu ni ushambulizi dhidi ya mashirika yasiyo ya serikali ya haki za binadamu, lakini kama shambulizi dhidi ya wizi wa programu. Jitahidini sana kuwa waangalifu kuhusu vibali vya programu zenu na kamwe msiruhusu programu zinakilishwe kiholela na yeyote afisini. Programu zilizonakiliwa kiharamu zinaweza pia kuwa si salama kwa kuwa zinaweza kusheheni virusi. Daima tumia huduma ya kukabiliana na virusi wakati wote wa kuiweka programu kwenye kompyuta.

Msimamizi anafaa kuwa na udhibiti wa programu mpya inayowekwa ili ahakikishe kwamba inakaguliwa kwanza. Usiruhusu uwekaji wa programu zinazoweza kuwa si salama kwenye kompyuta, bali hakikisha kwamba unaziweka zile zinazofaa pekee.

Viweke viunga vya sasa vya usalama kwenye programu zote zinazotumika, hasa *Microsoft Office, Microsoft Internet Explorer na Netscape*. Tishio kubwa zaidi dhidi ya usalama linatokana na programu za ndani ya kompyuta na diski ngumu

zilizoletwa na udhaifu unaojulikana. Bora zaidi, unaweza kubadili programu hadi ile ya *Open Source*, ambayo haitegemei mtindo wa "usalama kupitia kwa vizuizi", bali huwaruhusu wataalamu wa usalama na wapenyezi wa kisiri kujaribisha misimbo yote. Kutumia programu ya "*Open Source*" na program nyinginezo zaidi ya Microsoft kuna faida ya ziada ya kufanya usiwe na tishio la programu yako kuambukizwa virusi vya kawaida na kuwa na wapenyezi wasio mahususi katika kompyuta yako. Virusi vichache vinaundwa kwa ajili ya mifumo ya utendakazi wa kompyuta ya *Linuz* au *Macintosh* kwa sababu watu wengi hutumia *Windows Outlook* na ndiyo programu maarufu zaidi inayotumiwa kwenye harakati za barua pepe, na hivyo basi ndiyo maarufu zaidi kwa wapenyezi wa kisiri katika kompyuta yako.

## Desturi za kutumia barua pepe

Ufichaji wa barua pepe unapaswa kuwa desturi. Ni rahisi kukumbuka kuficha kila kitu kuliko kuwa na sera kuhusu lini barua pepe inafaa kufichwa na lini isifichwe. Kumbuka, ikiwa barua pepe hufichwa kila wakati, hakuna yeyote anayechunguza mtiririko wako wa barua pepe atawahi kujua wakati ambao mawasiliano yenu yana umuhimu na ni nyeti.

## Hoja chache muhimu nyinginezo:

- Hifadhi barua pepe zote kila mara katika mtindo wa ufichaji data. Unaweza kuifichua tena wakati wowote baadaye, lakini iwapo mtu mwingine ataifungua kompyuta yako, itakuwa tu na hatari ambayo haikufichwa.

- Endelea kuwa pamoja na yule mnayebadilishana barua pepe zilizofichwa ili kuhakikisha kwamba watu wengine hawazifichui wala hawazitumi upya kwa watu wengine, au kuzijibu bila ya kuwa na bughudha ya kuzificha. Uzembe wa mtu binafsi ndilo tishio kubwa zidi katika mawasiliano yenu.

- Unaweza kuwa unapenda kuunda akaunti chache zilizo salama za barua pepe kwa ajili ya watu walio nyanjani na ambazo kijumla hazitumiki, kwa hivyo usije ukakumbana na watumizi wa mtandao wanaotumia barua pepe zilizo taka. Anwani hizi zinafaa kukaguliwa kila mara lakini zisitumike, ila na wafanyikazi walio nyanjani. Hivi unaweza kuharibu anwani za barua pepe zinazopokea barua pepe taka bila kuhatarisha hifadhi ya watu unaowasiliana nao.

## Vidokezi vya kijumla kwa ajili ya migahawa ya mtandao na zaidi ya hapo

Barua pepe zilizotumiwa katika matini ya kawaida, au ambazo hazikufichwa kwenye mtandao zinaweza kusomwa na watu wengi, iwapo watakuwa na juhudi ya kufanya hivyo. Mojawapo wa hii, inaweza kuwa huduma ya utoaji mtandao pale kazini au huduma kama hiyo yoyote ambayo barua pepe zako hupitia. Barua pepe hupitia kwenye kompyuta nyingi zikitoka kwa mtumaji hadi kwa mpokezi; huwa zinapuuza mipaka ya kisiasa,ya jiografia ya nchi na huweza kupitia katika vitengo vya utoaji mtandao wa nchi nyingine hata kama unatuma barua pepe katika nchi uliyomo. Baadhi ya vidokezi vya kijumla kuhusu masuala ambayo hayajaeleweka vizuri na watumizi wa mtandao:

- Kutumia neno la siri ili kulinda faili hakuna natija kubwa katika kuilinda, hivi kwamba haiwezekani kulinda stakabadhi zilizo na habari nyeti. Kufanya hivyo huleta tu dhana potofu ya kwamba usalama upo.

- Kuifunga faili hakuizuii kutazamwa ndani na yeyote anayetaka kufanya hivyo.

- Iwapo ungependa kuhakikisha kwamba faili au barua pepe imetumwa kwa njia ya salama, tumia mbinu ya ufichaji data (tazama www.privaterra.com).

- Iwapo unataka kutuma barua pepe au stakabadhi kwa njia ya salama, tumia mbinu ya kuficha katika kila hatua hadi itakapomfikia mpokezi. Si bora kutuma barua pepe iliyofichwa kutoka kwa afisi ya nyanjani mahali ulipo hadi New York au London au popote pale kisha kuwatumia wengine barua iyo hiyo bila ya kuificha.

- Kiasili mtandao ni wa ulimwengu mzima. Hakuna tofauti baina ya kutuma barua pepe kati ya afisi mbili kule Manhattan na kutuma barua pepe kutoka kwa mgahawa wa mtandao nchini Afika Kusini hadi afisi iliyo na kompyuta kule London.

- Tumia mbinu ya kuficha data kila mara iwezekanavyo, hata kama barua pepe au data unayotuma si nyeti.

- Hakikisha kwamba kompyuta unayotumia ina programu ya kuilinda dhidi ya virusi. Virusi vingi huandikwa ili kuchopoa habari kutoka kwa kompyuta yako, iwe ni ile inayopatikana kwenye diski ngumu au hifadhi za barua pepe zako, vikiwemo vitabu vya anwani za barua pepe.

- Hakikisha kwamba programu zako zina idhini ya sawasawa. Iwapo unatumia programu ambayo haijaidhinishwa, basi moja kwa moja unakuwa mwizi wa programu machoni mwa serikali na vyombo vya habari badala ya kuwa mwanaharakati wa haki za binadamu. Chaguzi bora ni kutumia programu ya open source – ni ya bure!

- Hakuna suluhu yenye usalama wa asili mia mia moja katika matumizi ya mtandao. Tahadhari kwamba mtu aweza "kuingia kiharamu" katika mfumo wa mtandao wa kompyuta kwa kusingizia kwamba yeye si mmoja wao kwenye simu au barua pepe. Fanya uamuzi wako ulio bora na pia tumia mantiki ifaayo.

## Muhtasari

Kumbuka kwamba watu walio na haja ya kazi yako hawajasubiri teknolojia ije ndiposa wajaribu kuchopoa habari kutoka kwako.

Watetezi wengi wa haki za binadamu hawana hamu kubwa ya kutumia teknolojia ili kuhifadhi habari. Ilhali, taratibu za kimsingi za kufanya hivyo ni nyepesi.

Taratibu rahisi za kimsingi ni: busara katika mawasiliano ya simu na yale ya moja kwa moja, utumiaji wa mbinu ya kuficha data katika mawasiliano ya barua pepe, na faili zenye habari nyeti, maneno ya siri ya kufungua kompyuta yako.

Lakini kuwa na programu ya sawa siyo suluhisho la kila kitu. **Watu binafsi huwa ndio kiunganisho kilicho dhaifu zaidi, siyo teknolojia.**

# SEHEMU YA PILI

# USALAMA WA SHIRIKA

Katika sehemu ya pili ya mwongozo huu, tunashughulikia usalama kwenye kiwango cha shirika, yaani tunarejelea njia za kuimarisha usalama katika mashirika ya watetezi wa haki.

Usalama/ulinzi hauna maana tu ya kuwa na mpango wa usalama.

Unahitaji umiliki wa harakati yote nzima, kuanzia kwa kuimarisha kiwango cha kiasili cha shirika, hadi kile cha utekelezaji na hatimaye kusimamia mchakato wenyewe wa uimarishaji.

Kupata umiliki wa mchakato wote mzima ni sehemu ya usalama wenyewe.

Mchakato wa usalama wa shirika ni yakinifu na jumuishi.

Unahitaji kuwa wa kihalisia na unaofaa umbo kamili la shirika.

Ingawa utahitaji rasilimali, kubadilika kimwenendo hakuna gharama yoyote na kunaunda siala muhimu katika kuimarisha usalama.

## YALIYOMO KATIKA SEHEMU YA PILI:

**2.1** Kutathmini utendaji wa usalama wa shirika: "gurudumu la usalama"

**2.2** Kuhakikisha kwamba sheria na taratibu za usalama zinafuatwa

**2.3** Kusimamia mabadiliko ya shirika hadi kwenye sera ya kuimarisha usalama

# Kutathmini utendaji wa usalama wa shirika: Gurudumu la usalama

**Lengo:**

Kutathmini njia yenu ya kudhibiti usalama.

Kukadiria kiwango ambacho usalama umejumuishwa kwenye kazi ya watetezi wa haki za binadamu.

## Ili kutimiza haya, tunazingatia mkondo wenye sehemu mbili:

- Shirika lenyewe kujitathmini kuhusu utekelezaji wake wa usalama: shirika linachunguza utendaji wake wa usalama kwa kukusanya habari isiyoegemea upande wowote. Mchakato huu wa kujitathmini kwa shirika unaweza kuwa wa pamoja/au wa mtu binafsi. Inashangaza kuona jinsi wanachama wa shirika moja wanaweza kufikia suluhu zilizo tofauti kuhusu utendaji wa usalama wa shirika zima.

- insi "watu wengine" wanavyolichukulia shirika.

## Utathmini wa kibinafsi wa shirika kuhusu usalama

### Gurudumu la usalama

Utathmini huo unaweza kufanywa kwa kushirikisha gurudumu la usalama na tindi zake nane. Ni lazima gurudumu liwe la mviringo ili lizunguke yaani, tindi zote zinafaa ziwe za urefu ulio sawa.

Hali inaweza kuwa hivyo katika gurudumu la usalama na tindi zake (vijenzi) zinazowakilisha udhibiti wake wa usalama katika shirika au kundini mwa watetezi wa haki.

Tathmini hii yaweza kufanywa katika makundi:

- Chora kielelezo cha gurudumu.
- Jaza kila tindi kutegemea jinsi unavyofikiri imeundwa.

- Orodhesha sababu (changizaneni mawazo) za kwa nini tindi fulani hazijarefushwa zaidi; kwa kuwa tindi zote zinafaa kuwa angalau ndefu kama vilivyo tindi ndefu zaidi, pendekeza njia za kutimiza tokeo hili: andaa malengo na michakato ifaayo, onyesha matatizo yanayoweza kutokea kisha pendekeza suluhisho.
- Utakapomaliza zoezi hili, hifadhi gurudumu lako la usalama kisha rudia zoezi hilo tena halafu tathmini hatua baada ya nyingine iwapo kuna mwimariko wote.

## Tindi nane (vijenzi) za gurudumu la usalama

- **Mshikamano na tajiriba ya usalama uliopatikana:** maarifa ya kivitendo na yenye kubadilishanwa ya usalama na ulinzi, yaliyokusanywa kupitia kwa kazi. Sehemu za kuanza na kumaliza kwa tathmini hiyo.
- **Mafunzo ya usalama:** mafunzo ya usalama kupitia kwa kozi chuoni au kupitia kwa juhudi ya kibinafsi ya mtu katika harakati za kila siku.
- **Ufahamu na mwelekeo kuhusu usalama:** unahusisha iwapo watu binafsi na shirika lote kwa jumla wanachukulia kihakika ulinzi na usalama kama vitu vya kimsingi na kwamba wako tayari kufanya kazi kuhakikisha kwamba vyote viwili vinakuwa vya kimsingi.
- **Kuupangia usalama:** kuujumuisha usalama na ulinzi katika kazi yako.
- **Kugawa majukumu:** ni nani anawajibikia nini kuhusu usalama na ulinzi? Na ni nini hutendekea kunapotokea hali ya dharura?
- **Kiwango cha umiliki wa kanuni za usalama/ utekelezaji:** ni kwa kiwango gani watu huheshimu sheria za usalama na taratibu zake?





- **Kuchangua na kukabiliana na matukio ya usalama:** ni kwa kiwango gani matukio ya usalama yanachanganuliwa? Je, majibu ya shirika yanatosha?
- **Kutathmini udhibiti wa usalama na ulinzi:** ni kwa kiwango gani shirika linatathmini udhibiti wa usalama na ulinzi wake na kwa kiwango gani linaufanyia marekebisho?

## Hapa kuna mfano kielelezo wa gurudumu la usalama:

Gurudumu hili halijawahi kukamilika: vijenzi vinginevyo vimeendelezwa zaidi kuliko vingine. Hivyo basi ni muhimu zaidi kukadiria kiwango cha maendeleo ya kila kijenzi. Katika hali hii, unaweza kutambua ni aina gani za hatua zinazohitaji kupewa kipaumbele ili kuimarisha usalama na ulinzi wako. Mistari yenye vitone kutoka katikati ya gurudumu hadi ukingoni mwake inaonyesha namna ambavyo kijenzi hiki cha gurudumu kimeendelea.

matatizo yanayohusiana na sehemu hii ya gurudumu na ambayo yanaweza kutokea…

… na suluhu zinazoweza kutolewa kwa matatizo haya




*Nakilisha gurudumu hili kwenye karatasi au asetati kisha ongeza rangi kwenye mianya baina ya tindi ili kuonyesha kidhahiri umbo halisi la gurudumu la kundi au shirika lenu. Hivyo basi, utaweza kuona kwa urahisi ni vijenzi gani vimeendelezwa sana au kwa uchache.*

## Uchanganuzi wa hatua kwa hatua wa “gurudumu la usalama”

Utathmini mzuri wa sera ya usalama wa shirika huhitaji muda wa kutathmini maana halisi ya kila kijenzi cha gurudumu la usalama.

### 1 • Mshikamano na uzoefu wa usalama uliopatikana kupitia kwa uzofu wa kazi na kubadilishana

Maarifa ya kivitendo yaliyokusanywa pamoja na mshikamano wa usalama na ulinzi. Sehemu ya kuanzia na kumalizia utathmini.

Kumbuka kwamba uzoefu wa wanachama wachache tu hauwezi kulingana na uzoefu wa usalama kwenye shirika lakini hulingana na uzoefu wa kijumla wa wanachama wote wa shirika: kubadilishana uzoefu hivyo basi kutachangia kulea mshikamano wa usalama.

Ujuzi wote utaonekana kwenye tindi: utakapokuwa umemaliza kuendeleza vijenzi vyote upendavyo tokeo ni kuwa ujuzi wote utakuwa umeshaongezeka zaidi. Kuna uwezekano kwamba maarifa ya usalama yatakuwa yameendelezwa vizuri zaidi na zile tindi nyinginezo zitahitaji kuwa hivyo. Ni shughuli isiyokamilika kwa sababu tu kwamba wanachama huja kisha wakaenda, hali ya kisiasa hubadilika na vilevile kwa usalama. Hata hivyo, habari njema ni kuwa kama yalivyo matokeo ya tindi 7 nyinginezo, hutahitaji kufanya chochote kuhusu hii tindi moja maalum (kinyume na 7 nyinginezo).

### 2 • Mafunzo kuhusu usalama

Bainisha mafunzo yoyote ya usalama ya awali ambayo umepitia ama kusoma chuoni au kutokana na juhudi yako ya kibinafsi kupitia kwa harakati za kila siku.

**Maswali yanayohitaji kuendelezwa zaidi:**

Je, taratibu za mafunzo ya usalama zinapatikana kwa kila mmoja? Je, tunazistawisha? Je, wafanyikazi wapya wamepata mafunzo? Tungekumbana na matatizo yepi iwapo tungempa kila mtu mafunzo? Ni suluhu zipi zinaweza kupatikana?

### 3 • Kujenga ufahamu kuhusu usalama na mielekeo inayofaa

**Maswali yanayoweza kutumiwa kukadiria kiwango cha sasa cha ufahamu:**

Je, kila mtu anafahamu kihakika kuhusu usalama na ulinzi? Tunaweza kutimiza haya vipi?

Kujenga ufahamu hakuna maana ya utekelezaji (kwa mfano, wavutaji sigara wanafahamu madhara ya sigara lakini wangali wanavuta).

**Maswali ya kujenga ufahamu:**

Masiala yepi yanachochoea urudiaji wa usalama?

Ni visa vipi vinavyosimuliwa na ni elimu ipi ya usalama isiyo rasmi inayopatikana kwenye shirika? Tungekumbana na matatizo yepi katika harakati ya kujenga ufahamu? Ni suluhu zipi zinazoweza kupatikana?

## 4 ● Kuupangia usalama

**Maswali yanayoweza kutumiwa kukadiria kiwango cha sasa cha mpango wa usalama:**

- Je, tuupangie usalama na ulinzi katika kazi yenu?
- Je, suala la usalama limeshirikishwa (limepewa uzito) katika mkabala mzima wa taasisi? (Lengo, mipango ya mikakati, sehemu za kazi, dhamira za kandokando)?
- Je, suala la usalama limejumuishwa miongoni mwa ajenda kwenye mikutano mingi: (na sio suala la mwisho kwenye orodha)?
- Ni mikakati ipi ya bajeti (je, ni mikakati maalum kwa ajili ya amani, au inajumuishwa tu miongoni mwa mingine) na usimamizi wa fedha?
- Je, tufanye uchunguzi wa mazingira ya kazi – katika makundi – (kwenye viwango vya ndani ya shirika, kieneo au kitaifa)?

**Je,:**

- Tuchanganue athari ya kazi na namna shirika linavyochukuliwa na washika dau wanaoweza kuwa tishio?
- Tufanye uchanganuzi mzima wa hatari:matishio, udhaifu na uwezo?
- Tuandae stakabadhi zote za usalama: turejelee upya yaliyomo na tuchunguze jinsi zinavyotumika.
- Tuandike na kuzifanyia marekebisho stakabadhi za usalama? Tukague iwapo ni za kisasa na kwa namna gani hili laweza kutimizwa? Tuchunguze iwapo athari za kazi na masiala ya hatari yamepewa mazingatio? Tuchunguze iwapo michakato ya mashauriano ya kila siku kuhusu usalama ipo?

**Je, tuna mipango ya usalama ambayo:**

- Ni rahisi na ya wazi? Je, ina habari ifaayo iliyoandikwa kwa maeneo ya wazi?
- Imewashirikisha watu wote walioathiriwa wakati inapoundwa?
- Inafaa kwa kila mazingira ya kazi?
- Imeimarishwa, ikaendelezwa na kurekebishwa? Shukrani kwa juhudi ya watu tofauti wanaofanya kazi kwenye shirika.
- Ni halali na inaweza kutumiwa katika "ulimwengu halisi".

**Je, mipango yetu ya usalama inashughulikia:**

- Vipengele vyote muhimu?
- Mawasiliano, teknolojia ya habari na usimamizi wa habari?
- Usimamizi wa wafanyikazi (ukiwemo uajiri wa kazi)? Udhibiti wa msongo wa akili?

Je, kila mtu anafahamu kwamba kundi linalofanya kazi na lenye muundo mzuri, mtiririko mzuri wa mawasiliano ya ndani, mahusiano mazuri ya kijamii na ushirikiano mzuri ni mahitaji ya kimsingi ya usalama?

**Maswali yaliyolengwa kuendeleza zaidi mpango wa usalama:**

- Ni matatizo yepi tutakayokumbana nayo iwapo tutajaribu kushughulikia kila mojawapo wa vipengele vya hapo juu?
- Ni zipi zinaweza kuwa suluhu?

## 5 ● Kugawa majukumu

**Maswali yanayoweza kutumiwa kukadiria kiwango cha sasa cha ugawaji wa majukumu ya usalama:**

- Je, tunafahamu vizuri ni nani anayewajibikia jambo lipi la usalama na ulinzi iwapo kutatokea tukio la kidharura?
- Je, yapo majukumu na wajibu wa shirika kwa wafanyikazi na wenye kushirikiana nao (ikiwemo mienendo yao mbali na kazini na nyumbani)?
- Je, kila mtu anatekeleza wajibu wake wa kulinda usalama na je, kuna majukumu mahususi ya vipengele mbalimbali vya usalama? (Tunakumbana na ugumu upi)?

**Maswali yanayohusu kuimarisha ugawaji wa majukumu ya usalama:**

- Tunakumbana na matatizo yepi iwapo tutahitaji kugawa au kugawana majukumu ya usalama?
- Ni zipi zinaweza kuwa suluhu?

Kugawa majukumu kunachangia kugawana usalama

## 6 ● Kiwango cha umiliki wa sheria za usalama/kuzitii

**Maswali ya kukadiria kiwango cha sasa cha umiliki wa sheria za usalama/kuzitii:**

- Ni kwa kiwango gani watu huheshimu sheria na taratibu za usalama?
- Ni kwa kiwango gani kila mmoja na hata kundi zima huchangia katika kuandika mpango wa usalama, na pia kuzitii sheria za ulinzi na usalama?
- Je, tunaweza kutambua iwapo sheria za usalama hazifuatwi, na kama sivyo, kwa nini?
- Je, watu wanatii sheria za usalama kutokana na hofu kwamba watalaumiwa wasipofanya hivyo au kwa sababu wanashawishiwa na ukweli kwamba kuzifuata sheria hizi kutapunguza matokeo ya hatari? (kwa mfano dereva anaweza kuvaa mshipi wa usalama ama kwa kuhofia kwamba atapigwa faini asipofanya hivyo au anashawishiwa kwamba kufanya hivyo kutapunguza uwezekano wa kutokea ajali).

**Maswali yanayohusu kuimarisha kiwango cha umiliki wa sheria za usalama/kuziti:**

- Ni matatizo yepi tungekumbana nayo katika uimarishaji wa kiwango cha kuzipa uzito sheria za usalama?
- Ni suluhu zipi zinaweza kupatikana?

## 7 • Kuchanganua tukio la usalama na hisia

**Maswali yanayotumiwa kukadiria kiwango cha sasa cha kuchanganua tukio la usalama pamoja na hisia za wanashirika:**

- Ni kwa kiwango gani matukio ya usalama yanachanganuliwa na je, yanaibua maonirejea ya kutosha kutoka kwa shirika? Ni matukio yepi ya usalama yalitokea? Yalichukuliwa vipi na uharibifu gani ulisababishwa?
- Je, tunaandaa ripoti ya hayo (na vipi)?
- Je, tunafanya uchanganuzi (vipi na kwa kiwango gani)?
- Ni yepi maonirejea (makataa, utaratibu wa kutoa maonirejea, majukumu)?
- Tunatathmini vipi maonirejea?
- Je, mafunzo yanatolewa kwenye shirika kwa msingi wa matukio yaliyotokea (je, yanatolewa kweli? Je, kuna njia za kitaasisi zinazofuatia kwa hili)?
- Kwa ufupi, matukio haya hufanyiwa nini?
- Je, kuna utaratibu wa kufuatwa katika ukusanyaji, uchunguzi na uchanganuzi wa matukio ya usalama ili kujenga maonirejea ya msingi kwa ajili ya mikakati na mipango yetu? Je, mahitimisho yamejumuishwa katika kazi na tathmini zetu (panapofaa)?
- Ni kwa aina gani za kidharura ambazo mipango hiyo hutumiwa?
- Je, kuna mipango na majukumu ya wazi yanayoshughulikia makabiliano iwapo kutatokea dharura?

**Maswali kuhusu uimarishaji wa makabiliano na uchanganuzi wa matukio ya usalama:**

- Ni matatizo yepi yanatokana na uimarishaji wa kila kipengele kilichotajwa hapo juu?
- Ni suluhu zipi zinaweza kupatikana?

## 8 • Kutathmini usimamizi wa usalama na ulinzi

**Maswali ya kukadiria kiwango cha sasa cha utathmini wa usimamizi wa usalama na ulinzi**:

- Ni kwa kiwango gani shirika linatathmini usimamizi wa usalama na ulinzi wake? Na ni kwa kiwango gani hili hurejelewa upya?
- Je, ukadiriaji huo ni shughuli ya kitaasisi?
- Je, tunafahamu kuwa kazi na harakati za kila siku kunapotokea dharura ya matukio ya usalama, zinafaa (harakati na kazi) kuchanganuliwa kwa mtazamo wa kiusalama ili ziweze kuchangia kwa ujuzi na uzoefu wa kila mmoja na wa shirika?

**Maswali yanayolenga kuimarisha utathmini wa usimamizi wa usalama na ulinzi:**

- Ni matatizo yepi tutakumbana nayo katika kuimarisha utathmini wa usimamizi wa usalama na ulinzi?
- Ni suluhu zipi zinaweza kupatikana?

## Jinsi 'watu wengine' wanavyolitambua shirika

### Usalama na heshima yetu

Ni muhimu kuchunguza mazingira ya shirika ili kutazama jinsi hadhi yake ya kiuendeshaji inavyotambuliwa na iwapo inalingana na hadhi ambayo shirika hili linafaa kuwa nayo. Ni muhimu pia kutaka kujua namna watu wengine wanavyotambua usalama na ulinzi wa shirika. Hili linafaa kutekelezwa kwa misingi ya mitazamo ifuatayo:

- Kutokana na mtazamo wa watu tunaofanya nao kazi: wafanyikazi wenza, wanaofaidika na shirika
- Wenzi wetu wa kazini na mashirika kama hilo letu.
- Wafadhili wenye kudhamini taasisi kifedha na (wengine wanaweza kukubali kudhamini kuliko wengine)
- Mamlaka tunazohusiana nazo
- Washika dau wengine wanaoweza kuhujumu
- …..

Ni muhimu pia kuwa na uhakika wa kiwango gani cha ushirikiano wa usalama tulio nao na mashirika au miungano mingine, na wenzi wetu, na watu tunaofanya nao kazi, nk.

### Hapo kuna orodha mbili zisizo kamilifu za maswali muhimu kuhusu mada hii:

**I ♦ Hadhi ya shirika na athari ya kazi yake. Tunaweza kutathmini vipi hili?**

- Tutajifunza vipi kuhusu hadhi ya shirika letu?
- Jinsi gani ya kuwaeleza watu wengine?
- Ni nini lengo la shirika?
- Shughuli zetu ni zipi?
- Shughuli zetu huathiri vipi washikadau waliojihami au wengineo?
- Ni uwezo au mamlaka yepi tuliyo nayo ya kuendeleza shughuli za kazi yetu?
- Tufanye nini ili tuidumishe shughuli hii?

- Tunafikiri namna gani kuhusu namna anavyotuchukulia yeyote anayeweza kutekeleza hujuma dhidi yetu?
- Je, tunachukuliwa kama shirika linaloshughulikia masuala yanayohusiana na usalama na ulinzi kwa njia bora?
- Je, kuna yeyote anayeibainisha kazi yetu, au namna tunavyoshughulikia masuala mbalimbali, katika mtazamo wa kiusalama? Kwa nini? Tunaweza kutambua vipi hili?

**II ♦ Hadhi ya shirika na athari ya kazi yake. Tunatambuliwa vipi?**

Jaribu kujibu maswali yafuatayo kutuhusu sisi kutokana na mtazamo wa mtu "anayeuliza"; (rudia zoezi hilo kwa waulizaji wengi unavyopenda: "wao" ni wewe na "sisi" ni muulizaji).

- Wao ni nani?
- Wanatarajia nini?
- Kazi yao ni nini?
- Wanazuia vipi kazi yetu? Mipaka ya kazi yetu ni ipi?
- Tunaweza kufanya nini? Tunaweza vipi kujilinda?
- Tunaweza vipi kupata tutakalo?

Mtakapokuwa mmeshatathmini utambuzi wa wengine, mnafaa sasa kuzingatia kubadili hadhi yenu iwapo haiwafai. Sio utambuzi wote unaweza kubadilishwa, bila shaka. Lakini husaidia katika kujihadhari nao kwa kuwa wanaweza kuwa na athari fulani kwa usalama na ulinzi wenu.

## Muhtasari

Ili kutathmini usalama wako, unahitaji kutumia njia yenye mikondo miwili:

**Utathmini wa kibinafsi** (kujitazama) na pia utathmini wa namna watu wengine wanavyokuchukulia.

Utathmini wa kibinafsi unaweza kutimizwa kupitia kwa gurudumu la usalama lililo na tindi zake nane.

Ni picha halisi ya kiwango chako cha sasa cha usalama na ulinzi.

Unaruhusu kustawi kwa kila tindi ili kutimiza gurudumu zima la usalama.

Ili kuendeleza gurudumu lako la usalama, unapaswa kuanza na orodha ya mambo kuhusu hali yako ya sasa, unda malengo kisha amua ni michakato ipi ifaayo ya kuimarisha usalama wako. Jaribu kujenga matarajio ya vizuizi vinavyoweza kutokea kadiri unavyoendelea katika kutimiza malengo yako. Jaribu pia kutarajia suluhu.

**Utathmini wa namna watu wengine wanavyokuchukulia** unaweza kutimizwa kwa kujaribu kukisia namna watakavyokuwa wanazungumza juu yako.

Bila shaka, unaweza pia kuwasilisha maswali kwa watu wengine waaminifu.

Unafaa kutafuta njia ya kubadilisha mwelekeo wowote wa watu kukuhusu usiokufaa. Siyo mielekeo yote kukuhusu inaweza kubadilishwa bila shaka. Lakini husaidia sana katika kujenga ufahamu kuihusu mielekeo hiyo kwa kuwa unaweza kuwa na athari fulani kwa usalama na ulinzi wako.

# Kuhakikisha kwamba sheria na taratibu za usalama zinafuatwa

**Lengo:**

Kufikiria kuhusu ni kitu gani kinachowafanya wanachama wa mashirika na mashirika yenyewe kutoweza au kutopenda kufuata mipango na taratibu za usalama, na vile vile kutafuta suluhu zifaazo.

## Usalama ni suala linalomhusu kila mtu

Ni suala tata kubainisha iwapo kweli watu na mashirika wanafuata kihakika sheria na taratibu za usalama. Inawezekana sana kuwa na mpango mzuri wa usalama uliokamilika na ulio na sheria za kuzuia, na taratibu za kidharura, na pia kuweka usalama kama ajenda kuu kwenye mikutano mikuu n.k lakini pamoja na hayo kuna watu wasiotii sheria za usalama za shirika.

Hili linaweza kuonekana kama jambo lisiloaminika, kutokana na ukweli kwamba watetezi wa haki za binadamu hupewa matishio na shinikizo la mara kwa mara, hata hivyo jambo hili hutendeka.

Ikiwa kuna watu ambao wangependa kujua kitu kuhusu kazi yako, hawatajaribu kutafuta habari hiyo kutokana kwa mtu aliyemakini zaidi kwenye shirika. Badala yake watajaribu kusonga karibu na mtu aliye na mazoea ya kulewa kila Jumamosi usiku. Vivyo hivyo, iwapo kuna watu ambao wangependa kutoa tishio kwa shirika lenu, labda watamtenga mtu ambaye mara nyingi hajali kuhusu usalama. Vivyo hivyo, inawezekana kwamba yule aliyemakini anahujumiwa kwa kuwa yule asiyejali aliuacha mlango wazi... Hoja hapa ni kwamba kutojali kwa mtu mmoja kunaweza kuhatarisha zaidi kila mmoja. Usalama utakuwa muhimu tu iwapo mambo madogomadogo ya kimsingi yatapewa uzingatio – katika hali hii, mapuuza ya mtu mmoja.

Hii ndiyo sababu usalama unafaa kuelezwa kama suala linalokabili shirika zima, na pia watu binafsi wa shirika hilo. Ikiwa watu watatu juu ya kumi na wawili wanafuata sheria za usalama, basi shirikia lote, wakiwemo wale wanaotii sheria watakuwa wanakabiliwa na hatari. Ikiwa hali itaimarika kisha watu tisa waanze kufuata taratibu za usalama, hatari itapungua. Lakini hatari hiyo ingekuwa imepungua zaidi ikiwa watu wote 12 wangefuata sheria.

**Usalama ni suala la shirika zima,
na pia la watu binafsi kwenye shirika hilo**

Kuwa na mpango mzuri wa usalama hauna maana yoyote isipokuwa labda uwe unafuatwa. Tuseme ukweli: Watu wengine hawafuati sheria na taratibu.

Ukosefu wa utii unajenga tofuati kati ya nia nzuri na matendo halisi. Hata hivyo, ni rahisi kukabiliana na tatizo hili kuliko kukabiliana na matokeo yake.

## Kwa nini watu wanakataa kufuata sheria za usalama, na tunaweza kuzuia vipi hali hii kutoka mwanzo?

Kwanza kabisa, neno "kutii" lina maana nyinginezo za unyenyekevu na usikivu na hivyo linapasa kuepukwa. Watu hufuata tu sheria wanazozielewa na kuzikubali, kwa sababu wanaweza kuzifanya ziwe zao hasa. Kwa hivyo, neno muhimu hapa ni "umiliki".

Ili utaratibu wowote wa usalama ufuatwe, kila mtu katika shirika hana budi kuukubali. Hili halitendeki mara moja. Ili kundi la wanachama liweze kuukubali utaratibu wa usalama, ni lazima waruhusiwe kushiriki katika kuuandaa kisha kuutekeleza. Ni muhimu sana pia kutoa mafunzo, kujenga uelewa na kukubalika kwa utaratibu huo.

**Jedwali 1**: Uhusiano baina ya watu binafsi na mashirika katika mahusiko ya usalama

| Dhana | Mbinu: "kila mmoja hana budi kufuata sheria." | Mbinu: watu binafsi pamoja na shirika wamekubaliana kwa pamoja kuhusu sheria." |
|---|---|---|
| Mbinu | Inayolenga sheria | Inayotokana na mahitaji ya kiusalama wa shirika na mtu binafsi. |
| Aina ya uhusiano baina ya mtu binafsi na shirika | Bora au "ya ubaba" | Unaotokana na mazungumzo. |
| Kwa nini tunafuata sheria? | Kwa kulazimika, ili kuepuka kuwekewa vikwazo au kufukuzwa. | Kuheshimu mapatano na kuwepo kwa nafasi kukosoa na kuimarisha (Umiliki na ubembelezwaji unatimizwa tutakapokuwa tumeshawishiwa kwamba inakidhi mahitaji yetu na itapunguza uwezekano pamoja na matokeo ya hatari na kwamba itachangia katika kuwalinda wafanyi kazi wenzetu na wengine tufanyao nao/ tunawafanyia kazi. |
| Jukumu la usalama | Halijagawanywa | Limegawanywa |

Umiliki hauhusu tu "kufuata sheria," bali unahusu makubaliano kuhusu sheria zitakazowapelekea watu binafsi kuzifuata kwa kuwa wanazielewa, wanaziona kama zinazowafaa na ni bora, na wanahisi kwamba wanaziwajibika kibinafsi. Kutokana na sababu hii, sheria hizo zinafaa pia kuenda sambamba na kigezo cha kimaadili na utu pamoja na mahitaji ya kimsingi.

**Umiliki hauhusu tu "kufuata sheria," lakini unahusu kuheshimu makubaliano baina ya shirika na wanachama wa kundi kuhusiana na usalama**

Ili kudumisha makubaliano baina ya wanachama wa kundi na shirika, ni muhimu kwamba **mtu au watu binafsi wanaowajibikia usalama wanafaa kuwashirikisha watu wengine kila mara** kupitia kwa mikutano mifupi, kukumbushwa kuhusu vipengele vya makubaliano, na kwa kutaka maoni ya watu kuhusu jinsi gani sheria zinafaa au zinafanya kazi vizuri katika utekelezwaji wazo.

Kushirikishwa kama huko hata hivyo hakutakuwa na faida kubwa bila ya utamaduni wa usalama wa shirika ambao huimarisha mipango au taratibu za utendakazi ulio rasmi na usio rasmi.

**Kwa muhtasari, misingi ifaayo ya watu kuizingatia sheria na taratibu za usalama inaweza kutimizwa kupitia kwa hatua zifuatazo:**

- Kukuza uelewa kwamba usalama ni muhimu kwa ulinzi wa waathirwa, mashahidi, wanafamilia, na wafanyikazi wenza ili kuendeleza lengo la kimsingi la shirika;
- Kukuza na kuthamini utamaduni wa usalama wa shirika;
- Kuunda umiliki wa taratibu na sheria za usalama;
- Kuhakikisha kwamba wanachama wote wa kundi wanashiriki katika kuandaa na kuimarisha sheria na taratibu za usalama;
- Kuwapa watu mafunzo kuhusu masuala ya usalama;
- Kuhakikisha kwamba wanachama wote wa kundi wamewashawishi kuhusu kufaa na kutenda kazi barabara kwa sheria na taratibu za usalama;
- Kuandaa na kuhitimisha makubaliano baina ya shirika na watu binafsi kuhusu kuziheshimu sheria na taratibu za usalama;
- Kuwashirikisha wale wanaowajibikia usalama katika mikutano ya muda mfupi na kuwapa watu mafunzo, katika kuwakumbusha wanachama wa makundi kuhusu masharti ya mkataba na katika kutaka kujua maoni yao kuhusu jinsi sheria zinatekelezwa kwa njia ifaayo.

## Kwa nini sheria na taratibu za usalama hazifuatwi?

Hakuna yeyote katika watetezi wa haki za binadamu asiyefuata sheria za usalama. Watu wengi katika shirika aghalabu hufuata baadhi ya sheria lakini si zingine au huzifuata sheria hizo mara moja moja.

Kuna sababu nyingi zinazoweza kuelezea jambo hili. Ili kubadili tabia hii na kuhakikisha umiliki wazo, ni muhimu kutambulisha sababu za hayo yote kuwepo kisha kutafuta suluhu, pamoja na watu wengine walio na haja. Itakuwa pia bora kutofautisha baina ya sababu tofauti walizonazo watu za kutofuata sheria, kwa sababu bila shaka zitatofautiana.

**Baadhi ya sababu zinazoweza kuwafanya watu wasizingatie sheria na taratibu za usalama:**

## Zisizo za makusudi:

- Mtetezi hazijui sheria hizo
- Hazitumii sheria ipasavyo

## Za Makusudi:

**Matatizo ya Kijumla:**

- Sheria hizo ni changamano sana na ngumu za kufuata.
- Taratibu haziwezi kupatikana kwa urahisi au zimewasilishwa kwa njia ambayo ni vigumu kuzitumia kila siku.

**Matatizo ya Kibinafsi**:

- Sheria hizo haziambatani kikawaida na mahitaji au maslahi ya kibinafsi ya mtu na mgogoro huu hautatatuliwa.
- Mtu binafsi hawezi kukubaliana na baadhi ya sheria au zote kisha huzichukulia kama zisizofaa, au zisizo na natija yoyote kutokana na uzoefu wake, mafunzo au habari aliyowahi kusoma ya hapo nyuma au kwa sababu ya imani zake za kibinafsi.

**Matatizo ya Kikundi**:

- Wanachama wengi wa kundi huwa hawazifuati sheria, nao viongozi wa makundi ama hawazifuati kabisa au hufanya hivyo lakini huacha nyinginezo, kwa sababu hakuna mazoea ya shirika ya kuzingatia usalama.
- Ukosefu wa kijumla wa motisha pale kazini unaweza kupelekea watu kuzipuuza sheria za usalama.

**Matatizo ya Kishirika:**

- Hakuna rasilimali za kutosha za kifedha na kiufundi ambazo zitawarahisishia wanachama wa kundi kufuata sheria za usalama.
- Hakuna uwiano baina ya sheria na maeneo mahususi ya kazi. Kwa mfano, sheria zimewekwa na wanaosimamia usalama lakini zikapuuzwa au kutotekelezwa vizuri na wafanyi kazi katika vitengo vya akaunti au uundaji wa mipango. Baadhi ya sheria zinaweza zikafaa katika eneo moja la kazini kisha zisitekelezeke katika eneo jingine.
- Wanachama wa kundi pamoja na wafanyi kazi wana rundo kubwa la kazi ilhali muda wao ni mchache, hivyo basi hawapi kipaumbele baadhi ya sheria au hata zote.
- Ukosefu wa kijumla wa motisha, kutokana na msongo wa akili, mabishano katika maeneo ya kazi n. k.

Utamaduni wa shirika u katika hali rasmi na pia isiyo rasmi, na hauna budi kukuzwa si tu kwenye shirika kijumla, bali pia kwenye makundi. Utamaduni mzuri wa shirika utaonekana katika ishara kama vile kuzungumza kusiko kwa rasmi, mizaha, karamu n.k.

## Kufuatilia uzingatiaji wa taratibu na sheria za usalama

### Ufuatiliaji wa moja kwa moja:

Taratibu na sheria za usalama zinaweza kujumuishwa katika tathmini za utendakazi na "orodha ya kukagulia," na pia kwenye mikutano kabla na baada ya ziara za nyanjani, katika ripoti za kazi kwenye ajenda za mikutano n.k.

Mapitio ya baada ya kipindi fulani ya masuala kama vile uhifadhi mzuri wa habari nyeti, nakala na miongozo ya usalama, yanaweza kutekelezwa na makundi husika; kuhusu itifaki za usalama kwa ajili ya ziara za mako makuu ya shirika; kujiandaa kwenda ziara za nyanjani na kadhalika.

### Ufuatiliaji usio wa moja kwa moja:

Kutafuta maoni ya watu kuhusu taratibu na sheria za usalama, bila kutaka kujua iwapo zinafaa au ni rahisi kufuata, n.k. kunaweza kuonyesha iwapo kweli wanachama wa kundi wanazifahamu sheria, iwapo zimekubalika kikamilifu au iwapo kuna kutoelewana fulani ambako hakuna budi kushughulikiwa.

Wanachama wa kundi kuweza kutumia kitabu cha mwongozo wa usalama, itifaki na sheria nyinginezo zilizopo kwa pamoja kunaweza pia kupitiwa.

Pamoja na watu au makundi husika, inajuzu kutunga na kuchanganua maoni ya tathmini ya watu ya taratibu na sheria za usalama. Hili linaweza kutekelezwa mbali na rekodi/bila ya kujulikana au na mtu mwingine.

### Ufuatiliaji wa mambo yaliyotendeka:

Usalama unaweza kukaguliwa tena kwa kuchanganua matukio ya usalama kadiri yanavyotendeka. Jambo hili linafaa kutekelezwa kwa uangalifu zaidi. Mtu yeyote ambaye amekumbana na tukio la usalama anaweza kuhofia kwamba lilikuwa kosa lake na/au kwamba uchunguzi wa tukio utapelekea kuwekwa vikwazo dhidi yake. Anaweza kushawishika kuficha tukio hilo, au kutoliripoti lote au baadhi ya vipengele vyalo.

### Ni nani hufuatilia?

Kwa kutegemea utendakazi wa shirika, yeyote anayewajibika na kushughulikia usalama, sehemu mahususi za kazi katika usalama wenyewe na kusimamia wanachama wa kundi la usalama, atakuwa pia na jukumu la kuufuatilia usalama.

## Tunaweza kufanya nini iwapo sheria na taratibu za usalama hazifuatwi?

1 ♦ Bainisha sababu, tafuta suluhu na ziweke katika matendo. Orodha ya chaguzi katika Jedwali 1 hapo juu inaweza kutumiwa kama mwongozo.

2 ♦ Iwapo tatizo ni la makusudi na iwapo tu linahusisha mtu mmoja, jaribu:

a • Kumhusisha katika mazungumzo ili kuibanisha sababu au lengo

b • Fanya kazi na kundi zima la mtu huyo binafsi (mara nyingine, hili halitafaa, kutegemea hali yenyewe)

c • Tumia mfumo wa ilani au onyo, ili mtu huyo afahamu kikamilifu kuhusu tatizo.

d • Tumia mfumo wa kuweka vikwazo polepole ambao unaweza kumfanya mtu huyo afutwe kazi hatimaye.

3 ♦ Jumuisha sharti linalohusu kutii taratibu na sheria za usalama katika kandarasi zote za kazi, ili wafanyi kazi wote wawe na ufahamu wa jinsi gani jambo hili ni muhimu kwa shirika.

## Kwa kuhitimisha...

Kuna watu wanaoweza kudai kwamba mjadala kuhusu sababu za watu kutofuata sheria ni kupoteza wakati kwa vile kunaweza kuwepo mambo mengine muhimu ya dharura kufanya. Wale wenye maoni haya huamini kwamba sheria zipo ili zifuatwe, basi. Wengine wanafahamu kwamba hali si kama hivyo.

Kwa vyovyote vile, tunakutaka sasa urudi nyuma kisha uchanganue ni kwa kiwango gani taratibu na sheria za usalama zinafuatwa katika shirika (mashirika) unamofanya kazi. Matokeo yanaweza kuwa yanashangaza na yenye kuhitaji muda katika kuyaangalia ili uepuke matatizo mengineyo.

### Muhtasari

Usalama ni jambo linalomhusu kila mtu.

Usalama ni suala la shirika zima, na pia la mtu binafsi anayeshirikiana nalo.

Sababu za watu kutofuata sheria za usalama zinafaa kubainishwa; zinaweza kuwa:

- Zisizo za makusudi (tatizo la mtu binafsi)
- Za kimakusudi (tatizo la kijumla la mtu binafsi, kundi na la shirika).

Kuzijua sababu hizi kutachangia kutafuta njia zifaazo za kuzishughulikia. Hata hivyo, kufuatilia kupitia kwa shirika lililoteuliwa kunapendekezwa (kufuatilia kwa moja kwa moja, kusiko kwa moja kwa moja na kwa mambo yaliyotendeka).

Kukuza utamaduni wa usalama wa shirika ni jambo linalofaa zaidi.

# Kusimamia mabadiliko ya shirika hadi kwenye sera ya kuimarisha usalama

**Lengo:**

Kujifunza jinsi ya kusimamia kubadilika kwa shirika kuelekea kwenye sera ya kuimarisha usalama.

Hatua na masuala ambayo mchakato huo utajengewa:

- Kuimarisha usimamizi wa mbinu ya usalama
- Kuimarisha mchakato wa utekelezaji wa ulinzi wa usalama
- Kiingilio chake ni kipi? Ni nani anayekiwajibikia? Hatua ya kuanzia ni gani? Namna ya kuendelea? Na vipi kuhusu utekelezaji? Ni nini ubaya na uzuri wake? Vizuizi ni vipi?

## Kushughulikia changamoto zinazohusu usalama: Ulinzi wa usalama wa hatua kwa hatua

Ulinzi wa usalama hauwezi kuisha na mara nyingi huwa ni wa kivitendo, wa kiasi na wa kiuteuzi. Hii ni kwa sababu:

- Kuna mipaka kwa kiwango cha habari unachoweza kushughulikia – si maswala yote yanayoathiri usalama yanaweza kukusanywa na kushughulikiwa wakati mmoja.
- Ni mchakato ulio changamano – wakati na juhudi ni muhimu katika kujenga ufahamu, kukuza muafaka wa makubaliano, kuwapa watu mafunzo, kushughulikia kuacha kazi kwa wafanyikazi, kutekeleza shughuli, n.k.

Ni nadra kwa ulinzi wa usalama kuweza kuwa na maelezo ya jumla yaliyo mapana na ya muda mrefu. Mchango wake unajikita katika uwezo wa kuzuia mashambulizi na huangazia haja ya mikakati ya shirika ya kukabiliana na haya. Jambo hili laweza kutoonekana kama lililo kuu, lakini tusisahau kwamba aghalabu rasilimali chache sana zinatolewa kwa ajili ya usalama.

Katika kuyapitia matendo ya usalama ya mtetezi au ya shirika, utagundua kwamba miongozo, mipango au mitindo ya tabia tayari ipo. Hali zinazopingana pia zitahusishwa, kuanzia kwa fikra za kibaguzi zinazohusu matendo ya usalama hadi kwa hali ya kutaka kuzidisha kipimo cha kazi iliyopo kwa kujumuisha shughuli mpya za usalama.

Kihalisi, harakati ya usalama ni kazi inayoenedelea isiyo kamilifu na yenye hisia. Ulinzi wa usalama unapasa kulenga kufanya mabadiliko ya hatua kwa hatua ili kuimarisha utendakazi. Taratibu na sheria za usalama huibuka katika sehemu za shirika zenye kazi mahsusi, kama vile katika kubainisha utaratibu wa utendakazi wa kundi la watetezi walio nyanjani, au mkurugenzi anayepata shinikizo kutoka kwa mdhamini wake kuhusu suala la usalama, nk.

Ulinzi wa usalama wa hatua kwa hatua hukaribisha michakato isiyo rasmi na pia huruhusu nafasi ya matendo mapya kuendelea. Matukio ya ghafla, kama vile ya usalama, yatachochea maamuzi ya haraka na ya muda mfupi ambayo, yakisimamiwa vizuri yataboresha matendo ya usalama ya muda mrefu ya shirika zima.

## Uimarishaji wa mikakati ya Usalama: Vichangizi vinavyoweza kutumika

Haja ya kuimarisha usalama itakapokuwa imeibanishwa itahitaji kuendelezwa. Kuna vichangizi kadhaa vitakavyopelekea uendelezwaji huo (ama ndani au nje ya shirika):

**Ndani ya shirika:**

- Usimamizi, bodi ya wakurugenzi au viongozi
- Kiwango cha kati cha utendaji
- Wafanyikazi, cheo na faili
- Ujumuishwaji wa vichangizi vyote vya hapo juu.

**Nje ya shirika:**

- Wafadhili
- Marafiki, wanashirika wenza
- Mashirika sawia yanayofanya kazi na miungano sawa.

### Hebu tulinganishe uzuri na ubaya wa vichangizi hivi

| Vichangizi vinavyoweza kuendeleza mabadiliko yafaayo | Uzuri | Ubaya | Suluhu zinazoweza kupatikana |
|---|---|---|---|
| Vichangizi kutoka **ndani** ya shirika | | | |
| Usimamizi, bodi ya wakurungenzi au viongozi | • Wanaweza kuandaa mikutano au mabaraza ya kijumla.<br>• Wana kumbukumbu za historia.<br>• Uongozi wenye maadili.<br>• Usaidizi wa kitaasisi.<br>• ... | • Huchukuliwa kama wenye kulazimisha usalama kisha huibua hali ya kutojali – hufanya mikakati kuwa rasmi, ngumu, iliyotenga, dhalifu.<br>• Huchukulia usalama kama kitu kinachowaathiri wao pekee.<br>• Huukataa kuupa usalama kipaumbele.<br>• ... | • Mikutano au mabaraza ya kijumla.<br>• ... |

| | | | |
|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA KATI/ CHA UTENDAJI | • Ukaguzi wa viwango vya juu na chini.<br>• Kuweza kufikia viwango vyote viwili kwa urahisi.<br>• Mkondo wa mawasiliano machangamfu baina ya viwango hivyo viwili.<br>• Uwezo wa kiufundi wa kutekeleza mabadiliko ya kiusalama.<br>• ... | • Aghalabu kiwango hiki huwa hakipo.<br>• Kulenga sehemu/upande mmoja kwa kiasi pekee.<br>• Wameshughulishwa na taaluma zao za kibinafsi.<br>• Tata "sana" iwapo hawatahusika katika harakati za kisiasa na nyanjani.<br>• ... | • Taratibu za kujihusisha (kwa wakurugenzi na wanachama kwa jumla).<br>• ... |
| WAFANYIKAZI, CHEO NA FAILI<br>• ... | • Wanaweza kuhamasisha watu wengine<br>• Wanafahamu utaratibu na kina cha kazi. | • Wanaweza kuwa na matatizo na wasimamizi au na mfumo wa madaraka.<br>• ... | • Kwa jumla tambua tatizo la kundi, haja ya utendakazi wa kila mtu na haja ya kuleta suluhu. Kisha andaa kundi litakalotafuta suluhu.<br>• ... |
| VICHANGIZI KUTOKA **NJE** YA SHIRIKA | | | |
| WAFADHILI, MASHIRIKA MAKUU<br>• ... | • Nafasi zaidi<br>• Hakuna maslahi ya moja kwa moja<br>• Wanaweza wakawa na tajiriba pana zaidi<br>• Wanaweza kuandaa mikutano inayohusisha makundi ya hapo juu bila kuwa na mgogoro wa kimajukumu.<br>• ... | • Wanaweza kuwa na matatizo ya kuaminiwa au ufahamu finyu wa kazi inayofanywa.<br>• Mbinu ya utendakazi inaweza kuwachanganya "zaidi".<br>• ... | • Bainisha hoja inayolingana katika usalama.<br>• Shirika fadhili linapenda zaidi kuwekeza kwenye shirika linaloupa uzito usalama kuliko lile lisilofanya hivyo.<br>• Usalama wa baina ya mashirika hutegemea mielekeo na sheria za kawaida za usalama.<br>• ... |

Harakati ya kuingia inaweza kutekelezwa na mashirika yote, bila ya kujali ukubwa, uimara au mahali yalipo.

## Shirika gani hushughulikia harakati ya uimarishaji?

Sasa kwa kuwa lengo limeshatimia (haja imeshaendelezwa na kutambuliwa), sehemu fulani ya shirika haina budi kuongoza harakati hiyo. Ni shirika gani litawajibikia mchakato huo wa uamirishaji wa usalama? Kuna uwezekano kadhaa:

- Wanachama maalum wa shirika wa kushughulikia mambo ya dharura (wao ni sehemu ya shirika na wanachaguliwa nalo (mara nyingi wao pia huwa na majukumu mengi nayo). Linaweza pia kuwa kundi linalofanya kazi (lililo na watu kutoka sehemu mbalimbali za kazini).
- Mtu wa nje-ndani: mtu anayefanya kazi kwa kiasi fulani na upande mwingine anatangamana kila mara kwa ukaribu na wanashirika (mfano, mtu aliyekuwa akifanyia shirika kazi).
- Mwelekezi au mshauri: hutangamana na mlinda usalama maalum au wa kundi linalofanya kazi (utangamano wa muda mfupi).

**Hebu tuchunguze ubaya na uzuri wa mbinu hizi tofauti.**

| Shirika linalowajibikia uimarishaji wa usalama | Uzuri | Ubaya | Suluhu zinazoweza kupatikana |
|---|---|---|---|
| Mtu wa kutekereza jukumu maalum kutoka kwenye taasisi | • Habari iliyo mahali pamoja.<br>• Kuweza kuifikia habari kwa urahisi.<br>• Uwekaji wazi wa majukumu.<br>• Ufanyaji uamuzi kwa urahisi – watu wachache wanahusishwa.<br>• Wamechaguliwa kutokana na ujuzi wao. | • Kiwango kikubwa cha kazi kuhafifishwa kwa kujitolea kwa pamoja.<br>• Utegemeaji sana kwa mtu mmoja.<br>• Uwezekano wa kukosa maonirejea ya mipango na mawazo. | • Tofauti baina ya kupandishwa madaraka/ uratibu na utekelezaji.<br>• Kupunguzwa kwa kiwango cha kazi cha muda mfupi ili kulenga usalama.<br>• Wafanyikazi wasaidizi.<br>• Usambazaji wa kila mara wa mikakati ili kuhakikisha maonirejea yanaendelea kuwepo. |
| Kundi la wafanya kazi | • Kubadilishana mbinu changamano za kufanya kazi kwa usalama.<br>• Uzoefu mwingi ulio mpana.<br>• Wafanyi kazi zaidi<br>• Ugawaji wa majukumu: uwekaji wazi kwa ajili ya shughuli na ari.<br>• Uwezekano mkubwa wa itifaki kufuatwa. | • Kiwango kikubwa cha kazi.<br>• Makubaliano ya polepole katika ufanyaji wa uamuzi.<br>• Usambazaji wa habari isiyo badilika badilika – idadi kubwa ya watu kupewa mafunzo ya kazi. | • Ugawaji wa kutosha wa majukumu na ujuzi.<br>• Ujumuishwaji usimamizi.<br>• Kupokezana, kutoa mafunzo, na kujitolea kwa maendeleo bora ya usambazaji wa matokeo ili kupata maonirejea na kugawana majukumu. |
| Mtu wa nje-ndani | • Uchangunizi wa hatari usio wa mapendeleo.<br>• Mtu mwenye ujuzi, mwenye kuaminiwa na shirika.<br>• Mwenye kujitolea kabisa.<br>• Ni mpokezi aliyethibitishwa – ana ufahamu wa uzuri na ubaya. | • Anaweza kukosa kuungana na wengine.<br>• Anaweza kulifanya kundi liwe dhaifu.<br>• Anaweza kutoweza umiliki ufaao wa mchakato mzima na lengo. | • Wape mafunzo wanachama 12 wa kundi.<br>• Usambazaji wa kuendelea wa matokeo yaliyopo na maoni rejea kutoka kwa kundi.<br>• Uundaji wa makubaliano na mikataba. |
| Mwelekezi au mshauri | • Anaweza kulipa kundi mafunzo.<br>• Uelekezi wa kitaaluma.<br>• Uwazi katika kufuatilia harakati.<br>• Ushauri unaotambuliwa.<br>• Mchakato hai wa kufuatilia.<br>• Hajaathirika zaidi na masuala ya kindani ya shirika. | • Anaweza kutegemewa tu badala ya kutoa ujuzi.<br>• Anaweza kuonwa kama “mtu aliopo kufanya kazi” badala ya “mtu aliopo kugunguza kazi.”<br>• Anaweza kutoweza uaminifu ufaao katika shirika.<br>• Gharama zilizoongezeka.<br>• Waelekezi katika Nyanja hii ni wachache.<br>• Ugumu katika kuandaa ratiba ya kazi.<br>• Wanaweza wakawa na maarifa finyu ya eneo wanaloshughulikia.<br>• Wanaweza kuunda mpango na sheria zisizofaa kwa kazi fulani. | • Kuwe na uwazi wa kila mtu kadiri iwekavyo: fafanua jukumu la mshauri, mawanda.<br>• Bainisha umuhimu wa usalama kwa mashirika mengineyo.<br>• Kushughulikia na kugawana swala hilo kwa uzuri.<br>• Toa mafunzo kuhusu usalama kwa wakufunzi wa usalama kwenye mashirika na taasisi (watoaji mafunzo).<br>• Kuandaa mikutano ya muda mchache kuhusu mazingira ya kazi. |

## Ni wapi pa Kuanzia katika harakati hiyo?

Kwa kuwa kuingia kumeshatimia na shirika lifaalo limeshateuliwa, litaanza wapi sasa? Shirikia linafaa kuanza kwa kutathmini harakati ya sera ya utekelezaji wa usalama. Kuanzia kwa utathmini (au uchunguzi) utakadiria vipaumbele na suluhu zinazoweza kupatikana (matendo bora zaidi kulingana na mahitaji yaliyoorodheshwa, hadhi na uwezo wa shirika). Kisha mpango unaolenga harakati ya uimarishaji utaundwa. Mpango huo utahusisha malengo ya kati ili kufuatilia iwapo na vipi maendeleo yanatimizwa. Kwa kuongezea, mpango utaweka wazi kazi na majukumu ya mtu/watu wanaowajibikia harakati hiyo na wanachma wa shirika. Mpango huo pia utahusisha ratiba. Kufikia mwisho wa harakati iliyopangwa, utathmini wa mafanikio utafanywa.

Uchunguzi ➪ Vipaumbele ➪ Suluhu zinazoweza kupatikana
➪ Mpango wa uimarishaji ➪ Utathmini

Baada ya kukadiria tathmini, uamuzi kuhusu utaratibu wa kuzitekeleza unaweza kuwa mwepesi iwapo mbinu za dharura zitaundwa, rasilmali zilizopo za sasa n.k.

Uwezo wa kubadilika ni jambo muhimu katika harakati hiyo yote. Hata hivyo, ni uwezo upi wa kubadilika wa kiwango cha chini ufaao katika harakati ya uimarishaji utakaopelekea kupatikana kwa matokeo bora? Kulijua swali hili kabla ya harakati kuanza ni muhimu.

## Mpango wa Uimarishaji na Ugunduzi

Ugunduzi unaweza kutekelezwa kwa kutumia zana za "utathmini wa hatari" na "gurudumu la usalama," zilizofafanuliwa katika sura zilizotangulia za mwongozo huu (mbinu yoyote ya apitiaji tena wa shirika inaweza kufaa kwa hili).

Inajulikana wazi kwamba hatua hii inafaa kuhusisha watu wote wanaofaa na hata makundi ya kufanya kazi katika shirika.

Mpango wa uimarishaji unafaa kuwa wa **kihakika** na unaofaa kwa hadhi na mahitaji ya shirika. Hapa kuna utaratibu wa hatua hizo:

1 ♦ Tambulisha matarajio na matokeo yanayotarajiwa ya shirika kuhusu mpango wa uimarishaji wa usalama.

2 ♦ Fanya uchunguzi wa pamoja, fikieni makubaliano kisha badilishaneni fikira kuhusu muundo wa sasa wa ulinzi wa usalama (matumizi ya mbinu ya "uchanganuzi wa hatari" na "gurudumu la hatari"): onyesha maendeleo, upungufu na mahitaji yaliyodhihirika.

3 ♦ Dhihirisha na mjadiliane kuhusu njia bora zitakazotekelezwa katika kushughulikia upungufu na mahitaji yaliyodhihirika.

4 ♦ Dhihirisha malengo yafaayo ya mpango wa uimarishaji.

5 ♦ Orodhesha shughuli zinazohitajika ili kufikia malengo na nini hasa kinachoweza kutarajiwa kwa kila shughuli (hili litawezesha maendeleo ya kufikia malengo).

6 ♦ Orodhesha rasilimali zifaazo (za kifedha, za wafanyikazi, muda, na zile za kiufundi). Fafanua majukumu na ratiba ya kazi.

7 ♦ Fafanua ni hatari gani zinatokana na kutimiza malengo na matokeo haya.

8 ♦ Fafanua viashiria vya kufuatilia maendeleo na matokeo ya mwisho.

9 ♦ Badilishaneni mpango huo na watu wote wanaohusika ili maonirejea yapatikane na ili uimarishwe na kuleta kibali kifaacho katika kuutekeleza.

10 ♦ Utekeleze mpango kisha uamue kuhusu vipindi vya wakati wa kuufuatilia maendeleo na mabadiliko yanayoweza kutokea katika harakati hiyo.

### Mchakato: Kutekeleza mpango wa uimarishaji.

Mchakato huo unahusu mikutano na mahojiano mengi na watu au makundi yanayofanya kazi shirikani au kuwa na mawasiliano na (katika hali hii, ni lazima kuwepo na makubaliano ya hapo awali kutoka kwa shirika, yanayoonyesha watu mahususi na/au mashirika ambayo usalama unaweza kujadiliwa nayo). Ubadilishanaji unaweza kuanza kwa mkutano wa kijumla wa kutoa utangulizi, ambao unaweza kufuatiwa na mikutano mingineyo. Mikutano hutoa nafasi za kufafanua chunguzi na kujadili kuhusu utekelezaji wa mpango wa uimarishaji. Fauka ya hayo, vipengele mahususi vinaweza kujadiliwa kwenye mikutano au ikatumiwa kujadili kuhusu kazi mahususi ya shirika katika matazamo wa usalama na ulinzi.

### Upinzani dhidi ya mpango wa uimarishaji.

Kwa kuwa sasa lengo limeshatimia, shirika lifaalo kuteuliwa na mahali pa kuanzia na mipango ya harakati zote kuamuliwa, upinzani gani kutoka kwa watu binafsi unaweza kuwepo?

Kama ilivyo michakato yote inayoleta mabadiliko kwenye shirika mpango wa uimarishaji unaweza kukumbana na upinzani. Hata hivyo, unaweza pia kupata idhini na usaidizi. Kwa hivyo, hoja hapa ni kutafuta njiaya kupata usaidizi huo na kisha kukabiliana na uwezekano wowote wa upinzani.

Njia bora kabisa ya kutweza upinzani ni kuusikiliza tu kisha kujaribu kuelewa msingi wa mantiki yake. Hapa tena, kushiriki, usikilizaji mzuri wa maoni yote na matarajio ni muhimu katika kuwepo kwa mchakato mzuri.

Inafaa kwamba mpango wa uimarishaji unaweka wazi mikakati ya kushughulikia upinzani unaoweza kutokea ili kuepuka utekelezaji wa baadaye, jambo litakalopelekea kukubiliwa na hatari ya kutofaulu kwa mpango kutokana na kukataa kwa awali kwamba upinzani hauwezi kutokea.

Katika Jedwali hili kuna baadhi ya dhana potofu zilizopinzani, fikra kuhusu dhana hizo na namna za kukabiliana na upinzani huo.

| Dhana Potofu Kuhusu Upinzani Wa Kawaida | Fikira Kuhusu Dhana Hizo Potofu | Namna Za Kukabiliana Na Upinzani |
|---|---|---|
| "Hatupati imatishio" au "kazi yetu si dhahiri au tata kama ilivyo ya mashirika mengineyo." | • Hatari haibadiliki bali inabaki vivyo hivyo au kutegemea kweli kwamba mazingira ya kazi yanaweza kuharibika au hali inaweza kubadilika. | • Hatari hutegema hali ya kisiasa na hali ya kisiasa inabadilika: vivyo hiyvo ilivyo hatari. |
| "Hatari ni ya kiasili katika kazi yetu kama ilivyo kwa watetezi" na "tunafahamu tayari kile kinachotukabili". | • Watetezi hukiri hatari na kuwa haiwaathiri katika kazi yao. Au, hatari haiwezi kupunguzwa, ipo na hayo ndiyo yote kuihusu. | • Kukumbana na hatari ya kiasili hakuna maana ya kwamba umeikubali hatari hiyo.<br>• Hatari ina angalau athari ya kisaikolojia kwa kazi yetu: huleta upozo katika msongo unaoathiri kazi yetu.<br>• Hatari inatokana na mambo yasiyo ya mapendeleo: udhaifu na uwezo ni miliki ya watetezi na ndiyo mabadiliko wanayoweza kufanyia kazi watetezi. Kwa kupunguza udhaifu na kuongeza uwezo, hatari yaweza kupungua. Inaweza kukosa kuondolewa hata hivyo japo haina maana kwamba haiwezi kupunguzwa hadi kiwango cha chini zaidi. |
| "Tayari tunajua jinsi ya kukabiliana na hatari" au "tunafahamu namna ya kujilinda na tuna tajiriba pana." | • Ulinzi wa wakati huu wa usalama hauwezi kuimarishwa na haifai kufanya hivyo.<br>• Kutokana na ukweli hatujapata madhara huko nyuma tunahakika kwamba hatutayapata tena. | • Ulinzi wa usalama unatokana na elementi zisizoegemea kokote ambazo zinaweza kufanyiwa kazi.<br>• Jaribu kuchunguza ni watetezi wangapi wamepata madhara ingawa walikuwa na tajiriba. |
| "Naam, suala hilo linavutia, lakini pia kuna mambo mengineyo ya kupewa uzito." | • Kuna mengineyo yaliyo muhimu kuliko usalama wa watetezi. | • Maisha ndiyo kitu cha kupewa uzito.<br>• Tukiyapoteza, hatutaweza kushughulikia vipaumbele vinginevyo. |
| "Na je, tutaulipia vipi usalama?" | • Usalama ni kitu ghali na hauwezi kujumuishwa katika mapendekezo ya uchangishaji pesa. | • Unafikiri usalama una gharimu ngapi? Masuala machache ya usalama ni ya kimwenendo na hayagharimu pesa yoyote.<br>• Wawekezaji watapendelea kuwekeza katika mashirika yanayoshughulikia masuala ya usalama badala ya kuende kwingineko watakakokabiliwa na hatari ya kupoteza uwekezaji wao. |
| "Iwapo tutashughulika sana na usalama hatutaweza kufanya yaliyo muhimu zaidi ambayo ndiyo muhimu kwa watu tunaofaa tuwafanyie." | • Kutokana na ukweli kwamba tumeathiriwa na matatizo ya usalama haiwi kwamba watu tufanyao nao kazi wataathiriwa. Ubora wa kazi yetu kwa watu hautegemei iwapo tunahisi kwamba tu salama zaidi. | • Usalama ni suala la kufa na kupona.<br>• Kwa kuwa tunapaswa kuwapa watu usalama, hatuwezi kuhepa ukweli kwamba tunahatari ya kupoteza maisha yetu.<br>• Watu hawa na hatari kwa kutuaminisha sisi na hali zao na tusiposhughulikia usalama wetu utawaathiri pia; wanaweza kuamua kutumia shirika jinginelo ambalo lina mipango mizuri ya usalama na hivyo pia kuwasalama watu wengineo. |
| "Hatuna muda kwa kuwa sasa tuna kazi nyingi zaidi." | • Ni vigumu kupata muda katika ratiba ya kazi. | • Je, unafikiri usalama huchukua muda gani?<br>• Je, tunachua muda gani kukabiliana na matukio ya kidharura badala ya uzuiaji? (Labda mbali zaidi na wakati unaohitajika kupangia usalama katika kazi yenu). |

| | | |
|---|---|---|
| "Jamii inatunga mkono: ni nani anayeweza kuthubuta kutudhuru?" | • Sisi ni sehemu ya jamii. Jamii si ya makundi, haibadiliki katika mahusiko ya au wanachama au maoni.<br>• Jamii haiwezi kuathiriwa. | • Jamii si ya jinsi moja na inajumuisha pia wale wanaoweza kuathiriwa na kazi yetu. |
| "Katika kijiji chetu, mamlaka zimedhihirisha uelewa na ushirikiano." | • Serikali za mitaa haziathiriwi na kazi yetu ya kushughulikia rasilimali za wafanyikazi na haitabadilisha mawazo yao.<br>• Hakuna mfumo wa kimamlaka wa kuanzia juu hadi chini baina ya mamlaka ya kitaifa na ile ya mtaa. | • Kumbukumbu ya historia ya shirika itakuwa na nifano ya serikali ya mitaa inayopinga.<br>• Kazi ya kushughulikia rasilimali ya wafanykazi wakati ambapo mipaka ya uvumilivu wao imevuka.<br>• Serikali za mitaa zinafaa kutekeza maagizo ya mamlaka. Mamlaka ina watu wanaoweza kuwa na haja ya kuwatetea watu wanaohujumu wengine.<br>• Mabadiliko ya hali ya kisiasa. |

Kwa kuwa sasa lengo limeshatimia,shirika lifaalo limeshateuliwa na mahali pa kuanzia na mipango ya michakato imeshabainishwa, na kwamba upinzani wa mtu binafsi umeshaondolewa, ni masiala yepi ya shirika yanaweza kuzuia au kuharakisha mabadiliko.

**Masiala ya shirika ambayo yanaweza ama kuzuia au kuharakisha mabadiliko ya shirika hadi kuwa na sera ya usalama.**

| Ndani ya shirika | Masiala yanayozuia mabadiliko | Masiala yanayoharakisha mabadiliko |
|---|---|---|
| Utamaduni wa shirika | • Ujuujuu. Ufaraguzi. Kazi ya mtu binafsi.<br>• Usalama haujapewa uzito. | • Kufanya kazi kwa kundi ufahamu wa athari ya kazi, usiakiaji wa hali ya juu mashauriano, taratibu zao kufanya uamuzi wa pamoja.<br>• Usalama umepewa uzito. |
| Mwelekeo wa usimamizi | • Wa kimabavu na kiimla ni usimamizi wa kimatokeo mazuri. Wa mbali. Umuhimu unapewa tu kwa viongozi na hivyo basi huunda na kutii sheria zinazokidhi mahitaji yao pekee.<br>• Matarajio yasiyo ya kurejesha kwamba wanachama wengine wapo kuhudumia tu usimamizi.<br>• Wao wenyewe kujipa haki. | • Anawasiliana na wanachama wote.<br>• Utambuzi wa umuhimu wa uchangizi wa wote kwa mafanikio ya majukumu ya shirika.<br>• Haja za wafanyikazi wote, veyo na faili zao kupewa makini.<br>• Kuwa wazi.<br>• Kuheshimu sheria. |
| Muundo wa shirika | • Ngumu<br>• Umegawanywa<br>• Haufai kwa kazi. | • Unabadilikabadilika kwa njia inayofaa.<br>• Kutobadilika badilika kwa uratibu na mawasiliano kati ya viwango.<br>• Kuangazia haja za watu na kazi. |
| Ufahamu wa masuala ya usalama | • Ni wa mahali pamoja. Ni wa kiasi. Ufahamu mdogo wa masuala ya usalama nyanjani. Upendeleo, ufahamu usio mpana kuhusu masuala ya usalama. | • Kubadilishana uzoefu na maarifa. Ni jumuishi. Ni wa mambo halisi.<br>• Ufungaji habari kwa utaratibu fulani na pia marekebisho ya kila mara. |

| | | |
|---|---|---|
| Ukosefu wa uthabiti katika shirika; kubadilika kwa uchovu | • Wafanyi kazi kuacha kazi<br>• Ukosefu wa kumbukumbu ya historia.<br>• Uchovu kutokana na mabadiliko ya kuendelea.<br>• Ukosefu wa kuendelea kwa kazi | • Maelezo ya wazi kuhusu kazi na kandarasi yanayoonyesha kujitolea kutoa ilani ya kutosha ya kuondoka na kupokeza maarifa na ujuzi kabla ya kuondoka.<br>• Tathmini za kila mara.<br>• Ugawaji majukumu yanayokubaliana na wakati ambao wafanyi kazi watakuwa wamejitolea kuyatekeleza. Mafunzo ya kawaida na yale ya wakati wa kuingia. |
| Kiwango kikubwa cha kazi | • Wafanyikazi wasiotosha msonga wa akili kupoteza lengo. | • Kuipa uzito kazi na kuigawa upya.<br>• Nafasi ya kupumzika. |
| Kupangilia Kazi | • Usalama haujapewa kipaumbele kwa uwazi.<br>• Usalama haujahusishwa katika mpango wa kazi.<br>• Mpango wa kazi ni wa hiari na hivyo haukidhi sababu na malengo. | • Mpango wa kutosha wa usalama katika kazi.<br>• Mazingatio ya kutosha kwa shughuli ambazo usalama unaonekana kama usiotosha na maamuzi ya baadaye yanafanywa ambayo ni iwapo kuzitekeleza shughuli hizo ikiwa masharti ya usalama hayakutimizwa. |

Masiala yasiyoathiri mabadiliko ya shirika kwa njia mahsusi katika sera ya uimarishaji wa usalama:

- Ukubwa wa shirika
- Ukweli kwamba watu wanaowajibikia usalama wanayo/hawana elimu ya juu.
- Dini
- Jinsia

## Kanuni au matendo bora katika usimamizi wa ulinzi wa usalama.

Kwa kuwa sasa lengo limeshatimia (shirika lifaalo limeshateuliwa,mahali pa kuanzia na mipango ya harakati zote kubainishwa, upinzani wa mtu binafsi umeshaondolewa, masiala ya shirika yanayozuia au kuharakisha mabadiliko yameshazingatiwa) ni matendo yepi bora ya usimamizi wa ulinzi na usalama, huku ikijulikana kwamba yanategemea miundo ya shirika?

Zipo hiari kadhaa za kulinda usalama katika shirika na huenda ikawa vigumu kufanya uamuzi kuhusu ni ipi chauzi bora zaidi. Katika chati inayofuata tunajadili mitindo mitatu pamoja na uzuri na ubaya wake, pia suluhu kadhaa zipo.

| Mitindo ya Kimuundo | Ni wapi maamuzi ya usalama hufanywa? | Uzuri | Ubaya | Suluhu zinazoweza kupatikana |
|---|---|---|---|---|
| Mtindo wa Katikati | • Katika kiwango cha usimamizi, kwenye shirika lenye kujitolea. | • Rahisi kukagua kwamba uzoefu wa kutosha na maarifa yanapatikana katika shirika. | • Kiwango kikubwa cha kazi kinaweza kuzuia uwezo wa kufanya maamuzi yafaayo.<br>• Unaweza kuwekwa mbali na kazi katika maeneo fulani. | • Mtu mmoja katika kiwango cha usimamizi na uwezo wa utendaji anatenda kwa niaba ya usimamizi.<br>• Msimamizi wa usalama anateuliwa katika kiwango cha usimamizi lakini bila uwezo wa utendaji. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mtindo wa Muundo wa kati** | • Maamuzi yaliyo muhimu na ya kIlimwengu: katika kiwango cha usimamizi. Maamuzi mahsusi yanafanywa na watu wanaoyawajibikia katika sehemu zote za kazi. | • Usimamizi hauna kazi nyingi zaidi.<br>• Kuweka pamoja maarifa katika kiwango kifaacho. Kuwa karibu zaidi na kazi yenyewe ya kila sehemu. | • Migogoro ya kiusalama inaweza kuibuka baina ya kiwango cha usimamizi na sehemu nyinginezo. | • Kila mtu anayehusika na sehemu maalum anachukua jukumu la kulinda usalama mahali hapo.<br>• Mshauri kuhusu usalama anaweza kuteuliwa kwa ajili ya kushughulikia usalama wa shirika. Mtu anayehusiana na sehemu fulani, kwa mfano sehemu ya usimamizi au ya utaratibu wa ugari na usafirishaji wa watu na vitu, atachukua jukumu la kulinda usalama kwa kutangamana na Yule anayesimamia sehemu fulani lakini iliyo yake. |
| **Mtindo wa Ugatuzi** | • Maamuzi kuhusu usalama yanafanywa katika viwango vyote kwa kuwa kila mtu analo jukumu la wazi la kulinda usalama. | • Utoshelezi bora, kuchangia katika utamaduni wa shirika linalojishughulisha na usalama. | • Majadiliano yanaweza kuchukua muda mrefu. Inaweza kuhusishwa tu na mashirika madogo. | • Kunaweza kuwepo watu waliojitolea au wasiojitolea kabisa kwa usalama.<br>• Kila mtu anaweza kuwa na jukumu hilo katika maagizo yake ya kazi au katika kazi yake ya hapo awali. |

## Wafanyikazi wa shirika/mafunzo ya wanachama.

Kwa kuwa sasa lengo limeshatimia, (shirika lifaalo limeshateuliwa,mahali pa kuanzia na pia harakati za mipango zimeshabainishwa, upinzani wa mtu binafsi umeshaondolewa,masiala ya shirika yanayozuia na kuharakisha mabadiliko yameshazingatiwa, kanuni za ulinzi na usalama au matendo bora yameshakadiriwa) sasa je, nini kuhusu kuwapa wafanyikazi mafunzo?

Mafunzo hayo yanaweza kufanywa kutokana na rasilimali za ndani za shirika (wanaweza kuwa watu wa ndani ya shirika walio na mafunzo kuhusu usalama). Mafunzo hayo pia yanaweza kufanywa kwa pamoja na mashirika mengineyo (kuwapeleka watu wahudhurie vipindi vya mafunzo ya pamoja na watu kutoka katika mashirika mengineyo). Kama ni hivyo, kujenga ushirikiano na mashirika mengineyo kunaweza kuwezesha ubadilishanaji wa habari kuhusu usalama na pia uundaji wa miungano inayolenga kuimarisha usalama. Ni sharti kuwepo uaminifu baina ya mashirika yanayoshiriki katika mafunzo ya usalama. Zaidi ya hayo, ni muhimu kwamba mashirika yanakuwa na maslahi sawa na pia yanakuwa na maeneo na mazingira mamoja ya kazi; mashirika ya mashambani na mijini kwa mfano yana mahitaji tofauti kabisa ya usalama.

Mafunzo yanaweza kutekelezwa kwa njia nyingi tofauti. Zilizo za kawaida ni kama:

- Warsha (katika makundi madogo ya watu 10-15).
- Mafunzo ya kibinafsi (yanafaa kwa kazi zilizochangamana au majukumu mahususi, yaani aweza kupata mafunzo huku akifanya kazi).
- Mtindo wa kimazungumzo au mikutano ambayo si ya rasmi kabisa (kutoa maelezo, ushauri bora).

Kuwa na mafunzo hayo angalau nje ya mazingira ya kazi kunapendekezwa ili kuwezesha umakini na kuepusha wasiwasi wa kila siku. Hata hivyo, aghalabu haileti natija kwa kuwa na harakati hizi baada ya masaa ya kazi (yaani katika wikendi) kwa kuwa inaweza kuleta dhana mbaya: kwamba kulinda usalama kuna maana ya kutumia muda mrefu zaidi – hasa muda wa ziada, na kwamba suala la usalama halina umuhimu wa kutosha kujumuishwa katika ratiba ya kawaida ya kazi.

## Jinsi ya kuimarisha hadhi ya sheria za usalama

Kwa kuwa sasa lengo limeshatimia yaani shirika lifaalo limeshateuliwa, mahali pa kuanzia na harakati za mipango zimeshabainishwa, na kwamba sasa upinzani wa mtu binafsi umeshaondolewa, kwamba masiala ya shirika yanayozuia au yanayowezesha mabadiliko kupewa mazingatio, na wafanyikazi wameshapewa mafunzo, sasa je, hadhi ya sheria za usalama itaimarishwa vipi?

Masharti yafaayo ya kuheshimu mipango ya sheria na usalama yanaweza kutimizwa kupitia kwa hatua zifuatazo:

- Kuwepo na kuendeleza utamaduni wa usalama wa shirika.
- Umiliki wa sheria na mipango ya usalama.
  Ushiriki katika harakati za uundaji uimarishaji wazo.
  Kutoa mafunzo ili kuzibainisha na kuzielewa.
  Kuwashawishi watu kuzitekeleza ya kutoka na kwa uthabiti.
- Kuandaa mkataba baina ya mtu binafsi na shirika kuhusiana na kuitii mipango na sheria za usalama.
- Uingiliaji kati wa kila mara wa watu wanaowajibikia usalama au kwa malengo ya utoaji habari na mafunzo, wakiwakumbusha watu kuhusu mikataba yao ya kutekeleza kama walivyofanyiwa na kukusanya maoni yao kuhusu uthabiti na utimilifu wa sheria hizo.

Ni kitu gani kifanywe katika hali za kutotii sheria na mipango ya usalama?

I • Tafuta na suluhisha sababu za hali za kutotiii (tazama sura 2.2).

II • Iwapo sababu hizo ni za makusudi na zinategemea kwa ukamilifu mapendeleo ya mtu binafsi, hatua zifuatazo zaweza kuchukuliwa:

a • Zungumza na mtu huyo (kama hitimisho la harakati ya hapo awali linalolenga kutatua sababu za kutotii) ili uweze kuchochea motisha na kujitolea.

b • Wasilisha suala hilo kwa kundi linalofaa kulishughulikia, huku akiwepo mtu huyo (hatua hii inakuwa si timilifu, kulingana na hali).

c • Tumia mfumo wa kutoa ilani (kati ya ilani mbili na tatu).

d • Tumia mfumo wa kutoa vikwazo kwa njia ya polepole ambayo vinaweza kuishia kwa kumfuta kazi mtu huyo.

Ni muhimu kujumuisha kifungu cha utii wa sheria na mipango ya usalama katika mkataba, ili watetezi wote wawe na ufahamu mzuri wa umuhimu wa usalama wa shirika.

### Muhtasari

Kuwa na mpango wa usalama hakuna maana kwamba utatekelezwa na pia kuheshimiwa. Harakati ifaayo inafaa kuundwa ili kusimamia utekelezaji na kuimarisha usalama. Kadiri harakati hiyo inavyokuwa jumuishi zaidi, inavyoweza kukusanywa na ndivyo umiliki unavyoweza kutimizwa.

Hakuna muundo wa shirika ulio sawa au usio sawa: Kila mmoja una uzuri na ubaya wake. Ni bora hivyo basi, kuchangamua ili kuandaa harakati ifaayo na kasha kuipa nafasi nyingi iwezekanavyo ili kupata ufanisi.

Mpango wa uimarishaji unapaswa kuwa wa **kihalisia** na pia ufaao kwa hadhi na mahitaji ya shirika.

Hapa kuna hatua zifaazo za harakati itakayopelekea kupatikana sera nzuri ya usalama:

- Ni sharti kupatikane nafasi ya usalama.
- Shirika lifaalo linapaswa kuteuliwa.
- Shirika hilo lifaalo linafaa kuwa na mahali pa kuanzia na kupangia harakati hiyo.
- Upinzani wa mtu binafsi unafaa kuondolewa kwa kuwa na usikiaji hai ili kukadiria mantiki anayotumia mtu huyo ya kupinga harakati ya usalama, ili kuunda kauli itakayotumiwa kumpinga (haitoshi tu kutoa maoni yaliyo kinyume na dhana potofu pinzani, kwa kuwa yote hayo hutegemea mantiki ya dhana potofu: Iwapo mantiki ya mpinzani ni sawa, basi upinzani wake pia utakuwa sawa).
- Masiala ya shirika yanayozuia au kuwezesha mabadiliko yanafaa kuzingatiwa.
- Vipimo vya ulinzi na usalama au matendo bora yanafaa kukadiriwa.
- Wafanyi kazi/wanachama wanafaa kupewa mafunzo.
- Utiifu wa sheria za usalama unafaa kuimarishwa.

# SEHEMU YA TATU

# ITIFAKI, MIPANGO YA KIDHARURA NA SERA NYINGINEZO

Katika sehemu ya tatu ya Mwongozo huu, tunajenga mantiki ya uundaji wa itifaki, mipango ya dharura (ya kutumiwa katika hali mahususi) na sera zaidi za usalama. Yote haya yanatokana na matendo bora yanayobadilishanwa na kusomwa katika warsha tunazoziandaa.

Hata hivyo, si kamili wala hayawezi kutoa hakikisho kwamba yataleta matokeo bora, kwa kuwa mwongozo hauwezi kutoa upya mabadiliko yote ya hali fulani.

Hii ni kazi nyingi inayoendelea, na kwayo tunakaribisha maoni yenu, na pia mapendekezo mapya kuhusu itifaki na mipango.

Tutachapisha mambo mapya yanayojiri pamoja na maendeleo kwenye tovuti www.protectionline.org ili watetezi waweze kufaidika kutoka kwayo haraka iwezekanavyo, na tutajumuisha maendeleo yote katika toleo letu lijalo la mwongozo. Kwa sasa, tafadhali rejelea *Annex IV – General Risk Outline for Specific Human Rights Defender Profile*.

### YALIYOMO KATIKA SEHEMU YA TATU:


3.1 Jinsi ya kupunguza hatari zinazohusiana na upekuzi wa afisini.

3.2 Kumzuilia, kumkamata, kumtorosha au kumteka nyara mtetezi.

3.3 Kulinda habari kwa njia ya salama.

3.4 Usalama na wakati usio na shughuli.

# Jinsi ya kupunguza hatari zinazohusiana na upekuzi wa afisini na/au uvamizi wa afisini

Upekuzi unaweza kufafanuliwa bora zaidi kama kuingia kwa lazima katika nyumba, afisi, au katika nafasi ya kibinafsi. Upekuzi unaruhusiwa tu iwapo ni serikali ndiyo inayoamua kufanya hivyo na sheria zifaazo zitumiwe katika upekuzi huo.

Upekuzi hauruhusiwi tu ambapo kuingia huko kwa lazima kunaenda kinyume na sheria (kwa mfano uvamizi wa wizi wa usiku, upekuzi wa vikosi vya usalama bila ya kibali cha upekuzi au upekuzi wa lazima wa mshika dau aliye na silaha).

Ingawa hali inayofuata inatokana na upekuzi ulioruhusiwa, watetezi nao pia wataweza kuzidondoa sheria zinazotumika katika upekuzi usioruhusiwa kisha wazikamilishe kwa maelezo yanayopatikana katika kifungu kinachohusu usalama wa nyumba na afisi.

Serikali inaweza kufanya upekuzi kwa njia inayoruhusiwa. Sheria inayotumika katika hali hii itafaa kulingana na vipimo vya kimataifa kuhusu haki za binadamu na ulinzi wa uhuru wa kidemokrasia. Hata hivyo, inaweza kuwa tatizo kubwa ikiwa pekuzi zitatumiwa kama njia ya kuendelea kuwanyanyasa na kuwadhulumu watetezi wa haki za binadamu pamoja na makundi ya kijamii kupitia kwa pekuzi za kila mara, kinyume na vipimo vya kimataifa.

Tunaweza kutimiza hili vipi? Kwa kutumia msawazisho hatari na kuyaorodhesha matishio yote/matokeo (matokeo yanaweza kubadilishwa yakawa matishio). Kisha, kwa kila tishio/tokeo, orodhesha udhaifu na uwezo wote unaohusiana na kila tisho/tokeo, halafu uanze kuushughulikia ...

## Matishio/matokeo yanayohusiana na pekuzi

Upekuzi husababisha matishio/matokeo:

a • Tishio kwamba katika harakati ya upekuzi mtu yeyote aweza kupata madhara ya kimwili au kisaikolojia.

b • Tishio kwamba habari inaweza kuibiwa, kupotezwa au kuharibiwa.

c • Kuhusiana na hilo, kwamba habari inaweza kutumiwa visivyo na mtu mwingine.

d • Tishio kwamba vitu vinavyotatanisha vinaweza kuwa "vimefichwa" (silaha, dawa za kulevya, stakabadhi) ili baadaye, kulikabili shirika "kisheria".

e • Tishio/tokeo la pesa na mali fulani (kama vile kompyuta…) kuibiwa au kuharibiwa

**a ♦ Tishio kwamba katika harakati ya upekuzi mtu yeyote anaweza kupata madhara ya kimwili au kisaikolojia.**

Hakuna yeyote anayeweza kutabiri ni lini upekuzi utafanywa na ni zipi athari zitakazotokea. Hata hivyo, kuwa na habari kuhusu iwapo upekuzi huo utatekelezwa kunaweza kuchangia katika kuepuka mwenendo au msongo wa akili unaoweza kuleta madhara ya kimwili na kisaikolojia. Kunaweza kuchangia katika kujenga ufahamu wa vichocheo vya hatari na kudumisha mwenendo mzuri.

**Udhaifu:**

- Kutojua lengo la upekuzi
- Kuamini kwamba kupinga upekuzi huo kutakusaidia kuokoka na hali hiyo
- Hakuna bima ya matibabu

**Uwezo:**

- Kujua jinsi upekuzi wa halali unaweza kutekelezwa
- Kujua idara ambayo inaweza kutoa vibali vya upekuzi na kuwa na jina la afisa wa sasa anayesimamia harakati hiyo (kabla na wakati wa upekuzi ulioruhusiwa)
- Kujua namna kibali cha upekuzi kinavyofanana
- Kujua haki za kisheria za mashirika au watu binafsi waliopekuliwa (ikiwemo haki ya kutaka kuona kibali cha upekuzi na ikiwezekana kutafuta usaidizi wa kisheria)
- Kuweza kupata usaidizi wa kisheria (wakati wa upekuzi na hata baada yake)
- Jinsi ya kuepuka upinzani usiofaa
- Iwapo upekuzi umetekelezwa kwa fujo, ni muhimu kwamba watu wajiweke katika kundi ili kupunguza hatari ya kudhulumiwa kwa mtu binafsi

Shirika linaamua kubandika kibali hicho mahali pa wazi panaonekana;

- ■ Mfano wa kibali cha upekuzi
- ■ Utungaji sheria wote unaolingana (haki na majukumu yao wote)
- ■ Orodha ya majina na nambari za simu za wakili, daktari, mwanasaikolojia wa shirika, hospitali iliyo karibu zaidi… (orodha hii inapaswa pia kubandikwa mahali panapoonekana katika afisi ili kuongeza uwezekano wa kuifikia haraka kwa wafanyikazi waliopo.

Habari hii ni halali na ni ya umma. Hivyo basi inaweza kupatikana kwa kuonekana na watu wote. Hali hii haiwezi kuzuia upekuzi (iwapo mtu anacho au hana kibali cha upekuzi). Hata hivyo inaweza kusaidia kupunguza msongo na akili miongoni mwa wale wanaopekuliwa. Inaweza pia kuchangia katika kumpa mpekuzi ilani kwamba Yule mtu au shirika linalopekuliwa lina ufahamu wa haki zake na kwamba hatua itachukuliwa baadaye iwapo upekuzi unavuka mipaka ya kisheria ya uzuiaji.

### b ♦ Tishio kwamba habari inaweza kuibiwa, kupotezwa au kuharibiwa.

Kwa jumla, mashirika mengi huhifadhi habari zaidi ya ile inayohitajika. Katika hii kiwango kikubwa cha habari aghalabu hakitumiki na huwa sio ya siri. Yaani, ni kiwango kidogo tu cha habari ambayo ni ya siri na hii haifai kupatikana na wapekuzi. Kikamilifu, habari ya kibinafsi huwa inahusisha: orodha za watu (wanaofaidika kutokana na mradi, mashahidi wa kesi); ushahidi wa dharura katika kesi za kisheria; kesi maalum na uchanganuzi.

Habari inayochukuliwa kama ya hadharani au isiyokuwa tata inaweza kuhifadhiwa afisini ili wapekuzi wachukue (kama afanyavyo mtu anayesafiri na pesa, huku kiacha wazi zile tu zinazoweza kuibiwa na jambazi).

Sera bora ya usalama wa habari ina maana kwamba mengi ya matokeo yanayohusiana na hasara, wizi au uharibifu wa habari huwa yamepunguka pakubwa.

Ina maana pia kwamba watetezi wasihisi haja ya kujidhihirisha wazi ili kulinda habari (katika hali yoyote maisha ni bora kuliko chochote kile)l hili litapunguza uwezekano wa kutokea msongo wa akili unaotokana na upekuzi, hivyo kupunguza hatari ya kutokea fujo na majeraha ya kimwili na kisaikilojia (tishio/ tokeo la hapo juu likiwa linashughulikiwa).

**Udhaifu:**

- Habari ambayo haijahifadhiwa kutokana na tofauti iliyobainishwa baina ya kuwa siri au la
- Habari nyeti kuwekwa kwenye karatasi
- Habari ya kielektroniki kutofichwa (faili na viambatisho)
- Ukosefu wa usalama wa kutosha wa afisini na nyumbani: vizuizi na vichujio visivyotosha vya kuzuia kufikiwa na vitu visivyofaa au angalau kuruhusu muda wa kuifunga kompyuta au wa kuficha faili.

**Uwezo:**

- Nakala za habari za kila mara zilizohifadhiwa kwenye kompyuta ili zitumiwe kunapotokea dharura yoyote (angalau kila wiki), na ambazo zimewekwa mahali palipo salama. Upekuzi wowote unapotekelezwa, utajua bila shaka ni kiwango gani cha habari iliyodhihirika nje

(kutegemea tarehe ambayo upekuzi ulifanywa, ikilinganishwa na tarehe ambayo hifadhi kwa matumizi ya dharura ilifanywa/hifadhi ya habari).

- Nakala za habari iliyonakilishwa, au hata bora kuliko hizo, nakala za habari zilizopigwa skani, ili kuhifadhi rekodi za stakabadhi muhimu mahali palipo salama. Ikibidi zinaweza kusambazwa kwenye maeneo mengine yaliyo salama.
- Hatua za usalama za afisini na nyumbani zinatosha.
- Ilani itolewe mwanzoni mwa upekuzi ili kupata msaada wa kisheria (mawakili) na maombi kutoka kwa mashirika mengineyo ya kutoa msaada na pia upekuzi ushuhudiwe, angalau kutoka nje. Jambo hili litatoa shinikizo kwa wahujumu kwa matumaini kwamba watazingatia sheria watakapokuwa wakifanya upekuzi

| **Mlinganisho wa mifumo mbalimbali ya kuhifadhi data kunapotokea dharura** | | |
|---|---|---|
| **Jinsi ya kuhifadhi** | **Uzuri** | **Ubaya** |
| Kuchomeka kwenye CD/DVD | Kompyuta nyingi zina vichomezi vya santuri ya CD/DVD | Iwapo kuna idadi kubwa ya habari, santuri nyingi za CD zitahitajika, jambo linalofanya harakati hiyo nzima kuwa ndefu na tata zaidi |
| Diski ya mwako inayohifadhiwa habari | Kama hapo juu | Kama hapo juu japo ni rahisi kuhifadhi, hivyo basi, isiweze kudhibitiwa na watu wasiofaa |
| Hifadhi ngumu ya nje ya kompyuta | Huhifadhi kiasi kikubwa cha habari na haichukui muda mrefu kunakilisha. Inaweza kuwa na misimbo mingi ya kulinda habari | Hugharimu dola za Marekani baina ya 200 na 300 |
| Huduma ya mtandao iliyo sehemu ya mbali kiasi | Inaweza kudhibiti habari yote, ni ya haraka, haiwezi kuibiwa wala kupotea | Mnahitaji chombo kilicho na hifadhi ya mtandao na pia mtumie mbinu ya ufichaji data. Kampuni zinazotoa huduma ya mtandao zinaweza “kulazimika” kuwapa wapekuzi makavazi (dai la usalama wa serikali) |

**c ♦ Tishio/Tokeo kuhusu habari inayoibiwa na kutumiwa na mtu mwingine.**

Uwezekano mkubwa wa matokeo ya shirika na ya watu kuwekwa wazi katika habari hiyo.

**Matokeo ya shirika lililopekuliwa**

**Udhaifu:**

- Hakuna mazingatio ya mapema kuhusu taratibu za makabiliano yanaweza kutokea
- Kupuuza maadili, kufanya hesabu isiyofaa, programu zilizoibiwa (kunaweza kuashiria kwamba hatua za sheria zichukuliwe dhidi ya shirika)

**Uwezo:**

- Kuwepo nakala zilizohifadhiwa kwa sababu za kidharura
- Kuwepo kwa mpango wa makabiliano

**Matokeo ya watu waliotajwa katika habari**

**Udhaifus:**

- Kutokuwa na majadiliano ya hapo nyuma na watu wanaohusika kuhusu kuwepo kwa uwezekano
- Kutoweza kuwafikia kwa haraka

**Uwezo:**

- Kutoa maelezo ya kuwepo kwa hatari na kuhakikisha iwezekanavyo kwamba haitatendeka kwa sababu ya mapuuza ya shirika/watu
- Kuwa na mipango ya pamoja kuhusu jinsi ya kukabiliana na dharura (kuurejelea mpango kwa haraka, hatua za kujilidna, mahali pa kujificha nk)

**d ♦ Tishio kwamba vitu vinavyotatanisha vinaweza kuwa "vimefichwa" (silaha, dawa za kulevya, stakabadhi) ili baadaye, kulikabili shirika "kisheria".**

**Udhaifu:**

- Nafasi katika afisi imejaa vitu na karatasi zisizohusiana na kazi (vitu vya kibinafsi, majarida yaliyotawanyika …) ni vigumu zaidi kutambua iwapo kuna kitu kilichofishwa kwa maksudi wakati wa upekuzi, au ikiwa mgeni aliyekuwepo hapo awali ameficha/aliacha kitu/stakabadhi zinazotatanisha ambazo zinaweza kupatikana kwa urahisi na wapekuzi
- Hakuna orodha ya vifaa vya afisini kabisa, wachilia mbali orodha iliyopendekezwa na kusajiliwa na wakili
- Ni mtu mmoja pekee kutoka kwa shirika ambaye yupo wakati wa upekuzi

**Uwezo:**

- Panapowezekana, (katika hali ya upekuzi wa kisheria[1]), watu wameshajiandaa kujibanza kwenye kona/vyumba mbalimbali vya afisini (kwa mfano, kila mmoja yupo kwenye mahali pake pa kazi) ili aweze kutazama yanayotendeka wakati wa upekuzi. Kufanya hivi pia ni rahisi kugundua iwapo kuna kitu kinachoibiwa.
- Baada ya upekuzi (bila ya kujali aina ya upekuzi), shirika litakagua kikamilifu afisi au mahali pa upekuzi (ikiwezekana kwa msaada wa watazamaji kutoka nje), kurekodi (hata picha) kila kitu kinachoweza kupatikana na kuhakikisha kwamba chochote kisicho cha afisi/ambacho hakikuwepo kabla ya upekuzi, kinaripotiwa na kwama kisiguswe (tahadhari na alama za vidole). Tengeneza pia orodha ya vitu ambavyo vinakosekana.
- Andaa ripoti na uiwasilishe kwa polisi kisha chukua hatua za kisheria.

## e ♦ Tishio/Tokeo la pesa na mali fulani (kama kompyuta...) kuibiwa au kuharibiwa

Upekuzi usioruhusiwa unaweza kupelekea kuibiwa kwa vitu.

**Udhaifu:**

- Kiwango kikubwa cha pesa na vitu vya thamani vilivyohifadhiwa afisini
- Vitu visivyokuwa na ulinzi
- Hakuna orodha ya vifaa vya afisini kabisa, wachilia mbali orodha iliyopendekezwa na kusajiliwa na wakili
- Hakuna bima dhidi ya wizi

**Uwezo:**

- Wapange wafanyikazi wa afisini katika sehemu tofauti za afisini ili kushuhudia upekuzi[2]
- Ilani itolewe mwanzoni mwa shughuli ya upekuzi ili kupata usaidizi wa kisheria (mawakili) na ili mashirika mengineyo yaweze kuombwa kutoa usaidizi wao na hata kushuhudia upekuzi, angalau kutoka nje. Jambo hili litashinikiza wale wahujumu kutii sheria wakati wa shughuli ya upekuzi

1 Iwapo upekuzi umetekelezwa kwa fujo, ni muhimu kwamba watu wasalie kwenye kundi ili kupunguza hatari ya kudhulumiwa kwa mtu binafsi.

2 Tena, iwapo upekuzi umetekelezwa kwa fujo, ni muhimu kwamba watu wasalie kundini ili kupunguza hatari ya kudhulumiwa kwa mtu binafsi.

## Jinsi ya kukabili na kupunguza tishio la upekuzi wenyewe

Iwapo upekuzi utafuata sheria za kimataifa na una malengo ya kisheria na haki, basi hakuna hata haja ya kufikiria kuhusu kukabiliana au kupunguza tishio la upekuzi. Unapaswa kuwa wazi tu na uzingatie hatua za hapo nyuma za kushughulikia matokeo. Hata hivyo, iwapo pekuzi zitatumiwa kama kigezo cha kuzuia kazi ya watetezi wa haki za binadamu na mashirika ya kijamii, basi hatua dhidi yazo inafaa kuchukuliwa.

Ili kulikabili na kulipunguza tishio la upekuzi wa kisheria, mbinu bora ni kuongeza gharama yalo ya kisiasa kupitia kwa kampeini za umma na kulitolea mapendekezo bora zaidi kwa ushirikiano na mashirika na taasisi nyinginezo.

Iwapo kuna hatari ya upekuzi usio wa kisheria (au wizi) ni muhimu kuimarisha usalama kadiri iwezekanavyo katika nyumba, afisi au katika majengo mengine.

Hili litafaa pia iwapo afisi/nyumba yenu inapatikana maeneo ya mjini au mashambani.

## Muhtasari

**Jinsi ya kuzuia hatari ya upekuzi.**

Upekuzi unaweza wa halali wa haramu (upekuzi haramu utafanana na uvamizi).

Na kama itakavyokuwa kwa hatari nyingineyo mahususi, zidisha gharama za kisiasa za upekuzi.

Tumia mawasiliano na ufungue kila elementi kwa umbali unaoweza kuufikia.

Orodhesha matishio/matokeo na udhaifu na uwezo wa kila mojawapo kisha shughulikia hayo:

a • Tishio kwamba wakati wa upekuzi mtu aweza kudhuriwa kimwili au kisaikolojia

b • Tishio kwamba habari inaweza kuchukuliwa, kupotea au kuharibiwa

c • Kuhusiana na hilo, kwamba habari inaweza kutumiwa kwa njia isiyo kamilifu na mtu mwingine

d • Tishio kwamba vitu vinavyotatanisha vinaweza "kufichwa" (silaha, dawa za kulevya, stakabadhi) ili baadaye kulikabili shirika "kisheria"

e • Tishio/tokeo la pesa na mali fulani (kama vile tarakilishi...) kuibiwa au kuharibiwa

# Kuzuiliwa, kushikwa, kutoroshwa na kutekwa nyara kwa mtetezi

## "Hakuna habari kutoka kwa mtetezi"

Tutakapokosa habari kuhusu alipo mtetezi, changamoto ya kwanza itakuwa kutaka kubainisha hasa ni nini kilichotendeka kwake, na hili linaweza kuchukua muda. Mambo kadhaa yanaweza kuwa yametendeka:

- Mtetezi anaweza **kukataa** au **anaweza kuwa amesahau** kuwasiliana na shirika: anaweza kuwa ameamua kwenda ziara fulani au kujivinjari wakati wa wikendi, bila ya kumwambia yeyote (au aweza kuwa "hataki" tu kuwasiliana nao). Anaweza pia kujipata hana simu wala njia nyingine yoyote ya mawasiliano, au anaweza kuwa hashughuliki na kutaka kuingia afisini. Watetezi hao wanaweza kuwa hawakutaka mtu yeyote ajue wanayofanya (mara nyingine wakifanikiwa kwa hilo). Wanaweza (na hii ndiyo hiari isiyotumika zaidi) kuwa wamesahau au hawajagundua ukweli kwamba kutokuwepo kwao kunaweza kuwashughulisha wenzao.
- Mtetezi anaweza kuwa hakufanikiwa kuwasiliana na shirika kutokana na **sababu za kiufundi**: hili linaweza kutokea wakati ambapo, kwa hali isiyotabirika au kutarajiwa, mtetezi anakatika kimawasiliano kabisa akiwa katika maeneo ya mbali. Hili laweza kutokea wakati wa ziara ambapo kwa kutotarajiwa, mtetezi anajipata mahali pasipo na mawasiliano, ambapo barabara imezuiwa, au anapaswa kutumia njia nyingine mbadala, au aubadilishe mpango wake wa kazi kiufaraguzi, hili likisababisha aende mahali kusiko na mawasiliano. Inaweza pia kuwa kwamba mbinu ya mawasiliano aliyopania kutumia imeharibika kwa njia fulani (simu ya mkononi iliyoharibika, hakuna muda wa maongezi, betri isiyofanya kazi, mawimbi ya simu kuharibika nk).
- Mtetezi anaweza kuwa hawezi kwenda afisini kutokana na **magonjwa au kulazwa hospitalini** (kwa mfano kutokana na ajali ya barabarani, ugonjwa aliokuwa hajaubaini kwa muda, au ugonjwa alio nao kumwathiri zaidi ya ilivyo).
- Mtetezi anaweza kuwa **amezuiliwa, amekamatwa, ametekwa nyara** au **ametoroshwa**. Haya yote yanaelekea kufanana kwa namna kwamba mtetezi amenyimwa uhuru wake wa kutembea na anaweza kukumbana na hali yoyote, kuanzia kwa shinikizo lisilo la madhara hadi kutishiwa maisha.[1] Katika hali nyinginezo, mtetezi anaweza kwenda kwenye shirika, kwa maana kwamba shirika hilo litakuwa na habari zaidi kuhusu hali hiyo.

1 Katika sura hii tutaonyesha baadhi ya mambo yaliyo katika kitabu muhimu cha mwongozo wa usalama kilichoandikwa na Van Brabant (2000) (Sura ya 13).

*Uzuiliwaji* una maana kwamba wanachama wa shirika wamewekwa chini ya ulinzi wa kundi la (askari au kijeshi, utawala wa mitaa nk). *Kutiwa mbaroni* kwa maana ya kuzuiliwa na vikosi vya usalama (ili kanuni kuu ya ndani iweze kubatilishwa). *Utoroshwaji* una maana ya kukamatwa kwa nguvu kwa mtetezi na kutolewa kwa njia isiyoruhusiwa kutokana na sababu za kisiaa. *Utekwaji* nyara una maana ya kukamatwa kwa nguvu na kuzuiwa kwa sababu ya wazi ya kutaka makubaliano fulani kutoka kwa yule aliyetekwa nyara na watu wengineo. Katika sura hii itakuwa bora tukitumia istilahi *uzuiliwaji* ili kujenga uelewa mwepesi.

Kwa jumla, tunafaa kusema kwamba mara nyingi kukosa kupata kujua aliko mtetezi, huwa kunagawika mara mbili (kutotaka au kusahau kuwaisiliana, kutofanikiwa kuwasiliana kutokana na sababu za kiufundi). Hebu tuone jinsi ya kuzuia na kukabiliana na hali hizi mbili.

### Vidokezo vya kuzuia hali ya "Hatuna habari" kuhusu mahali aliko mtetezi.

**Mtetezi hangependa au amesahau kuwasiliana na shirika.**

- Kila mwanachama wa shirika na hususan wale walio na hatari zaidi hawana budi kufahamu ukweli kwamba suala la kudokeza mahali walipo litawashughulisha watu wengine. Iwapo hawangependa kuwasiliana na watu wengine, wanafahamisha wenzi wao kuhusu hilo, na wawajulishe kila mara ni lini watarejea. Katika hali ya watetezi walio na kiwango cha juu cha hatari, haitakuwa bora wao kukosa kuwa na mawasiliano ya mara kwa mara.
- Ni bora kubuni mtindo wa kila mara wa kuonyesha iwapo mtu ameingia kwenye shirika ili kuwa na mawasiliano ya kila mara na shirika (kwa kawaida huwa watu wenye jina moja au mawili). Hili huwa muhimu wakati ambapo viwango vya kukabiliana na hatari kwa mtetezi huongezeka (kwa kuwa wanasafiri kuelekea katika maeneo hatari, au wamepokea matishio nk.)

**Kutokana na sababu za kiufundi, mtetezi hawezi kuwasiliana na shirika.**

- Makubaliano ya kabla, ya kuingia katika shirika yanafaa kubainishwa, na matatizo ya kimawasiliano yanafaa kutarajiwa katika nyakati hizo: kwa mfano, iwapo wakati wa kuingia kwenye shirika unasadifu na ziara, inafaa kufikiriwa ni kwa jinsi gani na ni lini inawezekana kuwa na mawasiliano (kwa kutumia simu ya mkononi au ile ya mezani, au njia nyinginezo za mawasiliano) ili kuwa na uhakika kwamba itawezekana, na kuhakikisha kwamba kuharibika, kukatika kwa mawasiliano au kumalizika muda wa maongezi au kutofanya kazi kwa betri hakutazuia mawasiliano.
- Kuwa na njia mbadala za mawasiliano (kwa kutumia watu wengine kwa mfano).

**Mtetezi hawezi kuwasiliana kwa sababu yeye ni mgonjwa au amelazwa hospitalini.**

- Orodha za nambari za simu na anwani za hospitali na pia maeneo ya kiafya katika sehemu iliyozuriwa, zinafaa kuhifadhiwa, na inapowezekana pawe na namna ya kujua lolote kuhusu ajali za barabarani (kampuni za basi, polisi wa trafiki, mawasiliano kwenye njia nk).

- Watetezi hawafai kufanya ziara ila wewe katika hali nzuri ya kiafya.
- Tumia mbinu bora zaidi za usafiri (yakiwemo mabasi au mbinu nyinginezo).
- Watetezi wanapaswa kuwa na bima ya kisasa ya afya na ajali.

**Kuzuia uzuiliwaji.**

Si rahisi kutarajia kuzuia hali ya kuzuiliwa. Lengo kuu ni kupunguza sababu na uwezekano unaoweza kusababisha au kuwezesha uzuiliwaji wa mwanachama yeyote wa shirika.

- Tabia za kimaadili za watu binafsi na shirika ni muhimu ili kimantiki, uvunjaji wa sheria ya kawaida wa mtu binafsi na shirika uwekwe kando. Uvunjaji wa sheria ya kawaida bila shaka unaweza kutumiwa kama kisababu, japo wakili wa shirika atajua la kufanya. Zaidi ya hayo mtetezi aliyezuiwa atajua kwamba hatua zinachukuliwa na anaweza kuzikarriri binafsi kwa karibu ya makataa ya muda uliowekwa "abaki mtulivu" (athari ya kisaikolojia), akiwa anajua kwamba hatua za nje zimeshaanza kuchukuliwa. Hakuna haja ya kuyapa mamlaka changamoto au kuyapa fursa kisha mtetezi huyu kujiweka katika hatari zaidi ya ile anayokabiliwa nayo.
- Katika hali ambazo uvunjaji wa sheria unatumiwa kama hatua ya kisiasa, ukadiriaji mkamilifu wa hatari unabidi kisha mkakati wa kuzuia uharibifu hauna budi kuundwa, haya ni kutokana na hatari iliyoongezeka kwa watetezi.
- Uzuiliwaji wa kisheria unaweza kuwa kisingizio. Uzuiliwaji huu unaweza au usiweze kutokana na agizo na/au kibali cha kutiwa nguvuni na unaweza kutokea wakati wowote kwenye afisi/nyumbani au wakati wa ziara. Lengo lingekuwa ni kuzuia kutiwa nguvuni kwa mtetezi akiwa pekee ili kupunguza matokeo yanayohusiana na uzuiliwaji wenyewe. Kinachohitajika zaidi ni mkakati wa hatua ya kisiasa unaolenga kuzuia mamlaka kutowakamata watetezi; hata hivyo, mwelekeo katika nchi nyingi unaonekana ni kuwaweka chini ya sheria za kimahakama kisha kuwafunga jela kwa sababu mbalimbali, zikiwemo zisizohusiana na kazi yao.
- Si rahisi kuzuia utekwaji nyara. Licha ya kufanya ukadiriaji wa juu wa gharama ya hatari, na pale kunaposhukiwa kwamba tishio la utekaji nyara limetolewa, ni muhimu kupunguza udhihirikaji nje katika maeneo ambayo tishio hilo linaweza kutekelezwa, hakikisha kwamba mtu asibaki peke yake, na jaribu kuchunguza tendo lolote linaloweza kusababisha utekwaji nyara.
- Utekaji nyara unaweza kutekelezwa na wahalifu wa kawaida (kama kisingizio au (a) au na washika dau wa kisheria na/au askari wa kisheria, na/au makundi ya kisiasa yenye silaha nk. Tendo linaweza kutokea mahali popote, lakini hasa litatendeka wakati ambapo ama fursa hiyo italetwa na watu wanaoweza kuhujumu, au mtetezi mwenyewe awape na mara nyingi katika maeneo yasiyokuwepo na shahidi. Hivyo basi, si rahisi utekaji nyara kutokea afisini wakati wa mchana nk. (tazama mifano ya vitisho vya mauaji dhidi ya kiongozi wa shirika katika sura ya 1.7).

  Tofauti kati ya taratibu zisizoruhusiwa za uzuiliwaji wa kisheria na hujuma/ utekaji nyara ni finyu mno hivi kwamba tunapendekeza kuwa watetezi wa haki za binadamu wanazingatia vipengele vyote vya sehemu hizo mbili kama vyenye kukinzana badala ya kutoshelezana. Hata hivyo,

tunachukulia kwamba ni muhimu kutaja tofauti baina ya maana halisi za uzuiwaji na utekaji nyara kwa ajili ya mausala ya kisaikolojia na kimatendo.

- Utaratibu wa kuzuia hujuma/utekaji nyara unafaa kuzingatia mambo kama harakati za kila za kikazi za mtetezi katika sehemu yake ya kawaida ya kazi , wakati wake usio wa shughuli nk., halafu bila shaka katika ziara za nyanjani, ziwe zimepangwa na shirika na/au kutokana na mwaliko. Kuwa macho na chunguza mialiko yote kutoka kwa watu usiowajua

## Tunashuku kwamba mtetezi amezuiliwa (au ametiwa nguvuni, ametekwa nyara au ametoroshwa)…

Ni lini tunaweza kukashuku kwamba mtetezi amezuiliwa bila ya yeye kupenda? Naam, iwapo hatupati habari ya moja kwa moja kutoka kwa mtetezi, ni lazima tushuku hivyo iwapo tutapuuza uwezekano wa aina tatu ya kwanza… Kihalisi, utaratibu wa kukabiliana na kuzuiliwa au kuzuiliwa tunakoshuku kwamba kumetekelezwa hufuata utaratibu wa makabiliano unaotumiwa wakati mtu atakosa kufika kazini anapofaa kuwa.

Kwa hivyo, iwapo tutakosa habari kutoka kwa mtetezi tunafaa kuanza kuitafuta, ili tupuuze uwezekano wa aina tatu za kwanza. Ni vigumu kuwa na uhakika kwamba hatujahusisha uwezekano wa aina tatu za kwanza. Kutokana na sababu hii, ni muhimu kuwa na kipimo cha muda kabla ya kuzingatia uwezekano wa aina ya nne: masaa matatu bila habari, masaa sita, kumi na mawili… kutegemea muktadha, hali, kiwango cha hatari, ufahamu wa mtetezi kuhusu haja ya kuripoti, nk. Kadiri wakati ulivyo mdogo, ndipo tunapokuwa tumetoa tahadharisho; kadiri muda unavyokuwa mrefu, ndipo tunapochelewa katika kuchukua hatua ifaayo. Si uamuzi mwepesi wa kufanya.

**Tahadhari:** Ripoti inaweza kukosa kuwekwa kwenye faili kimakosa, kutokana na mapuuzo ya mtu anayepaswa kuwa amefanya hivyo, au kupitia kwa ukosefu wa mawasiliano – haya yote yanafaa kutarajiwa wakati wa kupanga ratiba ya kuripoti kwa ajili ya safari ya nyanjani.

**Kumbuka:** Tunaweza tukakabiliana na uzuiliwaji unaotuhumiwa na ule uliothibitishwa.

Ni muhimu kwamba makabiliano ya watu waliozuiliwa na yale ya shirika husika yajumuishwe pamoja, kisha jaribuni kuyatimiza malengo yanayolingana. Ni kutokana na sababu hii kwamba wanashirika wote wanafaa kuzielewa taratibu za kukabiliana na uzuiliwaji.

## KUZUILIWA (kutia nguvuni, kutorosha, kutekwa nyara):

Kuzuiliwa (kutia nguvuni, kutoroswa, kuteka nyara) kunaweza kutofautiana katika wakati, kwa mfano, kuanzia kwa masaa machache hadi kwa miaka mingi. Aghalabu suluhisho hupatikana kwa kumwacha huru yule aliyezuiliwa au hali inaweza kubadilika ikawa ya utekaji nyara iwapo lengo litabadilika kutoka hali ya kuzuiliwa hadi hali nyingine mbaya zaidi ya utoroshaji – jambo linaloweza kupelekea kuwepo kwa majeraha au hata vifo, au "kupotea.

**Uzuiliwaji unapaswa kukabiliwa kwa mujibu wa mitazamo mitatu:**

- Kutokana na mtazamo wa mwenye kuzuiliwa
- Kutokana na mtazamo wa shirika analotegemea mwenye kuzuiliwa
- Kutokana na mtazamo wa familia na jamaa ya mzuiliwaji.

**Malengo ya kijumla unapokabiliana na uzuiliwaji:**

- Punguza uwezekano wa uzuiliwaji kutokea
- Tambua kwa wepesi kuhusu uwezekano wa kuzuiliwa
- Orodhesha jinsi ya kukabiliana na hali kama hiyo:
  - Makabiliano ya papo hapo
  - Makabiliano ya muda wa wastani (si wa baadaye sana wala si papo hapo

Ili kufanya mwongozo huu kuwa mwepesi iwezekanavyo, tutashughulikia uzuiliwaji (zikiwemo haja) kando na na utekwaji nyara pia kando.

## Kuzuiliwa kwa mtetezi: kabiliano la papo hapo

### Malengo na hatua za makabiliano ya papo hapo dhidi ya uzuiliwaji:

Unda kundi maalum linalofanya kazi ili kukabiliana na uzuiliwaji.

1 ♦ Linda maisha na uhuru wa wanashirika.

2 ♦ Tambua eneo la kijiografia waliko watu waliozuiliwa, ukitumia ramani, ratiba ya ziada, majina ya watu uliowasiliana nao mwisho, mawasiliano ya simu na washika dau wa nyanjani, nk.

3 ♦ Tafuta kujua ni mshika dau yupi aliyejihami ambaye amemzuilia mtu, kwa nini akafanya hivyo na kwa kiwango gani?.

- Kwa kutumia mbinu ya kijiografia aliko mtu/watu, pamoja na ufahamu wa nyuma (unaweza kudokeza sababu za kuzuiliwa iwapo huzijui hadi sasa). Hivyo basi, itawezekana kukisia mtu aliyemzuilia mwenziye au angalau kuweza kuandaa orodha ya watu unaowashuku kufanya hivyo.
- Wasiliana na wenye mamlaka (ikiwa inatosha, inafaa na ikiwezekana).

4 ♦ Jitahidi kufikia kiwango cha kuwachiliwa huru kwa mtu aliyezuiliwa bila kudhuriwa.

■ Kama ilivyo kanuni ya kijumla, si muhimu kutaka kuunda mkataba, lakini badala yake uruhusiwe "kuondoka" kwa uhakika huku ukiacha nyuma majadiliano hadi atakapoachiliwa mtetezi.

■ Tathmini muungano uliojihami ambao ulihusika (kwa ushirikiano wa mamlaka ya kieneo palipo na uwezekano/panapofaa), ama kwa njia ya moja kwa moja katika muungano wa vikosi vya usalama, au kwa kutumia wasuluhishi – usaidizi wa miungano mingineyo kama vile makanisa, waheshimiwa au wazee wa eneo hilo, Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu, nk. … Kwa sababu hii ni muhimu kutegemea watu na miungano/mashirika haya. Utathmini huu utalenga kujenga hakikisho la sababu ya kuzuiliwa, na kujaribu kutafuta namna ya kuachiliwa kwa mtetezi aliyezuiliwa.

■ Zingatia kuwatahadharisha watetezi wengine wa haki za binadamu na mashirika ya kibinadamu ili wapate kujua, na kwamba waweze kuchukua hatua zifaazo za pamoja ili kujilinda na hali hiyo kukishukiwa kuwa utekaji nyara unaoweza kuwa wa majeraha kwa mtetezi utatokea (kama vile utekaji nyara unaofanywa na kikosi cha askari) ni bora kuchukua hatua ya haraka na kisha kuwalenga zaidi viongozi wa kawaida (panapofaa) wa

kundi linalowajibikia utekaji nyara huo, au kwenye miungano ya kisiasa inayokaribiana na ile iliyotekeleza, na ambayo inaweza kukabiliana na shinikizo la kitaifa na kimataifa.

- Peleka tahadhari kwa ubalozi iwapo mtu aliyezuiliwa anatoka katika nchi nyingine.

**Kuzuiliwa kwa mtetezi: makabiliano ya muda wa wastani (si papo hapo au baada ya muda mrefu wa kuzuiliwa kutokea**

Iwapo mtetezi amezuiliwa, na hatutarajii kwamba ataachiliwa baada ya muda mfupi, basi malengo na hatua za muda wa wastani zinapaswa kuchukuliwa lakini bila kusahau malengo ya muda mfupi.

**Malengo na hatua za makabiliano ya muda wa wastani wa kuzuiliwa.**

1 ♦ Salia katika kuzingatia malengo ya makabiliano ya muda mfupi.

2 ♦ Katika hali ya kutiwa nguvuni, pamoja na kutambua haraka iwezekanavyo mtu aliyemtia nguvuni mtetezi, jaribu kupata uhawilisho hadi kwenye ulinzi wa kisheria au kwa huduma ya usalama ambayo washika dau wana ushawisi fulani. Katika hali hii, jitahidi kupata msaada wa kisheria haraka iwezekanavyo (uwe umejiandaa mapema). Hivyo hatari ya kudhulumiwa na kuteswa inaweza kupungua.

3 ♦ Iwapo mtetezi ataendelea kuzuiliwa, jaribu kumpa mahitaji ya kimsingi – usalama, chakula, matibabu, mawasiliano na watu wa familia yake na hata shirika lake, nk. kuanzia mwanzo wa harakati hiyo (na hili pia linafaa kuwa limepangwa kabla – tazama hapa chini: mambo ya kuwafanyia watu wa familia na jamaa.

**Makabiliano ya watu waliozuiliwa**

- Kumbuka zile hatua na mipango iliyoundwa kwa kuzingatia uwezekano wa kutokea hali kama hizo. Ni muhimu kujua ni mfululizo upi wa utaratibu ulio sawa wakati kunapotokea hali ya uzuiliwaji au kutiwa nguvuni. Ili kupunguza shaka, tumia nguvu zako kwa njia bora kisha unda malengo mepesi ya kuupinga uzuiliwaji/utiwaji mbaroni.
- Salia mtulivu. Watetezi wanafahamu kwamba shirika lao lina itifaki ya makabiliano na kwamba hatua zinachukuliwa; wanaweza kuzikariri hadi kukaribia makataa ya muda wao kisha wakabaki watulivu.
- Kila kitu kinachosemwa na kufanywa kinapaswa kulenga kuhifadhi uhai na usalama wa wazuiliwa.
- Wasiliana na kiongozi mkuu wa kundi lililojihami, kisha chochea mazungumzo naye, ukitumia hoja za kimsingi kwa lengo la kutaka kuachiliwa kwa watu waliozuiliwa na kurejeshwa walikotoka, au wapelekwe mahali pengine popote palipo salama (usikusudie kujadiliana naye kuhusu “makazi”).
- Iwapo hili haliruhusiwi, tafuta ruhusa ya kutumia mbinu yoyote iliyopo kulifahamisha shirika kuhusu msimamo wako; usijaribu kupiga simu bila ruhusa iwapo u chini ya ulinzi, kwa kuwa hili linaweza kuleta hatari zaidi kuliko kutofanya lolote.

- ♦ Iwapo uzuiliwaji unatekelezwa na vikosi vya usalama, tumia hoja za kisheria za shirika kwa ajili ya kesi kama hizi.
- ♦ Salia mtulivu na usisahau kwamba shirika linajitahidi kwa haraka kujiweka tayari na mifumo ya usalama kadiri muda unavyosonga.

**Hatua zinazolenga familia na jamaa:**

- Julisha familia na jamaa iwapo aliyezuiliwa hataachiliwa hivi karibuni. Tambulisha na udumishe uaminifu.
- Tengeneza njia ya wazi ya kuwasiliana na familia. Toa usaidizi na uwajulishe kila kunapotokea jambo (jenga uhusiano wa karibu na mmoja katika jamaa zake).
- Familia itahitaji muda wa kupewa makini kutoka kwa shirika. Tarajia hisia na uamuzi usio wa mkondo mmoja kila wakati kutoka kwa familia – hasa wanapoletewa habari mpya.
- Katika hali ya kuzuiliwa kwa muda mrefu au kufungwa jela, ni muhimu kutengeneza mpango wa msaada kwa familia ya mtu aliyezuiliwa.

## Kumtorosha na kumteka nyara mtetezi[2]

### Kutokana na mtazamo wa shirika

Kudhibiti tatizo la utekaji nyara ni mchakato unaobadilika unaoweza kuchukua muda wa baina ya masaa machache hadi miezi au hata miaka. Masuala muhimu ni uhamasishaji wa kundi lenye umilisi wa kudhibiti matatizo; kushughulika na familia, mamlaka na vyombo vya habari; mawasiliano na majadiliano na watekaji nyara.

### Kuwasiliana na kujadiliana na watekaji nyara

Utekaji nyara, kama ilivyoeleweka hapa, ni tendo la kimakundi na lenye lengo Fulani. Watekaji nyara huanzisha mawasiliano ili kubainisha matakwa na masharti yao Kundi la kushughulikia matatizo linafaa kuwa na udhibiti wa majadiliano yao na watekaji nyara, lakini liepuke kuwasiliana nao kwa njia ya moja kwa moja; lengo ni kujaribu kupoteza muda ili kuruhusu ufanyaji uamuzi na mashauriano ya ndani na nje ya shirika. Ikiwa inafaa, unaweza kutaka ushahidi wa kujua iwapo waliotekwa nyara ni hai na pia ushahidi wa utambulisho wa watekaji nyara, kisha kuwahimiza na kutaka watekwaji nyara walindwe vizuri.

Ikiwa utekaji nyara ni hatari ya kihakika, basi ni muhimu kukubaliana kuhusu baadhi ya sheria na taratibu zinazohusiana na utoaji fidia ya kuwakomboa na pia maombi ya watekaji nyara, kisha ikiwezekana kuwatangaza hadharani kwa ushirikiano wa mashirika yaliyo kama hili. Kwa vyovyote vile, matukio ya kabla kama haya, yatatoa maelekezo ya hatua za utekaji nyara.

### Kutokana na mtazamo wa mtetezi aliyetekwa nyara/aliyetoroshwa

■ Nyakati hatari zaidi, ambapo watekaji nyara watakuwa na wasiwasi mwingi ni pale mtu anapotekwa nyara, wakati ambao aliyetekwa nyara atapelekwa kwa haraka kwa kuwa watekaji nyara wanahofia kwamba wenye mamlaka wako karibu nao, pale wanapomzingira au wanapomwachilia mtekwa nyara.

2 Tutatumia sana kazi ya Van Brabant (2000) kuhusu hii mada.

- Watekaji nyara wako wanakutaka unyamaze; unaweza kufungua kitambaa machoni, ukapigwa au pia ukapewa dawa za kulevya kwa sababu hiyo. Haina maana kulia au kung'ang'ana kuzuia mbinu zao hizi: kwa hakika kunyamaza tu kunaweza kukusaidia kuwaepuka (ila labda uwe unatarajia hilo kikweli unapotekwa nyara, kulia au kupiga ukemi kunaweza kuwaleta watu wengine wakusaidie).
- Mahali na masharti ambayo watekwaji nyara wamepewa hutofautiana pakubwa. Mnaweza kuwekwa mahali pamoja au mkasongeshwa mara nyingi; mnaweza kukaa pamoja na watekwaji nyara wengineo. Ni kawaida kwa watekwaji nyara kuwa na aina fulani ya uhusiano na walinzi wao kisha huwa vigumu kwao kuzoea kutokana na kubadili walinzi wao.
- Tii maagizo ya watekaji nyara wenu bila ya kujinyenyekeza sana: epuka kuwashangaza au kuwashtua.
- Jitahidi kudumisha afya ya kimwili na kimawazo.
- Ikiwa u katika kundi, jitahidi usitenganishwe kwa sababu kuwa na angalau mtu mmoja karibu nawe anaweza kukupa msaada wowote. Ni muhimu hata hivyo, kuwa tayari kutengwa na kubadilishwa, na kwa wasiwasi ambao utaletwa na siku mpya na ambao utahitaji kukabiliwa.
- Kupata ruhusa ya kuachiliwa sio tatizo lako, bali ni la shirika lenu. Usiwahi kuhusika moja kwa moja katika majadiliano ya kuachiliwa kwako. Hili litatatanisha mambo bure. Ukiamrishwa uzungumze kwenye redio, simu au kwenye video sema tu lile ulioambiwa au ulilоruhusiwa kusema kisha kataa kujadili kuhusu kuachiliwa kwako hata kama utashinikizwa na watekwaji nyara wako.

## TARATIBU ZA UZUIAJI: KUPUNGUZA HATARI ZA KUZUILIWA AU KUTEKWA NYARA WAKTI WA ZIARA

Hatari za kuzuiliwa au kutekwa nyara huwa katika kiwango cha juu wakati wa ziara au safari kwa sababu mtetezi amejiweka wazi, hana watu wengi wa kuwasiliana nao katika mazingira yake, na wale wanaomzunguka wanaweza kuchelewa kukabiliana na tishio au shambulizi. Kwa sababu hii tunataja hatari zinazohusiana na ziara ya nyanjani kwamba zinajumuisha mengi ya matishio/ matokeo yanayohusiana na kazi nzima ya watetezi wa haki za binadamu.

**Kwa mfano:**

Sehemu za kukaguliwa ⇨ kutiwa nguvuni ⇨ kuzuiliwa ⇨...

Hujuma ⇨ utekaji nyara ⇨ ghasia ⇨...

Ukosefu wa habari ⇨ athari kwa shahidi ⇨ athari kwa shirika ⇨...

Usafiri ⇨ wa umma/wa kibinafsi ⇨...

Wakati wa mapumziko uwanjani ⇨ kuweka silaha chini ⇨ matukio ya usalama ⇨...

Mawasiliano ⇨ simu ⇨ ya ana kwa ana ⇨...

Tungependa kuweka mkazo kwenye hatari ya kuzuiliwa/kutekwa nyara wakati wa safari ya nyanjani kisha tutoe mapendekezo kwamba itifaki ya uzuiaji kwenye safari ya nyanjani itahusisha angalau:

- Maandalizi kwa ajili ya safari zote, za nyanjani au katika maeneo ya mijini kama vile ujirani, patakapofaa.
- Usisafiri peke yako.

- Maelezo ya kutosha kuhusu eneo hilo na washika dau watakaotembelewa (kuwafahamu barabara washika dau, uchanganuzi wa vijenzi vya nyanjani tazama sura ya 1.1)
- Watetezi wanapaswa kujua sehemu za kuingilia na kutokea za mahali panapohusika.
- Kila mtu anayehusika katika safari anapaswa kuwa na stakabadhi zifaazo za utambulisho.
- Wasiliana na watu wanaoshughulika na mambo ya kidharura na ambao wako karibu nanyi wakati wote mtakaokuwa nyanjani (kuanzia mwanzo hadi mwisho wa safari).
- Tayarisha safari yenu kulinga na na taratibu zifaazo: jumuisha ajenda kisha uishughulikie hadi itekelezeke, na inafaa kuwa sehemu ya mwongozo wa usalama wa shirika.
- Kuwa na mpango wa mara kwa mara wa kueleza chochote kipya kilichojiri kuhusu hali ya safari yenu (kwa kawaida simu hutumiwa, wakati mwingine kama ilivyokubaliwa hapo nyuma). Ina-maanisha, ikiwezekana, kuangalia iwapo njiani na sehemu ya mwisho ya safari ina mapokezi ya simu. Ikiwa haiwezekani kuangalia au mapokezi ya simu hayapo, mtu aweza kuamua kuwatumia watu waaminifu wanaoishi katika maeneo ya njiani kuthibitisha kwamba kundi hilo limeonekana. Ni muhimu kuamua muda ambao mtu aliyechaguliwa anapaswa kusalia hapo karibu akisubiri kuitwa kwa ajili ya kutoa ripoti baada ya kujaribu kulitafuta kundi bila mafanikio. Kufanya hivyo ni kabla ya kuwa na hofu. Kumbuka kwamba ni rahisi zaidi kutekeleza utekaji nyara mwingine katika kipinidi cha masaa machache kuliko masaa mengi.
- Chunguza usalama wa mbinu ya usafiri mnayoitumia (hili linaweza wakati mwingine kuwa gari la shirika au usafiri wa umma ili muweze kuzungukwa na watu wanaoweza kuwa mashahidi). Katika hali ya usfiri wa umma, kadiria iwapo mtakaa pamoja au kando kando kisha mjifanye kwamba hamjuani. Hili litajenga uwezekano wa angalau mwanachama mmoja wa shirika aweze kulihadharisha shirika. Kuingilia kati kunaweza kuwa na maana ya kupoteza fursa.
- Iwapo ziara zitafanywa kwa kutumia gari la mtu binafsi, basi linapaswa kuwa linafanya kazi barabara kila wakati (zingatia mwendo usio wa kasi, na pia sheria za barabarani). Usiwabebe watembezi wanaoomba lifti.
- Panapofaa, sambaza habari ifaayo kwa raia, jeshi na mamlaka za kijamii, na pia kwa wale walio kwenye safari (ili waweza kuchukua jukumu la kulinda usalama wa safari hiyo na ili pia wasiseme tu kwamba “hawakujui)”.
- Wasilisha hoja ulizoziandaa zinazoeleza malengo na uwezo wa shirika kwa njia itakayokubalika zaidi kwa makundi yaliyojihami na vikosi vya usalama (ni muhimu kutojadiliana na kundi lililojihami na ambalo limekabiliwa, kwa kuwa inaweza kuwa vigumu kulitambua na hapo itakuwa rahisi kufanya kosa kubwa sana).
- Kadiria muda bora zaidi wa kuondoka nyanjani (wakati mwingine, kutokana na hali ya joto kali, itakuwa bora kuondoka alfajiri pasina kujali hali ya usalama). Katika hali ya kutekwa nyara baada tu ya kuondoka nyanjani, hata hivyo, wahudumu wa shirika wanaoshughulikia hali za kidharura wanaweza kuwa hawajaanza kazi; lakini muda mchache tu baada ya kutekwa huwa muhimu katika kujaribu kubainisha alipo mtekwaji nyara.
- Usisafiri usiku.

- Usithubutu wakati wowote kudhihirisha vitu vyako vya thamani (kama vile kamera au video kamera).
- Kuwa na mwenendo unaofaa unapokuwa ziarani.
- Kwa kawaida, litake shirika lipate idhini kutoka kwa jamii unakokwenda kufanya kazi (na panapowezekana jitahidi angalau kuwe na ustahamilivu kutoka kwa makundi yaliyojihami).

**Kwenda nyanjani kwa kupigiwa simu na mtu mwingine, pia:**

- Kuwa na uhakika wa utambulisho wa mtu huyo aliyekupigia simu (thibitisha tena na mashirika mengine maaminifu).
- Thibitisha tena habari kuhusu matukio yaliyotajwa.
- Chunguza iwapo ni muhimu kweli kwenda nyanjani au ikiwa haitakuwa salama kwenu nyote iwapo habari itapelekwa kwenye shirika (tazama ulinzi wa habari: itifaki ya kuizuia na kukabiliana nayo).
- Chunguza iwapo inafaa kwenda huko nyanjani wakati uo huo, baada tu ya kupigiwa simu, hususan iwapo mpigaji simu hajulikani (ni lazima angalau kwanza habari iweze kuthibitishwa tena). Pia, mtu anafaa kuzingatia kwamba safari ya kwenda nyanjani si ya kuzuia matukio kutendeka, kwani yameshatokea tayari,kwa hivyo kwenda nyanjani kutatokana na kupigiwa simu ya pale mwanzoni. Kwa jumla, ushauri bora ni kuepuka ufaraguzi na mabadiliko katika mipango unapokuwa kwenye ziara ya maeneo ya hatari.

**Muhtasari**

Tunaelewa kwamba kumzuilia mtu kunaweza kuwa utaratibu wa kisheria. Hali hii inapochupa mipaka ya kisheria, itaweza kuchukuliwa kama kumnyima mtu uhuru kusikokuwa na sababu. Muda wa kuzuiliwa unaweza kuwa tofauti, kuanzia sasa masaa machache hadi miaka.....

**Uzuiliaji unaweza kukabiliwa kutokana na mitazamo mitatu:**

- Kutokana na mtazamo wa mwenye kuzuiliwa.
- Kutokana na mtazamo wa shirika analofanyia kazi mwenye kuzuiliwa.
- Kutokana na mtazamo wa familia na jamaa za mwenye kuzuiliwa.

**Malengo ya kijumla unapokabiliana na hali ya kuzuiliwa:**

- Punguza uwezekano wa kutokea hali hiyo.
- Kuwa na utambuzi wa haraka wa uwezekano wa kuzuiliwa.
- Orodhesha mikakati au mbinu utakazotumia kukabiliana na uzuiliwaji: makabiliano ya papo hapo na yale muda wa wastani (si papo hapo wala si baadaye zaidi).

Utekaji nyara ni haramu na unaweza kutokea wakati wowote hasa kunapotekea uwezekano wa kutendeka kwa tendo hilo. Utekaji huo nyara ni moja katika matokeo mbalimbali ya “hujuma”. Kwa hivyo, hatua za usalama dhidi ya utekaji nyara zitaenda sambamba na zile za kuzuia hujuma (Sura ya 1.5) Jiepushe na kutoka nje kadiri uwezavyo....

# Ulinzi wa habari Ulio Salama

Mashirika ya kutetea haki za binadamu hulinda habari ambayo,katika mazingira ya uhasama dhidi ya watetezi, inaweza kutumika kuathiri usalama wa shirika, watu wengine na taasisi mbalimbali. Ni muhimu hivyo basi kuwa na utaratibu bora wa kulinda habari na mpango wa kukabiliana na tukio lolote linaloathiri usalama wa habari inayolindwa na shirika.

## Ulinzi bora wa habari: Utaratibu wa kuzuia

Kwa jumla, hata ambayo imo mikononi mwa mashirika ya kutetea haki za binadamu inaweza kuwekwa katika makundi mawili, kulingana na unyeti au usiri wake; usiri wa hali ya juu, na usiri usio mkubwa.

Kiwango chochote cha habari tuliyo nayo hupitia katika hatua nne kabla ya kutufikia na kabla ya kutondokea (panapofaa). Tutaweka wazi usalama unaohitajika katika kila hatua ya kuendelea:

1 • Asili – Ukusanyaji wa habari katika sehemu ya makutano

2 • Uhamishaji wa habari

3 • Kuishughulikia na kuihifadhi

4 • Kusambaza.

### 1 • Asili – Ukusanyaji wa habari katika sehemu ya kukutania.

Tatizo kuu hapa ni ulinzi wa habari na watu walioathiriwa na habari hiyo.

Mtu anayetoa habari huhitaji njia baina ya nyumbani/afisini pake na mahali pa kukutania; mahali pa kukutania (ni mahali ambapo mtoaji habari hukutana na mwanachama wa shirika); mahali hapa pa kukutania paweza pakawa nyumbani au mahali pake pa kazi, afisi za shirika au mahali pengine popote; na kuwepo njia ya kutoka kwenye makao makuu ya shirika (safari ya kwenda na kutoka katika mahali pa kukutania).

Mahali palipo salama na masharti ya kukutana yanahitajika, na pia njia au mbinu ya kusafirisha habari inayoelekea na kutoka kwa asili yake, na pia njia ya kuwasili na kuondoka kwa wanachama wa shirika ambao baadaye ndiyo watahamisha habari.

**Ulinzi wa habari huanza hata kabla ya kuipokea**.

- Je, hata shirika linafaa kupata habari hii? Je, shirika litaweza kutumia habari hiyo kuimarisha kazi yake au kuyafikia maazimio na malengo yake vizuri? Kama sivyo, ni bora kwamba shirika **lisipokee** habari hiyo; iwapo haliwezi kuimudu, linaweza kumtuma mtu huyo kwa shirika jinginelo bila ya kushughulikia na habari au hali ya namna hiyo.
- Mweleze mtoaji wa habari kutuhusu sisi, ni nini malengo ya kazi yetu, jinsi habari hiyo itakavyolindwa na shirika; aina ya habari tunayoihitaji, jinsi tutakvyoishughulikia na kuitumia – na ni yepi wanavyoweza kutarajia kutoka kwetu. Ni jambo la kimsingi na kimaadili kwamba mtoaji habari anafaa kujua mapema (ama moja kwa moja au kupitia kwa mtu mwingine) kuhusu hatari za kuiwasilisha habari, na matumizi ya habari hiyo kwa shirika.

Haitoshi kukisia kwamba mtu anayeishughulikia habari anajua haya yote. Ni muhimu kwetu sisi kumwelezea ili tuwe na uhakika kwamba analijua. Ni muhimu pia kuweka bayana hatua za usalama pamoja nao.

Mahali pa kukutania panafaa pawe salama na pasijulikane na mwengine yeyote. Nyumbani kwa mtoaji habari kunaweza kuwa si salama iwapo kuwasili kwa mfanyikazi wa shirika kutagundulika kwa haraka. Afisi za shirika zinaweza zikawa na usalama zaidi (mradi tu usiri unapewa uzito) au mahali penginepo palipo dhahiri kidogo ambapo watu huingia na kutoka kidesturi (kwa mfano katika jengo la parokia, makao ya kijamii) mradi tu usiri umepewa tena uzito. Iwapo makutano yameandaliwa mahali pasipofaa, yanaweza kusimamishwa hadi yatakapokuwa mahali pa salama zaidi kulingana na unyeti wa habari inayotolewa.

Mtu pia anaweza kuamua kutumia maelezo kuficha ukweli mtu anatoka nyumbani na kisingizio kilicho rasmi. Atahitaji kukikuza kizingizio hicho. Kumwona daktari wa meno (anaonyesha jino linalouma), kumwona daktari (ugonjwa wowote), sokoni n.k. mtu huyo atahitajika kurudi nyumbani na ushahidi wa hakika (maagizo ya daktari na dawa ununuzi wa vitu ambayo hangevipata kwake nyumbani).

Usisahau kwamba matatizo ya usalama yanaweza kutokana na mtu anayetoa habari baada ya kukutana mahali mlipokubaliana.

## 2 ● Uhamishaji wa habari

Habari inaweza kukusanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali: kumbukumbu, kuchapisha, maandishi ya mkono au kwenye kompyuta, picha n.k.

Mbinu ya kidesturi iliyo salama zaidi ya kuhamisha habari ni ya kutumia kompyuta ndogo inayowekwa mapajani, kidude kama kijiti chenye kumbukumbu au santuri yenye kumbukumbu ya kusoma pekee (CD Rom) iliyo na huduma ya ufichaji data ya usalama. Makutano hayo yanaweza kurekodiwa, picha zinaweza kuhifadhiwa na yaliyotendeka kuandikwa. Mbinu nyingine zote zinachukuliwa kama zisizo salama zaidi, hali inayohatarisha harakati nzima ya uhamishaji habari.

Habari ya kibinafsi inafaa kushughulikiwa tu na wanashirika walio na ufahamu wa lile wafanyalo.

Aghalabu watetezi wa haki za binadamu husafiri na vitabu vyao vikiwa na habari muhimu isiyohusiana na lengo la safari yao. Wao husafiri na vitabu vilivyojaa tayari badala ya kuchukua idadi ya karatasi au vifaa watakavyohitaji tu. Hili pia hutokea kwa yale yaliyohifadhiwa kwenye diski za mwako za USB (USB flash disks), kompyuta na vyombo vingene vya kuhifadhi habari.

## 3 ● Kuishughulikia na kuihifadhi habari

Badala ya habari kuzifikia afisi za shirika, huwa ni salama zaidi (kulingana na udhaifu wa afisi – tazama sura inayohusu usalama wa nyumbani na afisi).

Vipimo mahususi vya kufaa kwa habari ni:

Kuhifadhi kwa nyaraka zilizochapishwa: hili linafaa kufanywa tu pale palipo na uwezekano; uthibitisho ufaao wa maandishi kuhusu hali fulani unafaa kuwasilishwa na mtu mwenyewe aliyefanya hivyo. Habari ya kimaandishi kwenye karatasi, inapaswa kuhifadhiwa katika masanduku ya chuma yanayoweza kufungika; kutumia chumba kilicho imara ni aula katika kuhifadhi habari kama hii.

Mtu aweza pia kaumua kusambaza karatasi hizo kwenye maeneno kadhaa yaliyo salama au kuyapeleka katika sehemu nyinginezo zilizo salama kama maeneo, jinsi ilivyobainishwa katika "uhamishaji wa habari". Habari inaweza pia kupigwa mdaki, ikafichwa kisha ikatumwa kwa shirika linaloaminiwa (kwa mfano, shirika jinginelo la kimataifa).

Mbinu za ufichaji data na misimbo zinafaa kutumiwa kwa njia ifaayo.

Fanya uhifadhi wa kila wiki wa nakala za habari zinazoweza kutumiwa kwa hali ya dharura, kisha uzihifadhi hizi nakala zikiwa zimefichwa, mahali pa salama au penginepo.

## 4 ● Usambazaji wa habari

Vigezo vya kijumla vinavyohusiana na usambazaji wa habari vinajumuisha hoja zifuatazo:

- Thibitisha tena habari.
- Wakati ambapo ni shirika tu ndilo linalotoa habari kuhusu masuala fulani, basi kutokuwa na hatari zaidi na hivyo mikakati ya kushughulikia hali hiyo inafaa kuundwa.
- Idhini kutokana na ufahamu wa habari inapopaswa kuchukuliwa kutoka kwa watoaji habari, hasa pale ambapo watu hawa wanatambuliwa na wenyeji kama walio wa pekee katika utoaji habari.

- Habari yoyote ya kimaandishi ya kutoka kwenye shirika au mashirika yanayohusiana na hilo inafaa kuchukuliwa kama ya "watu wote" kutokana na hatari ya kuweza kusomwa na watu wasiofaa au kutokana na mabadiliko ya kila siku ya mbinu za mawasiliano.
- Ni muhimu kwa shirika linalochapisha habari kuwa na sera ya kujitolea ya uchapishaji; na hili linafaa kujumlisha vipimo vikuu vya usalama vinavyotumiwa katika uchapishaji habari (miongoni mwa sheria zinazotumiwa katika kuandika habari yenyewe).

**Kufikia habari kwa watu wasio wanachama wa shirika (wasaidizi waliojitolea, n.k)**

Kwa ajili ya usalama wa shirika, kufungua mahali palipohifadhiwa habari ya aina yoyote kwa watu wengineo, wasaidizi au wenye kujitolea kunapaswa kupigwa marufuku (amua kulingana na hali) na kufungua huko kunapaswa kufanywa na mwanachama mahususi wa shirika.

Inaweza kuwa bora (kujumuisha kwenye mkataba wa kazi au kandarasi za wasaidizi na waliojitolea kifungu cha usiri ambacho hakitakuwa na budi ila kutiwa wakati wote. Kifungu hiki cha usiri kinafaa pia kujumuishwa katika kandarasi za wafanyikazi waliochukuliwa kwa muda na shirika.

## Ulinzi wa data uliosalama: utaratibu wa makabiliano katika hali za wizi au kupotea kwa data.

Wizi au kupotea (inaweza kuwa vigumu kukisia ipi ni ipi) kwa data inayomilikiwa na shirika kunafaa kuchochea hisia zetu kama kwamba habari hiyo itaingia mikononi mwa watu wasiofaa na kwamba habari hiyo itaingia mikononi mwa watu wasiofaa na kwamba itatumiwa vibaya, kwa njia ambayo inaweza kuathiri watu wengineo (kama vile wale wanaoripoti habari au wenzi wao n.k) au shirika lenyewe.

Iwapo, licha ya taratibu zote za uzuiaji, wizi wa kupotea kwa habari kutatokea, basi hali hiyo inafaa kuchukuliwa kama ukiukaji mkubwa wa usalama, na hatua zifuatazo zinapaswa kuchukuliwa:

1 ♦ Wafahamishe kwa haraka watu kwenye shirika.

2 ♦ Tathmini unyeti habari nyingi iliyopotea, kulingana na iwapo: inawahatarisha watu wanaoathiriwa moja kwa moja na habari hiyo, watu wengineo au shirika na kwa sababu gani (au matokeo ya hatari). Tathmini hii inafaa kutekelezwa kwa kila aina ya habari iliyoibiwa, kwa aina mbalimbali za habari zilizoibiwa (kwa mfano orodha ya watu, marejeleo na habari iliyokusanywa kuhusu hali za watu binafsi).

3 ♦ Tathmini upashwaji habari wa baadaye wa watu na taasisi zinazoweza kuwa zimeathiriwa ili hatua zifaazo zipate kuchukuliwa kwa sababu za kujilinda.(hili linapaswa kufanywa kwa uangalifu).

4 ♦ Tathmini upashwaji habari wa viongozi wenye mamlaka na pia kuripoti matukio.

5 ♦ Ikibidi tumia hatua nyinginezo zinazofaa ili kuepuka hasara iwapo habari iliyopotea au kuibiwa itatumiwa.

Shirika pia litahitaji kuamua kiasi ambacho wanachama wake wataweza kujiweka hatarini ili kulinda habari: kwa mfano, katika hali ya upekuzi wenye fujo, mtu anapaswa kukadiria iwapo upinzani dhidi ya upekuzi huo "utafaa."

## Muhtasari

**Ulinzi ulio salama wa habari huhitaji itifaki za uzuiaji na makabiliano**.

Uzuaji unafaa kuzingatia awamu nne:

1 • Asili – Ukusanyaji wa habari, mahali pa kukutania.

2 • Uhamishaji wa habari.

3 • Kuishughulikia na kuihifadhi.

4 • Usambazaji.

Makabiliano yanafaa kujumuisha angalau:

1 • Kuwafahamisha watu wanaofaa katika shirika.

2 • Kutathmini wingi wa usiri wa habari iliyoibiwa au iliyopotea.

3 • Kutathmini upashwaji habari wa baadaye wa watu taasisi zinazoweza kuwa zimeathiriwa.

4 • Kutathmini upashwaji habari wa viongozi wenye mamlaka na pia kuripoti matukio.

5 • Hatua zinazohitajika ili kuepuka hasara iwapo habari iliyoibiwa au kupotea inatumika.

# Usalama na wakati wa mapumziko

## Tafakari ya nyuma

Kwa ujumla, sheria za usalama hufuatwa maadamu tu hazitapingana na masilahi ya kibinafsi ya mtu. Kwa hivyo itakuwa rahisi kushughulikia usalama wa afisini, kuliko wakati wa mapumziko kwa mfano. Japo kuwa na wakati wa mapumziko ni jambo la msingi kwa usalama. Inahitajika mjadala na uelewa wa namna mnahitaji ya kibinafsi yanaweza yakaingilia usalama.

## Wakati wa mapumziko

Hapa kuna maswali machache na tafakari zitakazosaidia shirika kutunga sera yake ya wakati wa mapumziko. Ni muhimu, kama kilivyo kipengele kingine cha usalama, kuyachunguza (maswali na tafakari hizo) kadiri iwezekanavyo hata kama uchunguzi huu utakiuka usiri wa mtu (matukio ya usalama yanaweza pia kukiuka usiri).

Tunaanza kwa tafakari mbili muhimu:

- Iwapo watu wangependa kuhujumu shirika, inawezekana kwamba hawatahujumu watu waliolindwa/waliojilinda barabara au wale waotii sheria za usalama, bali watawalenga wale walio na udhaifu fulani, hususan katika wakati wao wa mapumziko (usiku na wikendi n.k)
- Iwapo shirika lina wanachama kumi, kutoka kwa hao, wawili hawatii sheria za usalama wakati hawana shughuli, basi ni shirika zima, ambalo litakuwa hatarini na wala si hao wawili pekee, kwa sababu shirika lote litapata athari ya shambulizi dhidi ya hao wawili.

Swali la kimsingi daima huwa: "je kuna hatari ya usalama inayohusiana na….." Iwapo jibu ni "la", basi ni sawa. Lakini kama ni "ndiyo", litapaswa kuchunguzwa na kuamuliwa iwapo kuna njia za kuikidhi haja ya kibinafsi katika mazingira yaliyolindwa au kuamua iwapo haja inahitaji kuahirishwa hadi nyakati nyingine zilizo salama au kupuuzwa tu kama isiyoenda sambamba na usalama wa mtetezi wa haki za binadamu.

## Je, tunajali kuhusu usalama wakati wa kazi pekee au nyakati zote?

Ingawa ni vigumu kubainisha tofauti baina ya sera za shirika na uhuru wa kila mwanachama katika wakati wao wa mapumziko, uzuiaji wa mashumbulizi na makabiliano dhidi yao hakuleti tofauti kati ya mashambulizi wakati wa kufanya kazi na yale yatakayotekelezwa wakiwa katika mapumziko…. Hatupaswi kusahau kwamba mtu akiamua kuhujumu shirika kwa kutumia wanachama wa shirika hilo, hatafanya hivyo wakati wa kazi, lakini wakati ambao wanachama hao watakuwa hawana cha kufanya kabisa. Mtu anayepanga kutekeleza shambulizi dhidi ya mtetezi atatafuta fursa nzuri ya kufanya hivyo. Tunapaswa pia kukumbuka kwamba itakuwa rahisi sana kulificha shambulizi la usiku, au wakati unapoondoka kutoka kwa jumba la starehe, n.k.

## Katika nchi ambazo unywaji pombe ni desturi ya kijamii, je unywaji huo, hadi kufikia kiwango cha kulewa, ni hatari ya usalama?

Kulewa katika maeneo ya hadharani kuna athari ya moja kwa moja kwenye usalama. Mtetezi anaweza kuzungumza, tabia yake ikabadilika kisha asipate kujua kwamba kuna juhudi ya kimakusudi ya kumuuliza maswali au ya kumpa changamoto fulani.

Iwapo athari siyo ya moja kwa moja kwenye usalama wa nje wa watetezi wa haki za binadamu, basi itakuwa kwa hadhi ya shirika. Kisha kumbuka kwamba mtetezi wa haki aliyelewa hujenga fursa ya kundi lolote lenye uhasama kujaribu kufikiri kuhusu kushambulia shirika la watetezi (hii pia hutendeka kwa harakati za matumizi ya dawa za kulevya). Matumizi ya pombe na dawa nyinginezo kwa kurejelea suala la usalama, yasichunguzwe kwa mujibu wa mtazamo wa kimaadili au kiafya, bali kama suala la ukweli linaloathiri usalama.

## Je, Mahusiano ya kisiri na ya kimapenzi yanaweza kuathiri usalama?

- Kumetokea hali ambazo watetezi wa haki za binadamu wameshindwa kurejea kwenye mashirika yao kwa sababu walikuwa na mahusiano ya kimpenzi. Shirika tayari lilikuwa limeshafahamisha wafanyikazi wanaoshughulikia hali za kidharura ya kuwa wabainishe tu kwamba watetezi hawakuwa natatizo lolote, bila kujua tatizo linalowakabili. Hali kama hii bila shaka inawapa watu wengine nafasi ya kulidharau shirika na mtetezi anayehusika, kwa kurejelea matokeo yao ya sifa na ya kimaadili. Baadhi ya wao wenye kushughulikia hali za kidharura wanaweza hata kuamua kujiondoa kwenye shirika kufuatia mfumo wa kutoa onyo la mapema na shirika hilo.

- Tatizo sio uhusiano wa kimapenzi, lakini namna uhusiano huo utakavyoweza kuathiri mawasiliano na usalama. Tunasisitiza kwamba, hilo sio suala la kimaadili au la kiafya lakini ni la usalama. Ni muhimu kwamba shirika linaweza kukabiliana na masuala haya kwa namna ya wazi na kwamba litafute mikakati ya kuyashughulikia yote.

- Je, ni nini kitatokea ikiwa rafiki wa mtetezi anaonekana kama mwenye kutuhumiwa na wengine kwenye shirika? Je, shirika linaweza kuingilia kati?

- Ni kwa jinsi gani habari inaweza kupitishwa hadi marafiki, familia na jamaa? Je, mtetezi wa haki za binadamu ana wajibu wa kujua namna habari hiyo itakavyoweza kutumika?

Hivyo basi, namna watetezi wanavyotumia wakati wao wa mapumziko inaweza kuleta athari kwa usalama. Hoja siyo kukataa ukweli kwamba kuna haja ya kufurahia wakati wa mapumziko bali zingatia jinsi ya kuufurahia wakati huo.

**Mashirika yote ya watetezi wa waki za binadamu yaliyo hatarini yanahitaji sera ya kuufurahia wakati wa mapumziko, kuanzia masaa ya jioni hadi kwenye likizo. Haja maalum inahitajika katika kudhibiti matumizi ya pombe na dawa nyinginezo kwa umma. Ni kwa namna gani mahusiano ya siri yatazuia kuwepo kwa usalama na ni kwa jinsi gani wakati wa mapumziko unaweza kuathiri hadhi na usalama wa shirika?**

## Tutachukulia vipi usiri wa habari?

Na kwa kuwa habari inaweza kufichuka wakati wowote hata wakati wa mapumziko, hapa kuna mazingatio ya ziada kuhusiana na usalama wa habari.

Shirika linafaa kubuni viwango viwili vya usiri wa habari (kila mara kwenye shirika lenyewe):

a ♦ Yale ambayo wanachama wanapaswa kujua.

b ♦ Yale ambayo wanachama wote wanaweza kujua.

Harakati hii inaweza kupunguza hatari ya kufichuka kwa habari iliyo ya siri, ikiwa ni kutokana na tabia ya kupuuza na/au kupenya kwa habari tu. Pia, inaweza kulisaidia shirika kutambua mahali panapofichukia habari.

## Je, kuna uwezekano kwamba baadhi ya vipengele vya tabia vinaweza kuathiri hadhi ya shirika, wakati tukiwa mapumzikoni?

- Watu wengine wanatuchukulia vipi?
- Ni kwa kiwango gani wafanyikazi wenza wanajua yale tuyafanyayo wakati wa mapumziko?
- Je, hadhi ya shirika ina athari gani kwa usalama?

**Muhtasari**

Watetezi walio hatarini hawana budi kulinda usalama wao masaa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki katika harakati zote za maisha yao, ukiwemo wakati wa mapumziko.

Wakati wa mapumziko huhitaji mazingatiio yanayofaa.

Swali la kimisingi ni: "Je, kuna hatari ya usalama iliyoambatishwa kwenye…." Iwapo jibu ni "la," basi ni sawa. Lakini kama ni "ndiyo", suala hilo linahitaji kuchunguzwa na maamuzi kufanywa kuhusu iwapo kuna njia za kukidhi haja ya kibinafsi ya mtu katika mazingira yaliyolindwa au kama haja hiyo haina budi kuahirishwa hadi nyakati nyinginezo zilizo salama au kupuuzwa tu kama isiyoenda sambamba na masilahi ya mtetezi wa haki za binadamu.

Mashirika yote ya watetezi yaliyo hatarini yanahitaji sera ya kufurahia wakati wa mapumziko, kuanzia masaa ya jioni hadi wakati wa likizo. Pana haja maalum ya kushughulikia matumizi ya pombe na dawa nyinginezo kwa umma, namna mahusiano ya siri yanavyoweza kuzuia kuwepo kwa usalama na namna hadhi ya shirika kuhusu wakati wa mapumziko inaweza kuathiri usalama.

Kwa kuwa wakati wa mapumziko unaweza kuhusisha hatari, ni muhimu kutosahau kufanya tathmini pana ya hatari.

# KIAMBATANISHO CHA KWANZA

## Tamko La Umoja Wa Mataifa Kuhusu Watetezi Wa Haki Za Binadamu

UMOJA WA
MATAIFA

A

## Baraza Kuu

District.
GENERAL
A/RES/53/144
Machi 8, 1999

Awamu ya 53
Kipengele cha 110(b) cha ajenda

### MAAMUZI YA BARAZA KUU

*(Kuhusu ripoti ya Kamati ya Tatu (A/53/625/Add.2)*

**53/144 Tamko kuhusu Haki na Wajibu wa Watu binafsi, Makundi na Mashirika ya Kijamii katika kuendeleza na kulinda Haki zinazotambuliwa ulimwenguni za Binadamu na Uhuru wa Kimsingi.**

***Baraza Kuu***

*Kwa kusisitiza tena* umuhimu wa kuzingatia makusudio na kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa ili kuendeleza na kulinda haki zote za binadamu na uhuru wa kimsingi kwa watu wote katika nchi zote za ulimwenguni,

*Kuzingatia maamuzi ya 1998/7* yaliyofanywa April 3, 1998[1] ya Tume kuhusu Haki za Binadamu, ambapo tume iliidhinisha matini ya maazimio ya mswada kuhusu haki na wajibu wa watu binafsi, makundi na mashirika ya kijamii ili kustawisha na kulinda haki za binadamu zinazotambuliwa kote ulimwenguni na uhuru wa kimsingi,

*Kuzingatia pia* maamuzi ya Baraza la Kijamii na kiuchumi, 1998/33 yaliyofanywa Julai 30, 1998, ambapo Baraza hilo lilipendekeza tamko la muswada liidhinishwe na Baraza kuu,

*Kuwa makini* kuhusu umuhimu wa kuidhinisha tamko la muswada katika kuadhimisha mwaka wa kumi na tano baada ya kuzinduliwa kwa Maazimio ya Kilimwengu ya Haki za Binadamu[2],

1. *Huidhinisha* Tamko lililoambatishwa kwenye maamuzi ya sasa kuhusu Haki na Wajibu wa watu Binafsi, Makundi na Mashirika ya Kijamii katika Kuendeleza na kulinda Haki za Binadamu zinazotambuliwa katika Ulimwengu mzima na pia Uhuru wa Kimsingi,

2. *Hualika* Serikali, mawakala, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, mashirika ya kitaifa na yasiyo ya kitaifa ili kuweka pamoja juhudi zao za kueneza Tamko hilo na kuendeleza heshima na maelewano katika kila eneo na humwomba Katibu Mkuu kujumuisha matini ya Tamko hilo katika toleo linalofuata la Haki za Binadamu: Utunzi wa Hati rasmi za Kimataifa.

Mkutano wa 85 wa wajumbe wote
Disemba 9, 1998

1 Tazama Rekodi Rasmi za Baraza la Kijamii na Kiuchumi, 1998, nambari ya nyongeza 3 (E/1998/23), Sura ya II, Sehemu ya A.

2 Maazimio ya 217A (III)

**Tamko la kuhusu Haki na Wajibu wa Kila Mtu, Vikundi na Vyombo vya Jamii Kuendeleza na Kulinda Haki za Binadamu Zinazotambuliwa Kimataifa pamoja na Uhuru wa Msingi**

***Baraza Kuu***

*Kwa kusisitiza tena* umuhimu wa ushikaji wa madhumuni na kanuni za mkataba wa Umoja wa Mataifa kwa ajili ya uendelezaji na kulinda haki za binadamu na uhuru wa masingi kwa watu wote katika nchi zote duniani.

*Kwa kusisitiza tena* umuhimu wa Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu na Makubaliano ya Kimataifa,[3] kuhusu Haki za Binadamu kama vipengele vya msingi vya juhudi za kimataifa kuendeleza heshima ya kimataifa kwa ajili na ushikaji wa haki za binadamu, na uhuru wa msingi, na umuhimu wa hati nyingine wa haki za binadamu, zilizopitishwa ndani ya mfumo wa Umoja wa Mataifa pamoja na zile za ngazi ya kanda.

*Kwa kutilia mkazo* kuwa wanachama wote wa jumuiya ya kimataifa watatimiza kwa pamoja au mmoja mmoja wajibu wao muhimu wa kuendeleza na kuhimiza heshima kwa haki za binadamu na uhuru wa msingi kwa wote bila ya tofauti yoyote zikiwemo tofauti za jamii, rangi, jinsia, lugha, dini, siasa au maoni mengine, utaifa au asili ya kijamii, mali, mahala pa kuzaliwa au hadhi nyingine na kusisitiza tena umuhimu mkubwa wa kupata ushirikiano wa kimataifa katika kutimiza wajibu huu kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

*Kwa kukubali* wajibu muhimu wa ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya kazi muhimu ya mtu mmoja mmoja vikundi au vyama katika kuchangia utokomezaji unaofaa wa ukiukaji wote wa haki za binadamu na uhuru wa msingi wa watu wote na mtu mmoja mmoja ukiwemo ule unaohusiana na ukiukaji wa halaiki, dhahiri au wa mara kwa mara kama vile unaotokana na siasa za kibaguzi, aina zote za ubaguzi wa kijamii, ukoloni, utawala au kukaliwa na wageni, uvamizi au vitisho kwa uhuru wa kitaifa, umoja wa kitaifa au Umoja wa nchi na kukataliwa kutambua haki za watu kujiamulia na haki ya kila mtu kuwa na uhuru kwa mali yake na mali asili.

*Kwa kutambua* uhusiano kati ya amani na utulivu wa kimataifa na kufurahia haki za binadamu na uhuru wa msingi na kuelewa kwamba kukosekana kwa amani na utulivu wa kimataifa si sababu ya kutofuata haki za binadamu.

*Kwa kurudia* kwamba haki za binadamu na uhuru wa msingi vyote ni vya kimataifa havigawanyiki, vinategemeana na vinahusiana na lazima viendelezwe na kutekelezwa kwa hali ya usawa na haki, bila ya kuathiri utekelezaji wa kila moja ya haki na uhuru huo.

*Kwa kutia mkazo* kwamba jukumu kubwa na wajibu wa kuendeleza na kulinda haki za binadamau na uhuru wa msingi lipo kwa nchi.

*Kwa kutambua* haki na jukumu la kila mmoja, vikundi na vyama la kuendeleza heshima na kukuza maarifa kuhusu haki za binadamu na uhuru wa msingi katika ngazi ya taifa na kimataifa,

***Linatamka:***

*Ibara ya 1*

Kila mtu ana haki binafsi na kwa kushirikiana na wengine kuendeleza na kujitahidi kulinda na kutambua haki za binadamu na uhuru wa msingi katika ngazi ya taifa na kimataifa.

3 Maazimio ya 2200 A (XXI)

*Ibara ya 2*

1. Kila nchi ina jukumu kubwa na wajibu wa kulinda, kuendeleza na kutekeleza haki za binadamu na uhuru wa msingi vyote, miongoni mwa mambo mengine, kuchukua hatua zitakazoonekana kuwa ni muhimu kuweka mazingira yote muhimu katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na nyanja nyingine, pamoja na uthibitisho wa kisheria unaotakiwa kuhakikisha kuwa watu wote walio chini ya mamlaka ya sheria zake, binafsi na kwa kushirikiana na wengine wataweza kufurahia haki zote na uhuru zinavyotumika.

2. Kila Nchi itachukua hatua za kisheria kiutawala na hatua nyingine itakazoona ni muhimu kuhakikisha kuwa haki na uhuru uliotajwa katika Tamko lililopo unahakikishwa ipasavyo.

*Ibara ya 3*

Sheria za nchi kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa na wajibu mwingine wa kimataifa wa Nchi katika uwanja wa haki za binadamu na uhuru wa msingi ni mfumo wa kisheria ambamo haki za binadamu na uhuru wa msingi lazima vitekelezwe na kufurahiwa na ambamo shughuli zote zilizotajwa katika Tamko lililopo kwa ajili ya uendelezaji, kulinda na kutambua ipasavyo haki na uhuru vyote lazima vitekelezwe.

*Ibara ya 4*

Hakuna jambo lolote katika Tamko lililopo litakalofasiriwa kuwa linaharibu au kupingana na madhumuni na kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa au kuwekea mipaka au kuhitilafiana na masharti ya Tamko la kimataifa la Haki za Binadamu 2,makubaliano ya kimataifa kuhusu haki za binadamu na hati nyingine za kimataifa na ahadi zinazotumika katika uwanja huu.

*Ibara ya 5*

Kwa madhumuni ya kuendeleza na kulinda haki za binadamu na uhuru wa msingi, kila mtu ana haki, binafsi na kwa kushirikiana na wengine katika ngazi ya taifa na kimataifa ya:

a) Kukutana na kujumuika kwa amani

b) Kuunda, kujiunga na kushiriki katika asasi zisizo za kiserikali, vyama au vikundi.

c) Kuwasiliana na asasi zisizo za kiserikali na baina ya serikali.

*Ibara ya 6*

Kila mtu ana haki binafsi na kwa kushirikiana na wengine:

a) Kujua, kutafuta, kupata na kupokea na kuwa na taarifa kuhusu haki zote za binadamu na uhuru wa msingi, ikiwemo kupata taarifa za namna haki hizo na uhuru wa msingi zinavyotekelezwa katika mifumo ya sheria, mahakama au utawala

b) Kama ilivyoruhusiwa katika hati za haki za binadamu na hati nyingine za kimataifa zinazotumika kuchapisha bila ya kubugudhiwa, kueneza au kuwapa wengine maoni, taarifa na maarifa haki zote za binadamu na uhuru wa msingi.

c) Kuchunguza kujadili, kuunda na kuwa na maoni kuhusu ufuataji, kisheria na kwa vitendo wa haki zote za binadamu na uhuru wa kimsingi na kupitia njia hizi na njia nyingine zinazofaa, kuwaarifu wananchi kuhusu masuala hayo.

*Ibara ya 7*

Kila mtu ana haki binafsi na kwa kushirikiana na wengine, kubuni na kujadili mawazo mapya ya haki za binadamu na kanuni na kutetea kukubalika kwao.

*Ibara ya 8*

1 Kila mtu ana haki binafsi na kwa kushirikiana na wengine, kupata kwa ukamilifu, bila ya ubaguzi wowote, kushiriki katika serikali yake na katika kuendesha mambo ya umma.

2 Hii ni pamoja na miongoni mwa mambo mengine, haki binafsi na kwa kushirikiana na wengine kuwasilisha katika vyombo vya serikali na idara na mashirika yanayohusika na ukosoaji wa mambo ya umma na mapendekezo kwa kuboresha utendaji wake na kuzingatia kipengele chochote cha kazi yao kinachoweza kuzuia au kukwaza uendelezaji, kulinda na ufanikishaji wa haki za binadamu na uhuru wa msingi.

*Ibara ya* 9

1 Katika kutekeleza haki za binadamu na uhuru wa msingi, ikiwemo uendelezaji na kulinda haki za binadamu zilizotajwa katika tamko lililopo, kila mtu ana haki binafsi kwa kushirikiana na wengine kunufaika na tiba inayofaa na kulindwa utokeapo ukiukaji wa haki hizo.

2 Kwa hali hiyo, kila mtu ambaye haki au uhuru wake unasemekana kukiukwa ama haki ama binafsi au kupitia uwakilishi uliyoidhinishwa kisheria, kulalamika na malalamiko kupitiwa haraka na kusikilizwa mbele ya mahakama ya kisheria yaliyo huru yanafuata haki ya kitaalamu au mamlaka nyingine iliyoundwa kisheria na kupata kutoka kwenye mamlaka hiyo uamuzi huwa kwa mujibu wa sheria kutoa suluhisho ikiwemo fidia yoyote inayostahili, pale ambapo kumetokea ukiukaji wowote wa haki au uhuru wa mtu huyo pamoja na uhimizaji wa utekelezaji wa wa uamuzi wa kisheria na zawadi, vyote vitekelezwe bila ya ucheleweshaji wowote.

3 Hali kadhalika kila mtu ana haki binafsi na kwa kushirikiana na wengine, miongoni mwa hayo:

(a) Kukamilika kuhusu sera na hatua za maofisa wanaohusika na vyombo vya kiserikali kuhusu ukiukaji wa haki za binadamu na uhuru wa kimsingi kwa njia ya malalamiko au njia zinazofaa, kwa Mamlaka za Mahakama,Utawala au Utungaji Sheria za Kitaalamu nchini au Mamlaka nyingine za Kitaalamu zilizohusishwa na Mfumo wa Sheria wa nchi, zinazotakiwa kutoa uamuzi wao kuhusu malalamiko bila ya kuchelewa.

(b) Kuhudhuria usikilizaji wa mashauri, mashtaka na hukumu ili kuunda wazo kuhusu ufuataji wao wa sheria ya nchi na wajibu wa kimataifa unaotumika na ahadi.

(c) Kuahidi na kutoa msaada wa kisheria wa kitaalamu au ushauri mwingine wowote unaofaa na msaada katika kutetea haki za binadamu na uhuru wa msingi.

4 Vilevile na kwa mujibu wa hati za kimataifa zinazotumika na taratibu,kila mtu ana haki binafsi au kwa kushirikiana na wengine kupata bila kikwazo mawasiliano na vyombo vya kimataifa vyenye ujuzi maalumu au wa jumla wa kupokea na kuzingatia mawasiliano kuhusu masuala ya haki za binadamu na uhuru wa msingi.

5 Nchi itafanya uchunguzi wa haraka na wa haki au kuhakikisha kuwa tume ya uchuguzi inaundwa inapotokea sababu ya kutosha kuamini kuwa kumetokea ukiukaji wa haki za binadamu na uhuru wa msingi katika sehemu yoyote chini ya mamlaka yake.

*Ibara ya 10*

Hakuna atakayeshiriki kwa vitendo au kushindwa kutenda pale inapotakiwa, katika kukiuka haki za binadamu na uhuru wa msingi na hakuna atakayeadhibiwa au kuchukuliwa hatua kali ya namna yoyote kwa kukataa kufanya hivyo.

*Ibara ya 11*

Kila mtu ana haki binafsi na kwa kushirikiana na wengine, kutekeleza kisheria kazi au taaluma yake. Kila mtu ambaye kutokana na taaluma yake anaweza kuathiri hadhi ya binadamu,haki za binadamu na uhuru wa msingi wa watu wengine,ataheshimu haki za uhuru huo na kutii viwango vya kitaifa na kimataifa vinavyofaa vya maadili ya kazi na ya kitaaluma.

*Ibara ya 12*

1 Kila mtu haki, binafsi na kwa kushirikiana na wengine kushiriki katika shughuli za amani dhidi ya ukiukaji wa Haki za Binadamu na uhuru wa msingi.

2 Nchi itachukua hatua zozote muhimu kuhakikisha kulindwa na mamlaka zenye uwezo na utaalamu, kila mtu binafsi na kwa kushirikiana na wengine, dhidi ya vurugu,vitisho, kulipiza kisasi, kisheria au ubaguzi mbaya, shinikizo au hatua zozote za holela kama matokeo ya utekelezaji halali wa haki zilizotajwa katika tamko lilipo.

3 Kuhusiana na hayo, kila mtu ana haki binafsi na kwa kushirikiana na wengine, kulindwa kwa ukamilifu kwa mujibu wa sheria za taifa katika kukabiliana dhidi ya au kupinga, kwa njia ya amani, shughuli na vitendo, vikiwemo vya kuacha, vinavyohusu Nchi vinavyosababisha ukiukaji wa haki za binadamu na uhuru wa msingi, pamoja na vitendo vya vurugu vinavyofanywa na vikundi au watu binafsi vinavyoathiri kufurahia haki za binadamu na uhuru wa msingi.

*Ibara ya 13*

Kila mtu ana haki binafsi au kwa kushirikiana na wengine ya kutafuta, kupokea na kutumia rasilimali kwa lengo la kuendeleza na kulinda haki za binadamu na uhuru wa msingi kwa njia ya amani, kwa mujibu wa ibara ya 3 ya tamko lililopo.

*Ibara ya 14*

1 Nchi ina wajibu wa kuchukua hatua za kisheria, kimahakama, kiutawala au hatua nyingine zinazofaa kuendeleza kueleweka na watu wote chini ya mamlaka yao ya kisheria ya haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

2 Miongoni mwa hatua hizo ni:

(a) Uchapishaji na upatikanaji kwa wingi wa sheria za Kitaifa na Kanuni za hati za Msingi za Haki za Binadamu za Kimataifa zinazotumika

(b) Ufikiaji kamili na ulio sawa kwa nyaraka za kimataifa katika uwanja wa haki za binadamu, zikiwemo Taarifa za Vipindi vya Nchi kwa Vyombo Vilivyoanzishwa na mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu ambayo nchi ni mwanachama, pamoja na muhtasari wa kumbukumbu ya majadiliano na taarifa rasmi za vyombo hivi.

3 Nchi itahakikisha na kusaidia pale inapofaa, kuundwa na kuendelezwa kwa uhuru zaidi wa Asasi za Kitaifa kwa ajili ya Uendelezaji na Kulinda Haki za Binadamu na uhuru wa msingi katika maeneo yote yaliyo chini ya mamlaka yake kisheria, ziwe za kutetea malalamiko au tume za haki za binadamu au aina yoyote ya asasi ya kitaifa.

*Ibara ya 15*

Nchi ina wajibu wa kuendeleza na kuwezesha ufundishaji wa Haki za Binadamu na Uhuru wa Msingi katika ngazi zote za elimu na kuhakikisha kuwa wajibu wote wa kuwafunza wanasheria, maofisa wa uhimizaji, utekelezaji wa sheria, wanajeshi na viongozi wa umma unajumuisha vipengele vya ufundishaji wa haki za binadamu katika programu zao za mafunzo.

*Ibara ya 16*

Watu binafsi, asasi zisizo za kiserikali na asasi zinazohusika zina wajibu muhimu wa kutekeleza katika kuchangia kuufanya umma uelewe zaidi masuala yanayohusiana na Haki za Elimu zote na uhuru wa msingi kupitia shughuli kama vile elimu, mafunzo na utafiti katika maeneo haya katika kuimarisha zaidi miongoni mwa mambo mengine, uelewa, uvumilivu, amani na uhusiano wa kirafiki miongoni mwa mataifa na miongoni mwa vikundi vya dini na vinavyopinga ubaguzi wa rangi, kwa kuzingatia historia tofauti za jamii na jumuiya wanamofanya shughuli zao.

*Ibara ya 17*

Katika kutekeleza haki na uhuru ulioelezwa katika tamko lililopo, kila mtu binafsi na kwa kushirikiana na wengine, atalazimika tu kufuata ukomo huo ili mradi ni kwa mujibu wa wajibu wa kimataifa unaotumika na kutambuliwa kisheria kwa madhumuni ya kupata utambuzi wa heshima vinavyotakiwa kwa haki na uhuru wa wengine na kukidhi masharti halali ya uadilifu, utaratibu wa umma na ustawi wa jumla katika jamii ya kidemokrasia.

*Ibara ya 18*

1 Kila mtu ana wajibu kwake binafsi na kwa jamii, ambapo itawezekana kwa uhuru kuendeleza haiba yake.

2 Watu binafsi, vikundi, asasi na asasi zisizo za kiserikali zina wajibu muhimu wa kutekeleza na jukumu la kulinda demokrasia, kuendeleza, haki za binadamu na uhuru wa msingi na kuchangia katika kuendeleza na kukuza jamii/vyama vya kidemokrasia, asasi na michakato.

3 Watu binafsi, vikundi na asasi zisizo za kiserikali nao pia wana wajibu muhimu na jukumu la kuchangia kadri inavyofaa, uendelezaji wa haki za kila mtu katika taratibu za kijamii na kimataifa ambapo haki na uhuru vimebainishwa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu na Hati nyingine za Haki za Binadamu zinaweza kufanikisha kwa ukamilifu.

*Ibara ya 19*

Hakuna kifungu chochote kwenye Tamko Lililopo kitakachotafsiriwa kumhusisha mtu yoyote, kikundi, chombo cha jamii au Nchi yoyote katika ushiriki wa shughuli yoyote au kutekeleza kitendo chochote chenye nia ya kuharibu haki na uhuru uliotajwa katika tamko lililopo.

*Ibara ya 20*

Hakuna kifungu chochote kwenye tamko lililopo kitakachotafsiriwa kuruhusu Nchi kuunga mkono na kuendeleza shughuli za watu binafsi, vikundi na asasi zisizo za kiserikali kinyume na masharti ya mkataba wa Umoja wa Mataifa.

# KIAMBATANISHO CHA PILI

**BARAZA LA UMOJA WA ULAYA**

**Brussels, Juni 9, 2004**
**10056/1/04**
**REV 1**
**LIMITE**
**PESC 435**
**COHOM 17**

**UKUMBUSHO**

Kutoka kwa: Kamati ya kisiasa na Usalama

Hadi kwa: Coreper/Baraza

Mada: **Mahitimisho ya Mswada wa Baraza kuhusu Miongozo ya Umoja wa Ulaya inayowahusu Watetezi wa Haki za Binadamu**

1. Katika mkutano wake wa tarehe 8 Juni, Kamati ya Siasa na Usalama ilijadili na kutoa Mahitimisho ya Mswada wa Baraza yaliyotajwa hapo juu, na ambayo yametolewa tena katika Kiambatisho.
2. Katika Mkutano wake wa Juni 1, Kamati ya Siasa na Usalama ilikuwa imeidhinisha maandishi "Uhakikisho wa Ulinzi – Miongozo ya Umoja wa Ulaya kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu" yaliyotayarisha kwa ushauriano wa Chama cha Baraza la Haki za Binadamu, ambapo sasa haya maandishi yameambatishwa kwenye Mahitimisho ya Mswada wa Baraza.
3. Coreper imealikwa kutoa mapendekezo kwa Baraza liweze kuidhinisha mahitimisho haya na miongozo iliyoambatishwa iwe kama kipengele cha kwanza, katika mkutano wake wa tarehe 14/15 Juni.

**KIAMBATISHO**

## Mahitimisho ya Mswada wa Baraza

1. Baraza linakaribisha na kuidhinisha Miongozo ya Umoja wa Ulaya kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu (nakala imeambatishwa). Miongozo hiyo itakuwa ni sehemu muhimu ya mchakato wa kutia nguvu sera za haki za binadamu za Umoja wa Ulaya katika mahusiano na nchi nyingine. Baraza linafahamu kwamba miongozo itaimarisha shughuli za Umoja wa Ulaya za kulinda na kutoa msaada kwa watetezi wa haki za binadamu.
2. Baraza linafahamu kwamba kuwasaidia watetezi wa haki za binadamu, tayari ni suala lililokita mizizi la sera ya mahusiano ya nje ya haki za Binadamu ya Umoja wa Ulaya. Nia ya Miongozo ya Watetezi wa Haki za Binadamu ni kutoa mapendekezo yafaayo ya kuimarisha hatua ya Umoja wa Ulaya kuhusiana na suala hili. Miongozo hiyo inaweza kutumiwa kujenga uhusiano na nchi zinazoendelea kwenye viwango vyote, pamoja na kwenye makongamano ya watu wengi ya haki za binadamu, ili kusaidia na kuimarisha juhudi za Muungano zinazoendelea za kustawisha na kujenga heshima kwa haki za Binadamu. Miongozo hiyo pia hujenga nafasi ya kuingilia kati kwa Muungano kwa ajili ya watetezi wa haki za Binadamu walio hatarini na pia hupendekeza mbinu halisi za kutoa msaada kwa watetezi wa haki za binadamu.
3. Baraza lilifahamu kwamba Miongozo inashughulikia masuala mahususi ya watetezi wa Haki za Binadamu ambayo yatachangia kwa jumla katika kuimarisha sera ya Umoja wa Ulaya.

**KUHAKIKISHA ULINZI**

**MIONGOZO YA UMOJA WA ULAYA KUHUSU WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU**

## I. MADHUMUNI

1. Kuunga mkono watetezi wa haki za binadamu ni kipengele cha muda mrefu kilichomo katika sera ya uhusiano na nchi za nje ya Umoja wa Ulaya kuhusu binadamu. Madhumuni ya miongozo hii ni kutoa mapendekezo ya vitendo kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa Umoja wa Ulaya katika suala hili. Miongozo hii inaweza kutumiwa katika mawasiliano na nchi zinazoendelea, katika ngazi zote pamoja na nyanja na haki za binadamu, zinazohusisha pande mbalimbal,ili kuunga mkono na kuimarisha juhudi zilizopo za Umoja wa Ulaya, kuendeleza na kuhimiza heshima ya haki ya kutetea haki za binadamu. Miongozo hii pia inaruhusu Umoja wa Ulaya kuwatetea watetezi wa haki za binadamu walio katika hatari na kupendekeza hatua za vitendo za kuwaunga mkono na kuwasaidia watetezi wa haki za binadamu. Kipengele muhimu cha miongozo hii ni kuunga mkono taratibu maalum za Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, ikiwemo Makubaliano Maalum ya Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu na taratibu za kikanda zinazofaa kuwalinda watetezi wa haki za bianadamu. Miongozo hii itasaidia Tume za Umoja wa Ulaya (Ofisi za Ubalozi na Ofisi Ndogo za Ubalozi za Nchi Wanachama wa Umoja wa Ulaya na Ujumbe wa Tume ya Nchi za Ulaya) katika mkabala wao kwa watetezi wa haki za binadamu. Wakati madhumuni ya msingi ya miongozo hii ni kushughulikia masuala mahsusi kuhusu watetezi wa haki za binadamu, inachangia pia katika kuimarisha sera ya haki za binadamu ya Umoja wa Ulaya kwa jumla.

## II. MAANA

2. Maana ya watetezi wa haki za binadamu, kwa madhumuni ya Miongozo hii inatoka na na aya ya kwanza ya uendeshaji ya Tamko la Umoja wa Mataifa, kuhusu Haki na Wajibu wa Kila Mtu, Vikundi na Vyombo vya Jamii Kuendeleza na Kulinda Uhuru wa Msingi na Haki za Binadamu Zinazotambuliwa Kimataifa (angalia kiambatanisho I) linayotamka kuwa ‘kila mtu ana haki binafsi na kwa kushirikiana na wengine kuendeleza na kujitahidi kuhakikisha ulinzi na ufanikishaji wa haki za binadamu na uhuru wa msingi katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa.
3. Watetezi wa haki za binadamu ni watu, vikundi au vyombo vya jamii vinavyoendeleza na kulinda uhuru wa msingi wa haki za binadamu zinazotambuliwa Kimataifa. Watetezi wa haki za binadamu wanajitahidi kuhakikisha kuwapo kwa ulinzi, uendelezaji wa haki za kiraia na za kisiasa pamoja na uendelezaji, ulinzi na ufanikishaji wa haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Watetezi wa haki za kibinadamu pia wanaendeleza na kulinda haki za wanakikundi kama vile wenyeji. Maana hii haijumuishi watu au vikundi vinavyofanya au kueneza vurugu.

## III. UTANGULIZI

4. Umoja wa Ulaya unaunga mkono kanuni zilizomo katika Tamko la Haki na Wajibu wa Kila Mtu, Vikundi na Vyombo vya Jamii Kuendeleza na Kulinda Uhuru wa msingi na Haki za Binadamu Zinazotambuliwa Kimataifa. Ingawa wajibu wa msingi wauendelezaji na ulinzi wa haki za binadamu unahusu nchi,Umoja wa Ulaya unatambua kuwa watu binafsi, vikundi na vyombo vya jamii vyote vinatoa mchango mkubwa katika kukuza juhudi za kutetea haki za binadamu. Shughuli za watetezi wa haki za binadamu ni pamoja na:
    - Kutunza kumbukumbu za matukio ya ukiukaji haki za binadamu.
    - Kutafuta tiba kwa waathirika wa ukiukaji wa haki za binadamu kwa sheria, kisaikolojia, matibabu na msaada mwingine.
    - Kupambana na utamaduni wa kutoadhibiwa ambao ni kuficha ukiukaji wa mara kwa mara na wa mfululizo wa haki za binadamu na uhuru wa msingi; na
    - Kujumuisha utamaduni wa haki za binadamu na taarifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu, katika ngazi ya taifa, kanda na kimataifa.
5. Kazi ya watetezi wa haki za binadamu mara nyingi inahusisha ukosoaji wa sera za serikali na hatua zinazochukua. Hata hivyo serikali zisione kama kufanya hivyo ni uadui. Kanuni ya kuruhusu uhuru wa

mawazo na mjadala huru kuhusu sera na hatua za serikali ni ya msingi na ni njia iliyojaribiwa na kupimwa ya kuweka kiwango kizuri cha kulinda haki za binadamu. Watetezi wa haki za binadamu wanaweza kusaidia serikali katika uendelezaji na kulinda haki za binadamu. Kama sehemu ya mchakato ya uelekezi wanaweza kutoa mchango muhimu katika kutunga sheria zinazofaa na kusaidia kutayarisha mipango ya taifa na mikakati kuhusu haki za binadamu. Wajibu huu ni lazima utambuliwe na kuungwa mkono.

6. Umoja wa Ulaya unatambua kwamba shughuli za watetezi wa haki za binadamu kwa miaka mingi zimepata umaarufu. Zimezidi kuhakikisha ulinzi zaidi kwa waathirika wa ukiukaji wa haki. Hata hivyo, mafanikio haya hayakupatikana kwa urahisi, watetezi wenyewe wamezidi kuwa walengwa wa mashambulizi na haki zao zimekiukwa katika nchi nyingi. Umoja wa Ulaya unaamini kwamba ni muhimu kuhakikisha usalama wa watetezi wa haki za binadamu na kulinda haki zao. Kwa hali hiyo ni muhimu kutumia mtazamo wa jinsia wakati wa kushughulikia suala la watetezi wa haki za binadamu.

## IV. MIONGOZO YA UENDESHAJI

7. Sehemu ya uendeshaji ya miongozo hii inakusudia kubainisha njia na namna ya kufanikisha uendelezaji na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu kwa kuzingatia Sera ya Pamoja ya Nchi za Nje na Usalama.

### Ufuatiliaji, utoaji taarifa na tathmini

8. Mabalozi wa Umoja wa Ulaya wamekwishaombwa kutoa taarifa za vipindi kuhusu hali ya haki za binadamu katika nchi walikopangiwa kufanya kazi. Kamati ya utendaji wa baraza kuhusu haki za binadamu (COHOM) imeidhinisha muhtasari wa makala za taarifa kuwezesha kazi hiyo. Pamoja na makala za taarifa ofisi za ubalozi hazina budi kushughulikia hali ya watetezi wa haki za binadamu katika utoaji wao wa taarifa na kuonyesha matukio ya vitisho au mashambulizi yoyote dhidi ya watetezi wa haki za binadamu. Kwa hali hiyo Mabalozi (HOM) lazima waelewe kwamba muundo wa kitaasisi unaweza kuleta taathira muhimu kuhusu uwezo wa watetezi wa haki za binadamu kutimiza kazi yao kwa usalama. Masuala kama vile ya kisheria, mahakama, utawala au hatua nyingine zinazofaa yanayochukuliwa na Nchi kuwalinda watu dhidi ya vurugu, vitisho, ulipizaji kisasi, ubaguzi mbaya unaosemekana kutokea iwe kisheria au si kisheria, shinikizo au kitendo chochote cha holela kutokana na utekelezaji halali wa haki yoyote iliyotajwa katika Tamko la Umoja wa Mataifa Kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu, yote yana umuhimu kwa hali hii. Mabalozi wa Umoja wa Ulaya wanatakiwa kushughulikia hali ya watetezi wa haki za binadamu katika mikutano ya vikundi vya kazi vya nchi husika kuhusu haki za binadamu. Pale inapohitajika, Mabalozi (HOM) watoe mapendekezo kwa COHOM ya hatua inayoweza kuchukuliwa na Umoja wa Ulaya, ikiwemo kulaani vitisho na mashambulizi dhidi ya watetezi wa haki za binadamu, pamoja na uzuiaji wa maandamano na matamko ya wananchi, pale ambapo watetezi wa haki za binadamu wako hatarini au hatarini zaidi. Mabalozi (HOM) wanaweza kuamua kuendesha hatua ya haraka ya nchi husika kuunga mkono watetezi wa haki za binadamu ambao wako hatarini zaidi na kutoa taarifa ya hatua hiyo kwa COHOM na vikundi vingine vinavyoshughulikia mapendekezo kuhusu upeo wa kufuatilia hatua ya Umoja wa Ulaya. Mabalozi (HOM) lazima watoe taarifa kuhusu hatua ya umoja wa Ulaya kwenye taarifa zao. Aidha ofisi za Ubalozi lazima zizingatie hatari mahsusi zilizowakabili watetezi wanawake wa haki za binadamu.

9. Taarifa za HOM na taarifa nyingine muhimu kama vile taarifa na mapendekezo kutoka Ofisi Maalum kuhusu watetezi wa haki za binadamu. Ofisi Maalum za Umoja wa Mataifa na vyombo vya Mikataba na Kamishna wa haki za binadamu wa baraza la Ulaya, pamoja na asasi zisizo za serikali, vitawezesha COHOM na vyombo vingine vya utendaji kubainisha hali ambapo hatua ya Umoja wa Ulaya inatakiwa na kuamua hatua za kuchukuliwa au, pale inapofaa kutoa mapendekezo kwa hatua kama hiyo kwa PSC/Baraza.

### Wajibu wa ujumbe wa Umoja wa Ulaya katika kusaidia na kulinda watetezi wa haki za binadamu

10. Katika nchi nyingi **za tatu** ujumbe wa Umoja wa Ulaya (ofisi za ubalozi wa nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya na ujumbe wa Tume ya Ulaya) ni kiungo kikuu cha mawasiliano kati ya Umoja wa Ulaya na nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya na watetezi wa haki za binadamu walioko kwenye harakati. Kwa hiyo wana wajibu muhimu sana katika kutekeleza sera ya Umoja wa Ulaya kuhusu watetezi wa haki za binadamu. Kwa hiyo ujumbe wa Umoja wa Ulaya lazima ujitahidi kutumia sera ya kuunga mkono juhudi za watetezi wa haki za binadamu. Wakati huo huo lazima uelewe kwamba katika baadhi

ya matukio hatua zinazochukuliwa za Umoja wa Ulaya zinaweza kusababisha **vitisho** au mashambulizi dhidi ya watetezi wa haki za binadamu. Kwa hiyo ni lazima pale inapofaa zishauriane na watetezi wa haki za binadamu kuhusiana na hatua zitakazofikiriwa kuchukuliwa. Kwa niaba ya Umoja wa Ulaya, Ujumbe wa Umoja wa Ulaya lazima utoe mwitiko kwa watetezi wa haki za binadamu na familia zao. Hatua ambazo ujumbe wa Umoja wa Ulaya unaweza kuchukua ni pamoja na:

- Kutayarisha mikakati ya mahali husika kwa ajili ya utekelezaji wa miongozo hii, kwa kuzingatia zaidi ya watetezi wanawake wa haki za binadamu wanaoendeleza na kulinda haki za binadamu. Ujumbe wa Umoja wa Ulaya utazingatia kuwa miongozo hii inawahusu watetezi wa haki za binadamu wanaoendeleza na kulinda haki za binadamu, ziwe za kiraia, kiutamaduni, kiuchumi kisiasa au kijamii. Ujumbe wa Umoja wa Ulaya lazima uwahusishe watetezi wa haki za binadamu na mashirika yao katika kutayarisha na kufuatilia mikakati ya mahali husika;
- Kuandaa angalau mara moja kwa mwaka mkutano wa watetezi wa haki za binadamu na mabalozi kujadili mada kama vile hali ya haki za binadamu ya mahali husika, sera ya Umoja wa Ulaya katika uwanja huu na matumizi ya mkakati wa mahali husika kwa ajili ya utekelezaji wa miongozo ya Umoja wa Ulaya kuhusu watetezi wa haki za binadamu.
- Kuratibu kwa karibu na kupeana taarifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu wakiwemo walio hatarini.
- Kudumisha mawasiliano yanayofaa na watetezi wa haki za binadamu ikiwemo kuwapokea katika ujumbe na kutembelea maeneo yao ya kazi, ifikiriwe kuteua maofisa mahsusi wa ushirikiano pale inapobidi kuhusu kushirikiana matatizo kwa madhumuni haya.
- Kuruhusu pale inapofaa utambuzi wa kuonekana kwa watetezi wa haki za binadamu na kazi yao kutumia matumizi yanayofaa ya vyombo vya habari
- Ikiwemo internet na teknolojia mpya za habari na mawasiliano, uenezaji ziara au mialiko kwa madhumuni kama kukabidhi zawadi walizopata.
- Pale inapofaa kuwatembelea watetezi wa haki walio garezani au kizuizi cha nyumbani na kuhudhuria kesi zao kama watazamaji.

**Kuendeleza heshima kwa watetezi wa haki za binadamu kuhusiana na nchi za tatu katika mikutano inayohusisha pande mbalimbali.**

11. Madhumuni ya Umoja wa Ulaya ni kushaswishi nchi za tatu kutimiza majukumu yao ya kuheshimu haki za watetezi wa haki za binadamu na kuwalinda dhidi ya mashambulizi na vitisho kutoka nchi zisizoshiriki. Katika mawasiliano yake na nchi za tatu, Umoja wa Ulaya, kama ni lazima zitaonyesha umuhimu wa nchi zote kufuata na kutii kanuni na viwango vya kimataifa vinavyohusika, hasa Tamko la Umoja wa Mataifa. Madhumuni ya jumla ni kujenga mazingira ambapo watetezi wa haki za binadamu wanaweza kufanya kazi kwa uhuru. Umoja wa Ulaya utaeleza madhumuni yake kama sehemu muhimu ya sera yake ya haki za binadamu na utasisitiza umuhimu unaoweka katika kulinda watetezi wa haki za binadamu. Hatua za kuunga mkono madhumuni haya zitajumuisha zifuatazo:
    - Pale ambapo Rais au Mwakilishi wa Ngazi ya Juu wa Sera ya Pamoja ya Nchi za Nje na Usalama au Mwakilishi binafsi wa SG/HR kuhusu Haki za Binadamu au Wawakilishi Maalum na Ujumbe wa Umoja wa Ulaya au Wawakilishi wa Nchi Wanachama au Tume ya Ulaya wanatembelea nchi ya tatu, pale inapofaa, watajumuisha mikutano na watetezi wa haki za binadamu ambapo matukio moja moja na masuala yanayolalamikiwa na kazi ya watetezi wa haki za binadamu, yanayoshughulikiwa kama sehemu ya ziara zao.
    - Sehemu ya haki za binadamu ya mazungumzo ya kisiasa kati ya Umoja wa Ulaya wa nchi za tatu na mashirika ya kanda, pale inapofaa, yatajumuisha hali ya watetezi wa haki za binadamu. Umoja wa Ulaya utasisitiza kuunga mkono watetezi wa haki za binadamu na kazi yao na kuuliza kero la kila mtetezi pale inapofaa. Umoja wa Ulaya utakuwa makini kuwahusisha watetezi wa haki ya binadamu, katika utaratibu unaofaa katika matayarisho, ufuatiliaji na tathmini ya mazungumzo kwa mujibu wa Miongozo ya Umoja wa Ulaya kuhusu mazungumzo ya haki za binadamu.

- Viongozi wa ujumbe wa Umoja wa Ulaya na ofisi za ubalozi wa Umoja wa Ulaya watayakumbusha mamlaka ya nchi za tatu kuhusu wajibu wao wa kutekeleza hatua zinazofaa za kuwalinda watetezi wa haki za binadamu waliomo au wanaoweza kuwa katika hatari.
- Kushirikiana kwa karibu na nchi nyingine zenye mawazo sawa hasa katika Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa na baraza kuu la Umoja wa Mataifa.
- Kupendekeza pale inapofaa kwa nchi wakati zikifanyiwa Mapitio ya Kimataifa ya Kipindi ya Baraza la Haki za Binadamu kwamba sheria zao na desturi ziwiane na Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu.
- Kuendeleza uimarishaji wa taratibu za kikanda zilizopo kwa ajili ya kulinda watetezi wa haki za binadamu na za haki za binadamu na taifa, Kamishna wa Haki za Binadamu wa Baraza la Ulaya na Makubaliano Maalum Kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu na za Watu na Kitengo Maalum cha Watetezi wa Haki za Binadamu ndani ya Kamisheni ya Amerika kuhusu Haki za Binadamu na uundaji wa taratibu zinazofaa katika kanda ambazo hazina.

**Kuunga mkono Taratibu Maalum za Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, yakiwemo makubalino maalum kuhusu watetezi wa haki za binadamu**

12. Umoja wa Ulaya unatambua kwamba Taratibu Maalumu za Baraza la haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa (na watu au vikundi vinavyotekeleza makubaliano maalum, Wawakilishi maalum, wataalam wa kujitegemea na vikundi vya utendaji) ni muhimu kwa juhudi za kimataifa za kulinda watetezi wa haki za binadamu kutokana na uhuru wao na uadilifu wao na uwezo wao wa kutenda na kuzungumzia kuhusu ukiukaji dhidi ya watetezi wa haki za binadamu duniani na kufanya ziara za nchini. Wakati Makubaliano Maalum Kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu yana wajibu mahsusi kuhusiana na hilo, mamlaka ya Kanuni Maalum nyingine pia zina umuhimu kwa watetezi wa haki za binadamu. Hatua za Umoja wa Ulaya kuunga mkono Taratibu Maalum zitajumuisha:
    - Kuhimiza nchi kukubali kama jambo la msingi, maombi ya ziara za nchini chini ya Kanuni Maalum za Umoja wa Mataifa.
    - Kuendeleza kupitia Ujumbe wa Umoja wa Ulaya kutumia taratibu za kipaumbele za Umoja wa Mataifa na jamii za haki za kibinadamu za mahali na watetezi wa haki za binadamu wakiwemo, bali hawakomei, kuwezesha uanzishaji wa mawasiliano na kubadilishana taarifa kati ya taratibu za kipaumbele na watetezi wa haki za kinadamu.
    - Kwa kuwa mamlaka za Taratibu Maalumu haziwezi kutekelezwa bila ya rasilimali za kutosha kwa Ofisi ya Kamishna wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa.

**Misaada ya Vitendo kwa Watetezi wa Haki za Binadamu ikiwemo kupitia Sera ya Maendeleo**

13. Programu za Umoja wa Ulaya na Nchi Wanachama zinazolenga kusaidia kuendeleza michakato ya kidemokrasia na asasi, uendelezaji na kulinda haki za binadamu katika nchi zinazoendelea – kama Chombo cha Ulaya kwa ajili ya Demokrasia na Haki za Binadamu-ni miongoni mwa misaada mingi ya vitendo ya kuwasaidia watetezi wa haki za binadamu. Misaada hii inaweza kujumuisha lakini haikomei katika programu za ushirikiano wa Maendeleo ya Nchi Wanachama. Misaada ya vitendo inaweza kujumuisha yafuatayo:
    - Kusaidia watetezi wa haki za binadamu pamoja na kesi zisizo za serikali zinazoendeleza na kuunda shughuli za watetezi wa haki za binadamu, kwa njia ya shughuli kama vile kujenga uwezo na kampeni za kuelimisha wananchi na kuwezesha ushirikiano kati ya asasi zisizo za serikali, watetezi wa haki za binadamu na asasi za kitaifa za haki za binadamu.
    - Kuhimiza na kusaidia uanzishaji na kazi za vyombo vya kitaifa vya uendelezaji na kulinda haki za binadamu vilivyoanzishwa kwa mujibu wa Paris Principles, zikiwemo Asasi za kitaifa za haki za Binadamu, Ofisi za Kupokea Malalamiko na Tume za Haki za Binadamu.
    - Kusaidia uanzishaji wa mitandao ya watetezi wa haki za binadamu katika ngazi ya kimataifa, ikiwemo kuwezesha mikutano ya watetezi wa haki za binadamu ndani na nje ya Umoja wa Ulaya.

- Kujitahidi kuhakikisha kuwa watetezi wa haki za binadamu katika nchi za tatu wanapata rasilimali, zikiwemo fedha, kutoka nchi za nje na kwamba wanaweza kupashwa habari kuhusu upatikanaji wa rasilimali hizo na namna ya kuomba.
- Kuhakikisha kuwa programu za elimu ya haki za binadamu pamoja na mambo mengine zinaendeleza tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu.
- Kuchukua hatua kwa ajili msaada wa haraka na kulinda watetezi wa haki za binadamu walio hatarini katika nchi ya tatu, kama vile, pale inapofaa, kutoa viza za dharura na utoaji wa hifadhi ya muda katika nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya.

**Wajibu wa Vyombo vya Utendaji wa Baraza**

14. Kwa mujibu wa mamlaka yake COHOM itapatia utekelezaji na ufuatiliaji wa Miongozo kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu kwa uratibu wa karibu na ushirikiano na Vyombo vya Utendaji vya Baraza vinavyohusika. Hii itajumuisha:
    - Uendelezaji wa kuingiza suala la watetezi wa haki za binadamu katika sera za Umoja wa Ulaya zinazohusika na hatua zinazochukuliwa.
    - Kufanya mapitio ya utekelezaji wa Miongozo hii kwa muda unaofaa.
    - Kuendelea kuchunguza kadiri inavyofaa njia nyingine zaidi za ushirikiano na Umoja wa Mataifa na taratibu nyingine za kitaifa na kimataifa katika kusaidia watetezi wa haki za binadamu.
    - Kutoa taarifa kwa Baraza kupitia PSC na COREPER inavyofaa kila mwaka, kuhusu maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Miongozo hii.

**Kiambatanisho cha Kwanza hadi kwa Kiambatanisho hadi Kwa kiambatanisho kingine**
(Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu)

**Tamko la Haki na Wajibu wa Watu Binafsi, Makundi na Mashirika ya Kijamii la Kuendeleza na Kulinda Haki za Binadamu Zinazotambuliwa Kila Mahali na Uhuru wa Kimsingi**

**Kiambatanisho cha Pili hadi kwa Kiambatanisho hadi kwa KIAMBATANISHO**

**Mashirika Yafaayo ya Kimataifa**

- Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu
- Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa
- Mapatano dhidi ya Mateso na Adhabu au utendewaji mwingine ulio wa kikatili, unyama au unaodhalilisha
- Mapatano kuhusu Haki za Mtoto
- Mapatano kuhusu Ukomeshaji wa Ubaguzi Dhidi ya Wanawake
- Mapatano kuhusu Ukomeshaji wa Aina zote za Ubaguzi wa Kikabila
- Mapatano ya Ulaya kuhusu Haki za Binadamu, itifaki zake na sheria zifaazo za Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu
- Mkataba wa Kijamii wa Ulaya/Mkataba wa Kijamii wa Ulaya uliorejelewa
- Mkataba wa Kiafrika kwa Haki za Watu na Binadamu
- Mapatano ya Amerika kuhusu Haki za Binadamu
- Mapatano ya Geneva kuhusu Ulinzi wa Waathiriwa wa Vita na itifaki zake, pamoja na maagizo ya kitamaduni ya sheria za kibinadamu zinazotumika katika migogoro ya kivita
- Mapatano ya 1951 kuhusu Hali ya Wakimbizi na Itifaki yake ya 1967
- Sheria za Roma za Mahakama ya Uhalifu ya Kimataifa
- Tamko la Haki na wajibu wa Watu Binafsi, Makundi na Mashirika ya kijamii katika Kuendeleza na Kulinda Haki za binadamu zinazotambuliwa katika ulimwengu mzima na pia uhuru wa kimsingi.

# KIAMBATANISHO CHA TATU

## Mapendekezo ya *Protection International* ya kuwatetea watetezi wa Haki za Binadamu wanaohusiana na Jumbe za Muungano wa Nchi za Ulaya, Balozi za Mataifa wanachama wa Umoja wa Ulaya na Wawakilishi Maalum wa Umoja huo (vidokezo zaidi kwenye www.protectionline.org)

Kuanzia kuidhinishwa kwa Tamko la Umoja wa Mataifa, vyeo vifuatavyo vimebuniwa ili kuwalinda watetezi wote ulimwenguni:

- Cheo cha **Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu,** kilichobuniwa na Tume ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu
- Cheo cha **Ripota Maalum wa Tume ya Kiafrika kuhusu Haki za Watu na Binadamu**
- **Uamuzi wa Kuwalinda watetezi wa Haki za Binadamu katika Afrika** kupitia kwa mkutano wa Tume ya Kiafrika kuhusu Haki za watu na Binadamu kwenye awamu yake ya 35 iliyofanyika kuanzia tarehe 21 Mei 2004 hadi Juni 2004, kule Banjul, Gambia
- **Kitengo cha Watetezi wa Haki za Binadamu cha Tume ya Inter-American kuhusu Haki za Binadamu**
- **Umoja wa Ulaya pia umeidhinisha Miongozo Mahususi kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu** kama harakati ambayo jumbe za Umoja huo zinafaa kutekeleza ili kuwalinda watetezi wa Haki katika nchi zinazoendelea
- **Baraza la Uropa**: Kuidhinishwa kwa Tamko la Kamati ya Mawaziri tarehe 18 Februari 2008, ili kuwa na ulinzi ulioimarishwa wa watetezi wa haki za binadamu
- Tume ya Haki za Binadamu ya Kiasia

Katika mwaka wa 2004, Baraza la Mawaziri wa Umoja wa Ulaya liliidhinisha Miongozo ya Umoja huo kuhusu watetezi wa Haki za binadamu. Miongozo hiyo inasisitiza Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa Haki za Binadamu na hutoa mapendekezo mahususi yaliyo ya moja kwa moja kwa Jumbe zote za Umoja huo na Mataifa Wanachama wake. Mapendekezo ya Umoja yanalenga:

- Kuidhinisha sera tendaji za kuwalinda watetezi wa haki za binadamu.
- Kutumia njia za kidiplomasia ili kuzifanya serikali za mitaa na zile za kitaifa za wateezi walioathiriwa zijitolee katika kuziheshimu haki za watetezi wa haki za binadamu.

Miongozo ya Umoja wa Ulaya inaweza pia kupatikana kutoka kwa Meza ya Umoja huo na balozi za Mataifa Wanachama.

Jumbe za Umoja wa Ulaya (Balozi za Mataifa wanachama wa Umoja wa Ulaya na Jumbe za Tume ya Umoja huo) huunda nafasi ya kwanza ya mawasiliano kati ya Muungano wa Nchi za Ulaya, Mataifa Wanachama wake na watetezi wa Haki za Binadamu wa Nchini.

*Protection International*, kwa hivyo, inapendekeza kwamba angalau watetezi waweze:

- Kutaka miongozo ya Umoja wa Ulaya itafsiriwe katika lugha yao kisha yasambazwe kwenye mashirika yao, na katika mamlaka za kimaeneo na kitaifa.
- Kutuma habari ya sasa kuhusu hali yao kwa wakuu wa Ujumbe wa Umoja wa Ulaya na kwa mashirika yasiyo ya kiserikali kwenye viwango vya kitaifa na kimataifa ili kujenga ufahamu na kuchochea mawasiliano zaidi baina ya washika dau.

- Kudumisha mawasiliano ya mara kwa mara na Jumbe za Umoja wa EU ili watetezi wa nchini wapate kufahamu miongozo ya Umoja huo na mikakati ya Jumbe za Umoja wa EU ya kutoa ulinzi kwa watetezi. Mawasiliano ya aina hii yataruhusu Jumbe hizi ziwe na ufahamu kuhusu hali za watetezi na mapendekezo yao yaliyoripotiwa kuhusu kutetea na kuunga mkono hatua zitakazochukuliwa.
- Kutaka Jumbe za Umoja wa EU zibadilishane na kutekeleza hatua za kila mara za ulinzi na mikakati ya muda usiomrefu zaidi (wastani).
- Kuwaalika Wakuu wa Ujumbe wa Umoja huo au Maafisa wa Haki za Binadamu waweze kuzuru mahali pa kazi pa watetezi hasa katika maeneo ambayo yana hatari mahususi (kwa mfano, katika sehemu zenye migogoro au ambazo watetezi wameshambuliwa au kutishiwa wakiwa huko).
- Kuomba kuchukuliwa hatua ya haraka pindi watetezi wa haki za binadamu wanapotishiwa au kushikwa.
- Kuomba kupelekwa katika maeneo yaliyo salama kisha usaidizi uliokamilika upewe watetezi wa haki za binadamu walio hatarini.
- Kutafuta au kukubali mialiko na kupandishwa madaraka kutoka kwa Jumbe za Umoja wa EU baada tu ya watetezi wa Haki za Binadamu kutekeleza utathmini wa hatari itakavyoathiri sifa yao inayonawiri. Angazia masuala yote ya usalama yanayoweza kutokea kisha taka upewe usaidizi na uangalizi kutoka kwa Wakuu wa Ujumbe wa EU wakati wa kutoa hukumu kwa kesi zinazowakabili watetezi. Hili linaweza kuleta uadilifu katika kutoa uamuzi ingawa kuwepo kwa wakuu hao kunatakiwa wakati wa kikao chote (kuanzia kusoma mashtaka hadi kifungo) ili kuhakikisha kwamba uwazi utakuwepo. Waambie watazamaji wawasiliane na watetezi wanaoshtakiwa. Waambie watazamaji wa EU wawepo wakati wa kusoma mashtaka dhidi ya wakiukaji wa haki za binadamu ili kuhakikisha kwamba haki itatendeka kwa uhalifu waliotekeleza.
- Kuwa na habari mpya kuhusu ziara ya kirais ya EU, Mwakilishi Mkuu wa Sera ya Kigeni na usalama, wawakilishi maalum wa EU au Wanachama wa Tume ya EU na pia omba uwe na mikutano nao.
- Taka hali za watetezi zijumuishwe katika ajenda ya mazungumzo ya kisiasa baina ya EU, makao makuu ya nchi ya watetezi na mashirika ya kikanda.
- Taka kuwepo kwa hatua za kisiasa zinazolingana na washika dau wengineo, hususan na Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Taka kuwepo kwa mlingano na mashirika yaliyopo ya kimaeneo, wa kulinda haki za binadamu na watetezi wazo, kama vile Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu, Kitengo cha Watetezi cha Tume **ya Inter-American** ya Haki za Binadamu, Tume ya Kisiasa ya Haki za Binadamu.
- Kuzitaka ripoti za Wakuu wa Ujumbe wa EU zisomwe na kila mtu na pia ziwafikie watetezi wa Haki za Binadamu.

## Kuchangisha Fedha

Watetezi wa Haki za Binadamu wanaweza kuchangisha pesa moja kwa moja kupitia kwa balozi (Mipango ya Haki za Binadamu) na pia Muungano wa Nchi za Ulaya (EU) kupitia kwa European Instrument for Democracy and Human Rights (EIDHR). Shirika hili huruhusu Tume ya Ulaya kufadhili mashirika yasiyo ya serikali bila ya idhini ya serikali ya nchi inayoendelea. http://ec.europa.eu/europaid/projects/eidhr/index_en.htm en-htm au EIDHR tu. Maelezo zaidi kuhusu ufadhili mwingine wa kifedha yanapatikana katika kiungo kama hicho.

## Zaidi ya hayo:

Ingawa Miongozo ya EU imesheheni Jumbe za EU, Taasisi, Mataifa wanachama wake na pia Balozi zake, watetezi wa haki za binadamu wanafaa kukumbuka kwamba pia msaada unaweza kupatikana kupitia kwa kundi la mabalozi na mashirika ya kimataifa kwa kuwa Maazimio ya Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa Haki za Binadamu yanaweza kutumiwa na washika dau wote.

# Kiambatanisho Cha Nne

## Muhtasari wa Kijumla wa Hatari Kulingana na Makundi mahususi ya watetezi wa Haki za Binadamu

**Lengo:**

Kufafanua maana ya hatari kulingana na makundi mahususi ya haki za binadamu ili kuizingatia (maana) unapounda mikakati ya usalama/ulinzi na kuimarisha sera za shirika.

Zaidi ya hatari za kawaida wanazokumbana nazo watetezi wa haki za binadamu, sura ya 1.9 inabainisha namna umahususi wa kundi la watetezi hao unafaa kuzingatiwa wakati wa kuunda mpango wa usalama/ulinzi iwe ni kiwango cha mtu binafsi, shirika na/au kati ya shirika.

Mwongozo hauwezi kushughulikia kila kitu na kuchambua makundi yote mahususi ya watetezi wa haki za binadamu yanayofanya kazi katika mazingira tofauti ya kisiasa. Kila kundi na hali litahitaji angalau sura nzima kuhusu suala la ulinzi, ikiwa sio mwongozo mzima: taasisi za kidini, jumuiya za kiasili; makundi yanayoshughulikia haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni; makundi yanayoshughulikia haki za watoto; mawakili na wanasheria; wanahabari; mashirika ya mashambani; wanamazingira; vyama vya wafanyikazi; makundi ya idadi ndogo ya watu; LGBTI[1].

Kwa kuongezea, itahitaji marekebisho ya kila mara ili kuweka mambo yanayotendeka sasa kwa kuwa hali ya kisiasa hubadilika, na ndivyo ilivyo hatari.

Hata hivyo, tusisahau kwamba mantiki ya kimsingi ya uchunguzi wa hatari inabaki vilevile kwa makundi yote ya watetezi wa haki za binadamu na pia watu binafsi. Inahitaji tu kutekelezwa kwa kuzingatia maelezo ya kibinafsi yaliyo mahususi pamoja na vitisho, udhaifu na uwezo unaohusiana nayo.

Jedwali la hapa chini si kamilifu. Linahusu namna maelezo mahususi yanaweza kubainishwa kupitia kwa kuchangizana mawazo. Linaweza kuchukuliwa kama kituo cha kwanza ambacho kila kundi la watetezi litahitaji ili kuangazia kwa kina zaidi yanayolihusu.

Kwa mfano, miungano ya kidini na taasisi inaweza kuwa ya kikristo (ya Kikatoliki, Kitume, Kievanjelisti, Momoni, Kundi la Wakristo lisilopenda mikutano ya Rasmi…), Kiislamu (Sunni, Shia, Sufi…), Kihindi, Kibudha n.k; wanaweza kuwa wanafanya kazi mashambani au mjini; katika mazingira yasiyozingatia sana haki za binadamu; kuhusu mada ambazo si tata zaidi.

Tishio hilo moja linaweza kudhihirisha kwa mitindo tofauti, yaani tishio la hujuma linaweza kuwa dhidi ya watu, vifaa…

Chati ya 3 ingali inahitaji kutumiwa kujuliza maelezo kwa kila kundi.

1 Mwongozo wa ulinzi kwa watetezi wa LGBTI, PI© 2009.

| **Muhtasari wa Kijumla wa Hatari Kwa Mujibu wa Maelezo Mahususi ya Watetezi wa Haki za Binadamu (Haujakamilika)** | | | |
|---|---|---|---|
| **Makundi** | **Maeneo ya kazi** | **Vitisho kutokana na kazi** | **Udhaifu/uwezo** |
| Miungano ya kidini (…) | • Haki za Binadamu, Sheria ya kimataifa ya Binadamu, amali za kidini na chakula cha kutosha<br>• Makundi mbalimbali ya kimadhehebu<br>• (…) | • Wanaaibishwa wanapobandikwa majina “waungaji mkono wa makundi yaliyojihami”<br>• Hujuma kutokana na kubandikwa majina<br>• (…) | • Wanatengwa kimaeneo<br>• Ukosefu wa uungwaji mkono kitaasisi<br>• Kujiunga na miungano<br>• Kukutana ili kazi ifanywe (imani za kidini)<br>• (…) |
| Mashirika ya haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni | • Kuyapa nguvu mashirika na watu binafsi<br>• Chakula cha kutosha, utunzi na ulinzi wa mazingira, miradi ya ukulima, elimu<br>• Utambulisho na haki za makundi madogo<br>• (…) | • Uthabiti wa mashirika unavunja umoja wa washika dau waliojihami<br>• Vikwazo vya kiuchumi<br>• Upenyezi<br>• (…) | • Wao kujiweka wazi kwa washika dau waliojihami katika mahali pao pa kazi<br>• Kutengwa kimaeneo<br>• Kuifikia miungano inayoshughulikia mada inayofanana na yetu na aghalabu ambayo si tata zaidi kuliko masuala mengine ya haki za binadamu kama vile wafungwa wa kisiasa<br>• Uwezo wa kukubali kwa sababu kazi yao huleta faida za papo hapo kwa wenyeji<br>• (…) |
| Mashirika ya kisheria au kimahakama | • Utetezi wa haki za binadamu mara nyingi kupitia harakati za kinembo<br>• Mafunzo kuhusu Haki za binadamu<br>• Juhudi za kupambana na kutoadhibiwa baada ya kukosa na pia kushuhudia mashtaka<br>• Mashauriano ya kisiasa na kisheria<br>• Ukashifu wa wazi wa ukiukaji wa haki za binadamu<br>• Kampeni za malengo ya kisiasa<br>• (…) | • Kudunishwa<br>• Uhalifu<br>• Kupelekwa kortini<br>• Hujuma dhidi ya hadhi yao ya kijamii<br>• Upenyezi<br>• (…) | • Kuwa mbali na mamlaka za kisiasa na kiraia<br>• Usaidizi finyu wa ndani wa kisiasa<br>• Sifa za kitaasisi ziko juu kiasi<br>• Usaidizi wa kitaasisi<br>• Kushirikiana na miungano ya kimataifa ya aina hiyo<br>• (…) |
| Taasisi za kidini | • Msaada wa kibinadamu<br>• (…) | • Unyanyapaa na mateso<br>• (…) | • Udhihirikaji nje<br>• Kujiamini sana (Mungu akipenda/Mungu mlinzi/ kuzaliwa upya…)<br>• Uhalali<br>• Miungano na rasilimali zinazosadikika<br>• Ushawishi/tukio la kisiasa<br>• Mfumo wa madaraka ya kupokezana<br>• Utambulisho wa kiitikadi<br>• (…) |

| **Muhtasari wa Kijumla wa Hatari Kwa Mujibu wa Maelezo Mahususi ya Watetezi wa Haki za Binadamu (Haujakamilika)** | | | |
|---|---|---|---|
| **Makundi** | **Maeneo ya kazi** | **Vitisho kutokana na kazi** | **Udhaifu/uwezo** |
| Jamii za mashambani | • Kudai ardhi na kuipokea tena<br>• (…) | • Kulinda mipaka kwa watu wengine<br>• Uondolewaji au ufungiaji<br>• Kunyamazishwa na wamiliki wa ardhi wenye nguvu<br>• (…) | • Kutengwa<br>• Uongozi usio mzuri<br>• Umaskini<br>• Ujuzi wa kukuza mazao<br>• Ufahamu wa mipaka<br>• Maarifa ya kiuendeshaji<br>• Ugumu wa kupata habari na elimu<br>• Ugumu wa kupata umeme na maji<br>• Mpaka wa kilimo uliogawanywa<br>• Kutofautiana katika masilahi na uundaji<br>• (…) |
| Vyama vya wafanyikazi | • Haki za wafanyikazi<br>• (…) | • Kuaibishwa na kufanywa wahalifu<br>• Kufutwa kazi<br>• (…) | • Mashirika ya kijamii ulimwenguni kote yaliyo na uanachama uliosajiliwa<br>• Kuwa na mwelekeo wa uongozaji<br>• Mapendeleo ya kisiasa<br>• Kufanya kazi kwa makundi<br>• Uwezo wa kuhamasisha wanachama wengi na pia wasio wanachama<br>• Uwezo wa kuwa na athari katika mahusiko muhimu ya kiuchumi na kijamii<br>• Kudinda kushirikiana na watetezi wa Haki<br>• Utambulisho wa kisiasa<br>• Muundo wa mamlaka ya kimakundi<br>• (…) |
| Wanahabari | • Uchunguzi na uchapishaji wa makiuko ya haki za binadamu<br>• (…) | • Kuaibishwa<br>• Hujuma<br>• (…) | • Huwa na hatari ya kukabiliwa na ufisadi na vyombo vya habari<br>• Kutangamana na miungano ya kimataifa na ile ya wanahabari<br>• Kutangamana na vyombo vya habari<br>• Hadhi yao kwa umma<br>• Walinzi wa demokrasia<br>• Watu binafsi<br>• (…) |

| **Muhtasari wa Kijumla wa Hatari Kwa Mujibu wa Maelezo Mahususi ya Watetezi wa Haki za Binadamu (Haujakamilika)** | | | |
|---|---|---|---|
| **Makundi** | **Maeneo ya kazi** | **Vitisho kutokana na kazi** | **Udhaifu/uwezo** |
| LGBTI | • Haki za LGBTI<br>• (…) | • Kuaibishwa, kudunishwa na kufanywa wahalifu<br>• Kampeni ya hadharani dhidi ya LGBTI<br>• Utungaji wa sheria dhidi ya LGBTI<br>• (…) | • Kuweza kukabiliwa na mapendeleo ya kijamii, kitamaduni, kidini na kiari<br>• Kutangamana na Miungano ya Kimataifa<br>• Aghalabu hutengwa na mtetezi mwingine wa haki za binadamu<br>• Wakati mwingine hushusha hadhi<br>• Haki zao haziendelezwi kwa urahisi<br>• Mkingamo kwa mashirika yote yanayotetea haki za binadamu<br>• Kutambulika kwa urahisi<br>• Kuweza kuathiriwa na hofu ya jinsi moja na pia ile iliyo tofauti kutoka kwa mamlaka ifaayo kulinda raia wote<br>• Kuweza kukabiliwa na shinikizo na msongo wa kisaikilojia<br>• (…) |
| Utambulisho wa makundi ya watu wachache | • Haki za kutambuliwa<br>• (…) | • Kuaibishwa na kutengwa<br>• Kunyimwa haki zao za za kiraia<br>• (…) | • Kubadilishana utambulisho wa kikabila na kitamaduni<br>• Wanaweza kukaa katika maeneo tofauti ya kijiografia<br>• Kupendelea kufanya kazi kwa kujifungia pamoja<br>• Kutengwa<br>• Vigumu kutangamana na makundi mengine ya kutetea haki za binadamu<br>• Vigumu kuendeleza ufahamu kuhusu hali yao<br>• (…) |

# Marejeleo na vifaa vya ziada

## Marejeleo


- Amnesty International (2003): "*Essential actors of our time. Human Rights defenders in the Americas.*" AI International Secretariat (Index AI: AMR 01/009/2003/s
- AVRE na ENS (2002): "*Afrontar la amenaza por persecución sindical*". Escuela de Liderazgo Sindical Democrático. Kimechapishwa na Escuela Nacional Sindical and Corporación AVRE. Medellín, Colombia.
- Bettocchi, G., Cabrera, A.G., Crisp, J., na Varga, A (2002): "*Protection and solutions in situations of internal displacement*". EPAU/2002/10, UNHCR.
- Cohen, R. (1996): "*Protecting the Internally Displaced*". World Refugee Survey.
- Conway, T., Moser, C., Norton, A. na Farrington, J. (2002) "*Rights and livelihoods approaches: Exploring policy dimensions*". DFID Natural Resource Perspectives, no. 78. ODI, London.
- Dworken, J.T "*Threat assessment*". Series of modules for OFDA/InterAction PVO Security Task Force (Mimeo, iliyojumuishwa katika REDR, Security Training Modules, 2001).
- Eguren, E. (2000): "*Who should go where*? Examples from Peace Brigades International", katika "*Peacebuilding: a Field Perspective. A Handbook for Field Diplomats*", by Luc Reychler na Thania Paffenholz (wahariri). Lynne Rienner Publishers (London).
- Eguren, E. (2000), "T*he Protection Gap: Policies and Strategies*" in the ODI HPN Report, London: Overseas Development Institute.
- Eguren, E. (2000) "*Beyond security planning: Towards a model of security management. Coping with the security challenges of the humanitarian work*". Journal of Humanitarian Assistance. Bradford, UK. www.jha.ac/articles/a060.pdf
- Eriksson, A. (1999) "*Protecting internally displaced persons in Kosovo*". http://web.mit.edu/cis/www/migration/kosovo.html#f4
- Lebow, Richard Ned na Gross Stein, Janice. (1990) "*When Does Deterrence Succeed And How Do We Know?*" (Occasional Paper 8). Ottawa: Canadian Inst. for Peace and International Security.
- Mahony, L. na Eguren, E. (1997): "*Unarmed bodyguards. International accompaniment for the protection of human rights*". Kumarian Press. West Hartford, CT (USA).
- Martin Beristain, C. na Riera, F. (1993): "*Afirmación y resistencia. La comunidad como apoyo*". Virus Editorial. Barcelona.

- Paul, Diane (1999): "*Protection in practice: Field level strategies for protecting civilians from deliberate harm*". ODI Network Paper no. 30.
- SEDEM (2000): *Manual de Seguridad. Seguridad en Democracia*. Guatemala.
- *Sustainable Livelihoods Guidance Sheets* (2000). DFID. London, February 2000
- Sutton, R. (1999) *The policy process: An overview*. Working Paper 118. ODI. London.
- ACNUR (2004): "*About Human Rights Defenders*" (extensive information): http://www.unhchr.ch/defenders/about1.htm
- ACNUR (2004): "*Human Rights Defenders: Protecting the Right to Defend Human Rights*". Fact Sheet no. 29. Geneva.
- ACNUR (2004): On women defenders: www.unhchr.ch/defenders/tiwomen.htm
- ACNUR (1999): *Protecting Refugees: A Field Guide for NGO*. Geneva.
- ACNUR (2001): *Complementary forms of protection. Global Consultations on International Protection*. EC/GC/01/18 4 September 2001
- ACNUR (2002) *Strengthening protection capacities in host countries. Global Consultations on International Protection*. EC/GC/01/19 * / 19 April 2002
- ACNUR-Department of Field Protection (2002) *Designing protection strategies and measuring progress: Checklist for UNHCR staff*. Mimeo- Geneva.
- Van Brabant, Koenraad (2000): "*Operational Security Management in Violent Environments*". Good Practice Review 8. Humanitarian Practice Network. Overseas Development Institute, London.

## Marejeleo ya Ziada

Protection International-PI hutoa mafunzo na ushauri kuhusu ukadiriaji wa hatari, ulinzi na usalama kwa watetezi wa haki za binadamu tangu mwaka 2000. Tafadhali wasiliana na: **pi@protectioninternational.org** au barua ya posta: PI, Rue de la Liniere, 11-1060 Brussels (Belgium).

Simu: + 32 (0)2 609 44 05; +32 (0)2 609 44 07

Faksi: +32 (0)2 609 44 06

**www.protectioninternational.org**

**www.protectionline.org**

Tactical Technology Collective: **www.tacticaltech.org** (tangu 2003 – utaalamu wa kiufundi katika usalama wa teknolojia ya sasa): "NGO in a Box".

# Faharasa



NENO LA UTANGULIZI KUHUSU TOLEO LA KWANZA NA HINA JILANI ........................ 3

PROTECTION INTERNATIONAL (UWASILISHAJI) ............................................ 4

DIBAJI ........................................................................................ 6

UTANGULIZI .................................................................................. 9

**SEHEMU YA 1:** ULINZI NA USALAMA

UTANGULIZI ................................................................................ 15

**SUR 1.1** KUFANYA MAAMUZI BORA KUHUSU ULINZI NA USALAMA.................. 17

**SURA 1.2.** KUTATHMINI HATARI .................................................... 27

**SURA 1.3.** KUELEWA NA KUTATHMINI MATISHIO .................................. 39

**SURA 1.4.** MATUKIO YA USALAMA .................................................. 45

**SURA 1.5.** KUZUIA NA KUKABILIANA NA HUJUMA .................................. 53

**SURA 1.6.** KUUNDA MKAKATI WA KIMATAIFA WA USALAMA .......................... 65

**SURA 1.7.** KUANDAA MPANGO WA USALAMA ........................................ 75

**SURA 1.8.** KUIMARISHA USALAMA NYUMBANI NA KAZINI ............................ 83

**SURA 1.9.** USALAMA KWA WATETEZI WANAWAKE WA HAKI ZA BINADAMU ..........97

**SURA 1.10.** USALAMA KATIKA MAENEO YA VITA VYA KUJIHAMI...................... 109

**SURA 1.11.** USALAMA KATIKA TEKNOLOJIA YA MAWASILIANO NA HABARI .......... 113

## SEHEMU YA 2 USALAMA WA SHIRIKA

UTANGULIZI ........................................................................ 131

SURA 2.1. UKADIRIAJI WA UTENDAJI WA SHIRIKA: "GURUDUMU LA USALAMA" ... 133

SURA 2.2. KUHAKIKISHA KWAMBA SHERIA NA TARATIBU ZA USALAMA ZINAFUATWA ...................................... 143

SURA 2.3. NAMNA YA KUIMARISHA ULINZI WA USALAMA WA SHIRIKA ................................................ 149

## SEHEMU YA TATU: ITIFAKI, MIPANGO YA KIDHARURA NA SERA NYINGINEZO

UTANGULIZI ........................................................................ 161

SURA 3.1. JINSI YA KUPUNGUZA HATARI INAYOHUSIANA NA UPEKUZI WA AFISINI/AU UVAMIZI......................................163

SURA 3.2. UZUILIWAJI, KUKAMATWA, KUTOROSHWA NA KUTEKWA NYARA KWA MTETEZI......................................... 171

SURA 3.3. ULINZI WA HABARI ULIO SALAMA ........................................ 181

SURA 3.4. USALAMA NA WAKATI WA MAPUMZIKO ..................................... 187

## VIAMBATANISHO

MAAZIMIO YA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU ... 191

TAMKO LA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU ....... 197

MAPENDEKEZO YA UTETEZI YA PROTECTION INTERNATIONAL KWA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU ...................................................... 203

MUHTASARI WA KIJUMLA WA HATARI KULINGANA NA MAKUNDI MAHUSUSI YA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU ................................... 205

MAREJELEO TEULE PAMOJA NA YALE YA ZIADA ........................................ 209

FAHARASA YA VITENGO ............................................................ 211

FAHARASA YA MAUDHUI ............................................................ 213

# Faharasa ya maudhui



Azimio, Azimio la Umoja wa Mataifa
kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu, 191

barua pepe, utumiaji wa barua pepe ulio salama, 117, 118

dhuluma za kimapenzi, 181, 100, 101, 106

funguo, vifuli (tazama chini ya kuhusu usalama wa afisi)

habari iliyopotea, iliyoibiwa au kutwaliwa, 165, 186, 184

habari, usimamizi wenye ulinzi wa, 181

habari, usiri wa, 189

hadhi, hadhi ya Shirika na Usalama, 140

hatari, kukabiliana nayo, 66, 67

hatari, maelezo maalum ya wasifu wa mtetezi wa haki za binadamu, 205

jedwali la usalama, 133, 153

kamera (tazama chini ya  usalama wa afisi)

kampuni za kibinafsi za usalama, 88

kizuizi na nafasi ya kijamii na kisiasa ya mtetezi, 65-70

kompyuta na usalama wa faili, 115

kufuatilia utii wa sheria za usalama(tazama kuhusu sheria)

kukabiliana na ujasusi, 60

kulenga, 28

kupinga mipango ya kuimarisha usalama, 154

kutathmini hatari, 27

kutekwa nyara kwa mtetezi, 171

kutiwa nguvuni kwa mtetezi, 171

kuuliza maswali (mbinu ya uchunguzi wa mazingira yako ya kazi), 157

machimbo, 111

maduka ya mtandao na usalama, 126

magari, usafiri katika maeneo yenye vita, 111

mahali afisi ilipo na usalama, 84

mashambulizi, jinsi ya kuyakabili, 62

mashambulizi, kubainisha uwezekano
wa kutokea kwa shambulizi la moja kwa moja, 56

mashambulizi, kubainisha uwezekano
wa shambulizi kutoka kwa wahalifu, 57

mashambulizi, kubainisha uwezekano
wa shambulizi lisilo la moja kwa moja, 58

mashambulizi, kusaidia kutambua wakati shambulizi linaandaliwa, 54

mashambulizi, nani anaweza kumshambulia mtetezi?, 54

matishio, taratibu za, 41

matishio, ya kisadfa, ya moja kwa moja, matishio yaliyokusudiwa, 28

matokeo ya ulinzi (wakati wa kuzuia shambulizi), 73

matukio ya kiusalama (tazama chini ya matukio)

matukio, jinsi ya kutathmini tukio la usalama, 47

matukio, kukabiliana nayo, 47

matukio, kutoa hisia zilizovuka mipaka dhidi ya matukio, 47

matukio, kuyashughulikia haraka, 48

matukio, kuyatambua na kuyachunguza

matukio, kwa nini ni muhimu sana?, 45

matukio, kwa nini yanaweza
kuendelea bila kutambuliwa/kujulikana, 46

matukio, ni lini na kwa jinsi gani unaweza kuyatambua?, 45

matumizi ya dawa za kulevya na usalama, 188

matumizi ya pombe kupindukia na usalama, 188

mazoea ya shirika kuhusu usalama, 11, 75

mazungumzo na mawasiliano ya usalama, 113

mifumo ya ziada ya kuhifadhi data katika kompyuta, 166

migahawa, mtandao (tazama kuhusu mtandao)

mikakati ya kutoa majibu (mikakati ya kukabiliana na hatari), 65, 66

miongozo, miongozo ya Jumuiya ya
Ulaya kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu, 197

mitego, 111

mizinga ambayo haijalipuka, 111

mpango wa usalama (tazama kuhusu mpango)

mpango, kuendeleza matumizi ya ratiba ya usalama, 80

mpango, kuuandika taratibu za usalama, 75

mpango, ratiba ya vipengele vya
kujumuishwa katika mpango wa usalama, 78

mtandao na usalama, 116, 117

mtetezi, mtetezi ni nani?, 12

mtetezi, ni nani anaweza kuwa mtetezi, 12

nafasi, nafasi ya kijamii na kisiasa ya kufanya kazi ya watetezi, 68

risasi hatari ya moto, 110

ruhusa na nafasi ya kijamii na kisiasa ya mtetezi, 69, 70

shambulizi, kubainisha uwezekano wa shambulizi kutokea, 55

shambulizi, kuzuia shambulizi linaloweza kutokea, 59

sheria za usalama (tazama kuhusu sheria)

sheria, kufuatilia utii wa sheria za usalama, 147

sheria, kutotii kimakusudi sheria za usalama, 159

sheria, kutotii kusiko kwa makusudi kwa sheria za usalama, 146

sheria, kuunga mkono sheria za usalama, 134, 138, 144, 159

sheria, kwa nini watu hawafuati sheria za usalama, 144, 145

sheria, la kufanya iwapo hazifuatwi, 147

sheria, mitazamo mbalimbali kuhusu sheria za usalama, 144

simu na mawasiliano kuhusu usalama, 115

taratibu za usajili (tazama chini ya usalama wa afisi)

tishio, kubainisha iwapo linaweza kutekelezwa, 41

tishio, kubainisha ni nani anayetoa tishio, 41

tishio, kuelewa matishio kwa kina, 39

tishio, kuendeleza na kumaliza kesi inayohusu tishio, 42

tishio, kuunda tishio kwa mkabala na
kutoa tishio (kuwa tisho dhidi ya kutoa tisho), 40

tishio, ufafanuzi, 39

tishio,hatua tano za kutathmini tishio, 41

tukio, tofauti kati ya matishio na matukio, 45

tukio, tukio la kiusalama ni lipi?, 45

uchunguzi wa mazingira yako ya kazi (mbinu), 17

uchunguzi wa nyanjani (mbinu ya kuchunguza mazingira yako ya kazi), 19

udhaifu na uwezo, orodha ya kufuata, 31

udhaifu, huwa ni nini, 29

ufichaji habari kimaandishi, 119

uhusiano (afisini), uhusiano uliofichika na usalama, 188

uimarishaji wa usalama, 150
upekuzi ndani ya afisi (au uvunjaji wa afisi), 163
upelelezi (na kupinga upelelezi), 60
usalama wa afisi, taratibu za kuingia ndani, 89
usalama wa afisi, upokezi wa vifurushi na barua, 90
usalama wa afisi, vizuizi vya wazi na taratibu za kupokea wageni, 86, 89, 93
usalama wa afisi,funguo na vifuli, 87, 92, 93
usalama wa afisi,orodha ya upekuzi na upekuzi wa mara kwa mara, 94
usalama wa afisi,sehemu za mashambani, 95
usalama wa afisi,taa na ving'ora, 86
usalama wa afisi,udhaifu wa, 83
usimamiaji wa programu ya kompyuta, 125
usimamizi,usimamizi wa usalama, 149, 157
utamaduni, utamaduni wa shirika kuhusu usalama, 11, 145, 146, 156
utekwaji nyara wa mtetezi, 171
utendakazi, kutathmini utendakazi wa mbinu za kiuusalama, 133
utetezi, mapendekezo ya PI ya utetezi kwa mtetezi wa haki za binadamu yanayohusiana na ubalozi wa Umoja wa Ulaya (EU), 203
utii wa sheria za usalama (tazama kwenye sehemu ya sheria)
uwezo na udhaifu, orodha, 31
uwezo, uwezo ni nini katika usalama, 29
uwiano na sheria za usalama (tazama chini ya sheria),
uzuizi wa mtetezi, 171
uzuizi, kukinga uzuizi wa watetezi, 173, 178
uzuizi, kutoa hisia kutokana na uzuizi wa mtetezi, 174-176
ving'ora (tazama chini ya usalama wa afisi)
vitisho, taratibu za, 41
vitisho, vya kisadfa, vya moja kwa moja, vitisho vilivyokusudiwa, 28
wadau, uainishaji (kimsingi,watekelezi wa majukumu, wadau wakuu), 20
wadau, uchunguzi (mbinu za kuchunguza mazingira yako ya kikazi), 20
wakati wa burudani na usalama, 187
watetezi wa kike wa haki za binadamu, 97
watetezi, ni nani anawajibika kuwatetea watetezi, 13
zana za vita na kampuni za kibinafsi za kulinda usalama, 88
ziara, kuzuia kutiwa kizuizini wakati wa ziara, 178

### Luis Enrique Eguren



(Uhispania) ni daktari na mtaalamu kuhusu masuala ya ulinzi, mwanachama wa kitengo cha utafiti na mafunzo cha ***Protection International*** (PI). Amefanya kazi na PBI huko El Salvado, Sri Lanka na Colombia, pamoja na kazi za muda mfupi katika nchi nyinginezo na pia kwenye mashirika mengineyo ya kimataifa. Ni mshauri, mkufunzi na mtafiti ambaye ameandika makala na vitabu mbalimbali kuhusu mada ya utetezi.

### Marie Caraj



Mkalimani na mtaalamu wa masuala ya utetezi. Mwanachama wa kitengo cha utafiti na mafunzo cha ***Protection International*** (PI). Alifanya kazi na PBI na PBI-BEO (1985-2007). Amefanya kazi zilizofana za muda mfupi katika Afrika, Asia, Marekani Kusini. Ni mshauri, mkufunzi na mtafiti.

*"(…) ukubwa wa hatari zinazowakabili watetezi wa haki za binadamu kila siku ni wa kiasi kwamba ni muhimu pia kutafuta mbinu nyinginezo za kuimarisha utetezi wao. Katika hali hii, ninataraji kwamba kitabu hiki cha Mwongozo wa Utetezi kitawasaidia watetezi wa haki za binadamu kuimarisha mipango yao wenyewe ya usalama na mbinu za kujitetea. Watetezi wengi wa haki za binadamu wanashughulika sana na kazi yao ya kuwatetea watu wengine kwa kiasi kwamba hujipa wakati mdogo wa kushughulikia usalama wao binafsi. Ni muhimu kwamba sote tujali usalama wetu na ule wa watu tunaofanyia au tunaofanya nao kazi."*

**(Hina Jilan, aliyekuwa mwakilishi maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu).**

*"Tangu tuwe na mafunzo haya, mambo mengi yamebadilika katika shirika letu, kwa sababu tu kwamba hatukuwa tumeyafahamu mambo mengi tuliyojifunza katika kazi hii. Sasa, tumeimarika kutokana na mafunzo haya, na tunafahamu vizuri zaidi jinsi ya kukadiria hatari tunazokabiliana nazo kila uchao, na pia jinsi ya kufanya uamuzi bora kuhusu matukio ya usalama, vitisho na uwezekano wa yote haya kutokea."*

*"(…) mbinu zako za kufunza ni husishi zaidi, na hivyo ni faida kwa kuwa huturuhusu kubadilishana habari. Tuna uhakika kuwa matokeo yatatupa ufahamu wa kina."*

*"Nilihisi kwamba nilipata mafunzo ya hali ya juu zaidi ya jinsi ya kuwa mtetezi halisi wa haki za binadamu."*

**(watetezi wa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo)**

*"Heko kwa juhudi na mwongozo kwa kuwa ulitupa mafunzo na kutusaidia katika shughuli za maisha yetu ya kila siku."*

**(Mtetezi kutoka Guatemala)**

*"Nilijifunza mengi kuhusu ulimwengu nilioujua kwa muda mrefu, lakini ambao sikuwa nimeupa mtazamo wa aina hiyo."*

**(Mtetezi kutoka Mexico)**

*"(…) Ni mada mpya kabisa kwangu. Ingawa tunafanya kazi katika nyanja kama hii, kila mara hutokea tishio kwa usalama wetu, hatukuwahi kufikiria kuhusu haja ya kuwa na mafunzo kama haya au hatukuwahi kuwa na muda wa kufikiri kuhusu usalama wetu lakini baada ya mafunzo haya, mimi binafsi nilihisi kwamba panafaa kuwa na mazingatio makubwa ya mafunzo haya, kabla ya kuzindua mpango wowote. Yaani mafunzo haya ni muhimu zaidi!!!"*

**(Mtetezi kutoka Nepal)**

PROTECTION international

## Kwa ushirikiano na:

ifa Institut für Auslandsbeziehungen e. V.

Auswärtiges Amt

Iniciativa Europeia para a Democracia e os Direitos do Homen IEDDH


Mwongozo Mpya wa Ulinzi wa Watetezi wa Haki za Binadamu ulitafitiwa na kuandikwa na Enrique Eguren na Marie Caraj, kwenye kitengo cha utafiti na mafunzo cha Protection International.

Protection International, Rue de la Linière, 11, B-1060, Brussels
Tel.: +32(0)2 609 44 07 / +32 (0) 2 609 44 07; Fax: +32 (0) 2 609 44 07
Barua pepe: pi@protectioninternational.org www.protectioninternational.org


Tovuti pekee ya ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu: www.protectioninternational.org